

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 10 Mei, 2016**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

Spika (Mhe. Job Y. Ndungai) Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea na shughuli za leo za Mkutano wa Tatu, Kikao cha Kumi na Sita; Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha mezani.

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

**Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WAZEE NA WATOTO:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. BONNAH M. KALUWA (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA):**

Taarifa ya Msemajji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara. Katibu.

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Swali la kwanza linalekeea Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ilivyo ada, linaulizwa na Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe

Na. 130

**Mpango Mkakati wa Kuwawezesha Wananchi wa Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y MHE. ESTER A. MAHAWE)** aliuliza:-

Serikali kupitia mpango mkakati wa kuwawezesha wananchi wa vijijini iliahidi kutoa shilingi 50,000,000 kwa kila kijiji na mtaa:-

(a) Je, ni lini fedha hizo zitatolewa?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi juu ya njia bora ya kutumia fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi bilioni 59.5 katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 chini ya Fungu 21 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi vijijini kwa kutoa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Fedha hizo zitatolewa mara baada ya kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu na baada ya kukamilisha taratibu mbalimbali zinazolenga kuhakikisha uwepo wa tija katika matumizi ya fedha hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango bora wa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi, ili kuhakikisha matumizi bora ya fedha hizo Serikali inaendelea kukamilisha maandalizi ya utaratibu maalumu wa utoaji wa fedha hizo, ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya ujasiriamali. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepewa kazi ya kuratibu utekelezaji wa mpango huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay. Mbunge wa Mbulu Vijijini swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri je, ni lini sasa Serikali itaanza kutoa mikopo hiyo?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Manyara hasa Mbulu Vijijini wako tayari kabisa kwa elimu hiyo ya ujasiriamali, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kusema anaweza kuanza na Mkoa huo kwa kuwa uko tayari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la lini fedha hizo zitaanza kugawanywa lazima tuangalie *practical realities*. Kwa sababu elimu inahitajika na ahadi haikuwa imewekewa *time frame* ni vizuri tuelewe kwamba fedha hiyo itatolewa ndani ya kipindi hiki, na mapema iwezekanavyo, mara baada ya taratibu zote za kuhakikisha matumizi salama na yenye tija ya kifedha yanakamilika. Kwa hiyo siwezi nikasema exactly ni lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu whether kuanza na Mkoa upi, Manyara au mwingine na hili pia litategemea sana na hali halisi, lakini ninampongeza na ninawashukuru wananchi wa Manyara, kwa kuonesha utayari katika suala hilo.

**SPIKA:** Tunahamia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Waheshimiwa Wabunge swali linaulizwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe.

Na. 131

### **Stahiki kwa Watumishi Waliohamishiwa Wilaya ya Mbogwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Tangu kuanzishwa kwa Wilaya ya Mbogwe mwaka 2012 watumishi iliyokuwa Wilaya ya Bukombe walihamishiwa Wilayani Mbogwe lakini hawajalipwa stahiki zao za posho ya kujikimu pamoja na zile za usumbufo.

Je, ni lini watumishi hao watalipwa stahiki zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya watumishi waliohamishwa kutoka Wilaya ya Bukombe kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni 73 ambaa wanadai posho ya kujikimu na usumbufo ya shilingi milioni 164.14. Kati ya madai hayo fedha ambazo zimeshalipwa kwa watumishi ni shilingi milioni 15.15 kwa watumishi 18. Hivyo, kiasi ambacho watumishi bado wanadia shilingi 148. 99.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Halmashauri imeomba fedha hizo katika Wizara ya Fedha na Mipango ili kulipa deni hilo kwa watumisi 55 waliobaki. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kufuatilia Hazina fedha hizo ili ziweze kupatikana na kulipwa kwa watumishi wanaodai.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masele swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Naomba niiulize Serikali ni lini sasa madai ya hawa watumishi 65 waliosalia yatalipwa?

(ii) Kwa kuwa posho za kujikimu na posho ya usumbufo ni halali ya mtumishi, ni lini sasa Serikali itakuwa tayari kuwa inawalipa watumishi inapowahamisha malipo hayo kwa wakati?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Said Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni lini fedha hizi zitalipwa, nimesema katika jibu langu la msingi, kwamba ni kweli pale kuna watumishi ambao wamehamia katika Halmashauri mpya. Katika kuliona hilo sasa tukaona ni vema sasa hii fedha itengwe katika bajeti ya mwaka wa fedha huu ili watumishi waweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndungu yangu Masele naomba uwe na subira tu, kwa sababu katika Bajeti yetu tulivyopitisha tulizungumza mchakato mkubwa katika suala zima la Halmashauri mpya kwa hiyo katika suala hili la ujenzi wa miundombinu lazima uende sambamba na malipo ya madeni ya watumishi mbalimbali. Kwa hiyo, jambo hili tutakwenda kulifanya kwa kadri iwezekanavyo ili watumishi wale wapate utulivu, wafanye kazi yao kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni jinsi gani tutafanya Halmashauri zinapoanzishwa madai ya watumishi yaweze kulipwa kwanza, hili tutaliwekea maanani. Lakini Waheshimiwa Wabunge tukumbuke kwamba sasa hivi kuna Halmashauri mpya nyingi sana, ofisini kwangu mpaka sasa hivi nimeaandaa *matrix form* ya kuona Halmashauri ina Wilaya mpya ambazo Wabunge mbalimbali wameenda kupeleka maombi Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuweza kuanzishwa. Kwa hiyo, jukumu letu kubwa tutakuwanalo ni kuona ni jinsi gani haya matakwa ya wananchi katika maeneo husika yaweze kufikiwa, lakini hatuvezi kuzuia Halmashauri kuanzishwa kwa sababu posho bado hazijapatikana.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutakuwa tumezuia maendeleo ya wananchi katika maeneo husika, hata ninyi Wabunge hamtoridhika katika hilo. Kwa hiyo, tumechukua ushauri huo wote, lengo kubwa ni mipango yote iende sambamba, Halmashauri zinapoanzishwa na fedha ziweze kulipwa.

**SPIKA:** Bado tupo Wizara ya TAMISEMI swali linaulizwa na Mheshimiwa Bonnah Mosses Kaluwa, Mbunge wa Segerea.

Na. 132

### **Kupandisha hadhi Zahanati ya Tabata ‘A’ kuwa Kituo cha Afya**

**MHE. BONNAH M. KALUWA** aliuliza:-

Katika Jimbo la Segerea kuna zahanati kumi lakini hakuna zahanati moja iliyopandishwa hadhi kuwa kituo kikubwa cha afya chenye uwezo wa kulaza wagonjwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi Zahanati ya Tabata 'A' kuwa Kituo cha Afya kwa sababu ina miundombinu yote inayofaa kwa Kituo cha Afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali naomba nifanye correction ya data, kulikuwa kuna typing error hiyo mwaka 2015/2016 isomeke 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zahanati ya Tabata 'A' haina eneo la kutosha kukidhi upanuzi wa miundombinu unaohitajika na hivyo inakosa sifa ya kupandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya. Ili zahanati iweze kupandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya inatakiwa kuwa na wodi ya wanaume na wanawake zenye vitanda 24 kila moja, jengo la upasuaji, jengo la wagonjwa wa nje (OPD), huduma za mama na mtoto, chumba cha kuhifadhi maiti na kichomea taka incinerator.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zahanati ya Segerea ina eneo la kutosha, Halmashauri ya Manispaa ya llala imetenga shilingi milioni 75. katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ili kujenga wodi zinazotakiwa ikiwa ni maandalizi ya kuipandisha hadhi Kituo cha Afya. Taratibu za kupandisha hadhi zahanati kuwa Kituo cha Afya zinaanza katika Halmashauri yenyewe kupitia vikao vyake, hatimaye maombi hayo yatawasilishwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kuipatia kibali.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kata ya Vinguguti ina wakazi wengi na mpaka sasa hivi Kata ya Vinguguti haina zahanati yoyote.

Swali la Pili, kwa kuwa Kata ya Kipawa, Kata ya Minazi mirefu, Kata ya Kiwalani pamoja na Kata ya Kisukuru na Kimanga zina matatizo kama haya haya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inashirikiana na Manispaa ya llala ili Kata hizi ziweze kuwa na zahanati lakini pia tuweze kuwa na vituo vya afya ili kuondoa msongamano katika Hospitali ya Amana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, Vinguguti kweli ni eneo ambalo lina wakazi wengi sana na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba eneo hili lazima lipatiwe kipaumbele. Lakini naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge

japokuwa juhudii kubwa zinafanyika needs assessment wakati mwingine zinaanza katika Mabaraza yetu ya Madiwani.

Kwa hiyo, kwa sababu nia yako ni njema na Serikali tutakuunga mkono katika eneo hilo. Lakini kikubwa zaidi tutaweka nguvu zaidi katika lile eneo letu la Kituo cha Afya cha Mnyamani, kwa sababu ni eneo ambalo wenzetu wa *Plan International* walifanya juhudii kubwa sana kujenga kituo kile, jukumu letu kubwa ni kwamba kwanza kuwekeza vya kutosha kituo kile angalau kiweze kua-accommodate hii demand iliyokuwepo hivi sasa, wakati huo tukiangalia mtazamo wa mbali jinsi gani tutafanya, eneo lile la Vinguguti tuwe na sehemu ya kujenga zahanati kubwa na siyo zahanati kwa hadhi ya Vingunguti, kujenga moja kwa moja kituo cha afya kutokana na mahitaji ya idadi ya watu waliokuwa katika maeneo yale.

Mheshimwa Spika, eneo la Kipawa, Kiwalani na maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema ni kweli, ukiangalia yana sifa zinazofanana na maeneo ya Vingunguti kwamba watu ni wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba nisema kwamba mimi nipo radhi kabisa kukutana na Mheshimiwa Mbunge kubadilishane mawazo, kwamba tutafanya vipi na kwa sababu nikijua Halmashauri ya Manispaa ya Ilala wana mikakati mikubwa sana ya ujenzi wa sekta afya ukiangalia demand ya sasa hivi iliyokuwepo hivi sasa hospitali yetu ya Amana inazidiwa, hata Hospitali ya Taifa ya Muhimbili idadi ya wagonjwa imekuwa wengi, ni kwa sababu katika ngazi ya chini tunakosa facilities za kuwasaidai wananchi kiasi kwamba kila mngojwa anaona kwanza aende Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI jukumu letu kubwa ni kwamba katika mpango unaokuja tuhakikishe tufanye kila liwezekanalo. Huduma ya afya tuipeleke chini zaidi kupunguza ile *referral system* inayoenda juu ili kuhakikisha hospitali zetu za ngazi za juu ziweze kupata fursa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili kwa sababu Waziri wa Afya kesho ata-table bajeti yake hapa, tutaona mipango mipana katika Wizara Afya ambayo ina lenga moja kwa moja kutatua tatizo la suala la afya katika jamii yetu.

**SPIKA:** Mambo mengine ukiyasikia unaona kama vile unaota, kwamba Vingunguti nzima ile haina zahanati, Kipawa yote haina zahanati, kama vile hadithi ya kufikirika hivi! Ahsante, swali la nyongeza. (Makofi)

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa changamoto kubwa ya zahanati hizi katika Jimbo la Segerea na Manispaa ya Ilala ni maeneo lakini wapo watu wanaoishi jirani na maeneo

hayo, wapo tayari kutoa maeneo yao kwa ajili upanuzi wa maeneo ya zahanati hizi.

Je, Serikali ipo tayari kusaidiana na Halmashauri ya llala kulipa fidia kwa ajili ya kuongeza ukubwa wa maeneo ili kupata zahanati na vituo vikubwa vya afya katika maeneo ya Jimbo la Segerea na Manispaa ya llala kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema katika jibu letu la awali, mahitaji ya afya hapa yamekuwa ni changamoto kubwa sana, nilipofanya reference tulipokuwa na Mbunge wa Segerea kipindi kilichopita, alipokuwa na timu iliyenda eneo la Vingunguti katika machinjio yale, vilevile akaja katika ofisi yangu kuona jinsi gani tutafanya, licha ya suala la machinjio lakini wananchi wana changamoto ya afya.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini hayo mawazo ni mazuri, tutakaa vizuri kubadilishana mawazo ili tuone ni jinsi gani tutafanya ujenzi wa zahanati au kituo cha afya maeneo yaweze kupatikana. Lengo kubwa ni kwamba kina mama na watoto wa maeneo yale waweze kupata huduma kama wengine.

Mheshimiwa Spika, ajenda yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba hospitali zetu za rufaa sasa tupunguze idadi ya wagonjwa siyo mtu anaumwa mguu mpaka aende Muhimbili au Amana haiwezekani hata kidogo. Lazima tuhakikishe mfumo mzuri unatengenezwa katika sekta ya afya katika ngazi za chini kusaidia sekta za juu ziweze kufanya huduma kubwa zinazohitajika.

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti.

Na. 133

**Tatizo la Maji Kibiti**

**MHE. ALLY S. UNGANDO** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji kwenye Jimbo la Kibiti kwenye maeneo ya Delta kama Nyamisati, Mchinga, Mfisini, Kiomboi, Masala, Kiongoroni, Naparoni na Mbunchi.

Je, Serikali imejipangaje kutatua tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Jimbo la Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Delta yanakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 25,780; ambapo wakazi wapatao 12,942 sawa na asilimia 50.2 wanapata huduma ya maji kwa sasa. Hivyo ninakubalianana ipo changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua changamoto hiyo Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 iliidhinisha shilingi milioni 403 na tayari zimepokelewa shilingi milioni 272.1 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika viji kumi. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri imetenga shilingi milioni 83.2 kwaajili ya ujenzi wa mfumo wa maji ya bomba katika kijiji cha Nyamisati.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika maeneo yaliyobaki kadri rasilimali fedha zitakavyo patikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ungando nimekuona.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya ndugu yangu Naibu Waziri.

Je, Serikali haioni kila sababu ya kupeleka visima vyta maringi kwa kuanzia katika maeneo hayo ya Delta?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niweke rekodi sawa katika harakati za kutekeleza miradi mimi naomba nimsifu huyu Mbunge maana siku zote anakuja pale ofisini kwangu na amekuwa akifanya juhudini kubwa kwa Jimbo lake, wakati mwingine anatumia hata resource zake mwenyewe kwa ajili ya Jimbo lake. Lakini mahitaji yake ni jinsi gani tutafanya visima vyta ringi viweze kujengwa, naomba niseme ngoja tulichukue hili.

Lakini kwa ukubwa wake zaidi lazima tuseme kwamba maeneo ya Delta yote yana shida kubwa sana, nikisema suala la Delta halikadhalika hata juzi nilikuwa najibu swalii la ndugu yangu Mbunge wa Jimbo la kule Mwanza, ni kwamba maeneo haya yenye delta yana matatizo makubwa sana siyo maji peke yake hata huduma nydingine za afya na elimu.

Kwa hiyo, nikuombe ndugu yangu kwamba tutajitahidi kufanya kila liwezekanalo ikiwezekana ni kwamba maeneo haya tuweze kuyapatia huduma ya maji ili wananchi wa Kibiti na wao wajisikie kama sawa na wananchi wengine.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Bunda Mjini tangu nikiwa Mbunge wa Viti Maalum nilikuwa nazungumzia mradi wa maji wa kutoka Nyabeu kuja Bunda Mjini. Huo mradi una miaka nane, sasa niulize hivi ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi ule, wananchi wa Bunda ambao hawajawahi kupata maji safi na salama tangu uhuru waone na wenyewe ni wananchi wa Tanzania na ndiyo liwe swali la mwisho kuuliza katika Bunge hili Tukufu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nikiri wazi kwamba Mheshimiwa Ester toka tukiwa katika timu moja alikuwa akiuliza swali hili, naomba niseme.

Mheshimiwa Spika, lakini najua kabisa katika mpango wa maji ambao nadhani Wizara ya Maji watakapokuja ku-table bajeti yao hapa watazungumzia jinsi gani wana programu kuhakikisha maeneo haya miradi yote ya maji inaenda kukamilika. Ukiangalia jinsi gani watazungumza katika bajeti yao ya Wizara ya Maji, sitaki kuwazungumzia sasa. Lakini nikijua kwamba Wizara ya Maji na TAMISEMI ni Wizara pacha, tunahusiana Wizara ya Maji, TAMISEMI, Kilimo halikadhalika na Wizara ya Afya. Mambo yetu yanaingiliana yote kwa pamoja kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Ninajua kabisa katika mpango wa maji wa sekta ya maji namba mbili imeweka mipango ya kumalizia miradi yote ya muda mrefu. Mimi ninaamini wananchi wa Bunda kipindi hiki sasa ule mradi wa maji kama Serikali ilivyokusudia utaweza kukamilika katika kipindi hiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuhamie Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali linalizwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka Mbunge wa Same Mashariki, Mheshimiwa Susan Lyimo kwa niaba ya Naghenjwa.

Na.134

### **Ujenzi wa Barabara ya Same - Mkomazi Mjini**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA)** aliuliza:-

Kumekuwepo na ahadi nyingi wakati wa kampeni kutoka kwa Marais wa Awamu ya Nne na ya Tano kuwa barabara ya kutoka Mkomazi kupitia Bendera, Kihurio, Ndungu, Maore, Kisiwani hadi Same Mjini itajengwa kwa kiwango cha Lami.

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu ahadi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkomazi - Kihurio - Ndungu – Kisiwani hadi Same ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometra 96 inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*). Ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika katika majira yote ya mwaka, Serikali imeendelea kutenga fedha za kufanya matengenezo ya aina mbalimbali. Aidha, julma ya kilometra 19.2 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami katika maeneo yenye watu wengi ya Kisiwani, Gonja, Maore na Ndungu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi za Serikali kuhusu barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imepanga kufanya usanifu wa kina kuanzia Same- Kisiwani- Gonja- Bendera hadi Mkomazi ambapo ni kilometra 96 katika mwaka wa fedha 2016/2017 ikiwa ni maandalizi ya kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami kama viongozi wetu wakuu walivyokuwa wameahidi. Mara usanifu wa kina utakapokamilika Serikali itatafuta fedha ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, hujaridhika swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli sijaridhikia kwa sababu ukiangalia kwa miaka takribani kumi toka wameanza kujenga hivi vipande vidogo vidogo wamejenga kilometra 19 tu, ina maana hizi kilometra 96 labda zitatumia miaka mingine 30.

Swali, kwa kuwa barabara hii sasa ilianza kujengwa kwa vipande vyatya lami toka mwaka 2008 ambapo lami zile ziliziba kabisa makalavati hali inayopelekea

wananchi wa Ndungu na Maore ama kufariki au mazao yao kuharibika kutokana na mvua au maji yale yanayoutuama.

Je, ni lini sasa mtahakikisha kwamba makalavati yale yanajengwa ili watani zangu kule wasipate matatizo pamoja na vifo?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, naelekeea kwangu sasa, kwa kuwa barabara ya Kawawa hadi Marangu Mtoni ilijengwa kwa lami mpaka kiasi cha nusu, lakini cha ajabu barabara hiyo imejengwa kiwango cha lami madaraja yote hayajajengwa hali ambayo inapelekea magari kuanguka na watu wameshafariki, ni lini madaraja katika barabara hiyo yatajengwa hasa ukizingatia *land scape* ya Kilimanjaro? (Makofi)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ile barabara ya kwanza ya Mheshimiwa Naghenjwa ya kutoka Same - Kihurio - Ndungu ndiyo barabara pekee katika Mkoa wa Kilimanjaro isiyokuwa na lami, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (Makofi/Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara hiyo ambayo umeisema haina lami na ni barabara pekee isiyo na lami..

**SPIKA:** Ni katika barabara za TANROADS za Mkoa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, ni kama tulivyosema katika jibu la msingi kwamba sasa tumedhamiria kujenga barabara hiyo yote kwa lami na tutaanzia na upembuzi yakinifu pamoja na usanifu wa kina ambao unafanyika katika mwaka huu ujao wa 2016/2017 wa fedha na ninaamini Waheshimiwa Wabunge mtaipitisha bajeti yetu ili tuweze kuifanya hiyo kazi tuweze kutekeleza ahadi za viongozi wetu wawili waliopita kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wa maeneo hayo wanapenda.

Mheshimiwa Spika, kwa swalii la pili nimejulishwa na CEO wa TANROADS kwamba amelisikia na tutakuja kulitolea jibu wakati wa bajeti ya Wizara.

**SPIKA:** Ahsante sana, majirani wa Same, Mbunge wa Mlalo, Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Kwa kuwa ukikaa karibu na waridi unanukia basi na mimi naomba niombee barabara yangu ya kutoka Mkomazi kwenda Mnazi, Lunguza hadi

Mng'aro sasa ifikiriwe kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini barabara hii itaingia katika mchakato huo? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Injinia Ngonyani kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea ombi lake na tutaenda kulifanya kazi, muda siyo mrefu tutamletea majibu yaliyo sahihi.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda naona kabisa mnahitaji maswali ya nyongeza hapo, sasa ni zamu ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa.

Na.135

**Barabara ya Gulwe - Berege - Igoji Kaskazini - Iwondo hadi  
Fufu kuwa chini ya TANROADS**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Barabara kutoka Gulwe - Berege - Chitemo- Mima- Sazima - Igoji Kaskazini - Iwondo - Fufu inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ni mbaya sana na inapitika kwa shida sana hasa wakati wa mvua/masika.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba ipo haja kubwa ya barabara hiyo kuhudumiwa na Serikali Kuu (*TANROADS*) badala ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ambayo uwezo wake kifedha ni mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, baba yangu na Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na kama ambavyo tumeongea kwamba maombi hayo yaanzie katika Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Dodoma na ninamhakikishia Mheshimiwa Lubeleje na kama ambavyo tumewasiliana maombi haya yatakapofika Wizarani tutayafikiria pamoja na maombi yale mengine yote na nina uhakika yatafika mahali pale ambapo yanatakiwa. Hayo yote ni kwa mujibu au matakwa ya Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 na Kanuni ya 43(1) ya Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009.

Aidha, ninatoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kuendelea kuifanya matengenezo ya aina mbalimbali barabara hii kwa kutumia fedha za

Mfuko wa Barabara zinazotengwa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ili iweze kupidika majira yote ya mwaka na kwa kweli tusiendelee kumpa kazi kubwa Mheshimiwa Lubeleje ya kuja Wizarani kwetu kama ambavyo anaifanya ili tuweze kuikamilisha hii barabara iweze kupidika na kusiwe tena na malalamiko makubwa kama yalivyo kwa sasa, kwa mujibu wa Mheshimiwa Lubeleje kadri anavyoyaleta Wizarani kwetu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, nimeleta maombi yangu Wizarani kwa sababu Halmashauri ya Wilaya haina uwezo wa kukarabati barabara hii ya Gulwe - Berege - Chitemo - Mima - Sazima - Igoji Kaskazini - Fufu na Iwondo, sasa hivi haipitiki wananchi wanapata taabu hasa abiria kufika Makao Makuu ya Wilaya na ndiyo maana nimeleta. Tayari tulikuwa na kikao cha Bodi ya Barabara tarehe 29 mwezi wa Februari nilipeleka ombi hili. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri muifikirie barabara hii kuipandisha hadhi ili TANROADS waweze kuitengeneza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya kutoka Mbande - Kongwa kwa Mheshimiwa Spika, Mpwapwa na Kibakwe kwa Mheshimiwa Simbachawene Waziri wa TAMISEMI, hii barabara imeahidiwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami na ahadi hiyo ni ahadi ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Kikwete mwaka juzi na mwaka jana wakati wa kampeni za CCM Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu aliahidi kuitengeneza barabara hii ya Mbande - Kongwa - Mpwapwa mpaka Kibakwe kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Waziri huoni kwamba kuna umuhimu wa kutengeneza barabara hii ambayo ni kiungo kikubwa cha Majimbo matatu Kongwa, Mpwapwa na Kibakwe? (Makof)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya Mheshimiwa Lubeleje kumbuka na Mheshimiwa Simbachawene anakusikiliza kwa makini sana hapo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, barabara hii kama ambavyo tumejibu hapo nyuma kwamba Serikali imedhamiria kuijenga na imeanza kuijenga na itaikamilisha mapema kwa kiwango cha lami kutokea Mbande - Kongwa - Mpwapwa hadi Kibakwe kama ambavyo Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na Mheshimiwa Simbachawene walivyokuwa wakitusukuma katika kuhakikisha hii barabara inakamilika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ninawahakikisha mtapata majibu mazuri zaidi wakati wa bajeti kuhakikisha kwamba ninachokisema hapa na kwa kweli hatutarajii kitu ambacho Mheshimiwa Lubeleje mnafahamu ni mtu wa siku nyingi sana

na hatungependa aendelee kufika mara zote ofisini kwetu kufuatilia barabara hii mara kwa mara ni lazima tuifikishe mwisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Gulwe - Berege - Mima hadi Fufu pamoja na nilivyojibu katika jibu langu la msingi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lubeleje kwamba Mfuko wa Barabara utaangalia kwa makini na hasa kwa kuzingatia kwamba mwaka huu mvua imekuwa nyingi sana na zimeharibu barabara nyingi sana uwezo wa Halmashauri wa kuzirudisha hizi barabara ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, tutaomba Mfuko wa Barabara na TANROADS wajaribu kusaidia maeneo mbalimbali katika kurudisha mawasiliano katika barabara zote zilizokatika nchini ikiwa ni pamoja na hii ya Gulwe - Berege - Mima hadi Fufu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe.

Na. 136

#### **Tatizo la Makazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi**

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING** aliuliza:-

Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la makazi kwa askari wa Jeshi la Polisi na Mheshimiwa Rais aligusia azma hiyo alipokuwa akilihutubia Bunge hili la Kumi na Moja kwenye kikao cha ufunguzi.

Je, Serikali imepanga kujenga mikoa mingapi majengo hayo ikiwemo Zanzibar?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ninamuona Mheshimiwa Engineer Hamad Yussuf Masauni, Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge wa Jang'ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuchukua hatua za makusudi kukabiliana na uhaba wa nyumba za Jeshi la Polisi. Kwa kutumia mifuko ya Hifadhi ya Jamii, chini ya mpango wa mikopo wenye riba nafuu Serikali imeshajenga nyumba 360 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inakusudia kujenga nyumba nyingine 4,136 katika mikoa 17 ya Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, Serikali itaendelea kutatua changamoto za uhaba wa nyumba za askari kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo mikopo yenye riba nafuu, Miradi Shirikishi (PPP) na kwa kutumia fedha za bajeti ya Serikali kadri hali ya uchumi itakavyokuwa ikiimarika.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu utakwenda sambamba na Mipango ya Maendeleo ya Serikali ukilenga kufikia idadi ya nyumba za makazi kwa askari wote waliopo sasa na watakaotarajiriwa kuajiriwa baadaye.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuimarisha ulinzi na usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika majengo hayo ambayo yamejengwa 360 kwa misimu hiyo iliyopita ni jengo moja ninalolikumbuka mimi ambalo lipo pale Mkao wa Mjini - Ziwan Polisi kwenye Jimbo langu. Pia Serikali imejenga jengo lingine kwa upande wa Zanzibar kule Pemba, haya majengo ukitazama ki-percentage ni madogo zaidi. Lakini mimi sina uhakika na taarifa hizi za 360; sasa namuuliza Mheshimiwa Waziri katika 360 ni majengo mangapi yalijengwa kule Zanzibar na katika haya 4,130 mangapi yanatarajia yatajengwa kule Zanzibar? Hilo swalii la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili Serikali iliji-commit katika mwaka 2011, Juni kwamba kwa kupitia bajeti wa mwaka ule ingelifanya ukarabati majengo ya Ziwan Polisi, lakini pia wangelijenga na uzio na mpaka hivi sasa ninavyozungumza kwamba askari wanajitegemea wenyewe kufanya ukarabati katika nyumba ambazo wanaishi.

Je, Waziri atanihakikishia ni lini Serikali itakuja kufanya ukarabati wa majengo yale ya Ziwan Polisi pamoja na kujenga uzio? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jang'ombe kwa ushirikiano wake mzuri sana ambao anatupa kwani ameshiriki katika ujenzi wa Kituo cha Afya pale Ziwan pamoja na uchimbaji wa kisima cha maji. Tunampongeza sana na tunamuahidi ushirikiano zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maswali yake mawili, ni kwamba mradi wa nyumba 4,136 ambazo tunatarajia tujenge ni nyumba 200 ambazo zinatarajia kujengwa Unguja na nyumba 150 zinatarajia kujengwa Pemba, kwa hiyo ukifanya jumla ya idadi ya nyumba zote 350. Pia ameuliza kuhusiana

na zile nyumba ambazo zilijengwa kupitia mradi wa NSSF. Ni kwamba nyumba zilizojengwa ni kweli maghorofa yale yalikuwa ni mawili kwa maana ya Unguja na Pemba lakini yana uwezo wa kukaa familia 12 kila moja kwa hiyo kufanya jumla ya familia 24.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la ukarabati wa nyumba za Ziwani ni kweli nyumba zile ni chakavu lakini kama ambavyo tunazungumza siku zote kwamba, nyumba hizi za Polisi nyingi ni chakavu. Ndiyo maana tuna mchakato wa kuweza kurekebisha nyumba hizi pamoja na kujenga mpya. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tunafahamu gharama za ujenzi wa nyumba hizo, ukarabati huo ambaa unakadirwa kufika takribani shilingi milioni 400; kwa hiyo tutajitahidi kwamba pale fedha itakapopatikana tuweze kuanza hiyo kazi haraka itakapowezekana.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu umuhimu wa nyumba za Ziwani, ikiwa ni Makao Makuu ya Jeshi la Polisi na chimbuko la historia hata Mapinduzi ya Zanzibar yalianzia pale.

**MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kuniona kwa sababu ni mgeni ndiyo maana jina langu hukunitaja naitwa Raisa Abdallah Mussa, Viti Maalum kutoka Zanzibar CUF. Napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Waziri katika vituo vidogo vya polisi vilivyoko Zanzibar, kuna baadhi ya vituo vimehamwa na nikutajie kwamba kituo cha Kidongo Chekundu *Mentally Hospital*, pale ni kituo muhimu sana kwa maeneo yale ya Kidongo Chekundu na Sogea, sasa hivi kile kituo kimehamwa na pamekuwa hasa kama gofu mpaka pamfanywa vijana wamekaa maskani yao pale pembedi yake.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka uniambie una mpango gani na kukihiisha kituo kile cha Polisi cha Kidongo Chekundu? Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna baadhi ya vituo vya polisi ambavyo kidogo havifanyi kazi ikiwemo kituo hicho ambacho nilizungumza Mheshimiwa Mbunge, lakini pia kuna kituo cha Vuga na Shaurimoyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna sababu mbalimbali ambazo zinasababisha vituo hivi kwa muda visiweze kufanyakazi. Vingine ni kwamba mahitaji ya vituo katika maeneo hayo yanakosekana umuhimu kulingana na changamoto za

uhalifu na ukaribu wa vituo vingine vikubwa vya polisi vilivyopo maeneo hayo. Hata hivyo, kutokana vilevile na uhaba wa idadi ya askari waliopo tunashindwa kufungua vituo vyote katika maeneo yote ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwamba, kituo cha Kidongo Chekundu ni moja kati ya vituo hivyo, hata hivyo nimuhakikishie Mbunge pamoja na wananchi wanaosikiliza kwamba Serikali haijakitupa kituo hicho, pale ambapo mahitaji yatakapoonekana ya muhimu tutakifanyia ukarabati na kuweza kikitumia kwa haraka sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunahama, tuhamie Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa swali linaulizwa na Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini.

Na. 137

### **Unyanyasaji Unaofanywa na Askari wa JWTZ kwa Wavuvi Nchini**

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED** aliuliza:-

Kumekuwa na unyanyasaji mkubwa unaofanywa na JWTZ wa kuwanyang'anya wavuvi samaki wao licha ya kwamba watu hao wanajitafutia kipato kupitia bahari kama Watanzania.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa unyanyasaji huo unaofanywa na Jeshi la Wananchi kwa wananchi wake?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa haijawahi kupokea tuhuma yoyote inayohusu unyanyasaji unaofanywa na askari wa JWTZ kwa wavuvi nchini. Aidha, kama tuhuma hizi zina ushahidi ni bora zikafikishwa sehemu husika ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, wanajeshi kama walivyo raia wote wanapaswa kuheshimu sheria za nchi na pale wanapokwenda kinyume huchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria na kanuni za jeshi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed unaleta tuhuma ambazo hazina ushahidi mzee!

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini pia sikuridhika sana na majibu yake ambayo ameyatoa ya kubahatisha zaidi. Tunao ushahidi wa kutosha kabisa mpaka wahanga walipigwa na kunyang'anywa samaki wao wavuvi na JW (Jeshi la Wananchi) sasa sijui Mheshimiwa Waziri na kisingizio hapa ni license zinazotumika wanadai kwamba sizo.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu la kwanza katika swali la nyongeza ni aina gani ya license zinazotakiwa kutumika na wavuvi hawa?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana na mimi tukamuonesha wale wahanga ambaeo walipigwa na wakati mwingine walinyang'anywa samaki wao, matendo haya yanafanyaika zaidi katika bahari ya Kigamboni na Kunduchi? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuwaona hao ambaeo inasemekana ni wahanga wa kipigo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nirudie yale niliyoyasema kwenye jibu langu la msingi kwamba kwa kuwa nchi hii inafata utawala wa sheria ni vema basi Mheshimiwa Mbunge anapopata tuhuma kama hizo akazifikisha sehemu husika.

Mheshimiwa Spika, siyo vema suala kama hili tulisikie mara ya kwanza ndani ya Bunge, sisi tupo, ofisi zetu zipo, Mheshimiwa Mbunge alipaswa kutufikishia ili tufanye uchunguzi na pale inapothibitika tuchukue hatua stahili, ningependa tuende kwa mwendo huo zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni aina gani za leseni niseme tu kwamba hili ni suala ambalo liko chini ya Wizara inayohusika na masuala ya uvuvi. Wanajeshi wanajukumu moja la kuhakikisha kwamba wavuvi hawatumii njia za uvuvi wa haramu basi, siyo suala la kuangalia leseni, leseni ina mamlaka zake.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tunachoweza kusema hapa ni kwamba yanapotokea matukio kama haya toa taarifa ili tufanye uchunguzi na kuchukua hatua zinazostahili. (Makofii)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata leo ni siku ya Wizara ya Ulinzi, kwa hiyo kama mna hoja zenu Waheshimiwa mtapata fursa ya kutosha ya kufikisha ujumbe wenu kwa Wizara.

Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 138

### **Kutenga Maeneo ya Kilimo na Mifugo**

**MHE. GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Wakazi wengi wa Mkoa wa Simiyu huendesha maisha yao kwa kutegemea kilimo na ufugaji, ambapo Mkoa huo umepakana na maeneo makubwa na mazuri kwa kazi hizo jirani na Mbuga ya Serengeti:-

(a) Je, Serikali itatenga lini maeneo ya kilimo na mifugo kwenye vijiji vinavyopakana na Mbunga ya Serengeti?

(b) Je, Serikali itathamini lini mifugo na mazao ya wakulima hawa kama vile inavyothamini wanyamapori wa mbugani kwani huonekana ni halali kwa wanyama pori kuua/kuharibu mazao ya wananchi wakati siyo halali wananchi kuingiza mifugo au kuchimba hata mizizi ndani ya mbuga ya wanyama?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi na kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zenye vijiji vinavyopakana na mbuga ya Serengeti imeshachukua hatua za kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji vinavyohusika. Tayari vijiji 73 katika Wilaya za Serengeti, Tarime, Bunda na Bariadi vimeshakamilisha mipango hiyo, kinachotakiwa sasa ni kwa Halmashauri hizo kuhakikisha kwamba vijiji ambavyo tayari vina mipango ya matumizi bora ya ardhi vinaitekeleza ipasavyo na kuimarisha usimamizi. Naomba Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na Halmashauri husika ili vijiji visivyokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi navyo viweze kuwa nayo ili faida za mipango hiyo ziwafikiwe wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inathamini mifugo na mazao ya wakulima na imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuepusha migogoro kati ya binadamu na wanyama pori na pia kuhakikisha kwamba maisha ya binadamu na mali zao yanalindwa kikamilifu. Hii inadhihirishwa na jinsi Serikali inavyosaidia vijiji kuwa na miradi ya ujirani mwema kwa vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi na vijiji hivyo kuwa na mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi.

Aidha, kwa kutambua umuhimu wa maisha ya binadamu, mazao na mifugo Serikali imeweka utaratibu wa kuchukua hatua za haraka za kufukuza wanyama pori mara inapotokea wameingia katika makazi na mashamba ya wananchi na wakati mwiningine inapobidi Serikali hutoa kifuta machozi au kifuta jasho kwa waathirika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi swali la nyongeza.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Pamoja na majibu ya Waziri katika majibu yake ya msingi amekiri kwamba Serikali inachukua hatua kuhakikisha kwamba wanatatua migogoro inayohusiana na wafugaji na hifadhi.

Sasa swali, Waziri utakuwa tayari kuongozana na mimi kuelekea Mkoani Simiyu kwenda kutatua migogoro inayoendelea katika vijiji vyta Nyantugutu, Lumi na Longalombogo kwenda kutatua migogoro hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hilo mpaka Spika atoe ruhusa! Mheshimiwa Mbunge, endelea na swali la pili. (Kicheko)

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Spika, swali la pili wananchi wa Wilaya ya Meatu na Wilaya ya Maswa wengi wao hawana maeneo ya kuchungia mifugo yao. Je, Serikali itakuwa tayari kurudisha Pori la Akiba la Maswa ili wananchi hawa waweze kutumia kama malisho, kwa sababu pori hilo limekosa sifa ya kuwa Hifadhi ya Taifa? (Makofii)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu kama nitakuwa tayari kuandamana na yeye ndani ya Bunge hili kwenda kutatua migogoro, nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba labda baada ya kikao cha leo tukutane nimshauri zaidi namna ya kutatua hili kwa sababu itabidi aongee na watu wa maliasili kwa sababu Wizara yetu hasa haihusiki na migogoro kati ya hifadhi na wananchi lakini nitamshauri namna ya kufanya hivyo na nitamshauri vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Pori la Akiba la Maswa kutolewa kwa ajili ya wafugaji nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba mimi ni jirani yake, mimi natoka Ngorongoro nafahamu changamoto iliyopo kati ya wafugaji na pori la Maswa.

Mheshimiwa Spika, kuna mkakati ambao unaendelea sasa Serikalini kama ulivyosikia wiki iliyopita Waziri Mkuu alivyozungumza wa kuangalia namna ya kuondoa migogoro hii, vilevile kuangalia namna ya kutafuta ardhi kwa ajili ya

wafugaji ikiwa ni pamoja na kutafuta uwezekano wa baadhi ya maeneo ambayo yamepoteza hadhi ya kihifadhi ili wafugaji waweze kugaiwa.

Mheshimiwa Spika, hili linaendelea siwezi kusema moja kwa moja sasa kwamba, Pori la Maswa ni moja kati ya haya maeneo lakini kuna mipango ya kujadili suala kama hilo. Nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na migogoro hii kuongezeka lakini bado kama Taifa tuna jukumu la kuhifadhi wanyama, tunafahamu kwamba ni rasilimali muhimu, tusipohifadhi baada ya muda inawezekana tusiwe na wanyama pori ambao wanaendelea kuletea nchi yetu fedha za kigeni lakini vilevile sifa. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Maghembe upo tayari ku-de-gazette Maswa Game Reserve?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mawazo kuhusu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama mtakuwa mmeangalia takwimu za sensa ya mwaka 2012 mtaona kabisa katika ile Sensa ya Watu na Makazi kwamba eneo la asilimia 10 la surface area ya Tanzania Bara limetengwa kwa ajili ya mifugo, eneo hilo bado halitumiki ipasavyo. Niseme tu kwa sababu muda mwenyewe ni mfupi kwamba Serikali haina mpango wa kuhuisha maeneo ya hifadhi kuwa maeneo ya kuchunga. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nataka pia niseme kwamba wote kabla hatujawa Wabunge hapa baada ya kushinda uchaguzi tulipa kiapo cha uaminifu cha kulinda, kuihifadhi na kuitunza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sehemu ya 27 ya Katiba hiyo inasema; kila mtu anao wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Chenge, swali la nyongeza!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali napenda tu nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba katika vile vijiji 73 ambavyo vimeshaandaa Mpango Shirikishi wa Matumizi Bora ya Ardhi, ni vijiji vingapi viro katika Wilaya ya Bariadi. Ahsante.

**SPIKA:** Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa vijiji vilivyoulizwa kwenye swalii msingi baadhi yake mimi nilishafika akiwa amenipeleka Mheshimiwa Njalu enzi zile nimeenda na helicopter wakati wa kampeni na nikapokea kile kilio cha wananchi wake, nilipanga kwamba nitafika katika eneo hilo baada ya bajeti kwa ajili ya kujionea hali hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tukirudi kwenye swalii hili alilolisemea Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge linalohitaji idadi ya vijiji, suala hili la migogoro limekuwa endelevu kutokana na kupanuka kwa idadi ya mifugo pamoja na ongezeko la wanadamu na mahitaji ya matumizi ya ardhii, kwa hiyo, kila wakati panapokuwa pamepimwa, panakuwa pana uhitaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea tayari zaidi ya vijiji 23 vilishafanya upimaji huo lakini mahitaji ni makubwa kuliko idadi hiyo ya vijiji na nitawaomba Wabunge wanaotoka maeneo ya wafugaji waungane na viongozi wa wafugaji ambaa tumewaomba watuorodheshee mapendekezo ya maeneo yanayoweza kutatua matatizo haya, lakini pia na maeneo ambayo yana migogoro ili Serikali tuweze kupitia mgogoro mmoja baada ya mwingine ili tuweze kupata majibu ya kudumu kwa ajili ya watu wetu wanaogombana katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tumelipanga kati ya Ijumaa na Jumatatu tutakuwa tumeshapata taarifa hiyo na Waheshimiwa Wabunge wote mnaotoka maeneo ya aina hiyo mtatangaziwa ili tuweze kukaa pamoja. Jambo hili linahitaji ushirikiano wa pamoja na uamuzi wa pamoja katika kupata majawabu ya kudumu na kuondokana na tatizo hili.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda tuvumiliane Waheshimiwa Wabunge naona muda wangu umeisha kabisa tulitendee haki swalii la mwisho kwa siku ya leo nalo ni la Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo swalii la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani.

Na. 139

### **Shirikisho la Mpira Tanzania Kujisajili FIFA**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y. MHE. HAFIDH ALI TAHIR)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la 2005 – 2010 kulitokea hoja ya TFF kujunga katika Shirikisho la Mpira la Kimataifa (FIFA) bila ridhaa ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; hoja hiyo ilipelekea aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda kuunda Kamati Maalum yenyewe Wajumbe kutoka ZFA na TFF ili kuondoa utata huo:-

(a) Je, ni nini matokeo ya Kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutopatikana muafaka au uamuzi uliofikiwa kwa pamoja ni kuchelewesha agizo la Waziri Mkuu?

(c) Je, Serikali inasemaje kuhusu ubabaishaji unaofanywa na TFF?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwamoto ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Hafidh. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye karatasi yenu pale imeandikwa Wasanii, hii Wizara inaitwa ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo siyo kama ilivyoadikwa hapo. (Makofi)

#### **WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatia majadiliano na vikao kadhaa vilivyoandikwa katika kipindi cha mwaka 2005/2010 kumbukumbu zinaonyesha kwamba suala zima la uanachama wa TFF na ZFA lilifanyiwa kazi kwa ukamilifu na Serikali za pande zote mbili kwa ushirikiano na vyama vyote viwili.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa ZFA kupata uanachama wa FIFA, mwaka 2010 Ujumbe wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ukiongozwa na aliyekuwa Naibu Waziri Kiongozi Mheshimiwa Juma Shamhuna pamoja na aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Mheshimiwa Joel Bendera walikwenda Zurich-Switzerland ambako walikutana na Rais wa FIFA wa wakati huo. Aidha, katika msafara huo walifuatana na viongozi wa TFF na ZFA. Madhumuni ya safari hiyo ilikuwa ni kuwasilisha maombi ya ZFA kupewa uanachama wa FIFA.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni 2011, FIFA iliiandikia ZFA ikiwajulisha kuwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo isingwezekana Zanzibar kupata uanachama wa FIFA kwa kuwa uanachama wao ni nchi zinazotambuliwa na Jumuiya ya Kimataifa kama ilivyoelezwa katika aya ya 10 ya Katiba hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, ni dhahiri kuwa suala la usajili wa TFF na ZFA linafahamika vyema ndani ya Serikali ya Mapinduzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa uanachama wa TFF katika FIFA upo kwa mujibu wa muafaka wa pande zote mbili.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utaratibu huo wa FIFA kuhusu suala hilo, Wizara yangu imewaelekeza TFF na wako tayari kufanya maridhiano na ZFA ili kukamilisha utaratibu wa wazi wa kukidhi mahitaji ya Zanzibar kushiriki katika masuala ya FIFA kuititia TFF bila kuathiri ushiriki wa klubu za Zanzibar katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Barani Afrika yaani CAF.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri. Niulize maswali yangu mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kilichopelekea kuunda Tume hii mpaka kwenda Zurich ilikuwa ni swali ambalo liliulizwa hapa ndani na Mheshimiwa Hafidh Ali na imekuwaje Serikali imeshindwa kutoa jibu mapema mpaka leo baada ya kuuliza swali ndiyo majibu yamekuja?

Swali la pili, kwa kuwa kutotambuliwa kwa ZFA na FIFA kutapelekea bado kuwa na timu ya Taifa moja na kwa kuwa TFF na ZFA zinaposhiriki Kimataifa zinapata tatizo la ukosefu wa fedha na hivyo kupelekea timu zetu za Taifa kufanya vibaya, je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka kuzichukua timu za Taifa wakati zinaposhiriki kwenye mashindano ya Kimataifa ili tusiendelee kuwa kichwa cha mwendawazimu? (Makofij)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri Nape Mosses Nauye.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwamoto kwa mchango wake mkubwa kwa michezo ya nchi yetu, hasa kwa michezo ya hapa Bungeni kila asubuhi namkuta uwanjani anafanya kazi nzuri, namshukuru sana.

(a) Ni kweli kwamba suala hili la mvutano kati ya ZFA na TFF limechukua muda mrefu sana. Limekuwa likijadiliwa kwa muda mrefu pamoja na magizo ya Serikali kwamba jambo hili liwe limemalizika, moja ya sababu pamekuwa na mivutano na tumeshuhudia mivutano mikubwa kwenye ZFA kwa maana ya uongozi, lakini juzi wamefanya uchaguzi na tunaamini sasa hali ya ZFA imetulia na Serikali tutaweka juhudzi za kutosha kuhakikisha kwamba ZFA na TFF wanakaa chini na kusaini makubaliano. Lakini sababu ya pili, walipokaa mara ya kwanza wakatengeneza makubaliano, upande mmoja wa pande hizi mbili ulisita kusaini hayo makubaliano mpaka leo. Kwa hiyo, tutakachofanya tutaweka nguvu kuhakikisha pande hizi mbili zinakuja pamoja, zinasaini makubaliano na utekelezaji wa makubaliano yale unaanza kutekelezwa.

(b) Sehemu ya pili ya swali lake ameuliza kama Serikali sasa iko tayari kufadhili timu ya Taifa. Kwa kweli nchi yetu ina michezo mingi na haiwezekani Serikali ikatenga pesa kwa ajili ya michezo yote. Tunachofanya ni kuvizwesha vyama vya michezo nchini kwanza viwe na vyanzo vya mapato vya kutosha kufadhili na kuendesha michezo, lakini pia kuhamasisha sekta binafsi na wafadhili wengine wawewe kusaidia kazi hii ya kufadhili michezo nchini na wako ambao wamekuwa wakifanya vizuri, ndiyo mana ligi zetu nyingi zinakwenda vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tukubaliane muda hauko upande wetu. Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye kwa majibu mazuri. Sasa tuendelee na mpangilio wa shughuli ulivyo, ni wakati wa wageni sasa.

Tunaanza na wageni 14 wa Mheshimiwa Waziri Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ambao ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Ndugu Job David Masima, Katibu Mkuu karibu sana. Naibu Katibu Mkuu Ndugu Immaculata Ngwale, Karibu sana.

Pia Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis Mwamunyange. (Makofi)

Makofi hayo Mheshimiwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ni appreciation ya kazi yako na Jeshi zima la JWTZ. (Makofi)

Lakini pia yuko Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Jenerali Venance Mabeyo, huyu ni *Leftman General*. Yupo pia Mkuu wa Mipango na Maendeleo Jeshini, Meja Jenerali Simon Mumwi, yupo Mkuu wa Utumishi Jeshini Meja Jenerali Harrison Masebo, Mkuu wa Jeshi la Nchi Kavu Meja Jenerali James Mwakibolwa, Mkuu wa Jeshi la Wanamaji (*Rear Admiral*)Rogastian Laswai, Mkuu wa JKT Brigedia Jenerali Michael Isamuhyo na Mkuu wa Jeshi la Anga Brigedia Jenerali George Ingram. (Makofi)

Pia wapo Wakuu wa Mashirika na Wakuu wa Matawi Jeshini, wapo Wakuu wa Idara na vitengo vyote, wako Makanali wote, wako viongozi wa Chama cha Wafanyakazi (*TUGHE*) kutoka Wizarani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge leo Jeshi liko hapa. Wale ambao huwa mnianisumbua sumbuu mjue kabisa leo nimekaa vizuri. Leo niko kisawa sawa leo. (Kicheko/Makofi)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, wapo wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni wanafunzi 40 kutoka shule ya msingi wanaofadhiliwa kimasomo na Shirika linaloitwa Compassion la kutoka Kanisa la EAGT Kongwa ambao wanaongozwa na walimu 10 na Kiongozi wao ni Diwani wa Viti Maalum Kongwa Mjini Mheshimiwa Monica Nyabu, naomba pale mlipo msimame wote, karibuni sana wanafunzi na walimu kutoka kule Kongwa mijifunze namna

Bunge linavyofanya kazi, ile barabara yenu mbaya sana mliyopita ile ya kutoka Kongwa hadi Mbande ndiyo hiyo mmemsikia Waziri anasema tarehe 16/17 Mei ataitolea maelezo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ambaao ni wana kikundi 15 kutoka Chama cha Watuma Salamu mionganii mwao wa kutuma salamu redioni kutoka Kongwa almaarufu wanaajiita Wasakatonge wakiongozwa na Stanley Machaka. Wasakatonge pale mlipo msimame, karibuni sana Bungeni, karibuni sana.(Makofi)

Wapo wageni watatu kutoka Tanzania Parliamentarian Friends of Environment and Conservation (TAPAFE) ambaao ni Mheshimiwa Mbunge tuliyekuwa naye hapa kwa kadri ya miaka 15 akiwa mionganii mwetu Mheshimiwa Abdulkarim Shah, aliyekuwa Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa karibu sana. Ndugu Christopher Camponovo, karibu pale ulipo na Ndugu Hitesh Divecha, karibuni sana.(Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni kama wafuatao; wageni kumi wa Mheshimiwa Jesnista Mhagama Mbunge kutoka Jimboni kwake Peramiho, wakiongozwa na Mchungaji Rose Amani, ahsanteni sana wageni wetu kutoka Peramiho, Mheshimiwa Jenista Mhagama yupo amejaajaa tele, anafanya kazi zake kama kawaida. (Makofi)

Wageni 44 wa Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ambaao ni wanachuo wanaotoka Ukerewe wanaosoma UDOM, wale wanafunzi wa UDOM kutoka Ukerewe 44 wale naona hawaonekani hawa watu wa UK hawa!

Pia kuna wageni 14 wa Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha kutoka Jimboni kwake Serengeti, wale wa Ikoma na nini kutoka Serengeti kule wako wapi? Wameingia mitini? Gallery limejaa kweli. (Makofi)

Wageni 3 wa Mheshimiwa Anne Lupembe ambaao ni Viongozi wa UWT kutoka Mkoa wa Katavi wakiongozwa na Katibu wa Mkoa wa UWT Ndugu Getruda Kaminda, karibuni sana.

Pia kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Susan Maselle ambaao ni vijana wajasiriamali kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jackline Kyabwazi, karibuni sana popote pale mlipo. (Makofi)

Mgeni wa Balozi Dkt. Deodorus Kamala ambaye ni Ndugu Fredrick Kitone, mtaalam wa usindikaji wa mazao ya kilimo Misenyi, Bukoba na Karagwe, Chama cha Maendeleo ya Wakulima, karibu sana.

Kuna wanafunzi 40 na walimu wawili kutoka shule ya sekondari ya Kigwe iliyoko Dodoma, karibuni wanafunzi wa Kigwe, karibuni sana. Waswahili mnapaita Kigwe wenye wa Mkoa wa Dodoma tunapaita Chigwe, kwa sababu watu wa Dodoma hawana neno "ki" popote pale, wao badala ya "ki" wanatumia neno "chi". (Makofii)

Wageni 21 wa Mheshimiwa Deogratius Ngalawa amba ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma UDOM. Wageni 21 kutoka UDOM wa Mheshimiwa Ngalawa, karibuni kokote kule mliko. Lakini pia kuna wanafuzi 23 na walimu wawili kutoka shule ya msingi ya *Living Life* ya Dodoma, *Living Life*, karibuni sana sana, mnapendeza kweli, karibuni sana *Living Life*. Waheshimiwa wabunge leo tuko na wageni wengi kweli kweli inatia moyo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu matangazo ya kazi; naomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Uongozi kuwa leo kutakuwa na Kikao Maalum cha Kamati ya Uongozi kitakachofanyika kuanzia saa 8.00 mchana kwenye Ukumbi wa Spika, ghorofa ya kwanza. Aidha, Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge mnaombwa kuhudhuria kikao hicho. Kwa hiyo, naomba Wenyeviti wote na Makamu Wenyeviti wote saa nane kamili juu ya alama tuanze hicho kikao.

Mheshimiwa Margaret Sitta, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG) anawaomba niwatangazieni Wabunge Wanawake wote kuwa leo tarehe 10 Mei, kutakuwa na semina ya Wabunge Wanawake wote itakayofanyika katika ukumbi mkuu wa Msekwa mara baada ya kuahirishwa Kikao cha Bunge hili mchana wa leo.

Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo anaomba Wajumbe wa Kamati yake ya Sheria Ndogo mkutane katika Ukumbi Na 229 Jengo la Utawala.

Tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge waumini wa makanisa ya Protestant CCT mnaombwa Waheshimiwa wote waumini wa CCT kuhudhuria ibada katika jengo la Pius Msekwa leo siku ya jumanne tarehe 10 Mei saa saba mchana mara baada ya kuahirishwa kwa Bunge. Wabunge wa makanisa ya CCT mnaombwa kuhudhuria misa ukumbi wa Msekwa baada ya saa saba mchana kuahirishwa shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:**  
**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha  
2016/2017 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHE. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB) KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA WIZARA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma kwa kulijalia Taifa letu na wananchi wake wote kwa kutuvusha salama katika mchakato wote wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2015. Watanzania tunayo kila sababu ya kujivunia kuwa Uchaguzi Mkuu huo ambao kikalenda ni wa tano tangu kurejeshwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992 uliendeshwa na kuhitimishwa kwa amani, utulivu na mshikamano mkubwa kinyume na maadui wetu wa ndani na nje ya nchi waliotutabiria mabaya.

Kwa muktadha huo, nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendeleza misingi ya umoja, mshikamano na amani wa nchi yetu.

Aidha, nawapongeza aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kusimamia utekelezaji mzuri wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010/2015. Pia nawapongeza Mheshimiwa Anne Makinda, Spika Mstaafu, akisaidiana na Mheshimiwa Job Ndugai na Wenyeviti wetu kwa kuliongoza Bunge la Kumi kwa hekima, busara na mafanikio makubwa. (Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia, kuwapongeza viongozi wa Kitaifa kwa kuchaguliwa

kwenye nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Kipekee nawapongeza kwa dhati kabisa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na CCM kupeperusha bendera ya chama na hatimaye kuchaguliwa kwa kura nyngi kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, kwa kuteuliwa na Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa ushindi uliouopata katika Jimbo la Kongwa na kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili la 11. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nachukua fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa ushindi kwenye Majimbo yao na kuchaguliwa katika nyadhifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza Wabunge wenzangu tuliochaguliwa katika majimbo yetu, waliochaguliwa kupitia Viti Maalum, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kuunda Bunge lako hili Tukufu la Kumi na Moja. Aidha, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali chini ya falsafa makini ya Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kunitfea kuiongoza tena Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ni dhahiri kuwa heshima na dhamana niliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa na adhimu. Hivyo, nachukua fursa hii kumhakikisha Mheshimiwa Rais, Makamu wake, Waziri Mkuu, Chama changu cha Mapinduzi na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi niliyopewa kwa uwezo wangu wote, akili zangu zote na nguvu zangu zote. Namuomba Mwenyezi Mungu aniongoze na kunisaidia.

Aidha, napenda kuwashukuru wapiga kura na wananchi wote wa Jimbo langu la uchaguzi la Kwahani, kwa imani waliyonayo juu yangu kwa kunichagua kwa mara ya tatu kuendelea kuwa Mbunge wao katika kipindi kingine cha miaka mitano. Imani hiyo kwangu imemwezesha Mheshimiwa Rais wetu kunitfea katika nafasi hii. Nawashukuru sana. Ahadi yangu kwao na wananchi wote ni kuendelea kufanya kazi kwa moyo na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwezesha uchaguzi wa marudio wa Zanzibar uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016 kukamilika kwa amani na utulivu. Hivyo, natumia fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar

katika kipindi kingine cha miaka mitano. Vilevile nampongeza Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti. Naomba kuwapongeza pia wajumbe wote wa Kamati hii. Naahidi kushirikiana nao kwa dhati katika kutekeleza majukumu inayoyasimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kuwasilisha hotuba yangu ambayo kiujumla inahusu maeneo makuu yafuatayo:-

- (i) Malengo na majukumu ya Wizara;
- (ii) Utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama;
- (iii) Hali ya ulinzi na usalama nchini mwetu;
- (iv) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2015/16; na
- (v) Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, wajibu na majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kama tulivyokwisha kuitangaza dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwa taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa. Aidha, dhima ya Wizara ya Ulinzi na JKT ni kuilinda mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya maadui kutoka nje na ndani ya nchi na kuhakikisha kuwa uhuru na maslahi ya Taifa letu yanakuwa salama wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 hadi 2020 Ibara ya 146 (i), (ii), (iii), (iv) na (vi), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/2017 - 2020/2021), maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara inasimamia utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

- (i) Kuvizezesha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania likiwa ni mionganini mwa vyombo vya ulinzi na usalama, litaendelea kuandikisha vijana wenyewe sifa na ujuzi stahiki ili kufikia azma ya kuwa na Jeshi dogo lenye weledi, uwezo na zana bora za kisasa. Katika kufanya hivyo, utaratibu wa kuandikisha

vijana wa kuijunga na JWTZ utaendelea kuwa ni ule ule wa kuwapata kutoka kwenye Kambi za JKT. Kwa upande wa rasilimali fedha, Wizara itaendelea kutenga fedha za kutosha kuhudumia mahitaji ya Jeshi kutegemea na bajeti ya Serikali.

(ii) Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. Wizara itaendelea kuboresha maslahi ya Wanajeshi hususan mishahara, posho, makazi na vitendea kazi. Aidha, tutaendelea na ujenzi wa nyumba mpya za makazi ya wapiganaji na ofisi, pamoja na kutoa mafunzo na stahili mbalimbali kwa Maafisa na Askari.

(iii) Wizara yangu itaendelea kuliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kifedha, rasilimali watu na kuimarishe miundombinu ili kuweza kutoa mafunzo kwa vijana wote wa mujibu wa sheria na wa kujitolea kulingana na uwezo wa kifedha.

(iv) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaendelea kushiriki katika shughuli za operesheni za Kimataifa na Kikanda kama zitakavyokuwa chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi za Afrika au chini ya Jumuiya za Kikanda.

(v) Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, mamlaka za kiraia na mataifa mengine kupambana na matishio mapya ya kiusalama yakiwemo ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu, biashara haramu ya dawa za kulevyta na usafirishaji haramu wa binadamu.

(vi) Suala la ulinzi ni la Muungano. Hivyo, Wizara kwa kutumia vyombo vyake itaendelea na jukumu lake la kuhakikisha ulinzi na usalama wa mipaka yote ya nchi imeimarishwa ili kudumisha amani na utulivu kwa Taifa lote.

(vii) Wizara itaendelea kusimamia na kuimarishe taasisi na viwanda vyake katika shughuli za utafiti, uzalishaji na utoaji huduma za kihandisi kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia. Hivyo, uzalishaji wa mazao mapya kupitia viwanda vyetu utaimarishwa. Aidha, shughuli za ukarabati wa miundombinu, ununuza wa mashine na mitambo inayoendana na teknolojia za kisasa na malighafi za kutosha zitaendelezwa.

(viii) Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), litaendelea kutekeleza miradi ya kilimo, ufugaji na uvuvi kwa kuwahusisha vijana wakati wa mafunzo yao. Mafunzo haya yanahuisha pia shughuli za ujenzi. Wizara inafanya tathmini ya ushiriki wa JKT katika shughuli za kuzalisha na kusambaza mbegu ili ziwe na tija. Vivyo hivyo, tunatafakari ushiriki katika uuzaji wa matrekta kwani kasi ya ulipaji madeni na urejeshaji wa mikopo ni mdogo mno.

(ix) Kama nilivyoeleza hapo juu, Wizara yangu inaendelea kutekeleza kwa ukamilifu agizo la Mheshimiwa Rais kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuandikisha askari wapya kupitia vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT. Hivyo, natoa rai kwa vyombo vingine vya ulinzi na usalama kutekeleza agizo hilo. Sambamba na kupata ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama, JKT litaendelea kuwapatia vijana wanaojiunga na Jeshi hilo mafunzo ya ufundi stadi yanayowaongezea uwezo wa kupata ajira katika Taasisi nyingine za uzalishaji mali na kujiajiri. Aidha, JKT linatarajia kufungua kituo kikubwa cha VETA katika eneo la Kongwa-Dodoma ili kuendelea kutoa mafunzo kwa vijana waliojiunga na mafunzo ya JKT. Eneo la ekari 500 kwa ajili ya mafunzo hayo limepatikana na lipo kwenye hatua ya kufanyiwa tathmini na upimaji ili fidia iweze kulipwa na kuwezesha taratibu nyingine za ujenzi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majukumu; katika kutekeleza dira, dhima, ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja, Wizara itahakikisha kuwa uhuru na usalama wa nchi unalindwa na kusimamiwa, hivyo, majukumu yetu yatajikita katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine hasa nchi jirani na nchi rafiki kwa lengo la kudumisha amani na usalama;
- (ii) Kusaidia mamlaka za kiraia katika kuzuia uporaji wa rasilimali za Taifa, kukabiliana na athari za majanga inapobidi na kudhibiti vitendo vinavyoweza kuhatarisha amani na utulivu nchini;
- (iii) Kuandaa umma wa Watanzania katika mapambano dhidi ya adui kupitia mafunzo ya Jeshi la Akiba;
- (iv) Kutafiti, kuendeleza na kuzalisha teknolojia za kijeshi; na
- (v) Kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, umoja wa Kitaifa, usawa, nidhamu na ukakamavu na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundi kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuyatekeleza majukumu haya mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara itafanya shughuli zifuatazo:-

- (i) Kuendelea kuandikisha wanajeshi kwa kuzingatia sifa zinazohitajika ili kulijengea Jeshi uwezo kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa;
- (ii) Kuendelea kuwapatia wanajeshi zana, vifaa na vitendea kazi bora na vya kisasa;

(iii) Kusimamia matunzo na matumizi mazuri ya zana, vifaa na vitendea kazi vilivyopo;

(iv) Kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi ikiwa ni pamoja na shughuli za uendeshaji mafunzo ya ulinzi wa Jeshi la Akiba;

(v) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea vijana wa Kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, ujasiri, maadili mema na utaifa;

(vi) Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia za kijeshi na kuzalisha mali kuititia mashirika ya Mzinga na Nyumbu;

(vii) Kuwezesha uzalishaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kuwa wa tija na faida na hivyo kuchangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa;

(viii) Kushirikiana na mamlaka za kiraia pale inapobidi katika kukabiliana na majanga na dharura za Kitaifa;

(ix) Kuendeleza ujenzi wa makazi na miundombinu ili kuimarisha mazingira bora ya kuishi na kufanya kazi;

(x) Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine duniani katika masuala ya ulinzi wa amani;

(xi) Kuendelea na upimaji, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi; na

(xii) Kuendelea kuwapatia wanajeshi, vijana wa JKT na watumishi wa umma stahili zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tangu uteue Kamati za Kudumu za Bunge mapema mwaka huu Wizara imepokea ziara za wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kufanya nao ziara mbili pamoja na kufanya nao vikao vinne. Aidha, kilifanyika kikao kimoja cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Katika ziara na vikao hivyo Kamati zilitoa hoja na maelekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utendaji wa majukumu ya Wizara.

Hivyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hizi yamefanyiwa kazi na majibu yake yameainishwa katika Kiambatanisho Na.1 (a) na Na. 1(b).

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama; hali ya usalama wa mipaka. Hali ya ulinzi na usalama wa mipaka yetu na nchi jirani kwa jumla ni shwari. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutekeleza jukumu la ulinzi wa mipaka kwa weledi na hivyo kudhibiti ipasavyo mipaka yote ya Tanzania na kuhakikisha kuwa nchi yetu iko salama. Hata hivyo, migogoro na viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi jirani yamesababisha ongezeko la wakimbizi na wahalifu mbalimbali wanaoingia nchini wakiwemo wenye silaha za moto kinyume na sheria na kisha kuzitumia silaha hizo kutenda uhalifu.

Pia matukio ya uharibifu wa alama za mipakani kwenye baadhi ya maeneo ya mipaka ya nchi yetu havijapatiwa ufumbuzi. Mazungumzo kati ya Tanzania na nchi inazopakana nazo yanaendelea kupitia Wizara za Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Lengo ni kuhakikisha alama za mipaka zinajengwa na zile zilizoharibiwa zinarejeshwa ili mipaka yote iwe inaonekana kwa uwazi. Pamoja na hayo, hali ya mipaka yetu imekuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka wa Kaskazini; kwa upande wa Kaskazini kwa ujumla hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, vitendo vya uharibifu wa mawe ya mpakani yaani beacons na ujenzi holela unaofanywa na watu waishio mpakani vinaendelea. Aidha, matukio ya kujipatia ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, biashara na ujenzi wa makazi vimeendelea kuwa changamoto kubwa. Maeneo yaliyoathirika zaidi ni Jasini, Namanga, Holili na Horohoro. Juhudi za kujenga alama za mipakani zinaendelea. Aidha, katika maeneo ya Sirari na Tarime kwa upande wa Tanzania na Isebenia na Kurya kwa upande wa Kenya yameimarishwa kwa kujengwa alama za mipakani zilizobomolewa.

Mheshimiwa Spika, Mpaka wa Mashariki; Mpaka huu unahuishaa eneo la nchi yetu katika Bahari ya Hindi. Hali ya usalama katika mpaka huu imekuwa shwari. Hakuna matukio ya uharamia yaliyotokea na vikosi vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania vyenye jukumu la kuhakikisha usalama wa mpaka huu vimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Katika kipindi hiki Jeshi letu la Wanamaji limeongezewa nguvu kwa kupewa Meli Vita mpya zenyet uwezo wa kufanya doria katika bahari kuu. Vivyo hivyo, Jeshi kwa kushirikiana na mamlaka husika, limeendelea kuchukua hatua za kudhibiti uvuvi haramu na usafirishaji wa bidhaa haramu ili kulinda rasilimali na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Mpaka wa Magharibi; Changamoto kubwa inayokabili mpaka wetu wa Magharibi ni athari ya machafuko ya kisiasa yanayosababisha wimbi la wakimbizi kuingia nchini kwetu. Pia yamekuwepo matukio ya ujambazi kwa kutumia silaha maeneo mbalimbali katika Ziwa Tanganyika yanayoteklezwa na watu wenyewe silaha na vikundi vinavyohasimiana katika nchi hizo jirani. Pamoja na changamoto hii, Jeshi letu limejidhatiti kizana, kivifaa na kimikakati kukabiliana navyo.

Mheshimiwa Spika, Mpaka wa Kusini; hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, utata wa mpaka katika Ziwa Nyasa bado haujapatiwa suluhisho. Serikali yetu kuitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu. Pamoja na hali hiyo, wananchi wa pande zote wanaendelea na shughuli zao bila bughudha yoyote.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Hali tete ya usalama katika baadhi ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ni tishio kwa usalama wa nchi yetu hasa kutokana na machafuko ya kisiasa katika nchi hizo. Ukanda huu umekuwa katika tahadhari ya kiusalama dhidi ya mashambulizi ya kigaidi kutoka kundi la Al-Shabab. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na raia wema vitaendelea kuwa macho katika kufuatilia nyendo za makundi mbalimbali yanayodhaniwa kuhatarisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika nchi za Somalia na Jimbo la Darfur nchini Sudan imeendelea kuwa changamoto kwetu. Aidha, nchini Somalia mapambano yanaendelea baina ya majeshi ya AMISOM na kundi la kigaidi la Al-Shabab. Kwa upande wa eneo la Darfur mapigano baina ya vikosi vya Serikali na vikundi vya uasi yanaendelea. Nchini Sudan Kusini, kurejea kwa uhusiano kati ya Serikali inayoongozwa na Rais Salva Kiir na kikundi kinachomuunga mkono Dkt. Riek Machar, Makamu wa Rais yanatoa dalili njema za kufikia muafaka wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, ugaidi na uharamia; matukio ya ugaidi wa Kimataifa yameendelea kuwa tishio la usalama duniani. Kuwepo kwa makundi ya Al-Shabab, Al-Qaeda, Boko Haram, *Islamic State* kunafanya tishio la ugaidi kusambaa duniani. Hivyo tuna kila sababu ya kujizatiti na kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama. Taarifa za kuwepo kwa baadhi ya Watanzania wanaojiunga na makundi ya Al-Shabab na *IS* kunahatarisha usalama wa Tanzania, hasa ikizingatiwa kiujumla mwingiliano mkubwa uliopo kati ya wananchi wetu na watu wenyewe malengo tofauti. Hatari iliyopo ni uwezekano wa baadhi ya vijana waliojiunga na makundi haya ya kigaidi ya kimataifa kurejea nyumbani kwa malengo ya kutekeleza vitendo vya kigaidi nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita kumejitokeza viashiria vyenye mwelekeo wa kigaidi kama ifuatavyo:-

(i) Kuvamiwa kwa baadhi ya Vituo vya Polisi, kuporwa silaha na baadhi ya askari kuuawa na kundi ambalo nia yake haijafahamika;

(ii) Matukio yenye mwelekeo wa kigaidi kama vile yaliyotokea katika mapango ya Amboni Tanga na katika kitongoji cha Nyandeo, Tarafa ya Kidatu, Wilayani Kilombero; na

(iii) Kukamatwa kwa mabomu ya kutengenezwa kwa mkono katika maeneo mbalimbali kama vile Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mbinu mbalimbali zinazotumiwa na vikundi vya kigaidi na makundi ya kihalifu na pia kwa kuzingatia ukubwa wa maeneo ya mipaka ya nchi yetu, Wizara yangu imeendelea kuliimarisha Jeshi letu na kushirikisha wadau wengine kukabiliana na makundi hayo pamoja na kudhibiti kuenea kwa itikadi zenye msimamo mkali pamoja na ugaidi. Nawaomba Watanzania wenzangu kuchukua tahadhari na kutoa taarifa za matukio yanayotishia usalama wa nchi pindi yanapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vya hapa nchini pamoja na majeshi ya nchi nyingine, katika kukabiliana na vitendo vya kigaidi kwa kuimarisha doria na kuhakikisha maeneo yote ya mipakani ikiwemo ya nchi kavu na maji yanabaki salama. Ushirikiano na majeshi ya nchi mbalimbali umekuwa katika nyanja za mazoezi na operesheni za pamoja ambapo katika kipindi hiki, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilifanya mazoezi na operesheni za pamoja na majeshi hayo, ili kujenga utayari wa kukabiliana na matishio ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2015/2016; Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2015/2016. Katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 72,606,000 kutoka katika Mafungu yake matatu ya Ngome, JKT na Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 44,913,500 sawa na asilimia 61.9 ya makadirio. Kwa upande wa uchangiaji kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, makusanyo haya ni madogo kwa vile chanzo chake kikuu ni mauzo ya nyaraka za zabuni ambapo kwa sasa utangazaji huo unafanywa pia na Wakala wa Ununuzi na Ugavi Serikalini (GPSA) na hivyo kufanya mapato yake kupungua.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 na mapitio yake, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilidhinishiwa jumla ya

shilingi 1,679,209,285,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,447,071,327,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 232,137,958,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2016, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 1,069,758,080,337 sawa na asilimia 63.71 ya bajeti. Kati ya fedha hizo shilingi 1,027,758,080,336.65 sawa na asilimia 71 ya bajeti ya fedha za matumizi ya kawaida ambazo zilitumika kwa shughuli za kawaida ikiwemo kulipa mishahara, chakula cha wanajeshi na stahili mbalimbali muhimu za wanajeshi na watumishi wa umma.

Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, fedha zilizopokelewa ni shilingi 42,000,000,000 sawa na asilimia 18.1 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mafungu yote matatu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi mwezi Machi, 2016 unaoneshwa katika Kiambatisho Namba 2.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango kwa mwaka wa fedha 2015/2016, fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zimetumika kwa shughuli za kuwapatia stahili mbalimbali wanajeshi, watumishi wa umma na vijana walioko katika mafunzo ya JKT, kutoa huduma muhimu za chakula, tiba, sare, umeme, maji, simu na mafuta ya uendeshaji kwa ajili ya majukumu ya kiulinzi. Hata hivyo, kutokana na baadhi ya miezi kutolewa fedha pungufu kulinganisha na mahitaji halisi, utoaji wa baadhi ya stahili na huduma kwa wanajeshi, vijana wa JKT na watumishi wa umma ulikuwa chini ya viwango vinavyostahili. Aidha, upungufu katika kugharamia mahitaji muhimu umesababisha uendeshaji wa majukumu muhimu ya kimsingi kuwa mgumu na kusababisha madeni katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya fedha za maendeleo, sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa zimetumika katika kuimarisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kizana na kivifaa. Sehemu nyingine ya fedha imetumika kugharamia miradi ya ujenzi wa nyumba 6,064 ambazo ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa jumla ya nyumba 10,000 za makazi ya wanajeshi. Aidha, fedha hizo zimetumika katika kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji safi na maji taka katika vikosi vilivyopo Ngerengere na Msangani. Uthamini wa fidia kwa baadhi ya maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, kuendeleza ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi (RTS) Kihangaiko, ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) eneo la Duluti, Tengeru- Arusha. Pia ujenzi wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC) eneo la Kunduchi, jijini Dar es Salaam, ujenzi wa Chuo cha Tiba Lugalo, ujenzi wa karakana ya 601KJ, kuendeleza ujenzi wa

maghala ya kuhifadhi silaha na zana na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa mawasiliano jeshini katika maeneo ya Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya kiulinzi yaliyotekelizwa katika kipindi hicho ni pamoja na kufanyika mafunzo na mazoezi ya kijeshi; mafunzo ya ulinzi wa Jeshi la Akiba, upatikanaji wa huduma za afya na tiba kwa maafisa, askari na wananchi, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine, ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa, ushirikiano wa Jeshi na mamlaka za kiraia na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa kujitolea na wa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya utekelezaji wa majukumu hayo ya kiulinzi kwa kila eneo yanapatikana katika kitabu cha hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 25 hadi ukurasa wa 35.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya shughuli za maendeleo katika kipindi cha nusu mwaka 2015/2016, utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa ujumla haukuwa wa kuridhisha kwa baadhi ya mafungu. Katika kipindi hiki Fungu 57 - Wizara ilipata fedha za maendeleo kiasi cha shilingi 41,000,000,000, Fungu 38 - Ngome lilipata shilingi 1,000,000,000 na Fungu 39 JKT halikupata fedha yoyote ya maendeleo. Kwa wastani kwa mafungu yote matatu yalipokea asilimia 18.1 ya bajeti iliyoishnishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mapokezi hayo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeweza kuendeleza utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

Kulipia madeni ya kimikataba kwa ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, kuendeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 10,000 za makazi ya wanajeshi, ukarabati wa miundombinu katika makambi ya JWTZ, makambi na viteule vya JKT, uendelezaji wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, uboreshaji wa mawasiliano salama Jeshini, ukamilishaji wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu Duluti na Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya, Lugalo. Aidha, shughuli za uzalishaji mali katika Shirika la Uzalishaji Mali (SUMAJKT) na uendelezaji wa utafiti na teknolojia katika Shirika la Mazao ya Kijeshi Mzinga na Nyumbu ziliendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi. Katika mwaka 2015/2016 Serikali imeendelea na kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa ili kufikia azma yake ya kuwa na Jeshi dogo na la kisasa. Katika kipindi hicho, Jeshi limeendelea kupokea zana na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi wa nchi kavu, anga na majini. Upokeaji wa zana na vifaa hivyo, umeimarisha uwezo wa Jeshi letu kutekeleza majukumu yake ya ulinzi kwa ufanisi mkubwa. Kulingana na mahitaji ya Jeshi na mabadiliko ya teknolojia na mpango wa maendeleo wa

Wizara, ununuzi wa zana na vifaa bora na vya kisasa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi ni endelevu na wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba na makazi ya wanajeshi. Wakati nawasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu mwaka wa fedha 2015/2016 nililitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya kuendelea kwa ujenzi wa nyumba 10,000 za kuishi wanajeshi vikosini unaoteklezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa nyumba 6,064 unaendelea katika mikoa tisa ya Tanzania Bara na Visiwani. Ujenzi huo umekuwa ukiendelea vizuri katika mikoa hiyo ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2016 jumla ya nyumba 4,744 zilikuwa zimekamilika kujengwa sawa na asilimia 78.2 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kwamba hadi mwezi Aprili, 2016, ujenzi kwa ujumla katika mikoa hiyo umeendelea vizuri zaidi na kufikia asilimia 85.5 ambapo nyumba 5,184 zimekamilika na nyumba 880 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ambao unaendelea vizuri. Mchanganuo wa nyumba zilizokamilika ni kama ifuatavyo; Arusha nyumba 664, Dar es Salaam 2,256, Pwani 840, Tanga 312, Morogoro 416, Dodoma 376 na Pemba 320.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT, Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali la SUMA JKT limeendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, uhandisi na ujenzi, viwanda na biashara ili kuzalisha mali. Aidha, Shirika lina kampuni tanzu ya SUMA JKT Guard Ltd. inayojishughulisha na masuala ya ulinzi kwa Taasisi za Umma na watu binafsi na SUMA JKT Seed Co. Ltd. inayojishughulisha na ununuzi na usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 SUMA JKT limeendelea kuagiza matrekta ikiwa ni awamu ya tatu kwa ajili ya kuyauza kwa wakulima na taasisi mbalimbali ili kufanikisha kauli mbiu ya kilimo kwanza. Katika kipindi hicho jumla ya matrekta 108 na majembe 110 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 1.9 yaliagizwa kutoka India. Hadi kufikia Januari, 2016 jumla ya matrekta 98 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.38 yalikuwa yameuzwa na vipuri vyenye thamani ya shilingi milioni 241.5 vilikuwa vimeuzwa.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT limeanzisha mradi mpya wa kuchakata kokoto eneo la Pongwe Msungula, Msata ujulikanao kwa jina la Suma JKT Anit Asfalt Company Ltd. Mradi huu ulizinduliwa rasmi mwezi Oktoba, 2015 na Rais wa Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete. Mradi huu unamilikiwa kwa ubia kati ya Suma JKT yenye asilimia 30 ya hisa na Kampuni kutoka nchini Uturuki inayojulikana kama Anit Asfalt inayomiliki asilimia 70 ya hisa.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Shirika la Mzinga; katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Shirika kupitia mapato yake madogo ya ndani limeendelea na uzalishaji katika mkondo wa risasi katika kaliba mbalimbali na utekelezaji wa majukumu mengine ikiwemo kufanya ukarabati wa miundombinu ya shirika. Kwa upande mwingine kampuni yake tanzu ya *Mzinga Holding* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya taasisi za Serikali na binafsi kwa ajili ya kupata kipato. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa awamu ya kwanza wa jengo la Halmashauri mpya ya Ikungi Singida, Ofisi ya Wilaya mpya ya Mkalama Singida, ujenzi wa jengo la *TUAKA SACCOS Ltd.*, Karagwe na ujenzi wa jengo la Biashara la Kanisa Katoliki Morogoro.

Mheshimiwa Spika, shughuli za Shirika la Nyumbu. Shirika la Nyumbu linafanya utafiti na uendelezaji wa teknolojia wa magari ya kijeshi. Katika mwaka 2015/2016, shirika lilipanga kutekeleza shughuli zake za kuendeleza utafiti katika teknolojia ya magari na mitambo ya kijeshi, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuhawilisha teknolojia mbalimbali za utafiti na kukarabati miundombinu ya shirika. Kutokana na ukosefu wa fedha za maendeleo, shirika halikuweza kutekeleza shughuli zake za msingi.

Hata hivyo, kwa kutumia mapato madogo ya ndani shirika limeendelea kufanya utafiti wa zana na vifaa mbalimbali vya kijeshi ikiwa ni pamoja na magari ya deraya, zana za kilimo kama trekta ndogo, vipuli vya treni, na uzalishaji mdogo wa bidhaa na vipuli mbalimbali kwa ajili ya sekta za kilimo, viwanda na usafirishaji. Aidha, shirika lipo katika mazungumzo na Kampuni ya Histomart ya Afrika Kusini kwa ajili ya uhawilishaji wa teknolojia na kujielekeza katika kuboresha matengenezo ya magari na Kampuni ya NORINCO kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya kuhawilisha teknolojia ya utengenezaji wa magari ya deraya na mapigano.

Mheshimiwa Spika, uthamini, upimaji na ulipaji fidia wa maeneo kwa matumizi ya Jeshi. Kama ilivyoelezwa awali, mionganoni mwa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kutafuta, kuyaendeleza na kuyatunza maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za majeshi yetu. Pamoja na shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanyika ndani ya maeneo hayo, lililo muhimu pia ni kuyamiliki kisheria. Maeneo mengi ya Jeshi yaliyopo bado kumilikiwa kisheria, hivyo kumekuwepo na migogoro ya umiliki kati ya Jeshi na wananchi wachache.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016 tumeweza kufanya uthamini wa fidia maeneo ya llemtela na Lukobe Mkoa wa Mwanza na hatua inayofuatia ni ya ulipaji fidia. Aidha, maeneo ya Jeshi yaliyopo KTC Kunduchi na Ubungo Kibangu yamepimwa na kuwekewa alama mpya ili kuzuia kuvamiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la upimaji, uthamini na ulipaji fidia maeneo ya Jeshi ni endelevu, mwaka wa fedha 2016/2017 upimaji na uboreshaji mipaka ya maeneo ya Jeshi unategemewa kufanyika katika maeneo ya Bihamulo, Kaboya na Muleba mkoani Kagera, Uyui, Mirambo na Usule mkoani Tabora, Tunduru mkoani Ruvuma, Mtanda mkoani Lindi, Mtipa mkoani Singida, Maziwa ya Ng'ombe na Masuke - Pemba, Bawuai, Chukwani na Bububu - Unguja. Kuhusu uthamini na ulipaji fidia, maeneo yatakayohusika ni Kimbiji, Temeke na Tanganyika Packers mkoani Dar es Salaam, Kigongo Ferry mkoani Mwanza, Ronsoti, Tarime mkoani Mara na Rasi Nondwa mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inakabiliwa na migogoro ya ardhi ya muda mrefu inayotokana na baadhi ya wananchi na taasisi kuvamia maeneo ya ardhi ya Jeshi. Ili kukabiliana na changamoto hizi hatua mbalimbali zikiwemo za kisheria zinaendelea kuchukuliwa. Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuwasihii wananchi wasivamie maeneo ya Jeshi wala kuendesha shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo. Naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kusaidia kuwashamasisha wananchi kuheshimu maeneo yanayomilikiwa na Jeshi ili kuepuka kuingia kwenye migogoro na Jeshi. Wizara yangu itaendelea na utaratibu wake wa kulipatia Jeshi maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji wa mpango na bajeti katika mwaka 2015/2016; Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kupatiwa kiwango pungufu cha fedha ikilinganishwa na mahitaji halisi ambayo ni makubwa.

Aidha, hali ya mapokezi ya fedha imekuwa hairidhishi, kwa mwaka 2015/2016 wakati kiasi kilichoidhinishwa ni shilingi 1,679,209,285,000, fedha iliyopokelewa hadi sasa ni shilingi 1,069,758,080,337, sawa na asilimia 63.7 ya bajeti. Katika bajeti hiyo, fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo ni shilingi 232,137,958,000. Mapokezi hadi mwezi Machi, 2016 yalikuwa ni shilingi 42,000,000,000 sawa na asilimia 18.1 ya bajeti. Hata hivyo, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida, mapokezi yamekuwa ya kuridhisha ambapo tumepokea asilimia 71 ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, hali ya kutengewa bajeti ndogo na kupatiwa fedha pungufu imekuwa ikiathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Jeshi na pia kusababisha ulimbikizaji wa madeni hususan ya kimkataba ambayo tumeingia na makampuni mbalimbali kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi kizana na kivifaa. Aidha, madeni mengine ni yale yanatokana na madai ya maafisa na askari, watumishi wa umma, huduma za simu, umeme, maji na madai kutoka kwa wazabuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mwaka 2016/2017 mpango wa utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wa mwaka 2016/2017, umekusudia kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kulingana na dira na dhima ya Wizara. Vilevile, mpango umelenga kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, shughuli zitakazotekelzwa katika mpango huo zitakuwa katika maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuliimarisha na kuliongezea uwezo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika utendaji kivita kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa wanajeshi dhidi ya adui wa ndani na nje;

(ii) Kulijengea Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania mazingira mazuri ya kufanyia kazi na makazi ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi na kuimarisha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya msingi kama vile chakula, tiba, sare, usafiri, maslahi na stahili kwa wanajeshi na watumishi wa umma;

(iii) Kuimarisha uwezo wa Jeshi katika utafiti na kuendeleza teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya jeshi na kiraia hapa nchini na nje ya nchi; na

(iv) Kuendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya uzalendo, umoja wa Kitaifa, ukakamavu na kuwapatia stadi za kazi ili kuwaandaa katika uzalishaji mali na kuimarisha ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi na nchi nyingine duniani kupitia Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na ushirikiano wa nchi moja moja.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka 2016/2017. Makadirio ya Mapato; kutokana na majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni bayana kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake haina chanzo kikubwa cha kuiingizia mapato na kuiweseha kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maduhuli ya Serikali. Chanzo kikuu cha mapato kwa sasa kimebaki kuwa ni makusanyo ya mauzo ya nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 70,806,000 katika mchanganuo ufuatao:-

Fungu 38 – Ngome shilingi 18,000,000; Fungu 39 JKT shilingi 52,003,000; Fungu 57 Wizara shilingi 803,000 na jumla ni shilingi 70,806,000.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kama nilivyoeleza katika hotuba hii, katika mwaka wa fedha 2016/2017 naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,736,530,413,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,488,530,413,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 248,000,000,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

Fungu 38 Ngome - Matumizi ya Kawaida ni shilingi 1,187,496,021,000; Matumizi ya Kaendeleo ni shilingi 10,000,000,000, jumla ni shilingi 1,197,496,021,000.

Fungu 39 JKT - Matumizi ya Kawaida shilingi 282,034,214,000, Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 8,000,000,000, jumla ni shilingi 290,034,214,000;

Fungu 57 Wizara - Matumizi ya Kawaida ni shilingi 19,000,178,000, Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 230,000,000,000. Jumla ni shilingi 249,000,178,000.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba hotuba yangu iingie yote kama ilivyo kwenye kitabu katika Hansard kwa sababu ya ufinyu wa muda, naomba pia nitoe taarifa kwamba hotuba hii pia inapatikana katika tovuti za Wizara ambayo ni [www.modans.go.tz](http://www.modans.go.tz); Ngome [www.ulinzi.go.tz](http://www.ulinzi.go.tz) na JKT [www.jkt.go.tz](http://www.jkt.go.tz)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi na Jeshi la Kujenga Taifa hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Tunakushukuru sana kwa hotuba nzuri ya uhakika na kama ulivyosema mwenyewe yale maeneo ambayo hayajawa covered watu wa Hansard yachukueni kama yalivyo.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHE. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB) KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA WIZARA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/17.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kulijalia Taifa letu na wananchi wake wote kwa kutuvusha salama katika mchakato wote wa uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2015. Watanzania tunayo kila sababu ya kujivunia kuwa Uchaguzi Mkuu huo ambao kikalenda ni wa tano tangu kurejeshwa kwa mfumo wa demokrasia ya Vyama vingi mwaka 1992, uliendeshwa na kuhitimishwa kwa amani, utulivu na mshikamano mkubwa kinyume na maadui wetu wa ndani na nje ya nchi waliotutabiria mabaya. Kwa muktagha huo, nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendeleza misingi ya umoja, mshikamano na amani ya nchi yetu. Aidha, nawapongeza: aliyekuwa Makamu wa Rais, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal; na Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kusimamia utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2010-2015. Pia, nawapongeza Mhe. Anne Semamba Makinda, Spika Mstaafu, akisaidiana na Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb) na Wenyeviti wetu kwa kuliongoza Bunge la Kumi kwa hekima, busara na mafanikio makubwa.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia, kuwapongeza Viongozi wa kitaifa kwa kuchaguliwa kwenye nafasi mbalimbali katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Kipekee nawapongeza kwa dhati kabisa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wake Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na CCM kupeperusha bendera ya Chama na hatimaye kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Taifa letu Tukufu.

4. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza Mhe. Kassim M. Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa, kwa kuteuliwa na Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge lako kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nakupongeza wewe Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb), kwa ushindi ulioupata katika jimbo la Kongwa na kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge hili la Kumi na Moja. Vilevile, nampongeza Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nachukua fursa hii pia, kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge na Kamati za Bunge kwa ushindi kwenye Majimbo yao na kuchaguliwa katika nyadhifa hizo.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuwapongeza Wabunge wenzangu tuliochaguliwa katika majimbo yetu, waliochaguliwa kuitia Viti Maalum, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na walioteuliwa na Mhe. Rais kuunda Bunge lako hili Tukufu la Kumi na Moja. Aidha, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali chini ya falsafa makini ya "Hapa Kazi Tu".

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kunitua kuiongoza tena Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ni dhahiri kuwa heshima na dhamana niliyopewa na Mhe. Rais ni kubwa na adhimu. Hivyo, nachukua fursa hii kumhakikishia Mhe. Rais, Makamu wake, Waziri Mkuu, Chama changu, Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi, Chama Nambari "One" na Wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi niliyopewa kwa uwezo wangu wote, akili zangu zote na kwa nguvu zangu zote. Namuomba Mwenyezi Mungu aniongoze na kunisaidia. Aidha, napenda kuwashukuru wapiga kura na wananchi wote wa jimbo langu la uchaguzi la Kwahani, kwa imani waliyonayo juu yangu kwa kunichagua kuendelea kuwa Mbunge wao katika kipindi kingine cha miaka mitano. Imani hiyo kwangu imemwezesha Mhe. Rais wetu kunitua katika nafasi hii. Nawashukuru sana. Ahadi yangu kwao na wananchi wote ni kuendelea kufanya kazi kwa moyo na uadilifu mkubwa. Asanteni sana.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwezesha uchaguzi wa marudio wa Zanzibar uliofanyika tarehe 20 Machi, 2016 kukamilika kwa amani na utulivu. Hivyo, natumia fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar katika kipindi kingine cha pili cha miaka mitano. Vilevile, nampongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

8. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuwapongeza Mhe. Balozi Adadi Rajabu (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, na Mhe. Kanali Mstaafu Ally Khamis Masoud (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti. Naomba kuwapongeza pia wajumbe wote wa Kamati hii. Naahidi kushirikiana kwa dhati na Kamati hii katika kutekeleza majukumu inayoyasimamia.

9. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii pia, kuwakumbuka wagombea ubunge wenzetu waliopoteza maisha. Wagombea hao ni pamoja na Celine Kombani (Ulanga Magharibi), Dkt. Abdallah Kigoda, (Handeni Mjini), Deo Filikunjombe (Ludewa), Estomih Mallah (Arusha Mjini), Mohamed Mtoi (Lushoto), na Dkt Emmanuel Makaidi (Masasi). Tunatoa pole kwa ndugu, jamaa, rafiki na

wananchi wa majimbo yao kwa kuondokewa na wapendwa hao. Tunaomba Mwenyezi Mungu azirehemu roho zao. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote waliopoteza ndugu, jamaa, na marafiki kwa sababu mbali mbali katika kipindi hiki. Pia nawapa pole wote waliopatwa na majanga katika matukio mbalimbali.

10. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo sasa naomba kuwasilisha hotuba yangu ambayo kiujumla inahusu maeneo makuu yafuatayo:- Malengo na Majukumu ya Wizara; Utekelezaji wa Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama; Hali ya Ulinzi na Usalama nchini mwetu; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2015/16 na, Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/17.

## WAJIBU NA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JKT

11. **Mheshimiwa Spika**, kama tulivyokwisha kuitangaza Dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa. Aidha, Dhima ya Wizara ya Ulinzi na JKT ni kuilinda Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya maadui kutoka nje na ndani ya nchi na kuhakikisha kuwa uhuru na maslahi ya Taifa letu yanakuwa salama wakati wote.

12. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2015- 2020) Ibara ya 146 (i), (ii), (iii), (iv), (vi), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara inasimamia utekelezaji wake kama ifuatavyo:-

i. **Kuviwezesha vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na rasilimali fedha**

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) likiwa ni mionganini mwa vyombo vya Ulinzi na Usalama, litaendelea kuandikisha vijana wenyewe sifa na ujuzi stahiki ili kufikia azma ya kuwa na Jeshi dogo lenye weledi, uwezo na zana bora za kisasa. Katika kufanya hivyo, utaratibu wa kuandikisha vijana wa kuijunga na JWTZ utaendelea kuwa ni ule ule wa kuwapata kutoka kwenye Kambi za JKT. Kwa upande wa rasilimali fedha, Wizara itaendelea kutenga fedha za kutosha kuhudumia mahitaji ya Jeshi kutegemea na bajeti ya Serikali.

ii. **Kuendelea kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama**

Wizara itaendelea kuboresha maslahi ya Wanajeshi hususan mishahara, posho, makazi na vitendea kazi. Aidha, tutaendelea na ujenzi wa nyumba

mpya kwa makazi ya wapiganaji na Ofisi, pamoja na kutoa mafunzo na stahili mbalimbali kwa Maafisa na Askari.

**iii. Kuendelea kuweka mazingira yatakayowezesha JKT kuimarisha mafunzo kwa vijana wa Kitanzania**

Wizara yangu itaendelea kuliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kifedha, rasilimali watu na kuimarisha iundombinu ili kuweza kutoa mafunzo kwa vijana wote wa Mujibu wa Sheria na wa Kujitolea kulingana na uwezo wa kifedha.

**iv. Kuendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kwenye majukumu ya ulinzi wa amani**

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaendelea kushiriki katika shughuli na Operesheni za Kimataifa na Kikanda kama zitakavyokuwa chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa nchi za Afrika, au chini ya Jumuiya za Kikanda.

**v. Kuendelea kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka**

Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama, Mamlaka za Kiraia na Mataifa mengine kupambana na matishio mapya ya kiusalama yakiwemo, ugaidi, uharamia, uhamiaji haramu, biashara haramu ya madawa ya kulevyta na usafirishaji haramu wa binadamu.

**vi. Kuimarisha Muungano**

Suala la ulinzi ni la Muungano. Hivyo, Wizara kwa kutumia vyombo vyake itaendelea na jukumu lake la kuhakikisha Ulinzi na Usalama wa mipaka yote ya nchi unaimarishwa ili kudumisha amani na utulivu kwa Taifa lote.

**vii. Maendeleo ya Viwanda**

Wizara itaendelea kusimamia na kuimarisha Taasisi na viwanda vyake katika shughuli za tafiti, uzalishaji na utoaji huduma za kihandisi kwa ajili ya matumizi ya Kijeshi na Kiraia. Hivyo, uzalishaji wa mazao mapya kupitia viwanda vyetu utaimarishwa. Aidha, shughuli za ukarabati wa miundombinu, ununuzi wa mashine na mitambo inayoendana na teknolojia za kisasa, na malighafi za kutosha zitaendelezwa.

**viii. Kilimo na Mifugo**

Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa na Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), litaendelea kutekeleza miradi ya kilimo, ufugaji na uvuvi kwa kuwahusisha vijana wakati wa mafunzo yao. Mafunzo haya

yanahusisha pia shughuli za ujenzi. Wizara inafanya tathmini ya ushiriki wa JKT katika shughuli za kuzalisha na kusambaza mbegu ili ziwe na tija. Vivyo hivyo, tunatafakari ushiriki katika uuzaji wa matrekta kwani kasi ya ulipaji madeni na urejeshaji wa mikopo ni mdogo mno.

## ix. Ajira

Kama nilivyoeleza hapo juu, Wizara yangu inaendelea kutekeleza kwa ukamilifu agizo la Mheshimiwa Rais kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama kuandikisha askari wapya kutoka vijana waliohitimu mafunzo ya JKT. Hivyo, natoa rai kwa vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama kutekeleza agizo hilo. Sambamba na kupata ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama, JKT litaendelea kuwapatia vijana wanaojiunga na Jeshi hilo Mafunzo ya Ufundis Stadi yanayowaongezea uwezo wa kupata ajira katika Taasisi nyingine za uzalishaji mali na kujiajiri. Aidha, JKT linatarajia kufungua kituo kikubwa cha VETA katika eneo la Kongwa-Dodoma ili kuendelea kutoa mafunzo kwa vijana waliojiunga na mafunzo ya JKT. Eneo la ekari 500 kwa ajili ya mafunzo hayo limepatikana na lipo kwenye hatua ya kufanyiwa tathmini na upimaji ili fidia iweze kulipwa na kuweshe taratibu nyingine za ujenzi kuendelea.

### Majukumu

13. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Dira, Dhima, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bunge la Kumi na Moja, Wizara itahakikisha kuwa uhuru na usalama wa nchi unalindwa na kusimamiwa, hivyo, majukumu yetu yatajikita katika maeneo yafuatayo:-

- i. Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine hasa nchi jirani na nchi rafiki kwa lengo la kudumisha amani na usalama;
- ii. Kusaidia Mamlaka za Kiraia katika kuzuia uporaji wa rasilimali za Taifa, kukabiliana na athari za majanga inapobidi na kudhibiti vitendo vinavyoweza kuhatarisha amani na utulivu nchini;
- iii. Kuandaa umma wa Watanzania katika mapambano dhidi ya adui kupitia mafunzo ya Jeshi la Akiba;
- iv. Kutafiti, kuendeleza na kuzalisha teknolojia za kijeshi; na
- v. Kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, umoja wa Kitaifa, usawa, nidhamu na ukakamavu na kuwaandaa katika uzalishaji mali na ufundis kupitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa.

14. **Mheshimiwa Spika**, Katika kuyatekeleza majukumu haya, mwaka wa fedha 2016/17 Wizara itafanya shughuli zifuatazo:-

- i. Kuendelea kuandikisha wanajeshi kwa kuzingatia sifa zinazohitajika ili kulijengea Jeshi uwezo kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa;
- ii. Kuendelea kuwapatia wanajeshi zana, vifaa na vitendea kazi bora na vya kisasa;
- iii. Kusimamia matunzo na matumizi mazuri ya zana, vifaa na vitendea kazi vilivyopo;
- iv. Kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi ikiwa ni pamoja na shughuli za uendeshaji mafunzo ya ulinzi wa Jeshi la Akiba;
- v. Kuendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea vijana wa Kitanzania moyo wa uzalendo, ukakamavu, ujasiri, maadili mema na utaifa;
- vi. Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia za kijeshi na kuzalisha mali kupitia mashirika ya Mzinga na Nyumbu;
- vii. Kuwezesha uzalishaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) kuwa wa tija na faida na hivyo kuchangia katika uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa;
- viii. Kushirikiana na Mamlaka za kiraia pale inapobidi katika kukabiliana na majanga na dharura za kitaifa;
- ix. Kuendeleza ujenzi wa makazi na miundombinu ili kuimarisha mazingira bora ya kuishi na kufanya kazi;
- x. Kuimarisha ushirikiano nan chi nyingine Duniani katika masuala ya ulinzi na amani;
- xi. Kuendelea na upimaji, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yanayotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi; na
- xii. Kuendelea kuwapatia wanajeshi, vijana wa JKT na watumishi wa Umma stahili zao mbalimbali.

**UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI**

15. **Mheshimiwa Spika**, tangu uteue Kamati za Kudumu za Bunge mapema mwaka huu Wizara imepokea ziara ya wajumbe wa Kamati na kufanya vikao na Kamati zako mbili za kudumu za Bunge kama ifuatavyo; Ziara mbili za

wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na kufanya nao vikao vinne. Aidha, kilifanyika kikao kimoja cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Katika ziara na vikao hivyo Kamati zilitoa hoja na maelekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utendaji wa majukumu ya Wizara. Hivyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati hizi yamefanyiwa kazi na majibu yake yameainishwa katika **Kiambatanisho Na.1a na 1b**.

## HALI YA ULINZI NA USALAMA

### (i) Hali ya Usalama wa Mipaka

16. **Mheshimiwa Spika**, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka yetu na nchi jirani kwa jumla ni shwari. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutekeleza jukumu la ulinzi wa mipaka kwa weledi na hivyo kudhibiti ipasavyo mipaka yote ya Tanzania na kuhakikisha kuwa nchi yetu ni salama. Hata hivyo, migogoro na viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi jirani yamesababisha ongezeko la wakimbizi na wahalifu mbalimbali wanaoingia nchini, wakiwemo wenye silaha za moto kinyume na sheria na kisha kuzitumia silaha hizo kutenda uhalifu. Pia, matukio ya uharibifu wa alama za mipakani kwenye baadhi ya maeneo ya mipaka ya nchi yetu hayajapatiwa ufumbuzi. Mazungumzo kati ya Tanzania na nchi inazopakana nazo yanaendelea kupitia Wizara za Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Lengo ni kuhakikisha alama za mipaka zinajengwa na zile zilizoharibiwa zinarejeshwa ili mipaka yote iwe inaonekana kwa uwazi. Pamoja na hayo, hali ya mipaka yetu imekuwa kama ifuatavyo:-

#### (a) Mpaka wa Kaskazini

17. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Kaskazini, kwa ujumla hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, vitendo vya uharibifu wa mawe ya mpakani (beacons) na ujenzi holela unaofanywa na watu waishio mpakani vinaendelea. Aidha, matukio ya kujipatia ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho ya mifugo, biashara na ujenzi wa makazi vimeendelea kuwa changamoto kubwa. Maeneo yaliyoathirika zaidi ni Jasini, Namanga, Holili na Horohoro. Juhudi za kujenga alama za mipakani zinaendelea. Aidha, katika maeneo ya Sirari na Tarime kwa upande wa Tanzania na Isebenia na Kurya kwa upande wa Kenya, yameimariswa kwa kujengwa alama za mpakani zilizobomolewa.

#### (b) Mpaka wa Mashariki

18. **Mheshimiwa Spika**, mpaka huu unahusisha eneo la nchi yetu katika Bahari ya Hindi. Hali ya usalama katika mpaka huu imekuwa shwari. Hakuna

matukio ya uharamia yaliyotokea na vikosi vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania vyenye jukumu la kuhakikisha usalama wa mpaka huu vimeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kipindi hiki Jeshi letu la Wanamaji limeongezewa nguvu kwa kupewa Meli Vita mpya zenyenye uwezo wa kufanya doria katika Bahari kuu. Vivyo hivyo, Jeshi kwa kushirikiana na mamlaka husika, limeendelea kuchukua hatua za kudhibiti uvuvi haramu na usafirishaji wa bidhaa haramu ili kulinda rasilimali na usalama wa nchi yetu.

**(c) Mpaka wa Magharibi**

19. **Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa inayokabili mpaka wetu wa Magharibi ni athari ya machafuko ya kisiasa yanayosababisha wimbi la wakimbizi kuingia nchini kwetu. Pia, yamekuwepo matukio ya ujambazi wa kutumia silaha maeneo mbalimbali katika Ziwa Tanganyika yanayotekelizwa na watu wenye silaha na vikundi vinavyohasimiana katika nchi hizo jirani. Pamoja na changamoto hii, Jeshi letu limejizatiti kizana, kivifaa na kimikakati kukabiliana navyo.

**(d) Mpaka wa Kusini**

20. **Mheshimiwa Spika**, Hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, utata wa mpaka katika Ziwa Nyasa bado haujapatiwa suluhisho. Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa inaendelea kutumia njia za Kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu. Pamoja na hali hiyo, wananchi wa pande zote wanaendelea na shughuli zao bila bughudha yoyote.

**(ii) Hali ya Ulinzi na Usalama katika Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati**

21. **Mheshimiwa Spika**, hali tete ya Usalama katika baadhi ya nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ni tishio kwa usalama wa nchi yetu hasa kutohuna na machafuko ya kisiasa katika nchi hizo. Ukanda huu umekuwa katika tahadhari ya kiusalama dhidi ya mashambulizi ya kigaidi kutoka kundi la Al-Shabab. Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na raia wema vitaendelea kuwa macho katika kufuatilia nyendo za makundi mbalimbali yanayodhaniwa kuhatarisha usalama wa nchi yetu.

22. **Mheshimiwa Spika**, hali ya usalama katika nchi za Somalia, na jimbo la Darfur nchini Sudan imeendelea kuwa changamoto kwetu. Aidha, nchini Somalia mapambano yanaendelea baina ya majeshi ya AMISOM na kundi la kigaidi la Al Shabab. Kwa upande wa eneo la Darfur mapigano baina ya vikosi vya Serikali na vikundi vya uasi yanaendelea. Nchini Sudan Kusini, kurejea kwa uhusiano kati ya Serikali inayoongozwa na Rais Salva Kiir na kikundi kinachomuunga mkono Dkt. Riek Machar Makamu wa Rais yanatoa dalili njema za kufikia muafaka wa kudumu.

(iii) **Ugaidi na Uharamia**

23. **Mheshimiwa Spika**, matukio ya ugaidi wa kimataifa yameendelea kuwa tishio la usalama duniani. Kuwepo kwa makundi ya Al-Shaabab, Al-Qaeda, Boko Haram, Islamic State (IS) kunafanya tishio la ugaidi kusambaa duniani. Hivyo tuna kila sababu ya kujizatiti na kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama. Taarifa za kuwepo kwa baadhi ya Watanzania wanaojiunga na makundi ya Al-Shabab na IS kunahatarisha usalama wa Tanzania, hasa ikizingatiwa kiujumla mwingiliano mkubwa uliopo kati ya wananchi wetu na watu wenye malengo tofauti. Hatari iliyopo ni uwezekano wa baadhi ya vijana waliojiunga na makundi haya ya kigaidi ya kimataifa kurejea nyumbani kwa malengo ya kutekeleza vitendo vya kigaidi nchini mwetu.

24. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kilichopita kumejitokeza viashiria vyenye mwelekeo wa kigaidi ambavyo ni:

- a. Kuvamiwa kwa baadhi ya vituo vya polisi, kupoawa silaha na baadhi ya askari kuuawa na kundi ambalo nia yake haijafahamika;
- b. Matukio yenye mwelekeo wa kigaidi kama vile yaliyotokea katika Mapango ya Amboni Tanga na katika kitongoji cha Nyando, Tarafa ya Kidatu wilayani Kilombero, na
- c. Kukamatwa kwa mabomu ya kutengenezwa kwa mkono katika maeneo mbalimbali kama vile Zanzibar.

25. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua mbinu mbalimbali zinazotumiwa na vikundi vya kigaidi na makundi ya kihalifu, na pia kwa kuzingatia ukubwa wa maeneo ya mipaka ya nchi yetu, Wizara yangu imeendelea kuliimarisha Jesi letu na kushirikisha wadau wengine kukabiliana na makundi hayo pamoja na kudhibiti kuenea kwa itikadi zenye msimamo mkali (radicalization) pamoja na ugaidi. Nawaomba Watanzania wenzangu kuchukua tahadhari na kutoa taarifa ya matukio yanayotishia usalama wa nchi pindi yanapojitokeza.

26. **Mheshimiwa Spika**, Jesi letu limeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na usalama vya hapa nchini pamoja na majeshi ya nchi nyingine, katika kukabiliana na vitendo vya kigaidi kwa kuimarisha doria na kuhakikisha maeneo yote ya mpakani ikiwemo ya nchi kavu na maji yanabaki salama. Ushirikiano na majeshi ya nchi mbalimbali umekuwa katika nyanja za mazoezi na operesheni za pamoja ambapo katika kipindi hiki, Jesi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilifanya mazoezi na operesheni za pamoja na majeshi hayo, ili kujenga utayari wa kukabiliana na matishio ya namna hii.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2015/16

### Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2015/16

27. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 72,606,000.00** kutoka katika Mafungu yake matatu ya 38-NGOME, 39-JKT na 57-Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 44,913,500.00** sawa na **asilimia 61.9** ya makadirio. Kwa upande wa uchangiaji kwenye mfuko mkuu wa Serikali, makusanyo haya ni madogo kwa vile chanzo chake kikuu ni mauzo ya nyaraka za zabuni, ambapo kwa sasa utangazaji huo unafanywa pia na Wakala wa Ununuza na Ugavi Serikalini (GPSA) na hivyo kufanya mapato yake kupungua.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya MwakawaFedha2015/16namapitioyake,Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,679,209,285,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika Mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,447,071,327,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 232,137,958,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mchanganuo wa bajeti hiyo kwa kuzingatia mafungu ya Wizara ni ufuatao:-

FUNGU	MATUMIZI		
	KAWAIDA	MAENDELEO	JUMLA
NGOME	1,143,865,683,000	8,000,000,000	1,151,865,683,000
JKT	283,353,207,000	4,000,000,000	287,353,207,000
WIZARA	19,852,437,000	220,137,958,000	239,990,395,000
JUMLA	<b>1,447,071,327,000</b>	<b>232,137,958,000</b>	<b>1,679,209,285,000</b>

29. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2016 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,069,758,080,337.00** sawa na **asilimia 63.71** ya bajeti. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,027,758,080,336.65** sawa na **asilimia 71** ya bajeti ya fedha za Matumizi ya Kawaida ambazo zilitumika kwa shughuli za kawaida ikiwemo kulipa mishahara, chakula cha Wanajeshi na stahili mbalimbali muhimu za Wanajeshi na Watumishi wa Umma. Kwa upande wa Matumizi ya Maendeleo, fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 42,000,0000,000.00** sawa na **asilimia 18.1** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za

maendeleo. Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mafungu yote matatu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi mwezi Machi, 2016 umeoneshwa katika **Kiambatanisho Namba 2**.

### **UTEKELEZAJI WA MPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16**

30. **Mheshimiwa Spika**, Hali isiyoridhisha ya utolewaji wa fedha kama ilivyoelezewa hapo juu inatoa taswira pia isiyoridhisha ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2015/16. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zimetumika kwa shughuli za kuwapatia stahili mbalimbali Wanajeshi, Watumishi wa Umma na Vijana walioko katika mafunzo ya JKT, kutoa huduma muhimu za chakula, tiba, sare, umeme, maji, simu na mafuta ya uendeshaji kwa ajili ya majukumu ya kiulinzi. Hata hivyo, kutohana na baadhi ya miezi kutolewa fedha pungufu kulinganisha na mahitaji halisi, utoaji wa baadhi ya stahili na huduma kwa Wanajeshi, Vijana wa JKT na Watumishi wa Umma ulikuwa chini ya viwango vinavyostahili. Aidha, upungufu katika kugharamia mahitaji muhimu umesababisha uendeshaji wa majukumu muhimu ya kimsingi kuwa mgumu na kusababisha madeni katika baadhi ya maeneo.

31. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya fedha za maendeleo, sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa zimetumika katika kuimarisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kizana na kivifaa. Sehemu nyingine ya fedha imetumika kugharamia mradi wa ujenzi wa nyumba 6,064 ambazo ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa jumla ya nyumba 10,000 za makazi ya wanajeshi. Aidha, fedha hizo zimetumika katika kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji safi na maji taka katika vikosi vilivyopo Ngerengere na Msangani, uthamini wa fidia kwa baadhi ya maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, kuendeleza ujenzi wa Shule ya Mafunzo ya Awali ya Kijeshi (RTS) Kihangaiko, ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) eneo la Duluti, Tengeru- Arusha. Pia, ujenzi wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC) eneo la Kunduchi jijini Dar es Salaam, ujenzi wa Chuo cha Tiba Lugalo, ujenzi wa Karakana ya 601KJ, kuendeleza ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha na zana na kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano Jeshini katika maeneo ya Zanzibar, Pwani na Dar es Salaam.

32. **Mheshimiwa Spika**, majukumu ya kiulinzi yaliyotekeliza katika kipindi hicho ni pamoja na kufanya mafunzo na mazoezi ya kijeshi; mafunzo ya Ulinzi wa Jeshi la Akiba; upatikanaji wa huduma za afya na tiba kwa maafisa; askari na wananchi; ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine; ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa; ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana wa kujitolea na wa Mujibu wa Sheria.

33. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nitoe maelezo ya kina ya utekelezaji wa majukumu hayo ya kiulinzi kwa kila eneo kama ifuatavyo:-

**(i) Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi**

34. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2015/16, Serikali iliendelea kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kutoa mafunzo kwa maafisa na wapiganaji wake katika vyuo na shule za kijeshi ndani na nje ya nchi, ili kuwaendeleza kitaaluma katika fani zao na kuimarisha uwezo wao wa uongozi na utendaji. Jeshi letu pia, iliendelea kushiriki katika mafunzo na mazoezi ya pamoja na nchi rafiki. Mionganoni mwa mazoezi hayo yalikuwa ni **Ex-Okavanga (Air Forces)** yaliyofanyika nchini Botswana kuanzia tarehe 11-26 Julai, 2015, **Ex-Southern Accord** yaliyofanyika nchini Zambia, kuanzia tarehe 03-17 Agosti, 2015, **Ex-Tambua Uwezo** yaliyofanyika Arusha nchini Tanzania kuanzia tarehe 21 Agosti-11 Septemba, 2015, na **Ex-Timamu** yaliyofanyika Msata nchini Tanzania tarehe 18-23 Desemba, 2015, **Ex-Onesha Uwezo wa Medani** yaliyofanyika Arusha nchini Tanzania tarehe 07 -22 Januari, 2016 na **Ex-Ushirikiano Imara** yaliyofanyika nchini Kenya kuanzia tarehe 21 Machi - 4 Aprili, 2016. Mazoezi ya aina hii ni muhimu katika kuimarisha mahusiano ya Majeshi yetu na Majeshi ya nchi nyingine. Pia, mazoezi hayo huwajengea Wanajeshi wetu, weledi na umahiri wa kutumia zana na vifaa.

**(ii) Mafunzo ya Ulinzi kwa Jeshi la Akiba**

35. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika kipindi cha mwaka 2015/16 kwa kushirikiana na vyombo vyia Ulinzi na Usalama limeendelea kutoa mafunzo ya Mgambo katika ngazi ya awali. Jumla ya wananchi 6,756 walipata mafunzo hayo katika kipindi hicho. Idadi hii ni pungufu kwa asilimia 52.1 ya wahitimu wa mafunzo hayo katika mwaka 2014/15. Malengo yaliyowekwa ya kuwa na idadi kubwa ya wananchi kuhudhuria mafunzo hayo mwaka 2015/16 hayakufikiwa. Kutofikiwa kwa lengo hili kulitokana na kupisha mchakato wa uchaguzi mkuu. Hata hivyo, napenda kutoa wito kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika mafunzo haya na pia kutoa misaada stahiki katika kuendesha mafunzo hayo ikiwemo uhifadhi wa maeneo ya mafunzo.

**(iii) Huduma za Afya na Tiba**

36. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya kiulinzi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za tiba kwa maafisa, askari, Watumishi wa Umma, familia za Wanajeshi na Wananchi kwa ujumla. Katika kuboresha huduma hizo shughuli mbalimbali zilifanyika zikiwemo kuajiri wataalam wa tiba 143 (Madaktari Bingwa, Madaktari wa kawaida na Wataalam wengine wa tiba) na ujenzi wa Chuo cha kijeshi cha Sayansi za Tiba na miundombinu yake katika kambi ya Lugalo kilichojengwa kwa msaada wa Serikali ya Ujerumanî ambacho kilifunguliwa rasmi tarehe 29 Septemba, 2015. Chuo hicho kinatoa elimu ngazi ya Stashahada ya juu kwa fani za udaktari msaidizi, uuguzi, maabara na famasia. Wizara inafanya kazi ushauri wa Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama wa kupandisha hadhi chuo ili kufikia kiwango cha kutoa shahada.

37. **Mheshimiwa Spika**, gharama ya kutoa huduma za matibabu kwa wanajeshi ni kubwa, hususan upande wa madawa na vifaa tiba. Aidha, ufinyu wa bajeti umesababisha huduma za matibabu kwa Wanajeshi kutolewa chini ya kiwango. Wakati huo huo fedha zinazotolewa kwa ajili ya matibabu hazikidhi gharama halisi. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2012/13 fedha zilizoombwua ziliikuwa **Shilingi 6,431,381,023.00** na zilizotolewa ni **Shilingi 1,885,452,645.00** sawa na **asilimia 29**. Mwaka wa fedha 2013/14, fedha zilizoombwua ziliikuwa **Shilingi 6,450,948,623.00** na zilizotolewa ni **Shilingi 2,425,907,880.00** sawa na **asilimia 37.6** na mwaka wa fedha 2014/15 fedha zilizoombwua ziliikuwa **Shilingi 7,803,669,434.00** fedha zilizotolewa **shilingi 2,392,861,854.00** sawa na asilimia 30.7 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/16 fedha zilizombwa ziliikuwa **Shilingi 5,351,660,000.00** na hadi kufikia mwezi Machi, 2016 fedha zilizotolewa ni **Shilingi 2,461,700,000.00** sawa na **asilimia 46.0** ya fedha zilizombwa. Kutokana na hali hii ya upungufu wa fedha kutoka Serikalini, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuititia vikao mbalimbali iliona umuhimu wa kuanzisha mfuko wa Bima ya Afya mahsus kwa ajili ya Wanajeshi kama njia mbadala ya kuwawezesha Wanajeshi na familia zao kupata huduma zenye uhakika za matibabu.

### **Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine**

38. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza lengo la Serikali la kudumisha usalama na amani duniani, Jeshi limeendeleza ushirikiano na Majeshi ya nchi nyingine katika nyanja za kiulinzi ambapo, maafisa wa ngazi mbalimbali wameendele kusoma katika vyuo vya kijeshi katika nchi marafiki zikiwemo China, Kenya, Uganda, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Marekani, Ujeruman, Uingereza, Urusi na Falme za Kiarabu. Pia, maafisa kutoka katika baadhi ya Nchi hizi walikuwepo hapa nchini katika vyuo vyetu vya kijeshi kwa mafunzo. Vyuo hivyo ni Chuo cha Maafisa Monduli (TMA), Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC) Arusha na Chuo cha Ulinzi wa Taifa (NDC) Dar es Salaam. Kwa ujumla ushirikiano na nchi hizo umekuwa ni wa manufaa makubwa kwetu kwani kuititia ushirikiano huo, Jeshi letu limenufaika katika nyanja za mafunzo ya kijeshi na kitaaluma, zana na vifaa, mazoezi na michezo.

### **(v) Ushirikiano na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa**

39. **Mheshimiwa Spika**, ustawi na maendeleo ya Taifa letu yatakuwa salama ikiwa amani na utulivu utakuwepo baina ya nchi yetu na nchi majirani na pia ndani ya nchi hizo. Kwa kuzingatia umuhimu huo katika mwaka 2015/16 Jeshi limeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni

za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Operesheni hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kikosi kimoja cha Jeshi (TANZBATT -9) kipo Darfur nchini Sudan,
- Kikosi kimoja (TANZBATT -3) kipo Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ikiwa ni sehemu ya MONUSCO Force Intervention Brigade– FIB,
- Kombanii mbili za Polisi Jeshi zipo nchini Lebanon na,
- Maafisa wanadhimu na waangalizi wa Amani wapo katika nchi za Sudan, Sudan Kusini, Ivory Coast, Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

#### (vi) Ushirikiano wa Jeshi na Mamlaka za Kiraia

40. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 JWTZ limeendelea kushiriki shughuli mbalimbali za kiraia ikiwa ni pamoja na kusaidiana na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 umefanyika katika mazingira ya amani na utulivu. Aidha, Jeshi lilishirikiana na Mamlaka za Kiraia katika uokozi wa waathirika waliozama katika Kivuko cha Kilombero tarehe 27 Januri, 2016.

#### (vii) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana

41. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambuaumuhimu wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu, Serikali imeendeleza azma yake ya kuwajenga vijana wa Kitanzania katika uzalendo, ukakamavu, maadili mema, utaifa pamoja na kutoa stadi za kazi. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo kifedha, azma hiyo kwa sasa inatekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa baadhi ya vijana wa kujitolea na vijana wa Mujibu wa Sheria. Katika mwaka 2015/16 jumla ya vijana 27,463 walipatiwa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, kati yao vijana 19,946 ni wa Mujibu wa Sheria ambapo wavulana ni 15,212 na wasichana ni 4,734 na vijana 7,517 ni wa kujitolea ambapo wavulana ni 5,843 na wasichana ni 1,674. Mahudhurio hayo ya vijana wa mujibu wa sheria ni sawa na asilimia 58.5 ya lengo katika mwaka. Hata hivyo, idadi ya mahudhurio ni pungufu ikilinganishwa na lengo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo fedha kutopatikana kwa wakati na kadri ya bajeti, upungufu wa miundombinu katika makambi na vikosi hivyo kutoweza kuchukua vijana wote kwa mkupuo mmoja. Aidha, bado changamoto ya mgongano wa muda wa kuhudhuria mafunzo ya JKT awamu ya pili na muda wa kuanza kwa mafunzo ya Elimu ya Juu (mwezi Septemba) haijapatiwa ufumbuzi. Wizara inaendelea kutafuta uwezekano wa kuwawezesha JKT kuchukua kundi la vijana wa Mujibu wa Sheria kwa mkupuo mmoja wa Juni hadi Agosti ili kuwawezesha vijana wote kuweza kuhudhuria mafunzo hayo na kuwahi muhula wa kuanza masomo katika vyuo vya Elimu ya juu.

42. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuendelea kusitiza kuwa dhamira ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwalea vijana wa kitanzania katika maadili mema, kuwajenga kinidhamu, kuwajengea uzalendo kwa nchi yao, kuwajengea ukakamavu, na kuwapa ujuzi na stadi za kazi ili kuwaandalia mazingira mazuri ya kujiajiri mara wamalizapo mkataba wa mafunzo yao. Nichukue fursa hii kuwaomba vijana wanaopata mafunzo ya JKT wazingatие maarifa na ujuzi wanaoupata hususan wa stadi za kazi ili waweze kujiajiri badala ya imani ilioanza kujitokeza kwa baadhi ya wahitim JKT kudai ajira na kuandaa maandalaman badala ya kujivezesha.

43. **Mheshimiwa Spika**, katikahatuaya kutekeleza agizo la Serikali linalohusu vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuajiri kwa idadi kubwa vijana waliohitimu mafunzo ya JKT, hadi kufikia Februari, 2016 vijana 5,453 waliopitia mafunzo ya JKT walijiriwa na vyombo vya ulinzi na usalama ambapo kati yao vijana 3,521 walijiriwa na JWTZ, Polisi vijana 1,185, Usalama wa Taifa vijana 106, TAKUKURU vijana 24 na Jeshi la Zimamoto vijana 617. Hata hivyo, idadi ya vijana waliopata ajira katika vyombo hivi imeongezeka katika mwezi Machi na Aprili, 2016 ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2016 jumla ya vijana 7,170 wameajiriwa na vyombo hivyo katika mchanganuo ufuatao; Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeandikisha vijana 3,531, Jeshi la Polisi limeajiri vijana 1,185, Usalama wa Taifa vijana 106, Jeshi la Zimamoto vijana 617, Uhamiaji vijana 292, Magereza vijana 1,415 na TAKUKURU imeajiri vijana 24.

44. **Mheshimiwa Spika**, mtakumbuka kwamba katika mwaka wa fedha 2012/13, Wizara yangu iliratibu mafunzo maalum ya wiki tatu ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Waheshimiwa Wabunge vijana. Mafunzo hayo yaliyoanza rasmi tarehe 03 Machi, 2013 na kufungwa tarehe 26 Machi, 2013 yalienda sambamba na kuzinduliwa kwa mafunzo ya vijana kwa Mujibu wa Sheria. Ingawa wabunge 47 walijiandikisha, ni wabunge 24 tu ndiyo walihudhuria mafunzo hayo. Aidha, kati ya wabunge hao 24, Waheshimiwa Wabunge 22 ndiyo waliohitimu mafunzo hayo. Miiongoni mwa mapendekezo waliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge waliohitimu mafunzo hayo ni kuwa, mafunzo haya yawe endelevu na muda wa mafunzo uongezwe.

45. **Mheshimiwa Spika**, wakati wa kikao kati ya Wizara yangu na Kamati ya Kudumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Hesabu za Serikali uliofanyika tarehe 4 Aprili, 2016 jijini Dar es Salaam, Kamati ilishauri Wizara iandae mafunzo mengine ya JKT kwa Waheshimiwa Wabunge. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imefanya kazi ushauri huo na kuandaa utaratibu wa mafunzo maalum ya wiki 6 kwa Waheshimiwa Wabunge vijana. Mafunzo hayo yataanza rasmi tarehe 01 Julai, 2016. Hivyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge walioko tayari wajitokeze kupitia Ofisi ya Spika na kuwasilisha orodha yao mapema kwa maandalizi yetu.

**(viii) Mapambano dhidi ya UKIMWI**

46. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na janga la ukimwi na athari zake katika mwaka 2015/16 Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali katika vikosi na kamandi zote za Jeshi la Wananchi, Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Taasisi zake za Mzinga na Nyumbu. Mikakati inayotumika katika mapambano hayo ni uelimishaji rika, kuhamasisha upimaji wa hiari, utoaji wa dawa za kupunguza makali ya ukimwi (Anti-retravirals) na lishe kwa wale walioathirika wakiwemo Watumishi wa Umma na Wanajeshi pamoja na familia zao.

**(ix) Uwajibikaji kazini**

47. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua ya kudumisha dhana ya uwajibikaji sehemu za kazi, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa watumishi katika hatua mbalimbali za maamuzi na utekelezaji wa majukumu, mapambano dhidi ya rushwa na utekelezaji wa sheria na kanuni za manunuzi ya Umma. Ushirikishwaji wa wafanyakazi hufanyika kuitia wawakilishi wao kwa kutoa mawazo na kubainisha changamoto mbalimbali zinazowakabili wakati wa vikao vya Baraza la Wafanyakazi. Pia, watumishi hushirikishwa kwenye maamuzi kuitia vikao vya Idara na Menejimenti. Katika kudhibiti rushwa, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeongeza uwazi katika mawasiliano pamoja na kuendelea kuwa na dawati linaloshughulikia malalamiko ya wafanyakazi. Aidha, Wizara imeendelea kuhimiza watendaji wote wazingatie sheria ya manunuzi nyakati zote. Himizo hili pamoja na suala la kupambana na rushwa na kuepuka matumizi mabaya ya mali za Umma sasa ni agenda za kudumu kwenye vikao mbalimbali vya kiutendaji.

**MATUMIZI YA SHUGHULI ZA MAENDELEO**

48. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha nusu mwaka 2015/16, utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa ujumla haukuwa wa kuridhisha kwa baadhi ya mafungu. Katika kipindi hiki Fungu 57 - Wizara lilipata fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 41,000,000,000.00**, Fungu 38 – Ngome lilipata **Shilingi 1,000,000,000.00** na Fungu 39 JKT halikupatafedha yoyote ya maendeleo. Kwa wastani kwa mafungu kwa mafungu yote matatu yalipokea asilimia 18.1 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kwa mapokezi hayo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeweza kuendeleza utekelezaji wa miradi ifuatayo; kulipia madeni ya kimikataba kwa ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, kuendeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 10,000 za makazi ya wanajeshi, ukarabati wa miundombinu katika makambi ya JWTZ, makambi na viteule vya JKT, uendelezaji wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, uboreshaji wa mawasiliano

salama Jeshini, ukamilishaji wa chuo cha Ukomanda na Unadhimu Duluti na Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Lugalo. Aidha, shughuli za uzalishaji mali katika Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMAJKT) na uendelezaji wa utafiti na teknolojia katika Shirika la Mazao ya Kijeshi Mzinga na Nyumbu ziliendelea kufanyika.

(i) **Ununuzi wa Zana na Vifaa vya Kijeshi**

49. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16, Serikali imeendelea kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa ili kufikia azma yake ya kuwa na Jeshi dogo na la kisasa. Katika kipindi hicho, Jeshi limeendelea kupokea zana na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi wa nchi kavu, anga, na majini. Upokeaji wa zana na vifaa hivyo, umeimarisha uwezo wa Jeshi letu kutekeleza majukumu yake ya ulinzi kwa ufanisi mkubwa. Kulingana na mahitaji ya Jeshi na mabadiliko ya teknolojia na Mpango wa Maendeleo wa Wizara, ununuzi wa zana na vifaa bora na vya kisasa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi ni endelevu na wa kudumu.

(ii) **Ujenzi wa Nyumba na Makazi ya Wanajeshi**

50. **Mheshimiwa Spika**, wakati nawasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/16 nililitaarifu Bunge lako tukufu juu ya kuendelea kwa ujenzi wa nyumba 10,000 za kuishi wanajeshi vikosini unaotekeliza kwa awamu. Awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa nyumba 6,064 unaendelea katika mikoa 9 ya Tanzania Bara na Visiwani. Ujenzi huo umekuwa ukiendelea vizuri katika mikoa hiyo ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2016 jumla ya nyumba 4,744 zilikuwa zimekamilika kujengwa sawa na asilimia 78.2 ya lengo.

51. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kwamba hadi mwezi Aprili, 2016, ujenzi kwa ujumla katika mikoa hiyo umeendelea vizuri Zaidi na kufikia asilimia 85.5 ambapo nyumba 5,184 zimekamilika na nyumba 880 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi ambao unaendelea vizuri. Mchanganuo wa nyumba zilizokamilika ni kama ifuatavyo; Arusha (nyumba 664), Dar es Salaam (2,256), Pwani (840), Tanga (312), Morogoro (416), Dodoma (376) na Pemba (320).

(iii) **Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMAJKT)**

52. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Kujenga Taifa kuitia Shirika lake la Uzalishaji Mali (SUMAJKT) limeendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika Sekta za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Uhandisi na Ujenzi, Viwanda na Biashara, ili kuzalisha mali. Aidha, Shirika lina kampuni tanzu ya SUMAJKT GUARD LTD inayojishughulisha na masuala ya ulinzi kwa Taasisi za Umma na watu binafsi na SUMAJKT SEED CO. LTD inayojishughulisha na ununuzi na usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima.

53. **Mheshimiwa Spika**, katika msimu wa mwaka 2015 SUMAJKT ilifanikiwa kulima ekari 3,627.5 za mazao mbalimbali. Hadi kufikia Februari, 2016, sehemu kubwa ya mazao yaliyolimwa bado yapo shambani katika hatua mbalimbali. Kati ya hizo, ekari 1679 ni za mahindi, ekari 500 ni za mpunga, ekari 205 ni za mbogamboga, ekari 867 ni za ufuta na ekari 317 ni za alizeti na ekari 59.5 za mazao mengine mbalimbali. Aidha, kupitia kampuni yake ya mbegu bora SUMAJKT SEED CO. LTD, Shirika lilifanikiwa kuzalisha mbegu bora za aina mbalimbali za mazao tani 1,767 kutokana na ekari 1,023 zilizolimwa.

54. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na shughuli za kilimo, shirika liliijhusisha na ufugaji wa samaki ambapo kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) lilianza na kuendelea kujishughulisha na ufugaji wa samaki katika viteule vya Bulamba, Karukekekere na Tarime. Aidha, shirika limeweza kutoa mafunzo ya ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa na vizimba kwa wanakijiji 92 na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa 72. Vilevile, SUMAJKT imefanikiwa kujenga nyumba katika kambi ya Ruvu JKT itakayotumika kwa ufugaji wa samaki unaozingatia teknolojia ya uhifadhi wa uoto wa asili (aquaponic na hydroponic). Shirika pia limeanza ufugaji wa nyuki ambapo jumla ya mizinga 744 imetundikwa.

55. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/16 SUMAJKT limeendelea kuagiza matrekta ikiwa ni awamu ya tatu kwa ajili ya kuyauza kwa wakulima na Taasisi mbalimbali ili kufanikisha kauli mbiu ya kilimo kwanzu. Katika kipindi hicho jumla ya matrekta 108 na majembe 110 yenye thamani ya **USD 1,919,540.00** yaliagizwa kutoka India. Hadi kufikia Januari, 2016 jumla ya matrekta 98 yenye thamani ya **Shilingi 4,386,321,491.00** yalikuwa yameuzwa na vipuri vyenye thamani ya **Shilingi 241,545,633.00** vilikuwa vimeuzwa.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mapato ya shirika mwaka wa fedha 2015/16 SUMA GUARD Co. LTD ambayo ni Kampuni tanzu ya shirika, imeendelea kutoa huduma za Ulinzi katika Taasisi za Umma na Sekta binafsi zikiwemo Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Mali Asili na Utalii na vyuo vyake, Wizara ya fedha, TANESCO na vituo vyake, Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM), baadhi ya migodi ya Madini kama vile, Mgodi wa Tulawaka, Biharamulo na Chunya. Washitiri wengine ni pamoja na Chuo cha Madini Nzega, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, United Bank of Africa, CRDB na TEMESA (Kivuko cha Kivukoni). Hadi sasa Kampuni ina jumla ya walinzi 2,777, kati yao wanaume ni 2,275 na wanawake ni 502. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la walinzi 737 ikilinganishwa na walinzi 2,040 waliokuwepo mwaka wa fedha 2014/15. Pamoja na Kampuni kupanua wigo wa kutoa huduma zake, inakabiliwa na changamoto ya kutolipwa madeni kutoka kwa washitiri wake yanayofikia kiasi cha **Shilingi 2,962,245,741.00**. Hivyo Kampuni inakabiliwa na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua zana na vifaa bora vya kisasa. Aidha, rai

inatolewa kwa Washititri wote wanaodaiwa na Kampuni hii walipe madeni yao haraka ili kuiwezesha kampuni kusonga mbele.

57. **Mheshimiwa Spika**, SUMAJKT limeanzisha mradi mpya wa kuchakata kokoto eneo la Pongwe Msungula, Msata ujulikanao kwa jina la SUMAJKT ANIT ASFALT LTD. Mradi huu ulizinduliwa rasmi Mwezi Oktoba, 2015 na Rais wa awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mradi huu unamilikiwa kwa ubia kati ya SUMAJKT inayomiliki asilimia 30 ya hisa na Kampuni kutoka nchini Uturuki ijulikanayo kama ANIT ASFALT inayomiliki asilimia 70 ya hisa.

(iv) **Shughuli za Shirika la Mzinga**

58. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2015/16 Shirika kupitia mapato yake madogo ya ndani limeendelea na uzalishaji katika mkondo wa risasi katika kaliba mbalimbali na utekelezaji wa majukumu mengine ikiwemo kufanya ukarabati wa miundombinu ya Shirika. Kwa upande mwingine kampuni yake tanzu ya Mzinga Holding imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ya Taasisi za Serikali na binafsi kwa ajili ya kupata kipato. Miradi hiyo ni pamoja na:- ujenzi wa awamu ya kwanza wa jengo la Halmashauri mpya ya Ikungi Singida, Ofisi ya Wilaya mpya ya Mkalama Singida, ujenzi wa jengo la TUAKA SACCOS LTD. Karagwe na ujenzi wa jengo la Biashara la Kanisa Katoliki Morogoro.

(v) **Shughuli za Shirika la Nyumbu**

59. **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Nyumbu linafanya utafiti na uendelezaji wa teknolojia wa magari ya kijeshi. Katika mwaka 2015/16, Shirika lilipanga kutekeleza shughuli zake za kuendeleza utafiti katika teknolojia ya magari na mitambo ya kijeshi, kuimarisha na kuongeza uwezo wa kuhawilisha teknolojia mbalimbali za utafiti na kukarabati miundombinu ya Shirika. Kutokana na ukosefu wa fedha za maendeleo, Shirika halikuweza kutekeleza shughuli zake za msingi. Hata hivyo, kwa kutumia mapato madogo ya ndani shirika limeendelea kufanya utafiti wa zana na vifaa mbalimbali vyta kijeshi ikiwa ni pamoja na; magari ya deraya, zana za kilimo kama trekta ndogo (power tiller) vipuli vyta treni, na uzalishaji mdogo wa bidhaa na vipuli mbalimbali kwa ajili ya sekta za kilimo, viwanda na usafirishaji. Aidha, Shirika lipo katika mazungumzo na Kampuni ya Histomart (Pty) Ltd ya Afrika Kusini kwa ajili ya uhawilishaji wa teknolojia na kujielekeza katika kuboresha matengenezo ya magari na Kampuni ya NORINCO kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa ajili ya kuhawilisha teknolojia ya utengenezaji wa magari ya deraya na mapigano.

(vi) **Uthamini, upimaji na ulipaji fidia wa maeneo kwa matumizi ya Jeshi.**

60. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa awali, mionganoni mwa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kutafuta, kuyaendeleza na kuyatunza maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za majeshi yetu. Pamoja na

shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanyika ndani ya maeneo hayo, lililo muhimu pia ni kuyamiliki kisheria. Maeneo mengi ya Jeshi yaliyopo bado kumilikiwa kisheria, hivyo kumekuwepo na migogoro ya umiliki kati ya Jeshi na Wananchi wachache. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 tumeweza kufanya uthamini wa fidia maeneo ya Ilemela na Lukobe mkoa wa Mwanza na hatua inayofuatia ni ya ulipaji fidia. Aidha, maeneo ya Jeshi yaliyopo KTC Kunduchi na Ubungo Kibangu yamepimwa na kuwekewa alama upya ili kuzuia kuvamiwa na wananchi.

61. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa zoezi la upimaji, uthamini na ulipaji fidia maeneo ya Jeshi ni endelevu, mwaka wa fedha 2016/17 upimaji na uboreshaji mipaka ya maeneo ya Jeshi unategemewa kufanyika katika maeneo ya; Biharamulo na Kaboya, Muleba Mkoani Kagera, Uyui, Mirambo na Usule mkoani Tabora, Tunduru mkoani Ruvuma, Mtanda mkoani Lindi, Mtipa mkoani Singida, Maziwa ya Ngombe na Masuke Pemba, Bavuai, Chukwani na Bububu Unguja. Kuhusu uthamini na ulipaji fidia, maeneo yatakayohusika ni Kimbiji, Temeke na Tanganyika Packers mkoani Dar es Salaam, Kigongo Ferry mkoani Mwanza, Kaboya, Muleba mkoani Kagera, Ronsoti, Tarime mkoani Mara na Ras Nondwa mkoani Kigoma.

62. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inakabiliwa na migogoro ya ardhi ya muda mrefu inayotokana na baadhi ya wananchi na Taasisi kuvamia maeneo ya ardhi ya Jeshi. Ili kukabiliana na changamoto hii hatua mbalimbali zikiwemo za kisheria zinaendelea kuchukuliwa. Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kuwasihhi wananchi wasivamie maeneo ya Jeshi wala kuendesha shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo. Naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kusaidia kuwashamasisha wananchi kuheshimu maeneo yanayomilikiwa na Jeshi ili kuepuka kuingia kwenye migogoro na Jeshi. Wizara yangu itaendelea na utaratibu wake wa kulipatia Jeshi maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi yake.

## **CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA 2015/16**

63. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kupatiwa kiwango pungufu cha fedha ikilinganishwa na mahitaji halisi ambayo ni makubwa. Aidha, hali ya mapokezi ya fedha imekuwa hairidhishi. Kwa mwaka 2015/16 wakati kiasi kilichoidhinishwa ni **Shilingi 1,679,209,285,000** fedha iliyopokelewa hadi sasa ni **Shilingi 1,069,758,080,337.00** sawa na asilimia 63.7 ya bajeti. Katika bajeti hiyo, fedha kwa ajili ya shughuli za Maendeleo ni **Shilingi 232,137,958,000.00**. Mapokezi hadi mwezi Machi, 2016 yalikuwa ni **Shilingi 42,000,000,000.00** sawa na asilimia 18.1 ya bajeti. Hata hivyo, kwa upande wa fedha za Matumizi ya Kawaida, mapokezi yamekuwa ya kuridhisha, ambapo

kati ya **Shilingi 1,447,071,327,000.00** zilizotengwa mapokezi yamekuwa ni **Shilingi 1,027,758,080,337.00** sawa na **asilimia 71.02** ya bajeti.

64. **Mheshimiwa Spika**, hali ya kutengewa bajeti ndogo na kupatiwa fedha pungufu imekuwa ikiathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Jeshi na pia kusababisha ulimbikizaji wa madeni hususan ya kimikataba ambayo tumeingia na makampuni mbalimbali kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi kizana na kivifaa. Aidha, madeni mengine ni yale yanatokana na madai ya Maafisa na Askari, Watumishi wa Umma, huduma za simu, umeme, maji na madai kutoka kwa Wazabuni wengine.

65. **Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha usioendana na mahitaji halisi, pia huathiri utekelezaji wa shughuli nyingine za majengo na miundombinu mingine katika vikosi na makambi. Hali hiyo imeathiri mpango wa kuboresha viwanda, karakana na shughuli za utafiti. Aidha, imekuwa vigumu kwa Wizara kutoa huduma na mahitaji muhimu kwa Wanajeshi, Vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na Watumishi wa Umma. Athari nyingine ni Wizara kutolipa kwa wakati fidia ya maeneo tuliyotwaa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

## **MPANGO WA MWAKA 2016/17**

66. **Mheshimiwa Spika**, mpango wa utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wa mwaka 2016/17 umekusudia kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kulingana na Dira na Dhima ya Wizara. Vilevile, mpango umelenga kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2016/17 – 2020/2021). Shughuli zitakazotekelawa katika mpango huo zitakuwa katika maeneo makuu yafuatayo:-

- i. Kuendelea kulii marisha na kuliogezea uwezo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika utendaji kivita kwa kulipatia vifaa na zana bora za kisasa pamoja na kutoa mafunzo stahiki kwa wanajeshi dhidi ya adui wa ndani na nje,
- ii. Kulijengea Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania mazingira mazuri ya kufanya kazi na makazi ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga nyumba za kuishi wanajeshi katika makambi na kuimarisha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya msingi kama vile chakula, tiba, sare, usafiri, maslahi na stahili kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma,

- iii. Kuimarisha uwezo wa Jeshi katika utafiti na kuendeleza teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia hapa nchini na nje ya nchi,
- iv. Kuendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya uzalendo, umoja wa Kitaifa, ukakamavu na kuwapatia stadi za kazi ili kuwaandaa katika uzalishaji mali na,
- v. Kuimarisha ushirikiano wa kijeshi na kiulinzi na nchi nyingine duniani kupitia Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na ushirikiano na nchi moja moja.

## SHUKRANI

**67. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wafuatao kwa michango yao katika maandalizi ya taarifa hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu: Katibu Mkoo Bw. Job D. Masima; Naibu Katibu Mkoo, Bibi Immaculate P. Ngwalle; Mkoo wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis A. Mwamunyange; Mnadhimu Mkoo, Luteni Jenerali Venance S. Mabeyo; Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali James A. Mwakibolwa; Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, Rear Admiral Rogastian S. Laswai; Mkoo wa Jeshi la Kujenga Taifa, Brigedia Jenerali Michael J. Isamuhyo; Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Anga, Brigedia Jenerali George W. Ingram; Mkurugenzi Mkoo wa Shirika la Nyumbu, Brigedia Jenerali Anselm S. Bahati; na Meneja Mkoo wa Shirika la Mzinga, Brigedia Jenerali Jacob G. Kingu. Aidha, napenda kuwashukuru viongozi wa Wizara waliopita: Bi. Rose M. Shelukindo aliyekuwa Naibu Katibu Mkoo; Luteni Jenerali Samuel A. Ndomba (mst) aliyekuwa Mnadhimu Mkoo; Meja Jenerali Raphael M. Muhuga (mst) aliyekuwa Mkoo wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Salum M. Kijuu (mst) aliyekuwa Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali Joseph F. Kapwani (mst) aliyekuwa Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Anga na Meja Jenerali Dkt. Charles N. Muzanila (mst) aliyekuwa Meneja Mkoo wa Shirika la Mzinga.

**68. Mheshimiwa Spika**, naomba pia kuwapongeza viongozi walioteuliwa na Mhe. Rais: Meja Jenerali Projest Rwegasira kuwa Katibu Mkoo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Meja Jenerali Gaudence Milanzi kuwa Katibu Mkoo Wizara ya Maliasili na Utalii; Bibi Immaculate P. Ngwalle kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkoo wa Wizara ya Ulinzi na JKT; Luteni Jenerali Venance S. Mabeyo kuwa Mnadhimu Mkoo; Meja Jenerali James A. Mwakibolwa kuwa Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu; Brigedia Jenerali George W. Ingram kuwa Mkoo wa Kamandi ya Jeshi la Anga; Brigedia Jenerali Michael J. Isamuhyo kuwa Mkoo wa JKT na Brigedia Jenerali Jacob G. Kingu kuwa Meneja Mkoo wa Shirika la Mzinga. Aidha, nawapongeza Meja Jenerali Salum M. Kijuu (mst) kuwa Mkoo wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Ezekiel E. Kyunga (mst) kuwa Mkoo wa Mkoa wa Geita, Meja Jenerali Raphael M. Muhuga (mst) kuwa Mkoo wa Mkoa wa Katavi

na Brigedia Jenerali Emmanuel E. Maganga (Mst) kuwa Mkuu wa Mkoo wa Kigoma.

**69. Mheshimiwa Spika**, nawashukuru pia, Wakuu wa Idara na Vitengo (Makao Makuu ya Wizara), Wakuu wa Matawi (NGOME), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wa Wizara kwa ushirikiano wao katika kufanikisha majukumu ya Wizara. Aidha, naishukuru Kamati ya Wizara iliyoandaa hotuba hii na Mpiga Chapa wa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundis kwa kuchapisha kwa wakati.

**70. Mheshimiwa Spika**, mwisho, nawashukuru Wahisani mbalimbali ambao wametoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha maendeleo ya Jeshi. Kwa namna ya pekee naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Jeshi la Ukombozi la Watu wa China (PLA) kwa misaada yao ya hali na mali. Aidha, nawashukuru Wahisani wengine wakiwemo: Ujerumani, Canada na Marekani kwa misaada yao. Aidha, tunawashukuru nchi marafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu mbalimbali za kiulinzi. Marafiki hao ni pamoja na Nchi zote wanachama ya Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Marekani, Uingereza, Ufaransa, Italy, Uturuki, Misri, Umoja za Falme za Kiarabu (UAE), India, Bangladesh na Oman. Wahisani pamoja na nchi rafiki hizi wamekuwa wakishirikiana na Jeshi katika mafunzo, mazoezi ya kijeshi, kuongeza na kuimarisha miundombinu ya makazi na tiba.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA MWAKA 2016/17

### (i) Makadirio ya Mapato

**71. Mheshimiwa Spika**, kutokana na majukumu ya msingi ya Wizara yangu, ni bayana kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake haina chanzo kikubwa cha kuiingizia mapato na kuiwezesha kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maduhuli ya Serikali. Chanzo kikuu cha mapato kwa sasa kimebaki kuwa ni makusanyo ya mauzo ya nyaraka za zabuni.

**72. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 70,806,000.00** katika mchanganuo ufuatao:-

Fungu 38 - Ngome	<b>Shilingi 18,000,000.00</b>
Fungu 39-JKT	<b>Shilingi 52,003,000.00</b>
Fungu 57- Wizara	<b>Shilingi 803,000.00</b>
Jumla	<b>Shilingi 70,806,000.00</b>

(ii) **Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

73. **Mheshimiwa Spika**, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kama nilivyoeleza katika hotuba hii, katika mwaka 2016/17 naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,736,530,413,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,488,530,413,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 248,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

**Fungu 38 – NGOME**

<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>Shilingi 1,187,496,021,000.00</b>
<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>Shilingi 10,000,000,000.00</b>
<b>Jumla</b>	<b>Shilingi 1,197,496,021,000.00</b>

**Fungu 39 – JKT**

<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>Shilingi 282,034,214,000.00</b>
<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>Shilingi 8,000,000,000.00</b>
<b>Jumla</b>	<b>Shilingi 290,034,214,000.00</b>

**Fungu 57 – Wizara**

<b>Matumizi ya Kawaida</b>	<b>Shilingi 19,000,178,000.00</b>
<b>Matumizi ya Maendeleo</b>	<b>Shilingi 230,000,000,000.00</b>
<b>Jumla</b>	<b>Shilingi 249,000,178,000.00</b>

**MWISHO**

74. **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti za: Wizara ([www.modans.go.tz](http://www.modans.go.tz)); NGOME ([www.ulinzi.go.tz](http://www.ulinzi.go.tz)); na JKT ([www.jkt.go.tz](http://www.jkt.go.tz)).

**75. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja.**

**SPIKA:** Baada ya hayo, kabla sijamwita Msemaji wa Kamati, kuna wageni walishaulika wa Mheshimiwa Savelina Mwijage ambao wametoka Bukoba ni pamoja na wafuatao Mariam Mwijage, Jenista Mwijage, Christian Mwijage na Emmanuel Mwijage pamoja na Farouk Abdulazizi, pale mliko naomba msimame, ahsanteni sana na karibuni sana. Mama yenu yupo amejaa tele hana wasiwasi. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, anakuja Mwenyekiti mwenyewe kabisa! Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu sana.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha taarifa ya Kamati hiyo. Aidha, ninapenda pia kuwashukuru Wanamuheza kwa kuniamini na kuniweka kwenye jengo hili. Ninawashukuru sana. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii inalo jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta pamoja na mambo mengine zina jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia. Vilevile Kanuni ya 98(1) cha Kanuni za Bunge kimeweka sharti la Kamati ya sekta ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inahusisha mafungu matatu ya kibajeti; Fungu 38 – Ngome, Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo ya awali taarifa hii inafafanua mambo manne yafuatayo:-

- (i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo,
- (ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016,
- (iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maoni ya Kamati na ushauri ambao tutautoa.

Maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa na Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) na kufanya ziara ya ukaguzi kuanzia tarehe 29 Machi hadi tarehe 4 Aprili, mwaka huu 2016.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ilionesha kuwa, pamoja na Wizara hii kupangiwa kiasi cha shilingi 232,137,958,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hadi mwezi wa Februari 2016 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 40 tu. Hii ni sawa na asilimia 17.2 ya bajeti yote ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Wizara hii ilikuwa na miradi 13 ya maendeleo, Kamati iliweza kupata nafasi ya kukagua miradi mitano iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Miradi hiyo ni mradi wa kwanza ni namba 6103 uliojulikana kama Defence Scheme na kutekelezwa chini ya Kifungu 1001 – Defence Forces Headquarters' Command cha Fungu – 38 kwa kasma kubwa mbili ambazo ni kasma 220500 ambayo ni Military Supplies and Services na kasma 230500 amabyo ni Maintainance on Specialised Equipments. Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo.

Mheshimiwa Spika, pili; mradi namba 6327 uliojulikana kama Construction and Rehabilitation of Buildings na kutekelezwa chini ya Kifungu 1001 – Defence Forces Headquarters' Command na Fungu – 38 kwa kasma kubwa mbili ambazo ni kasma 411000 – Rehabilitation and Other Civil Works na 1100 – New Construction and Other Civil Works. Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, tatu; mradi namba 6103 uliojulikana kama Defence Scheme na kutekelezwa chini ya Kifungu 1009 – Independent Telecommunication Network cha Fungu 57. Mradi huu ni kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano salama Jeshini.

Mheshimiwa Spika, nne; mradi namba 6103 uliojulikana kama Defence Scheme na kutekelezwa chini ya Kifungu 2004 – Estate Management and Development Unit cha Fungu 57. Mradi huu ni wa kupima, kuthamini na kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, tano, mradi namba 6103 uliojulikana kama Defence Scheme na kutekelezwa chini ya Kifungu 2001 – Industries Construction and Agriculture cha Fungu 57. Mradi huu ni wa ujenzi na ukamilishaji wa viporo na miundombinu yake pamoja na kuendeleza uzalishaji katika Shirika la Mzinga.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu katika Shirika la Mzinga Morogoro. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa ukamilishaji wa miundombinu ya shirika. Hata hivyo, wakati Kamati inafanya ziara ya ukaguzi mradi ulikuwa haujapokea fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake za maendeleo. Kutokopatikana kwa fedha hizo zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya shirika kumeathiri kazi za uendelezaji wa shirika na uzalishaji wa mazao yake.

Mheshimiwa Spika, kwa ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa miundombinu ya shirika hususan majengo ya viwanda yamechakaa kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Aidha, shirika linakabiliwa na changamoto ya uzalishaji mdogo unaotokana na ukosefu wa fedha za mtaji, ili kuendeleza viwanda na upungufu wa wafanyakazi wenyewe fani mbalimbali za uzalishaji. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inashauri kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kwa ukamilifu hadi kufikia mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ulipaji wa fidia na kupima maeneo yaliyochukuliwa kwa matumizi ya Jeshi Makao Makuu ya Wizara. Kamati ilipokea na kuijadili taarifa kuhusu mradi wa ulipaji fidia na kupima eneo lililochukuliwa na Jeshi na kuelezwa kuwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 shilingi bilioni 7.390 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu, lakini hadi kufikia Februari, 2016 shilingi bilioni 180 tu ndiyo zilikuwa zimepokelewa, sawa na asilimia 2.4 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulilenga kutatua migogoro kwa maeneo ya Jeshi 74 yenyeye ukubwa wa hekta 183,550 ambayo ni asilimia 61 ya ukubwa wa maeneo yote ya Jeshi kwa kulipia fidia na kupima maeneo hayo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kufanyika chini ya mradi huo hazikufanyika kutokana na kutopatikana kwa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Hali hii inaonesha kuwa utatuzi wa migogoro katika maeneo hayo kwa kulipia fidia haukufanyika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa kuimarisha mawasiliano salama jeshini. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi 7,556,800,000 kwa ajili ya kuingiza umeme kwenye minara ya mawasiliano ya Jeshi nchi nzima ili iweze kuanza kazi. Hata hivyo, Kamati ilipoanza ziara na kukagua mradi hakukuwa na fedha zozote zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Jambo hili limesababisha utekelezaji usioridhisha kwa mradi kwani katika minara 135 iliyotakiwa kuwekewa umeme nchi nzima tangu mradi uanze ni minara isiyozidi kumi tu iliyopo Zanzibar, Dar es Salaam na Pwani pekee iliyokwishawekewa umeme.

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 miradi hii iliyopo chini ya Fungu 38 – Ngome ilitengewa jumla ya shilingi bilioni nane. Fedha hizi ziliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu ya JWTZ, hata hivyo Kamati ilipotembelea na kukagua miradi hii hakukuwa na fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kutopteka na ziara ya ukaguzi wa Kamati wa miradi ya mendeleo, kama ilivyoooneshwa hapo, Kamati imebaini kuwa kati ya miradi mitano iliyotembelewa na kukaguliwa hakukuwa na mradi hata mmoja uliopokea fedha zaidi ya asilimia tatu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wake. Hali hii imesababisha kutoptekeliza kwa shughuli za maendeleo kikamilifu kwa ajili ya mafungu yote ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaanini kuwa utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii utaimarisha ulinzi na usalama wa nchi hii. Ni vema basi Serikali iendelee kuzingatia umuhimu wa ulinzi wa Taifa na kuipa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa uzito unaotakiwa katika bajeti zinazofuata kwa kutoa fedha za maendeleo kama zinavyoainishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ulijikita katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari mpaka Machi, 2016 na mahojiano yalichangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa taarifa za ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya bilioni 72.606 lakini hadi mwezi Februari mwaka huu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilifanikiwa kukusanya jumla ya 29,913,500,000. Hii ni sawa na asilimia 41.2 ya makadirio yaliyowekwa. Katika makusanyo hayo Fungu 38 la Ngome lilikuwa limekaribia malengo yake kwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 11.050 sawa na asilimia 95 lakini Fungu la JKT lilikusanya shilingi 18,763,500,000, sawa na asilimia 37 wakati Fungu 57 lilikusanya shilingi 100,000 tu! Hii ni sawa na asilimia 0.9 ya makadirio yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara nyingi. Kwa kuzingatia hilo Kamati ilitaka kujiridhisha kuwa, utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa kulinganisha fedha zilizopatikana kwa mwaka wa fedha 2015/2016

hadi kufikia Februari 2016, kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara katika uchambuzi huo ilionekana kuwa hadi kufikia mwezi Februari Wizara ilikuwa imepokea asilimia 63.6 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti ya maendeleo uchambuzi unaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2016 Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 40 tu sawa na asilimia 17.2 ya shilingi 232,137,958,000 zilizoidhinishwa na Bunge. Fedha hizi ni chache sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ili kupata picha halisi kuhusu uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ililinganisha na kasma ya matumizi yao kwa jumla ya mafungu yote matatu ya Wizara hii na inaonekana kwenye chati namba moja (1).

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huu Kamati imebaini kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara ulikuwa wa kuridhisha ukilinganisha na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo na ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni dhahiri kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo na fedha za maendeleo ya uendeshaji wa shughuli za kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaathirika.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii kwa mwaka 2015/2016 Kamati ilishauri masuala sita yanayopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu bajeti hiyo ambayo masuala hayo ni:-

- (i) Ulipaji na malimbikizo ya madeni ya Wizara;
- (ii) Serikali kutoa fedha zote zilizoainishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara hususan fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu – 38;
- (iii) Kuongeza bajeti ya JKT kwa ajili ya vijana wanaomaliza kidato cha sita kuijunga na JKT;
- (iv) Kufanya marekebisho ya Sheria ya 16 ya mwaka 1964;
- (v) Kuhuisha malipo ya Wanajeshi Wastaifu ngazi zote; na
- (vi) SUMA Guard Limited kulinda taasisi zote za umma.

Mheshimiwa Spika, katika masuala sita yaliyotolewa maoni yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, mengine yanaendelea kuzingatiwa na ambayo hayajazingatiwa kikamilifu kama yanavyoonekana kwenye kiambatisho namba moja (1).

Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa moja ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu na Wizara hii ni kuhusu SUMA Guard Limited kutumiwa na Serikali katika kulinda taasisi za umma na miundombinu muhimu badala ya kuajiri walinzi binafsi baadhi ya malindo hayo ni Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, taarifa ilionesha kuwa Serikali inaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kulipa madeni ya Wizara ya Ulinzi na JKT yaliyofikia kiasi cha 483,980,463,090.91 hadi kufikia Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine uliotolewa ulihusu upatikanaji wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Serikali ilishauriwa kutoa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 38. Ushauri huu haukuzingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati ilijulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itaendelea kuliimarisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ili liwe la kisasa na lenye utimamu na utayari kutekeleza majukumu yake. Kamati iliridhika na lengo hilo ambalo linakamilisha dhima ya Wizara kulinda uhuru, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhakikisha kuwa mamlaka ya nchi yako salama. Hata hivyo, ili kufanikisha azma hiyo Kamati inasisitiza kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa utekelezaji wa majukumu tajwa zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ikizingatiwa kuwa suala la ulinzi na usalama ni nyeti sana na kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio wa mapato. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 70,806,000,000 kwa mchanganuo ufuatao; Fungu 38 - Ngome shilingi 18,000,000; Fungu 39 - JKT shilingi 52,003,000; Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa shilingi 802,000 jumla inakuwa shilingi shilingi 70,806,000.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa mafungu yote matatu ni shilingi 1,720,865,159,000. Kiasi hicho ni ongezeko la shilingi 41,767,262,000 sawa na asilimia 2.48 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya Fungu – 38 ni shilingi 1,197,496,021, hiyo ni sawa na asilimia 69.5 ya bajeti ya Wizara nzima kwa mafungu yote matatu. Ni dhahiri kuwa, fedha hizi zikitolewa zote kama zinavyoombwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaendelea kuimarika na kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, maoni sasa na ushauri wa Kamati, ni dhahiri kuwa kwa Taifa letu ni jambo la muhimu sana hivyo linatakiwa kupewa uzito unaotakiwa katika mipango ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Kwa kuzingatia hili Kamati inatoa ushauri wa namna kuu mbili zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, ushauri wa jumla ni kuwa kutokana na taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye vikao vya Kamati kwa kipindi cha Machi hadi Aprili, 2016, Kamati inatoa ushauri wa jumla ufuatao:-

- (i) Serikali ihakikishe kwamba, fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ili shughuli za ulinzi zitekelezwe kama ilivyopangwa.
- (ii) Serikali kupitia Hazina ilipe madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa.
- (iii) Mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kushirikiana na Wizara wawe wabunifu katika kutafuta mbinu za ziada na kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kiraia, ili kuongeza mapato yao ikiwa ni pamoja na mitaji ya kuzalisha silaha.
- (iv) Miradi ya nyumba za wanajeshi ilenge zaidi askari wa kawaida kwanza ambaeo ndio wenyewe uhitaji mkubwa wa makazi.
- (v) Ili kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima kati ya Jeshi na Wananchi, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi iruhusu Jeshi kumiliki maeneo yake kisheria na kwa kuifanya mabadiliko Sheria ya Ardhi Namba 4 na 5 ya mwaka 1999. Hii italisaidia Jeshi kutopoteza maeneo yake kutokana na kutokuwa na nyaraka za kumiliki ardhi kisheria.
- (vi) Kwa kuwa mpaka sasa Jeshi linahitaji takribani shilingi bilioni 35 kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Hazina kutoa fedha hizo mara moja ili kupunguza migogoro iliyopo.
- (vii) Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuwezesha maeneo yote ya Jeshi kupimwa ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima.
- (viii) Jeshi lifanye utaratibu wa kuongeza maeneo yake kwa kutwaa maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi ambayo hayana msongamano na watu.

(ix) Serikali iwe na mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa kila Mkuu wa Kikosi anaifahamu vizuri mipaka na analinda mipaka ya kambi yake ili kuzuwia uvamizi wa maeneo ya Jeshi.

(x) Maeneo yote yaliyotolewa na Mamlaka ya Mikoa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi yarasimishwe kisheria ili kuepuka migogoro pale ambapo uongozi wa mkoa unapobadilika.

(xi) Maeneo yote ya Jeshi yawekewe uzio ili kuепusha maeneo hayo kuvamiwa na raia.

Mheshimiwa Spika, ushauri mahsusni kuwa kumbukumbu zinaonesha kuwa Wizara imekuwa ikishauriwa kuhusu malipo ya wanajeshi wastaafu, bajeti ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria na fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT. Hata hivyo, taarifa zilizowasilishwa kwa Kamati hazioneshi kutekelezwa kwa ushauri huo. Kwa msingi huu Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, malipo ya wanajeshi wastaafu; mapendekezo ya maboresho ya malipo ya pensheni kwa wanajeshi wa vyeo vyote yaliyowasilishwa Serikalini katika mwaka wa fedha 2008/2009 hata hivyo, tangu kuwasilishwa kwa mapendekezo hayo Serikali imeboresha malipo ya pensheni kwa cheo cha Meja Jenerali hadi Jenerali tu kuanzia mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendele kuishauri Serikali kuhuisha malipo ya pensheni kwa wastaafu wa Jeshi kwa ngazi zote amba walistaafu kabla ya mpango mpya wa stahili mpya kutolewa ili pamoja na kuondoa malalamiko kutoka kwa wanajeshi wastaafu, kuthamini kazi na mchango wao wa kutunza ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya mafunzo ya JKT kwa vijana wanaomiliza kidato cha sita, zipo faida za vijana wanaomiliza kidato cha sita kuijunga na JKT ikiwa ni pamoja na kuondoa matabaka na kujenga umoja wa kitaifa baina ya vijana, kuwa na Jeshi la Akiba, pamoja na kukuza uzalendo wa vijana. Kwa kutambua umuhimu huo, mwaka wa fedha wa 2016/2017 Serikali imetenga jumla ya shilingi 20,100,000,000 kwa ajili ya mafunzo ya vijana hao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kiwango hicho bado ni kidogo sana ukilinganisha na lengo lililopo la kuwapatia mafunzo vijana 34,100. Kamati inashauri Serikali itenye bajeti ya kutosha kuliwezesha Jeshi kumaliza ukarabati wa makambi yake ili kuweza kuchukua wahitimu wengi zaidi wa mkupuo.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT limeendelea kuwa changamoto kwa Jeshi la Kujenga Taifa. Kifungu 34 cha Sheria ya 16 ya mwaka 1964 kinataja fidia kwa vijana kulipwa kwa kuzingatia Sheria ya Workers Compensation Act, kwa kuwa fidia yote inayofanywa chini ya sheria hii inafanywa na mahesabu ya vigezo vyta muda wa utumishi na mshahara.

Mheshimiwa Spika, vijana walioko kwenye mafunzo wanaathirika kwa muda wao ni mfupi na vilevile hawana mishahara bali posho tu, aidha kwa kifungu namba 23 cha Sheria namba 16 ya mwaka 1994. Kinaleza vijana huchukuliwa kuwa ni askari wa kudumu wakati wa mafunzo ya kijeshi na kivita, kwa madhumuni ya kufidiwa. Sheria bado haijaweka wazi ni kwa cheo gani kijana huyu atafanyiwa mahesabu hayo. Kamati inashauri ili kuondoa mkanganyiko huo uliopo, ni vema marekebisho ya sheria yakafanyika, ili suala la fidia kwa vijana liingizwe chini ya Sheria ya JKT ya mwaka 1964 au Sheria ya Ulinzi ya mwaka 1966. Aidha, kifungu cha 23 cha Sheria ya JKT kitaje wazi cheo gani kinachopendekezwa kwa ajili ya kufanyiwa mahesabu ya fidia kwa vijana hao.

Mheshimiwa Spika, hitimisho napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama wote ambao wameshiriki kikamilifu, kwa maoni yao, ushauri na ushirikiano wao ambao umeweza kumshukuru sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa ushirikiano wake mkubwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii. Aidha, namshukuru pia Katibu Mkuu ndugu Job Masima na Naibu Katibu Mkuu, Bi Immaculate Ngwale, pamoja na watendaji wote, Wakuu wa Majeshi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha nawashukuru Makatibu wetu wa Bunge ambao wamefanya kazi nzuri, kuweza kuratibu maelezo haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho baada ya maelezo hayo sasa, naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Yale ambayo sikuyaeleza naomba yote yachukuliwe kwenye Hansard.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (Makofi)

**SPIKA.** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab kwa hotuba yako nzuri, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama.

**TAARIFA YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA,  
KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA FUNGU 38, FUNGU 39, NA FUNGU 57  
KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO  
KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii inalo jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeainisha kuwa Kamati za Kudumu za Kisekta, pamoja na mambo mengine, zina jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Vilevile, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na kuchambua bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inahusisha Mafungu matatu (3) ya Kibajeti: Fungu 38- Ngome, Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maelezo hayo ya awali, Taarifa hii inafafanua mambo manne (4) yafuatayo:-

- i. Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
- iii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na
- iv. Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016

### 2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi kuanzia tarehe 29 Machi hadi 04 Aprili, 2016. Hali halisi ilionesha kuwa pamoja na Wizara hii kupangiwa kiasi cha Shilingi **232,137,958,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hadi mwezi Februari, 2016 Wizara ilipokea kiasi cha Sh. **40,000,000,000.00** tu, sawa na asilimia 17.2 ya bajeti yote ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa Wizara hii ilikuwa na Miradi kumi na tatu ya Maendeleo, Kamati ilikagua miradi mitano (5) iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Miradi hiyo ni:-

- i) Mradi Namba 6103 uliojulikana kama 'Defence Scheme' na kutekelezwa chini ya Kifungu 1001 – 'Defence Forces Headquarters' Command' cha Fungu 38 kwa Kasma kubwa mbili ambazo ni Kasma 220500- 'Millitary Supplies and Services' na Kasma 230500- 'Maintenance of Specialised Equipments'. Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo;
- ii) Mradi Namba 6327 uliojulikana kama 'Construction and Rehabilitation of Buildings' na kutekelezwa chini ya kifungu 1001-'Defence Forces Headquarters' Command' cha Fungu 38 kwa Kasma kubwa mbili ambazo ni Kasma 411000- 'Rehabilitation and Other Civil Works' na 411100- 'New Construction and Other Civil Works'. Mradi huu ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu;
- iii) Mradi Namba 6103 uliojulikana kama 'Defence Scheme' na kutekelezwa chini ya Kifungu 1009– 'Independent Telecommunication Network' cha Fungu 57. Mradi huu ni kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano salama Jeshini;
- iv) Mradi Namba 6103 uliojulikana kama 'Defence Scheme' na kutekelezwa chini ya Kifungu 2004- 'Estate Management Development Unit' cha Fungu 57. Mradi huu ni wa kupima, kuthamini na kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi; na
- v) Mradi Namba 6103 uliojulikana kama 'Defence Scheme' na kutekelezwa chini ya Kifungu 2001- 'Industries Construction and Agriculture' cha Fungu 57. Mradi huu ni wa ujenzi na ukamilishaji wa viporo na miundombinu yake pamoja na kuendeleza uzalishaji katika Shirika la Mzinga.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Mradi wa Ujenzi na Ukamilishaji wa Miundo mbinu katika Shirika la Mzinga – Morogoro

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu ultengewa jumla ya **Shilingi 6,000,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya Shirika. Hata hivyo, wakati Kamati inafanya ziara ya ukaguzi, Mradi ulikuwa haujapokea fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake za maendeleo. Kutopatikana kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo za Shirika hili, kumeathiri kazi za uendelezaji wa Shirika na uzalishaji wa mazao yake.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo Kamati ilibaini kuwa miundombinu ya Shirika hususan majengo ya viwanda, yamechakaa kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Aidha, Shirika linakabiliwa na changamoto ya uzalishaji mdogo unaotokana na ukosefu wa fedha za mtaji ili kuendeleza viwanda na upungufu wa wafanyakazi wenyewe fani mbalimbali za uzalishaji. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inashauri kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kwa ukamilifu hadi kufikia Mwezi Juni 2016.

### 2.2.2 Mradi wa Ulipaji wa fidia na kupima maeneo yaliyochukuliwa kwa matumizi ya Jeshi- Makao Makuu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu mradi wa ulipaji fidia na kupima maeneo yaliyochukuliwa na Jeshi na kuelezwu kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, **shilingi 7,390,000,000/=** zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Hadi kufikia mwezi Februari 2016, **shilingi 180,000,000/=** tu zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 2.4 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

Mradi huu ulilenga kutatua migogoro katika maeneo ya Jeshi 74 yenyewe ukubwa wa Hekta 183,550 (asilimia 61 ya ukubwa wa maeneo yote ya Jeshi) kwa kulipa fidia na kupima maeneo hayo. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kufanyika chini ya mradi huu hazikufanyika kutokana na kutopatikana kwa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Hali hii inaonesha kuwa utatuzi wa migogoro katika maeneo hayo kwa kulipa fidia haukufanyika kama ilivyokusudiwa.

### 2.2.3 Mradi wa Kuimarisha mawasiliano salama Jeshini

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 mradi huu uliotengewa jumla ya shilingi **7,556,800,000.00** kwa ajili ya kuingiza umeme kwenye minara ya mawasiliano ya Jeshi nchi nzima ili iweze kuanza kazi. Hata hivyo, Kamati ilipofanya ziara na kukagua mradi, hakukuwa na fedha zozote zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Jambo hili limesababisha utekelezaji usioridhisha wa mradi kwani kati ya minara 135 inayotakiwa kuwekewa umeme nchi nzima tangu mradi uanze, ni minara isiyozidi 10 iliyopo Zanzibar, Dar es Salaam na Pwani pekee iliyokwisha wekewa umeme.

### 2.2.4 Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo na Miundombinu (Miradi Namba 6103 na 6327)

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 miradi hii iliyopo chini ya fungu 38 (Ngome) ilitengewa jumla ya shilingi **8,000,000,000/=**. Fedha hizi ziliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kukarabati majengo na miundombinu ya JWTZ. Hata hivyo, mpaka Kamati inatembelea na kukagua miradi mwezi Aprili 2015, hakukuwa na fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli zilizopangwa.

### 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa hapo juu, Kamati imebaini kuwa kati ya miradi mitano iliyotembelewa na kukaguliwa, hakukuwa na mradi hata mmoja uliopokea fedha zaidi ya asilimia 3 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wake. Hali hii imesababisha kutokutekelezwa kwa shughuli za maendeleo kikamilifu kwa ajili ya mafungu yote ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa utekelezaji bora wa miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii utaimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Ni vyema basi Serikali iendelee kuzingatia umuhimu wa ulinzi wa Taifa na kuipa Wizara ya Ulinzi na JKT uzito unaotakiwa katika bajeti zinazofuata kwa kutoa fedha za maendeleo kama zinavyoidhinishwa na Bunge.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/ 2016 ulijikita katika makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo pamoja na upatikanaji wa

fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Februari na Machi, 2016, na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

### 3.2 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **72,606,000.00**. Hadi mwezi Februari 2016, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **29,913,500.00** sawa na asilimia 41.2 ya makadirio yaliyowekwa. Katika makusanyo hayo, Fungu 38- Ngome lilikuwa limekaribia malengo yake kwa kukusanya jumla ya shilingi 11,050,000.00 sawa na asilimia 95.3 ya lengo lake, wakati Fungu 39 - JKT lilikusanya **shilingi 18,763,500.00** sawa na asilimia 37.5 na Fungu 57 lilikusanya **shilingi 100,000.00** sawa na asilimia 0.9 tu ya makadirio yaliyowekwa.


### 3.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Serikali umeendelea kuwa changamoto kwa Wizara nyingi. Kwa kuzingatia hilo Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa Mipango ya Bajeti, kwa kulinganisha fedha zilizopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi kufikia Februari, 2016 na kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara. Katika uchambuzi huo, ilionekana kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2016 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 63.6 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, uchambuzi unaonyesha kuwa hadi kufikia Mwezi Februari 2016, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 40,000,000,000.00** tu sawa na asilimia 17.2 ya **shilingi 232,137,958.000.00** zilizoidhinishwa na Bunge. Fedha hizi ni chache sana ukilinganisha na mahitaji halisi ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, ili kupata picha halisi kuhusu uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ililinganisha kasma za matumizi hayo kwa jumla ya mafungu yote matatu ya wizara hii na kuwianisha kama inavyoonekana katika Chati Na. 1

## Chati Namba 1. Uwiano wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2015/2016



### Chanzo- Randama ya Wizara 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo na za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni dhahiri kuwa kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) na fedha za maendeleo, uendeshaji wa shughuli za kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaathirika.

#### 3.4 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2015/2016, Kamati ilishauri masuala sita (6) yanayopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo. Masuala hayo yalihusu:-

- i) Ulipaji wa malimbikizo ya madeni ya Wizara;
- ii) Serikali kutoa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara hususan fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu 38;
- iii) Kuongeza bajeti ya JKT kwa ajili ya vijana wanaomaliza kidato cha sita kuiunga na JKT;
- iv) Kufanya marekebisho ya Sheria namba 16 ya Mwaka 1964;
- v) Kuhuisha malipo ya wanajeshi wastaafu ngazi zote; na
- vi) SUMA GUARD LTD kulinda Taasisi za Umma.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya masuala (6) yaliyotolewa maoni yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, mengine yanaendelea kuzingatiwa na ambayo

hayajazingatiwa kikamilifu kama yanavyoonekana katika Kiambatisho Namba 1.

Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa moja ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu na Wizara ni kuhusu SUMA GUARD LTD kutumiwa na Serikali katika kulinda Taasisi za umma na miundombinu muhimu badala ya kuajiri walini binafsi. Baadhi ya malindo hayo ni Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais- Menejiment ya Utumishi wa umma, Wizara ya Maliasili na Utalii.

Aidha, Taarifa ilioneshwa kuwa Serikali inaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kulipa madeni ya Wizara ya Ulinzi na JKT yaliyofikia kiasi cha **shilingi 483,980,463,090.92** hadi kufikia Juni, 2015. Wizara, kwa kushirikiana na Hazina wamejiwekea utaratibu wa kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya kulipa madeni ili kuepuka tatizo la madeni kukua kutokana na riba ya kuchelewa kuyalipa.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri mwingine uliotolewa ulihusu upatikanaji wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Serikali ilishauriwa kutoa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 38. Ushauri huu haukuzingatiwa kikamilifu.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

##### **4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itaendelea kuliimarisha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ili liwe la kisasa na lenye utimamu na utayari kutekeleza majukumu yake. Kamati iliridhika na lengo hilo ambalo linakamilisha Dhima ya Wizara ya kulinda uhuru, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhakikisha kuwa mamlaka ya nchi yako salama. Hata hivyo, ili kufanikisha azma hiyo, Kamati inasilitiza kuwa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa utekelezaji wa majukumu tajwa zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ikizingatiwa kuwa suala la ulinzi na usalama ni nyeti sana kwa ustawi wa Taifa letu.

##### **4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 70,806, 000.00 kwa mchangano ufuatao:-

- a) Fungu 38 (Ngome)- Shilingi 18,000,000.00
- b) Fungu 39 (JKT)- Shilingi 52,003,000.00

c) Fungu 57 ( Wizara)- Shilingi 802,000.00

<b>Jumla</b>	<b>Shilingi <u>70,806,000.00</u></b>
--------------	--------------------------------------

#### **4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa mafungu yote matatu ni **shilingi 1,720,865,159,000.00**. Kiasi hiki ni ongezeko la **shilingi 41,767,262,000.00** sawa na asilimia 2.48 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2015/2016. Ongezeko hili lipo kwenye fedha za mishahara na za maendeleo ambapo jumla ya **shilingi 1,472,865,159,000.00** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikiwa ni ongezeko la **shilingi 25,905,220,000.00** ikilinganishwa na Bajeti ya 2015/2016. Fedha zinazoombwka kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi **248,000,000,000.00** ikiwa ni ongezeko la **shilingi 15,862,042,000.00** sawa na ongezeko la asilimia 6.8 kwa bajeti ya Mwaka 2015/2016.

Takwimu zinaonesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 bajeti inayoombwa kwa matumizi ya Wizara kwa mafungu yote matatu ni asilimia 5.86 ya bajeti Kuu ya Serikali ambayo ni **shilingi 29,353,000,000,000/-**. Kutokana na ufinyu wa mapato ya Serikali, Kamati imeridhika na Bajeti hii na inaamini kama itatolewa kama inavyoombwa itawezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ya msingi.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwka kwa ajili ya matumizi ya Fungu 38, ni **shilingi 1,197,496,021,000** sawa na asilimia 69.5 ya Bajeti ya Wizara nzima kwa mafungu yote matatu. Ni dhahiri kuwa fedha hizi zikitolewa zote kama zinavyoombwa, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litaendelea kuimarika na kutekeleza wajibu wake.

#### **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, Ni dhahiri kuwa ulinzi wa Taifa letu ni jambo la muhimu sana hivyo linatakiwa kupewa uzito unaotakiwa katika Mipango ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Kwa kuzingatia hili, Kamati inatoa ushauri wa namna kuu mbili zifuatazo:-

##### **5.1 Ushauri wa Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye vikao vya Kamati kwa kipindi cha Machi hadi Aprili, 2016, Kamati inatoa ushauri wa jumla ufuatao:-

- i) Serikali ihakikishe kuwa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati ili shughuli za ulinzi zitekelezwe kama ilivyopangwa;
- ii) Serikali kupitia Hazina ilipe madeni yote ya Wizara yaliyohakikiwa;
- iii) Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kushirikiana na Wizara wawe wabunifu katika kutafuta mbinu za ziada za kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kiraia ili kuongeza mapato yao ikiwa ni pamoja na mitaji ya kuzalisha silaha;
- iv) Miradi ya nyumba za wanajeshi zilenge askari wa kawaida kwanza ambao ndio wenye uhitaji mkubwa wa makazi;
- v) Ili kupunguza migogoro ya ardhi isiyo ya lazima kati ya Jeshi na wananchi, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iruhusu Jeshi kumiliki maeneo yake kisheria kwa kuifanyia mabadiliko Sheria ya Ardhi namba 4 na 5 ya Mwaka 1999. Hii italisaidia Jeshi kutopoteza maeneo yake kutokana na kutokuwa na nyaraka za kumiliki ardhi kisheria;
- vi) Kwa kuwa mpaka sasa Jeshi linahitaji takribani **shilingi bilioni 35** kwa ajili ya kulipa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi, Kamati inashauri Serikali kupitia Hazina kutoa fedha hizo ili kupunguza migogoro iliyopo;
- vii) Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuwezesha maeneo yote ya Jeshi kupimwa ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima;
- viii) Jeshi lifanye utaratibu wa kuongeza maeneo yake kwa kutwaa (kisheria) maeneo yaliyo pembezoni ya Nchi ambayo hayana msongamano wa watu;
- ix) Serikali iwe na mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa kila Mkuu wa Kikosi anaifahamu vizuri mipaka na analinda mipaka ya Kambi yake ili kuzuia uvamizi wa maeneo ya Jeshi;
- x) Maeneo yote yanayotolewa na Mamlaka za Mikoa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi yarasimishwe kisheria ili kuepuka migogoro pale ambapo uongozi wa mkoa unapobadilika; na
- xi) Maeneo yote ya Jeshi yawekewe uzio ili kuepusha maeneo hayo kuvamiwa na raia.

## 5.2 Ushauri Mahsus

**Mheshimiwa Spika**, Kumbukumbu zinaonesha Kuwa Wizara imekuwa ikishauriwa kuhusu malipo ya Wanajeshi wastaafu, bajeti ya Mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria na Fidia kwa Vijana wanaopata mafunzo ya JKT. Hata hivyo, Taarifa

zilizowasilishwa kwa Kamati hazoneshi kutekelezwa kwa ushauri huo. Kwa msingi huu, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

#### 5.2.1 **Malipo ya wanajeshi wastaafu**

**Mheshimiwa Spika**, mapendeleko ya maboresho ya malipo ya pensheni kwa wanajeshi wa vyeo vyote yaliwasilishwa Serikalini katika Mwaka wa Fedha 2008/2009. Hata hivyo, tangu kuwasilishwa kwa mapendeleko hayo, Serikali imeboresha malipo ya pensheni kwa cheo cha Meja Jenerali hadi Jenerali tu kuanzia mwaka 2009. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhuisha malipo ya pensheni kwa wastaafu wa Jeshi kwa ngazi zote amba walistaafu kabla ya mpango mpya wa stahili mpya kutolewa ili pamoja na kuondoa malalamiko kutoka kwa wanajeshi wastaafu, kuthamini kazi na mchango wao wa kutunza ulinzi na usalama wa Taifa letu.

#### 5.2.2 **Bajeti ya Mafunzo ya JKT kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita**

**Mheshimiwa Spika**, zipo faida za vijana wanaomaliza kidato cha sita kujunga na JKT ikiwa ni pamoja na kuondoa matabaka na kujenga umoja wa kitaifa baina ya vijana, kuwa na jeshi la akiba pamoja na kukuza uzalendo wa vijana. Kwa kutambua umuhimu huo, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali imetenga jumla ya **shilingi 20,100,000,000** kwa ajili ya mafunzo ya vijana hao. Hata hivyo, kiwango hicho bado ni kidogo sana ukilinganisha na lengo lililopo la kuwapatia mafunzo vijana 34,100. Kamati inashauri Serikali itenye bajeti ya kutosha kuliwezesha Jeshi kumaliza ukarabati wa makambi yake ili liweze kuchukua wahitimu wengi zaidi kwa mkupuo.

#### 5.2.3 **Fidia kwa vijana wanaopata mafunzo ya JKT**

**Mheshimiwa Spika**, Suala la fidia kwa vijana wanopata mafunzo ya JKT limeendelea kuwa changamoto kwa Jeshi la Kujenga Taifa. Kifungu cha 34 cha Sheria Na. 16 ya Mwaka 1964 kinataja fidia kwa vijana kulipwa kwa kuzingatia sheria ya Workers Compensation Act. Kwa kuwa fidia yoyote inayofanywa chini ya Sheria hii inafanywa kwa mahesabu na vigezo vya muda wa utumishi na mshahara, vijana walio kwenye mafunzo wanaathirika kwani muda wao ni mfupi na vilevile hawana mishahara bali posho tu. Aidha, kwa kuwa kifungu namba 23 cha Sheria namba 16 ya Mwaka 1964 kinaeleza vijana huchukuliwa kuwa ni askari wa kudumu wakati wa mafunzo ya kijeshi na vita kwa madhumuni ya kufidiwa, Sheria bado haijaweka wazi ni kwa cheo gani kijana huyo atafanyiwa mahesabu hayo.

Kamati inashauri kuwa, ili kuondoa mkanganyiko uliopo, ni vyema Marekebisho ya Sheria yakafanyika ili suala la fidia kwa vijana liingizwe chini ya Sheria ya JKT ya Mwaka 1964 au Sheria ya Ulinzi ya Mwaka 1966. Aidha kifungu na. 23 cha

Sheria ya JKT kitaje wazi cheo gani kinachopendekezwa kwa ajili ya kufanyiwa mahesabu ya fidia kwa vijana.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika, Mb, Mjumbe
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb, "
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb, "
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb, "
7. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb, "
8. Mhe. Cecilia Daniel Pareoso, Mb, "
9. Mhe. Alphaxad Kangi Lugola, Mb, "
10. Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb, "
11. Mhe. Cosato David Chumi, Mb, "
12. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb, "
13. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb, "
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb, "
15. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb, "
16. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb, "
17. Mhe. Joel Mwaka Makanyaaga, Mb, "
18. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb, "
19. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb, "
20. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb, "
21. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb, "
22. Mhe. Lazaro S. Nyalandu, Mb, "
23. Mhe. Stephen J. Masele, Mb, "
24. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb, "

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Job D. Masima na Naibu Katibu Mkuu Bi. Immaculate Ngwale, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah, Ndg. Grace Bidya na Ndg. Hamisi Mwinyimkuu kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu, **Mb**  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**  
10 Mei, 2016

**SPIKA:** Tunakushukuru sana. Sasa naomba nimuite Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kuhusu Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana Mheshimiwa. (Makofij)

**MHE. JUMA HAMAD OMAR - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Pili, napenda kuchukua nafasi hii adhimu na kwa sababu leo hii ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili, kukupongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi. Bila shaka kwa kuzingatia uzoefu wako katika nyanja za utawala na siasa, nina imani na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atakujalia, ulivushe Bunge hili kwa salama usalimini hadi kufikia mwisho wa maisha yake. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atakujalia, lazima nikiri kwamba Bunge hili ni kali sana ukilinganisha na Mabunge yaliyofuata ya chama kimoja ambayo mimi nilishuhudia kuwepo hapa ndani. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutumia muda huu kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbewe, kwa kunitueua kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninamuahidi yeye pamoja na Kambi nzima ya Upinzani kwamba nitafanya kazi kwa bidii katika kuibua mawazo mbadala ya kisera na kiutendaji ili kuboresha utendaji na ufanisi wa Wizara hii kwa maslahi ya Taifa letu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pongezi hizi za pekee kwa viongozi wetu wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuunganisha Watanzania kupitia vyama hivyo katika kuyatafuta mabadiliko na uhuru wa kweli, katika ushiriki wao katika siasa na utawala wa nchi yetu. Nitakuwa siyo muungwana ikiwa sitawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ole, kwa imani kubwa walijonayo kwangu, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge. Kwa hao wote hao nasema ahsanteni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ufanisi na weledi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua uwezo na uweledi mkubwa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika kulinda usalama wa mipaka ya nchi yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatambua pia mchango mkubwa wa Jeshi letu katika kupigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika, zikiwemo Zimbabwe, Angola, Msumbiji, Zambia, Malawi, Afrika ya Kusini, Uganda na nyaginezo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, aidha Jeshi la Wananchi limekuwa likishiriki katika operation mbalimbali za kimataifa za kulinda amani. Katika operation hizo, Jeshi letu limetajwa kwamba ni la kupigiwa mfano katika uhodari wa kazi na nidhamu ya hali ya juu. Kwa sababu hizo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeiletea nchi yetu heshima kubwa katika medani za Kimataifa. Pamoja na Jeshi letu kuwa na weledi na nidhamu kubwa inayopigiwa mfano duniani, watawala wamekuwa wakilitumia vibaya Jeshi letu la ulinzi jambo ambalo linalofanya ionekane kwamba Jeshi hili halizingatii maadili ya kazi yake. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kumezuka tabia ya watawala kulitumia Jeshi la Wananchi katika masula ya ndani ya kisiasa ili kutimiza matakwa yao ya kisiasa. Tabia hiyo ni mbaya, kwa sababu licha ya kuliondolea Jeshi letu sifa ya maadili lakini kitendo hicho kinachoweza kudumaza demokrasia katika Taifa letu. Kwa mfano, inapofikia kipindi cha uchaguzi.

Narejea tena kwa mfano, kinapofikia kipindi cha uchaguzi, Zanzibar inakuwa kama vile ni sehemu ya Jamhuri iliyovamiwa kijeshi (*invaded country or invaded territory*), kipindi chote cha uchaguzi Zanzibar vikosi vya Jeshi la

Wananchi Wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi na miaka ya nyuma Mgambo, kutoka Tanzania Bara wanapelekwa Zanzibar na kupiga makambi kwenye viwanja vya ndege, bandarini na kwenye vituo vya redio. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha wakati wote, vikosi hivyo vimekuwa vikipita mitaani na wakati mwingine kufanya mazoezi ya kijeshi katika maeneo ya makazi ya wananchi jambo ambalo huzua hofu kubwa kwa wananchi na kutoa taswira kama vile nchi inakabiliwa na vita. Aidha, zana mbalimbali nzito kama vile vifaru na mizinga husafirishwa kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na mara baada ya uchaguzi vifaa hivyo badala ya kubakia Zanzibar havibakii na vinasafirishwa back to Tanzania Bara. (Makofi)

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba ulinzi wa raia na mali zao unafanywa na Jeshi la Polisi, isipokuwa Jeshi la Ulinzi linaweza kuongeza nguvu ikiwa tu nchi iko vitani au kama hali ya hatari imetangazwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo tunalohoji hapa ni kwa nini Jeshi la Wananchi wa Tanzania lifanye kazi ya Jeshi la Polisi huko Zanzibar wakati Jeshi la Polisi lipo, nchi haipo vitani na pia hakuna hali ya hatari iliyotangazwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inalaani kitendo cha Serikali ya Muungano kutumia nguvu za kijeshi kutisha wananchi wa Zanzibar na kutumia mwanya huo kuchakachua mchakato wa kidemokrasia wa uchaguzi na kuiweka CCM madarakani kwa nguvu. Hali hii imedhihirika rasmi katika uchaguzi wa marudiano hivi karibuni huko Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba ielewewe kwamba unaweza kulazimisha utawala wa nguvu ya kijeshi, lakini kushinda hisia za wananchi ni jambo lingine kabisa. *Kwa lugha nyepesi ya kiingereza you can govern the country by barrel of gun, but winning the confidence of the people is entirely a different phenomena.* (Makofi)

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari upya matumizi sahihi ya Jeshi letu, kushiriki Jeshi katika mchakato wa kutwaa madaraka ya dola tena kwa njia za ujanja ujanja, ni hatari kubwa sana, ni vizuri demokrasia iachwe ichukue mkondo wake, kwa maana hiyo, nasisitiza Jeshi libakie kulinda mipaka ya nchi zetu, na kuilinda Serikali itakayowekwa madarakani na wananchi wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya Jeshi la Wananchi Tanzania na wananchi. Inakera na inaudhi pale ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa ushauri mzuri kwa Serikali, kwa maslahi ya Taifa, na mustakhabali mwema wa wananchi wetu halafu Serikali inapuuza ushauri huo. Nimeanza na kauli hii kwa sababu katika muda wote wa uhai wa Bunge la

Kumi, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipigia sana kelele suala hili la migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi na kuitaka Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kupitia upya mipaka ya Jeshi na wananchi katika maeneo yale yenye migogoro, na kuyaweka bayana ili wananchi watambue maeneo ya Jeshi, na hivyo kutoingilia maeneo hayo lakini mpaka sasa zoezi hili halionekani likifanywa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, wapo wananchi wengi sana ambaao wameathiriwa na migogoro hii ikiwa ni pamoja na kubomolewa makazi yao. Hivyo ni vyema Serikali hii ya Awamu ya Tano ikamaliza tatizo hili kabisa. Tunatambua kwamba Serikali kupitia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu wake wamekuwa wakishughulikia na kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi baina ya wananchi wenyewe kwa wenyewe, ila haifahamiki bayana kwamba kunapotokea mgogoro wa mipaka ya ardhi baina ya wananchi na taasisi ya Jeshi, unashughulikiwa na Wizara ipi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kwa mara nyingine tena, kulieleza Bunge hili kwamba ina mpango gani katika mwaka mpya wa fedha 2016/2017 wa kumaliza kabisa migogoro ya mipaka ya ardhi, kati ya jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba ajira katika Jeshi la Wananchi Tanzania zinatolewa kwa upendeleo na kwa usiri mkubwa na kwamba wanaonufaika na ajira hizi ni watoto wa maafisa wa ngazi ya juu Jeshini mbaya zaidi, kwa upande wa Zanzibar huwezi kupata ajira Jeshini kama hujauanganishwa na kiongozi wa CCM. Mifano mingi tunayo na wakati mwingine inabidi wale wanaoomba ajira kudaiwa chochote kama rushwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo hili la ajira za upendeleo lipo katika baadhi ya taasisi za umma, kwa mfano mwezi Julai 2014 Idara ya Uhamiaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilishawahidi kulalamikiwa kutoa ajira 200 za upendeleo, kwa ndugu na jamaa wa Maafisa wa Uhamiaji, jambo ambalo lilisababisha ajira hizo kufutwa na kutangazwa upya baada ya kubainika kwamba zilikuwa ni za upendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inatambua kwamba ajira za Jeshi zinaanza JKT, kwa wale wanaofuzu mafunzo ya JKT, lakini kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kwamba ajira zinatolewa kwa upendeleo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa tuhuma hii ya usiri na upendeleo katika ajira za Jeshi na kuchukua hatua stahiki ili kuwe na fursa sawa kwa kila raia wa Tanzania kupata ajira katika taasisi hii muhimu ya umma.

Mheshimiwa Spika, aidha katika muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya pia uchunguzi wa mchakato wa kujunga na JKT ili kuhakikisha kwamba hakuna ukiritimba wowote unaofanyika katika kuwachagua vijana wenyе nia ya kujunga na JKT.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wa Jeshi la Wananchi. Siyo nia yangu kuzungumzia kwa kirefu jambo hili kwa kuwa limeshasemwa sana huko nyuma na Kambi Rasmi ya Upinzani katika bajeti zinazozungumziwa kila mwaka za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kurudia tu neno moja kwamba wastaafu wa Jeshi nanukuu, ni Jeshi la Akiba yaani Reserved Army kama tusipotunza Jeshi hili la akiba hasara yake ni kwamba, tutapofikiwa kwa mfano madhila na majira ya kivita yanayohitaji msaada wa Jeshi hili la Akiba tutakwama, kwa kuwa wastaafu hawa wa jeshi watakuwa hawana nguvu tena ya kutoa msaada wowote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona wanajeshi wastaafu walitolitumikia Taifa hili kwa muda mrefu na kwa uadilifu na uzalendo mkubwa wakisota mitaani, kutokana na hali ngumu ya maisha inayosababishwa na kukosa kipato cha kujikimu maisha yao. Mimi mwenyewe kwa upande wa Zanzibar nimewashuhudia Makanali Wastaifu wakiajiriwa kama walini katika maghala ya wafanyabiashara binafsi. Baadhi yao wanajeshi hawa wastaafu wengine wamekuwa waganga wa jadi wakitoa mapepo katika vichwa wa wenyе mapepo. (Makofi)

Kutokana na Serikali kuwasahau wanajeshi wastaafu, na kuwaacha mitaani bila kujua ni kitu gani cha kufanya, tayari wanajeshi hao wameanzisha umoja wao unaojulikana kama Muungano wa Wanajeshi Wastaifu Tanzania Bara, yaani MUWAWATA na kwa upande wa Zanzibar wameanzisha umoja wao unaitwa UMAWA.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba pensheni za wastaafu wa Jeshi zinalipwa kwa wakati na kuboreshwa pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kutoa ruzuku kwa Muungano wa Wanajeshi wastaafu yaani MUWAWATA na UMAWA ili umoja walouanzisha uweze kutekeleza miradi mbalimbali ya kijasiriamali kwa maslahi ya wanachama wa umoja huo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kijeshi na mataifa mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua Jeshi la Wananchi wa Tanzania linashiriki katika operation za kijeshi, katika mataifa mengine kupitia katika mpango wa kulinda amani wa Umoja wa Afrika na ule wa Umoja wa Mataifa. Pamoja na kwamba ushiriki huo unaliongezea Jeshi letu uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira tofauti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari

upya faida hususani za kiuchumi na kiteknolojia ambazo kama Taifa tunanufaika nazo kwa Jeshi letu kushiriki katika operation hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mataifa yaliyoendelea kama vile Marekani na Uingereza, hayapeleki majeshi yao kupigana vita, au kulinda amani kama hakuna maslahi yoyote kwa mataifa yao na ndiyo maana sera zao za mambo ya nje ziko bayana, kwamba ni maslahi ya nchi zao kwanza, ndio mambo mengine yanafuata. Sera zao za mambo ya nje huweka bayana kwamba ni maslahi ya nchi zao kwanza ndiyo mambo mengine yanafuata. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba kama Taifa tusipojipanga kimkakati zaidi tutaishia kupeleka miili ya wanajeshi wetu waliokufa katika operation hizo huku Taifa likibaki bila manufaa yoyote na kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba kuwe na malengo mahususi na ya kimkakati Jeshi letu linapokwenda kushiriki operation katika Mataifa mengine. Mikakati hiyo iwe ni pamoja na kufanya utafiti wa masuala ya kiuchumi na kiteknolojia ili baada ya operation hizo kuwe na faida itakayopatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Jeshi katika nafasi za kisiasa. Serikali imekuwa na utamaduni wa kuwateua Maafisa wa vyombo vya dola walioko kazini na waliostaafu kushika nafasi za kisiasa kama vile Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Baada ya uteuzi huo Wakuu hawa wa Wilaya na Mikoa hufanya kazi kwa mujibu wa chama kinachotawala.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Wakuu wa Wilaya wanafungwa na Ibara ya 80(1)(c) ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977. Inawataja kwamba Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika Wilaya husika. Hali kadhalika Wakuu wa Mikoa wanafungwa na Ibara ya 94(1)(c) inayotajwa kuwa ni Wajumbe wa Kamati ya CCM katika Mikoa husika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itambue kwamba Ibara ya 147(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetamka kwamba nanukuu; "Itakuwa ni marufuku kwa Mwanajeshi yoyote kujunga na chama chochote cha siasa isipokuwa kama atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika Ibara ya tano ya Katiba hii," mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataku kujua hawa Maafisa wa Jeshi wanakuwa wamejiunga na CCM lini hadi kuteuliwa nafasi za kisiasa za CCM wakati wanakuwa wamefungwa na Katiba kutokujunga na chama chochote cha siasa? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba ili kulinda na kusimamia maadili ya kazi za Jeshi, Wanajeshi wasihusishwe kabisa na kazi za siasa, iwe wapo kazini au wamestaafu. Tunawashauri hivi kwa sababu kwa kuwateua kushika nafasi za siasa wanapostaafu kunaweza kukawafanya wale wengine waliopo kazini kutozingatia maadili yao ya kazi na kuanza kujipendekeza kwa watawala kwa imani kwamba pengine nao watateuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa au Wilaya watakapostaafu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatari kubwa zaidi ya kuwashirikisha wanajeshi katika mfumo wa utawala ni kwamba itawavutia wanajeshi wengi katika kushiriki siasa moja kwa moja ile hali imekatazwa na Katiba na matokeo yake utawala wa kiraia yaani civil governance utapoteza thamani yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba wanajeshi waachwe wafanye kazi za jeshi kwa mujibu wa taaluma na ujuzi wao wa kijeshi. Utawala wa nchi kwa mujibu wa Katiba ni wa kiraia. Nasisitiza tena utawala wa nchi kwa mujibu wa Katiba ni wa kiraia. Hivyo, tusichanganye mambo ambayo yanaweza kutushinda kuyatafutia ufumbuzi ikiwa yataharibika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa na dhana ya ujenzi wa Taifa. Ukitosha dhima ya Jeshi la Kujenga Taifa, utaona kwamba JKT pamoja na mambo mengine inawajibu wa kuwafunza vijana wetu kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ajili ya kujenga uchumi wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri miaka nenda miaka rudi kwamba Serikali itumie nguvu kazi iliyopo kwenye Jeshi la Kujenga Taifa na kujenga uchumi wa kweli nchini. Tunashauri kwamba Serikali itenye mashamba makubwa ili vijana hawa wa JKT wakiwepo mafunzioni wafanye mafunzo kwa vitendo ya kilimo ili nchi iweze kujitegemea kwa chakula. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Taifa hili kupata majanga ya njaa wakati Jeshi la Kujenga Taifa lipo na linamiliki mashamba yenyе rutuba nzuri. Kwa sababu hii tunashauri kwamba Serikali iwaagize Wakuu wa Makambi ya JKT kutengeneza programu maalum za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda, ufundu na kadhalika. (Makofi)

Aidha, kila mwaka tunapendekeza pia Waziri mwenye dhamana awe anatoa taarifa ya uzalishaji uliofanywa na JKT na mapato yaliyopatikana kutokana na uzalishaji huo katika kila Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Serikali imeweka rekodi mbaya sana ya kutoa fedha chini ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge kwa miradi ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na katika mafungu mingine fedha hazikutolewa kabisa! (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 220.14 katika Fungu 57 la Wizara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2016, fedha iliyokuwa imeshatolewa na Hazina ilikuwa shilingi milioni 40 sawa na asilimia 18 tu ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokuwa ikitekelezwa mingine inawagusa moja kwa moja wananchi hivyo kitendo cha kutotekerezwa kikamilifu kimewaathiri sana wananchi, kwa mfano mradi mmojawapo ulikuwa ni upimaji na ulipaji wa fedha katika maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi hili. Mradi huu ultengenewa takribani shilingi bilioni 7.4 lakini fedha iliyotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2016 ni shilingi milioni 277.1 sawa na asilimia 3.7 tu ya bajeti iliyoidhinishwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kutotoa fedha ya kutosha kutekeleza mradi huu kumeendelea kuchochea migogoro ya mipaka ya ardhi katika Jeshi na wananchi ambayo ingeweza kupekwa na hivyo kujenga uhasama kati ya Jeshi na wananchi jambo ambalo lingeweza kupekwa kama Serikali ingetoa fedha hizo zilizoidhinishwa na kwa wakati. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo la ajabu kabisa kuwahi kutokea ni kitendo cha kutopeleka fedha yote kutekeleza miradi ya maendeleo katika Fungu 38 la Ngome. Fungu hili lilitengewa jumla ya shilingi bilioni nane lakini hadi kufikia mwezi Machi hakuna hata senti moja iliyotolewa na Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wowote wa maendeleo ulipangwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokuwa itekelezwe chini ya Fungu hili ilikuwa ni ujenzi wa uwanja wa ndege Tanga, utafiti na ulinzi wa anga, ujenzi wa maghala ya mlipuko, ukarabati wa zana za ulinzi wa anga na ujenzi wa gati. Kambi Rasmi inaihoji Serikali hivi kweli ina nia ya kujenga Jeshi la kisasa lenye ufanisi ikiwa haitekelezi bajeti ya maendeleo katika Wizara hii iliyoidhinishwa na Bunge? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali kutotekerezwa bajeti ya maendeleo ya Wizara hii siyo tu kunalifiedhehesha Jeshi letu, lakini pia kinawaweka wananchi katika hali ya hatari kubwa. Kwa mfano, wote tunafahamu jinsi matukio ya mlipuko wa silaha katika maghala ya silaha ya milipuko huko Mbagala na Gongo la Mboto Dar es Salaam vilivyo sababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa makazi ya wananchi. Katika kukubaliana na hali hiyo Serikali iliahidi

kujenga na kukarabati maghala hayo ili kudhibiti ajali za milipuko, lakini jambo la ajabu Bunge limeidhinisha bajeti halafu Serikali haikutekeleza. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutofanya mzaha na masuala ya usalama na kwa maana hiyo tunaitaka Serikali kutoa maelezo ya kutosha mbele ya Bunge hili ni kwa nini haikutekeleza kabisa bajeti ya maendeleo katika Fungu 38 na 39. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, safari hii katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 fedha za maendeleo zilizotengwa na zinaombwa kuidhinishwa ni shilingi bilioni kumi katika Fungu 38 - Ngome na shilingi bilioni nane katika Fungu 39 - JKT. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji hivi kuna haja gani ya Bunge kuidhinishwa fedha hizo ikiwa fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2015/2016 hazikutumika kabisa. Je, Serikali inalihakikishiaje Bunge hili kwamba safari hii itatekeleza bajeti ya maendeleo kikamilifu kama itakavyoainishwa na Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nahitimisha hotuba yangu kwa kulipongeza sana tena sana Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa utumishi wao uliotukuka kwa kulinda nchi yetu kwa gharama ya uhai wao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa viongozi wakuu wa Jeshi kuendelea kuelimisha wanajeshi walio chini yao kuzingatia maadili ya kazi zao na kamwe wasikubali kutumika kisiasa kwa maslahi ya wanasasa waliopo madarakani. (Makofi)

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba Serikali ihakikishe kwamba Serikali inaacha kabisa kutumia Jeshi hili katika shughuli za kisiasa kinyume na Katiba ya nchi na kinyume na kanuni zinazoongoza maadili ya kazi za Jeshi la Ulinzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kwamba Bajeti ya Wizara ya Ulinzi haitekelezwi ipasavyo kwa hivyo, tunaitaka Serikali itambue kwamba kucheleweshewa na kutopeleka kabisa fedha zinazoidhinishwa na Bunge hili kwenye Wizara hii ni kuweka rehani ulinzi na usalama wa Taifa hili. (Makofi)

Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge inaitaka Serikali kutofanya mzaha kabisa na bajeti ya Wizara hii na kwa maana hiyo tunaitaka Serikali itekeleze kikamilifu bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha rasmi na ahsanteni sana kwa kuniskiliza. (Makofi)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA  
WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA MHESHIMIWA JUMA HAMAD  
OMAR (MB), AKIWASILISHA MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA  
FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kutumia muda huu kumshukuru Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe (Mb) kwa kunitfea kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninamwahidi yeye pamoja na Kambi nzima ya Upinzani kwamba; nitafanya kazi kwa bidii katika kuibua mawazo mbadala ya kisera na kiutendaji ili kuboresha utendaji na ufanisi wa wizara hii kwa maslahi ya taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, natoa pongezi za pekee kwa viongozi wote wakuu wa vyama vinavyounda UKAWA, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwaunganisha watanzania kuititia vyama hivyo katika kuyatafuta mabadilko na uhuru wa kweli katika ushiriki wao katika siasa na utawala wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, nitakuwa sio muungwana ikiwa sitawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ole kwa imani kubwa waliyonayo kwangu kwa kunichagua kuwa mbunge wao na kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge. Kwao wote nasema asenteni sana.

## **2. UFANISI NA WELEDI WA JESHI LA WANANCHI WA TANZANIA**

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua uwezo na weledi mkubwa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika kulinda usalama wa mipaka ya nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua pia mchango mkubwa wa Jeshi letu katika kupigania uhuru wa nchi za kusini mwa Afrika zikiwemo Zimbabwe, Angola, Msumbiji, Zambia, Malawi, Afrika ya Kusini Uganda na nyinginezo.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Jeshi la Wananchi limekuwa likishiriki katika Operesheni mbalimbali za kimataifa za kulinda amani. Katika operesheni hizo Jeshi letu limetajwa kwamba ni la kupigia mfano katika uhodari wa kazi na

nidhamu ya hali ya juu. Kwa sababu hizo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeiletea nchi yetu heshima kubwa katika medani za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jeshi letu kuwa na weledi na nidhamu kubwa inayopigiwa mfano duniani, watawala wamekuwa wakilitumia vibaya Jeshi letu la Ulinzi jambo linalolifanya lionekane kana kwamba halizingatii maadili yake ya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, kumezuka tabia ya watawala kulitumia Jeshi la Wananchi katika masuala ya ndani ya kisiasa ili kutimiza matakwa yao ya kisiasa. Tabia hiyo ni mbaya kwa sababu licha ya kaliondolea Jeshi letu sifa ya maadili lakini ni kitendo kinachodumaza demokrasia katika taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mfano, kinapofika kipindi cha uchaguzi, Zanzibar inakuwa kama vile nchi iliyovamiwa kijeshi (invaded country). Kipindi chote cha uchaguzi Zanzibar, vikosi vya Jeshi la Wananchi (JWTZ), Jeshi la Polisi, na Mgambo kutoka Tanzania bara wanapelekwa Zanzibar na kupiga makambi kwenye viwanja vya ndege, bandarini na kwenye vituo vya redio. Aidha, vikosi hiyo vimekuwa vikipita mitaani na wakati mwininge kufanya mazoezi ya kijeshi katika maeneo ya makazi ya wananchi jambo ambalo huzua hofu kwa wananchi na kutoa taswira kama vile nchi inakabiliwa na vita.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba ulinzi wa raia na mali zao unafanywa na Jeshi la Polisi isipokuwa Jeshi la Ulinzi linaweza kuongeza nguvu ikiwa tu nchi iko vitani au kama hali ya hatari imetangazwa. Jambo tunalohoji hapa; ni kwa nini Jeshi la Wananchi wa Tanzania likafanye kazi ya Jeshi la Polisi huko Zanzibar wakati Jeshi la Polisi lipo, nchi haipo vitani na pia hakuna hali ya hatari iliyotangazwa?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalaani kitendo cha Serikali ya Muungano kutumia nguvu za kijeshi kutisha wananchi wa Zanzibar na kutumia mwanya huo kuchakachua mchakato wa kidemokrasia wa uchaguzi na kuiweka CCM madarakani kwa nguvu. Naomba ieleteke kwamba, unaweza kulazimisha utawala wa nguvu ya kijeshi lakini kushinda hisia za wananchi ni jambo jingine kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari upya matumizi sahihi ya Jeshi letu. Kulishirikisha Jeshi katika mchakakato wa kutwaa madaraka ya dola tena kwa njia za ujanjaujanja ni hatari kubwa sana. Ni vizuri demokrasia iachwe ichukue mkondo wake. Kwa maana hiyo, Jeshi libakie kulinda mipaka ya nchi yetu na kuilinda Serikali itakayowekwa madarakani na wananchi wenyewe.

### 3. MIGOGORO YA MIPAKA YA ARDHI BAINA YA JESHI LA WANANCHI (JWTZ) NA WANANCHI

**Mheshimiwa Spika**, inakera na inaudhi pale ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa ushauri mzuri kwa Serikali kwa maslahi ya taifa na mustakabali mwema wa wananchi wetu halafu Serikali inapuuza ushauri huo.

**Mheshimiwa Spika**, nimeanza na kauli hii kwa sababu katika muda wote wa uhai wa Bunge la kumi, Kambi Rasmi ya Upinzani ililipigia sana kelele suala hili la migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya jeshi na wananchi na kuitaka Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kupitia upya mipaka ya Jeshi na Wananchi katika maeneo yale yenye migogoro na kuiweka bayana ili wananchi watambue maeneo ya Jeshi na hivyo kutoyaingilia hayo maeneo, lakini mpaka sasa zoezi hilo halionekani likifanyika kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, wapo wananchi wengi sana ambao wameathiriwa na migogoro hii ikiwa ni pamoja na kubomolewa makazi yao, hivyo ni vema Serikali hii ya awamu ya tano ikamaliza na tatizo hili kabisa. Tunatambua kwamba Serikali kupitia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu wake wamekuwa wakishughulikia na kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi baina ya wananchi wenyewe kwa wenyewe, ila haifahamiki bayana kwamba kunapotokea mgogoro wa mipaka ya ardhi kati ya wananchi na taasisi ya Jeshi unashughulikiwa na wizara ipi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kwa mara nyiningine tena kulieleza Bunge hili kwamba; ina mpango gani katika mwaka mpya wa fedha 2016/17 wa kumaliza kabisa migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya Jeshi na Wananchi?

### 4. AJIRA KATIKA JESHI LA WANANCHI WA TANZANIA

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba ajira katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania zinatolewa kwa upendeleo na kwa usiri na kwamba wanaonufaika na ajira hizo ni watoto wa maafisa wa ngazi za juu jeshini na mbaya zaidi kwa upande wa Zanzibar huwezi kupata ajira jeshini kama hujauanganishwa na kiongozi wa CCM.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili la ajira za upendeleo lipo katika baadhi ya taasisi za umma. Kwa mfano, mwezi Julai, 2014, Idara ya Uhamiaji katika Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi ilishawahi kulalamikiwa kutoa ajira 200 za upendeleo kwa ndugu na jamaa wa maafisa wa Uhamiaji, jambo lililosababisha ajira hizo kufutwa na kutangazwa upya baada ya kubainika kwamba zilikuwa ni za upendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba ajira za jeshi zinaanza JKT kwa wale wanaofuzu mafunzo ya JKT, lakini kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kwamba ajira zinatolewa kwa upendeleo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya uchunguzi wa tuhuma hii ya usiri na upendeleo katika ajira za Jeshi na kuchukua hatua stahiki ili kuwe na fursa sawa kwa kila raia wa Tanzania ya kupata ajira katika taasisi hii muhimu ya umma. Aidha, katika muktadha huo huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufanya pia uchunguzi wa mchakato wa kuijunga na JKT ili kuhakikisha kwamba hakuna ukiritimba wowote unaofanyika katika kuwachagua vijana wenyе nia ya kuijunga na JKT.

## 5. WASTAAFU WA JESHI LA WANANCHI

**Mheshimiwa Spika**, si nia yangu kuzungumzia kwa kirefu jambo hili kwa kuwa limesemwa sana na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kila bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inapojadiliwa. Ila napenda kurudia tu neno moja kwamba “Wastaifu wa Jeshi, ni Jeshi la Akiba” (Reserved Army). Kama tusipolitunza jeshi hili la akiba hasara yake ni kwamba; tutakapofikwa na madhila ya kivita yanayohitaji msaada wa Jeshi hili la akiba tutakwama kwa kuwa wastaifu hao wa jeshi watakuwa hawana nguvu tena ya kutoa msaada wowote.

**Mheshimiwa Spika**, Inasikitisha sana kuona wanajeshi wastaifu waliotumikia taifa hili kwa muda mrefu na kwa uadilifu na uzalendo mkubwa wakisota mitaani kutokana na hali ngumu ya maisha inayosababishwa na kukosa kipato cha kujikimu maisha yao.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Serikali kuwasahau wanajeshi wastaifu na kuwaacha mitaani bila kujua ni kitu gani cha kufanya, tayari wameanzisha umoja wao unaojulikana kama Muungano wa Wanajeshi Wastaifu Tanzania Bara (MUWAWATA) kwa upande wa bara na UMAWA kwa upande wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba pensheni za wastaifu wa Jeshi zinalipwa kwa wakati, lakini pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali kutoa ruzuku kwa Muungano wa Wanajeshi Wastaifu (MUWAWATA) na UMAWA ili Umoja waliouanzisha uweze kutekeleza miradi mbalimbali ya kijasiriamali kwa maslahi ya wanachama wa umoja huo.

## 6. USHIRIKIANO WA KIJESHI NA MATAIFA MENGINE

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua Jeshi la Wananchi wa Tanzania linashiriki katika operesheni za kijeshi katika mataifa

mengine kuitia katika Mpango wa kulinda amani wa Umoja wa Afrika na ule wa Umoja wa Mataifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba ushiriki huo unaliongezea jeshi letu uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira tofauti tofauti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutafakari upya faida hususan za ki-uchumi na kiteknolojia ambazo kama taifa tunanufaika nazo kwa Jeshi letu kushiriki katika operesheni hizo.

**Mheshimiwa Spika**, mataifa yaliyoendelea kama vile Marekani na Uingereza hayapeleki majeshi yao kupigana vita au kulinda amani kama hakuna maslahi yoyote kwa mataifa yao. Na ndio maana sera zao za mambo ya nje ziko bayana kwamba ni maslahi ya nchi zao kwanza ndio mambo mengine yafuate.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza hivi kwa sababu kama taifa tusipojipanga kimkakati zaidi, tutaishia kupokea miili ya wanajeshi wetu waliokufa katika operesheni hizo huku taifa likibaki bila manufaa yoyote. Kwa sababu hiyo, tunapendekeza kwamba kuwe na malengo mahsus na ya kimkakati Jeshi letu linapokwenda kushiriki operesheni katika mataifa mengine. Mikakati hiyo iwe ni pamoja na kufanya utafiti wa masuala ya kiuchumi na kiteknolojia ili baada ya operations hizo kuwe na faida iliyopatikana.

## 7. UTEUZI WA WANAJESHI KATIKA NAFASI ZA KISIASA

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa na utamaduni wa kuwateua maafisa wa vyombo vya dola waliopo kazini na wastaa fu kushika nafasi za kisiasa kama vile wakuu wa mikoa na wakuu wa Wilaya.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uteuzi wao, wakuu hawa wa Wilaya na Mikoa hufanya kazi kwa mujibu wa chama kinachoongoza Serikali. Kwa maana hiyo, wakuu wa Wilaya wanafungwa na ibara ya 80(1) (c) ya Katiba ya CCM ya 1977 inayowataja kuwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika wilaya husika. Hali kadhalika wakuu wa mikoa wanafungwa na Ibara ya 94(1) (c) inayowataja kuwa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM katika mikoa husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itambue kwamba Ibara ya 147 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetamka kwamba “*Itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujunga na chama chohote cha siasa, isipokuwa tu kama atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya 5 ya Katiba hii*”.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua hawa maafisa wa jeshi wanakuwa wamejiunga na CCM lini hadi kuteuliwa kushika

nafasi za kisiasa za CCM, wakati wanakuwa wamefungwa na Katiba kutojiunga na chama chochote cha siasa?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba; ili kulinda na kusimamia maadili ya kazi za Jeshi, wanajeshi wasihusishwe kabisa na kazi za siasa, iwe wapo kazini au wamestaafu. Tunashauri hivi kwa sababu kwa kuwateua kushika nafasi za siasa wanapostaafu, kunaweza kukawafanya wale wengine waliopo kazini kutozingatia maadili yao ya kazi na kuanza kujipendekeza kwa watawala kwa imani kwamba pengine na wao watateuliwa kuwa wakuu wa mikoa au wilaya watakapostaafu.

**Mheshimiwa Spika**, hatari kubwa zaidi ya kuwashirikisha wanajeshi katika mfumo wa utawala ni kwamba; itawavutia wanajeshi wengi kutaka kushiriki siasa moja kwa moja ilhali imekatazwa na katiba na matokeo yake utawala wa kiraia (civil governance) utapoteza thamani yake.

**Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba wanajeshi waachwe wafanye kazi za Jeshi kwa mujibu wa taaluma na ujuzi wao wa kijeshi. Utawala wa nchi kwa mujibu wa Katiba ni wa kiraia. Hivyo, tusichanganye mambo ambayo yanaweza kutushinda kuyatafutia ufumbuzi ikiwa yataharibika.

## 6. JESHI LA KUJENGA TAIFA NA DHANA YA UJENZI WA TAIFA

**Mheshimiwa Spika**, ukisoma dhima ya Jeshi la Kujenga taifa utaona kwaba JKT pamoja na mambo mengine ina wajibu wa kuwafunza vijana wetu kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ajili ya kujenga uchumi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri miaka nenda miaka rudi kwamba; Serikali itumie nguvu kazi iliyopo kwenye Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga uchumi wa kweli nchini. Tulishauri kwamba Serikali itenye mashamba makubwa ili vijana hawa wawapo mafunzioni, wafanye mafunzo kwa vitendo ya kilimo ili nchi iweze kujitegemea kwa chakula.

**Mheshimiwa Spika**, ni aibu kwa taifa hili kupata majanga ya njaa wakati Jeshi la Kujenga Taifa lipo na linamiliki mashamba yenye rutuba nzuri. Kwa sababu hii, tunashauri kwamba Serikali iwaagize wakuu wa makambi ya JKT kutengeneza programu maalum za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda, ufundi, uvuvi nk kila mwaka. Tunapendekeza pia kwamba waziri mwenye dhamana awe anatoa taarifa ya uzalishaji uliofanywa na JKT na mapato (maduhuli) yaliyopatikana kutokana na uzalishaji huo katika kila bunge la bajeti.

## 8. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2015/16, Serikali imeweka rekodi mbaya ya kutoa fedha chini ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge kwa miradi ya maendeleo katika wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na katika mafungu mengine fedha hazikutolewa kabisa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Bunge liliidhinisha jumla ya **shilingi bilioni 220. 14 (katika fungu 57 – Wizara)** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2016 fedha iliyokuwa imeshatolewa na hazina ilikuwa ni **shilingi bilioni 40** sawa na **asilimia 18** tu ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyokuwa itekelezwe, mingine inawagusa moja kwa moja wananchi, hivyo kitendo cha kutotekelezwa kikamilifu kimewaathiri sana wananchi. Kwa mfano mradi mmojawapo ulikuwa ni upimaji na ulipaji wa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa na jeshi. Mradi huu ultengewa takriban **shilingi bilioni 7.4**, lakini fedha iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2016 ni **shilingi milioni 277.1 sawa na asilimia 3.7 tu** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kitendo cha kutotoa fedha ya kutosha kutekeleza mradi huu kumeendelea kuchochea migogoro ya mipaka ya ardhi kati ya jeshi na wananchi ambayo ingeweza kuepukwa na hivyo kujenga uhasama kati ya Jeshi na Wananchi jambo ambalo lingeweza kuepukwa kama Serikali ingetoa fedha zote zilizoidhinishwa na kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, jambo la ajabu kabisa kuwahi kutokea ni kitendo cha kutopeleka fedha yoyote kutekeleza miradi ya maendeleo katika fungu 38 (Ngome). Fungu hili lilitengewa jumla ya **shilingi bilioni 8** lakini hadi kufikia Machi 2016, hakuna hata senti moja iliyotolewa na hazina kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wowote wa maendeleo uliopangwa kutekelezwa chini ya fungu hili. Hivyo Bajeti ya Maendeleo katika fungu 38 Ngome haikutekelezwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika** miradi iliyokuwa itekelezwe chini ya fungu hili ilikuwa ni ujenzi wa uwania wa ndege Tanga, utafiti na ulinzi wa anga, ujenzi wa maghala ya mlipuko, ukarabati wa zana za ulinzi wa anga na ujenzi wa gati.

**Mheshimiwa Spika**, katika muktadha huo huo, Fungu 39 (JKT) lilitengewa shilingi bilioni 4 kutekeleza mradi wa ujenzi na ukarabati wa makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, lakini hadi kufikia Machi, 2016 hakuna hata senti moja iliyotolewa kwa ajili ya mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali; hivi kweli ina nia ya kujenga Jeshi la kisasa lenye ufanisi ikiwa haitekelezi bajeti ya maendeleo katika wizara hii iliyoidhinishwa na Bunge?

**Mheshimiwa Spika, kitendo** cha Serikali kutoteketeza bajeti ya maendeleo ya wizara hii, sio tu kunalifiedhehesha Jeshi letu, lakini pia kinawaweka wananchi katika hali ya hatari kubwa. Kwa mfano wote tunafahamu jinsi matukio ya milipuko ya silaha katika maghala ya silaha za milipuko huko Mbagala na Gongo la Mboto – Dar es Salaam, yalivyosababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa makazi ya wananchi. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali iliahidi kujenga na kukarabati maghala hayo ili kudhibiti ajali za milipuko. Lakini jambo la ajabu, Bunge limeidhinisha bajeti halafu Serikali haikutekeleza. Kambi Rasmi ya Upinzani inaionya Serikali kutofanya mzaha na masuala ya usalama, na kwa maana hiyo, tunaitaka Serikali kutoa maelezo ya kuridhisha mbele ya bunge hili; ni kwa nini haikutekeleza kabisa bajeti ya maendeleo katika fungu 38 na 39 kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2015/16?

**Mheshimiwa Spika**, safari hii, katika fedha za maendeleo Serikali inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 10** katika fungu 38 (Ngome) na **shilingi bilioni 8** katika fungu 39 (JKT). Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji; kuna haja gani ya bunge kuidhinisha fedha hizi ikiwa fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha 2015/16 hazikutumika kabisa? Serikali inalihakikishiaje bunge hili kwamba safari hii itatekeleza bajeti ya maendeleo kikamilifu kama itakavyoidhinishwa na bunge?

## 9. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nahitimisha hotuba yangu kwa kulipongeza tena Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa utumishi wao uliotukuka wa kuilinda nchi yetu kwa gharama ya uhai wao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa viongozi wakuu wa Jeshi kuendelea kuwaelimisha wanajeshi walio chini yao kuzingatia maadili yao ya kazi, na kamwe wasikubali kutumika kisiasa kwa maslahi ya wanasiasa wachache wanaotaka kutimiza malengo yao ya kisiasa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kabisa kulitumia jeshi katika shughuli za kisiasa kinyume na Katiba ya chi na kinyume na kanuni zinazoongoza maadili ya kazi za Jeshi la Ulinzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini pia kwamba, bajeti ya Wizara ya Ulinzi haitekelezwi ipasavyo. Tunataka Serikali itambue kwamba; kuchelewesha au kutopeleka kabisa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye wizara hii ni kuuweka rehani ulinzi na usalama wa taifa hili. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni, inaitaka Serikali kutofanya mzaha kabisa na bajeti

ya Wizara hii na kwa maana hivyo tunaitaka Serikali itelekeleze kikamilifu bajeti itakayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Juma Hamad Omar (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA  
WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

10 Mei, 2015

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Wabunge vijana ambao hamfahamu Mheshimiwa Juma Hamad Omar amewahi kuwa mwanachama wa CCM na aliwahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii enzi hizo akiwa Waziri wangu pia. Ahsante sana wakati wa Serikali ya Awamu ya Pili ya Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. (Makofi/Kicheko)

Tunaendelea sasa na uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa mwanzo katika Wizara hii, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, majeshi ya ulinzi yana mchango mkubwa sana siyo katika kudumisha amani tu na usalama lakini katika kukuza uchumi, maendeleo na ustawi wa nchi. Nchi ambazo zimefanikiwa sana katika kuleta maendeleo ya watu wao wameyatulia vizuri sana majeshi yao ya ulinzi, mfano mzuri nchi kama Marekani, China na India walifanya uamuzi mahsuswa kujinyima na kuwekeza kwenye masuala ya uzalishaji hasa mashirika ya uzalishaji yanayoongozwa na Jeshi. Matokeo yake basi masuala ya utafiti wa mambo muhimu sana wa mataifa hayo yanayohusiana na uchumi, tiba na elimu yamefanywa na wanajeshi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua Tanzania na hasa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa bajeti wanayopewa ni ndogo sana, lakini kutokana na dhamira aliyoionesha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunakumbuka hivi karibuni alisema anatamani sana Jeshi la Ulinzi lifanye kazi zinazohusiana na masuala ya uzalishaji kwa kadri inavyowezekana. Kwa maana hiyo basi, tunaiomba Serikali ili tuweze kutimiza dhamira hiyo ya Mheshimiwa Rais tujinyime, lakini tufanye kila lililo katika uwezo wetu kuwekeza katika jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi wa Tanzania lina uwezo mkubwa sana wa kufanya shughuli ambazo hivi sasa katika nchi yetu zinafanywa na makampuni ya watu binafsi na wakati mwingine makampuni yanayotoka nje ya nchi. Sisi tunajua Jeshi letu la Ulinzi lina uwezo mkubwa sana wa kutengeneza madaraja, kuweka njia kubwa za umeme.

Mheshimiwa Spika, huwa ninasikitika sana ninapoona ziko shughuli ambazo Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanaweza kuzifanya vizuri tena kwa weledi mkubwa lakini wanapewa watu binafsi. Wakati mwingine tunafanya jambo la hatari sana kiulinzi na usalama, nitatoa mfano.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kutembelea nchi moja lakini sitaitaja Ulaya tukawa tunaangalia na wale wenyeji nikawauliza mbona barabara zenu ziko hivi pana sana, akaniambia hamjui sisi likitokea la kutokea nchi ikiingia kwa mfano kwenye vita barabara hizi zinafungwa na zinageuka kuwa njia za kupitia ndege za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, sasa sisemi tunaweza tukafikia huko, lakini inasikitisha utakuta kampuni ya ujenzi kutoka nje inakuja katika nchi yetu inajenga barabara na madaraja Jeshi la Wananchi wa Tanzania halishirikishwi, halijui! Hatari yake kiulinzi na usalama ikitokea hali ya hatari kuna baadhi ya madaraja hata vifaru haviwezi kupita. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine njia hizi za umeme tunawapa kazi makampuni kutoka nje yanaweka njia kubwa za umeme jambo ambalo ni hatari sana, Jeshi la Ulinzi na wataalam wake hawashirikishwi, mimi nasema hili ni jambo la hatari sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo Jeshi wanaweza kutoa mchango mkubwa iwapo watapewa fedha za kutosha. Wanajeshi wetu wapo na tunao wataalam kidogo katika masuala ya teknolojia ya habari na napenda kusema katika dunia ya leo, nafasi ya Jeshi kutumia silaha kubwa kama vifaru kwenda kwenye vita naiona katika karne hii na karne inayokuja inaweza ikapungua sana, lakini karne itakayokuja kuna uwezekano mkubwa sana wa mataifa mbalimbali watatumia cyber katika kuzishambulia nchi wanazotaka kuzishambulia na kwa maana hiyo Jeshi letu lijiandae kwenye eneo hilo. Ndiyo maana nasema Serikali ifanye kila linalowezekana iisaidie Wizara ya Ulinzi kuhakikisha kwamba wataalam wetu wa jeshi wanafunzwa ipasavyo katika masuala ya teknolojia ya habari na cyber kwa ujumla wake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua tutasema hatuna fedha labda nitoe ushauri kidogo wa namna ya kupata fedha. Najua bajeti hii haitoshi, lakini zipo Wizara ambazo zinaweza kufanya maamuzi ya makusudi kabisa kuunga mkono shughuli ambazo zinafanywa na Jeshi kwa sababu shughuli zao pia zinasaidiwa

na Jeshi. Kwa mfano, Wizara ya Biashara na Viwanda washirikiane na Jeshi, Wizara ya Elimu, Sayansi, Ufundu na Teknolojia ishirikiane na Jeshi, isishirikiane tu kwa maneno, hata inapowezekana watoe fedha kulisaidia Jeshi. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ishirikiane na Wizara ya Ulinzi na kila inapowezekana wanaweza kutoa fedha katika kuunga mkono miradi ambayo inatekelezwa na Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninalotaka kuchangia ni kwamba kwa muda mrefu vijana wetu wamekuwa wakipewa mafunzo katika Jeshi la Kujenga Taifa, lakini vijana hawa baada ya muda wao wa kujitolea unapomalizika wanarudi kwenye mitaa. Hili ni jambo la hatari. Vijana hawa tayari tumeshawapa mafunzo ya kijeshi na kwa bahati mbaya sana hatuna utaratibu wa kufanya tathmini wanaporudi uraiani vijana hawa wanafanya nini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nadhani sasa wakati umefika kwa Wizara ya Ulinzi kwanza ifanye utafiti na tathmini vijana hawa wanaporudi uraiani wanafanya nini. Lakini la pili Wizara iweke taarifa maalum ya vijana waliopitia Jeshi la Kujenga Taifa ili zikitokea nafasi katika Halmashauri zetu za kazi za ufundu, kazi za vibarua wanaangalia vijana wetu ambao wamepitia kwenye Jeshi la Kujenga Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mwisho, najua tuna ukosefu wa fedha lakini nadhani wakati umefika wa kuviiimarisha vyuo vya ufundu vilivyopo katika Jeshi la Kujenga Taifa ili viweze kutoa mafunzo mazuri kwa vijana wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kutuanzishia mjadala wetu, sasa tumsikilize Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, nikiwa Mbunge ambaye kwenye Jimbo langu kuna wanajeshi wengi wastaaifu, ninawajibika kutoa sauti yao ili pale ambapo itatokea Serikali itasikiliza basi na wao waweze kupata neema.

Kabla sijaanza mchango wangu nitambue mchango wa masemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Vilevile nitambue mchango mzuri sana wa Mheshimiwa Nahodha na aliywahi kuwa Waziri wa Ulinzi. Ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Mwinyi utayasikiliza na Serikali hii Wizara na Taasisi zake na Idara mbalimbali za Serikali zione zina jukumu la kufanya kazi collectively kwa

sababu Serikali ni moja na siyo kila mtu anaibuka na la kwake ndiyo maana kunakuwa na mkanganyiko wa aina hii. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambazo tulishazizungumza miaka miwili mitatu iliyopita. Imezungumzwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, suala la migogoro baina ya Jeshi na wananchi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unahitimisha leo naomba utueleze hatma ya mgogoro wa Kijiji cha Tondoroni kipo Kisarawe, mwaka jana, mwaka juzi nilizungumza kwenye hotuba ya ya Wizara ya Ardhi. Ningependa vilevile utupe hatma ya Kijiji cha Ihumwa, Dodoma, lakini vilevile Makuburi kwenye Kambi ya Jeshi wananchi sasa hii ni tofauti kwa sababu kwenye suala la Makuburi ni wananchi waliingia eneo la Jeshi kukawa na utaratibu ambao umefanyika Jeshi likaweka beacons upya. Sasa haieleweki hali ikoje sasa hivi ni muhimu vilevile ukatolea tamko ili wananchi wa maeneo yale waweze kukaa kwa amani.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ya pili ni pensheni ya wanajeshi wastaafu. Mheshimiwa Waziri huu ni mwaka wangu wa kumi na moja (11) Bungeni, katika kipindi chote hicho nikisimama kwenye hili Bunge Tukufu ninazungumzia suala la pensheni. Mheshimiwa Mkapa aliongeza kima cha chini kutoka shilingi 25,000 mpaka 50,000, Jakaya Kikwete akaongeza kima cha chini kutoka shilingi 50,000 mpaka 100,000, kima cha chini! (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa Sir Major kwa waliostaafu kipindi cha mwaka 2009 kushuka chini analipwa shilingi 190,000 kwa mwezi, kwa maisha ya sasa hivi hawa wanajeshi wetu wanaishije? Mheshimiwa Waziri, tunajua Rais ana dhamana ya kuongeza vima vya chini, tunajua Rais ana dhamana ya kuangalia hivi viwango, tunaomba hili suala lifanyiwe kazi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati amesema kuna mapendekezo, kwa sababu tulikuwa tukisema hizi hoja, yanakuja maelezo kwamba kwa mwaka 2009 mpaka sasa kwasababu ya mishahara yao na *blah blah* nydingi. Lakini tunafahamu kwamba mwaka 2008 na 2009 utafiti ulifanywa mapendekezo yakatolewa, hivi kizungumkuti ni nini, hivi shida kweli ni fedha? Leo tunalalamika kuna uhalifu wa kijeshi, mabenki yanaibiwa, hivi kama mtu unalipwa laki tano kwa miezi mitatu kwa sukari ya shilingi 4,000, sukari tu, shilingi 4,000 mpaka 6,000 hivi utaacha kwenda kuiba benki? Wakati una uwezo wa kutumia silaha? Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, hawa wastaafu wetu tuwaangalie kwa jicho pana. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 lilijibiwa swali hapa Bungeni, tunakumbuka kuna wanajeshi wetu hawa hawa wastaafu; mwaka 1978 walishiriki kwenye vita Uganda, mwaka 1978 na 1979. Serikali ya Uganda ikatoa

kiinua mgongo cha shilingi bilioni 59; Mheshimiwa Khalifa aliuliza swali hapa 2009 miaka saba iliyopita, hii hela imetolewa. Serikali mkajibu hiki kifuta jasho kwa wanajeshi wetu tutawapa, miaka saba baadaye mmechikichia na mkwanja wa watu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, tunaomba leo mtujibu kwamba hiyo shilingi bilioni 59 ambayo ilikuwa ni kifuta jasho cha wanajeshi wetu waliopambana usiku na mchana kuokoa nchi yetu kiko wapi? Naomba ujibu leo hapa usije ukatuambia ooh, muda hautoshi, nataka ujibu, kwa sababu wanajeshi wastaifu wanataka wajue ile fedha imekwenda wapi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wetu wanasema kama Serikali imeamua kwamba mnawapa hiki kiinua mgongo, ama pensheni ya chini chini, hivi kweli Serikali hatuwezi kufikiria kuandaa mfumo wa bima ya afya? Bima ya afya kwa nini, kwa sababu tunaweza tukatumia utaratibu huo huo wa hiyo pensheni ndogo wakati tunajipanga kuongeza kwa makato hayo hayo, ili wanajeshi wetu wastaifu waweze kwenda kupata tiba. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, wanasema mmewaambia wakiugua wataenda watatibiwa Lugalo. Mimi wakazi wangu wanajeshi wananiambia wakienda Lugalo wengi wao wananyanyapaliwa, wanachokwa! Unahudumiwa bure siku ya kwanza, na unajua uzee ni maradhi, siku ya pili, siku ya tatu unanyanyapaliwa. Wanasema kabisa tunaona wenzetu wakienda mwengine ana kufa, wa pili ana kufa, wa tatu ana kufa; wanahisi labda ukienda pale unadungwa sindano kumbe mtu tu amekufa kwa ugonjwa wake wa kawaida. (Makofij/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi tunaomba Serikali ifikirie, tunaweza tukaitumia pensheni hii ndogo, kuwakata makato kidogo kukawa kuna uhakika wa kupata tiba hawa wastaifu wetu na watoto wao. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Jeshi Zanzibar. Mimi ni mionganoni mwa watu ambao ninalipenda sana Jeshi letu, wanafanya kazi kubwa mno...

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Taarifa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kutoa taarifa fupi. Nataka nitoe taarifa fupi juu ya muongeaji anayeongea sasa ametoa kashfa kwa Jeshi letu kupitia hospitali zao kuchoma sindano za sumu wastaifu na hatimaye kufa. Ningependa kutoa taarifa kama ana uhakika na jambo hilo asije akaliingiza Jeshi katika kashfa, atupe ushahidi wa jambo hilo na mfano mmoja wapo. (Makofij)

**SPIKA:** Msemaji alitumia neno kwamba kuna hisia. Nimemsikiliza vizuri amesema kwamba kuna hisia. Mheshimiwa endelea mwenyewe kuliweka sawasawa. (Makofi)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nakushukuru kwa kumsaidia kwa sababu siyo size yangu. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namalizia hoja yangu kwa kusema hivi, natambua kazi nzuri sana ya Jeshi letu, lakini ni muhimu ikaeleweka kitu kimoja, tukiendelea kutumia haya majeshi Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wako wa 19 unasema ugaidi na uharamia. Ni muhimu tukaelewa ugaidi unatengenezwa ndani, watu wanapokuwa oppressed na kuchoka na kukata tamaa wanajengewa fikra za kufanya mambo ambayo walikuwa hawafanyi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unapoona mwenzio ananyolewa wewe tia maji. Kina Al Shabab, kina Boko Haram hawakuanza out of nowhere, watu walikuwa suppressed. Sasa for the sake of this country, for the sake ya kizazi kichanga, average ya kizazi cha Tanzania ni miaka 18, kwa hiyo haiingii akilini watu wazima wenye tamaa ya mamlaka wanalazimisha kubaki Zanzibar wakati Wazanzibar hawajawachagua kwa kutumia Jeshi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Zanzibar walikuwa wanakuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, wakati wa maandalizi ya kinachoitwa uchaguzi wa marudio, Mheshimiwa Waziri kuna mazombi, mazombi wanaandikisha madaftari, mazombi wanapiga watu, Waziri unakataa hakuna mazombi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kipindi cha uchaguzi, kipindi kuelekea uchaguzi tunaona watu na mask, tunaona mazombi wamepigwa picha. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima, nakushukuru muda haupo upande wako. Tunashukuru kwa mchangano wako, huku Bara mnatuacha barabarani ninaposikia mazombi najiuliza zombi ndiyo nini? (Kicheko)

Mheshimiwa Azzan Zungu ndiye mchangiaji anayefuata.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana. Kwanza naunga mkono asilimia mia moja hoja hii ya Waziri wa Ulinzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina history kubwa sana duniani siyo Tanzania tu. Jeshi hili limefanya kazi kukomboa nchi nyingi sana chini ya Jangwa la Sahara. Jeshi hili la Tanzania limefanya kazi kwa uadilifu

na kwa ujasiri mkubwa sana kukomboa na kufanya kazi Afrika. Mimi nampongeza sana Mkuu wa Majeshi na Makamanda wake wote kwa namna walivyotuweka na namna walivyoweka nchi hii kuipa heshima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jeshi hili ni jeshi kubwa sana mpaka Umoja wa Mataifa wanalitumia kwenda kulinda amani nchi zingine. Jeshi hili ni imara na linafanya kazi kwa kiwango kikubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba kumkumbusha Mheshimwa Waziri, mimi nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi, Usalama na Mambo ya Nje kwa miaka kumi toka mwaka 2005 mpaka 2010. Tumejenga hoja na tumekubaliwa na tukaambiwa na tuliihauri Serikali pensheni za vyombo vya ulinzi zitolewe kwenye utumishi wa kawaida, Serikali walikuwa tayari wameshaandaa Muswada kuja Bungeni, lakini walikuwa wanasubiri kidogo wenzao wa upande wa pili na wao waweke *inputs* zao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Waziri kipindi sasa kimefika, siyo jambo zuri kuona vikosi hivi au wanajeshi wetu, maafisa na wapiganaji kutokupata pensheni nzuri sababu tu ya mfumo wa utumishi uraiani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nitakuomba utueleze leo mmefikia wapi kuhusu kulifanya sasa Jeshi la Ulinzi na vyombo vya ulinzi kwa ujumla, viweze kupewa pensheni maalum kwa heshima na kazi kubwa wanayoifanya kwa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, najua Serikali ina nia njema na tunaamini ina ina nia njema, tunaomba sasa nia njema ile iwekwe ili iweze kuwasaidia wanajeshi hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine kwa mfano Asia, majeshi yanapewa miradi maalum yaweze kuijendesha na kusaidia mapato wanayopata kwenye miradi ile waweze kusaidia kuijendesha kwa namna ambayo wanaona inawafaa. Kuna nchi ya Asia, majeshi yamekabidhiwa kwa kwetu hapa tunaita National Housing, sijui kwa kwao wanaitaje, karibuni nyumba nyingi za mjini nchi zingine zimeachiwa jeshi kuziendesha ili na wao waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, najua kuna miradi siku za nyuma walipewa Jeshi, najua kilitokea matatizo lakini siyo sababu ya kuwanyima kuwapa fursa hiyo wao kuendesha miradi ili waweze kupata heshima na waweze kujipatia kipato cha kuendesha mambo yao.

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani Jeshi linashirikishwa kwenye masuala ya Contagious Disease Centre (CDC) lazima jeshi liwepo. Sasa sidhani kama kwetu wanashirikishwa. Jeshi wanatakiwa washirikishwe kwenye tafiti mbalimbali za kilimo, afya na za magonjwa; ndiyo wao wenye utaalamu wa kuweza

kuchambua na kuisaidia Serikali kufanya tafiti bora, Jeshi letu lina uwezo mkubwa sana wa kufanya mambo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuliomba kwenye Kamati yetu ya Ulinzi siku za nyuma kuwa Jeshi sasa lipewe jukumu la kufanya doria na kulinda ridge ambazo zipo baharini zinazotafuta tafiti za gesi. Ma-ridge hayo ya ajiri makampuni kutoka nje, wanatumia silaha nyingi sana katika maji yetu na sidhani na kama ipo control, fine, lakini tunazungumzia pato ambazo Jeshi letu lingeweza kupata kwa kufanya doria kwenye ridge hizi ambazo zipo kwenye maji ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Jeshi lina uwezo wa kupata mapato makubwa sana badala ya pesa hizi kutumiwa na makampuni ya nje kama Black Water na makampuni mengine ambayo yanakuja kulinda na yanalipwa pesa nyingi sana. *Insurance* hii inalipwa na Serikali ya Tanzania kwenye gharama za kutafuta gesi hii. Ni bora sasa na naamini kwa vifaa ambavyo tunavyo, Jeshi sasa lina qualify kwa asilimia mia moja kulinda bahari zetu, kulinda na mitambo hii ya ridge ya tafiti za gesi ili kuongeza usalama lakini vilevile kupata mapato ili na wao waweze kuijendesha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikuomba muda mfupi tu kwa sababu mara nyingi sichangii maneno mengi huwa nachangia point tu ambazo ni muhimu. Nitamuomba Mheshimiwa Waziri atupatie majibu haya.

Mheshimiwa Spika, lakini niendelee kusema Bunge hili tuendelee ku-support Jeshi, Bunge hili tuendelee kusaidia maslahi ya wanajeshi. Bunge hili lisaidie Jeshi letu liendelee kung'ara Afrika na Mataifa ya nje. Lidumu Jeshi letu, idumu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu, sasa tunaenda CUF mchangiaji ni Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mchana huu. Aidha, ninakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wa leo ni wakali sana, kule kwetu tunasema moto umepata magogo sijui kwenye chanja utawaka! Wapemba wana methali inasema; “ukilima patosha utavuna pashakwisha” na ukilima usipo palilia ukivuna utalia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, namshukuru mchangiaji aliyemaliza amemuonyesha chanzo kimoja cha mapato ambacho Mheshimiwa Waziri akikitumia anaweza

kuongeza pato katika Wizara yake. Sasa na mimi nataka nimuonyeshe chanzo ambacho kama atakitumia basi Jeshi letu litakuwa ni chanzo kikubwa cha mapato hata pengine kuliko utalii au vyanzo vingine vya mapato katika nchi yetu kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu limesifiwa sana na linasifiwa sana na ndiyo ukweli kwa utendaji kazi na weledi na nidhamu ya hali ya juu ndani ya nchi yetu na nje ya nchi yetu, ni ukweli kwamba Jeshi letu linashiriki katika UN - Mission nyingi. Tunaomba leo, Mheshimiwa Waziri utakapo kuja hapa utuambie Jeshi letu linashiriki katika mission nyingi za UN; je, ni kiasi gani cha fedha tunazopata kutoka katika mission hizo? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika Mission hizo kuna dry lease ambazo tunapeleka wanajeshi na logistic nyingine zinafanywa na UN, lakini wet lease ambazo tunapeleka wanajeshi na vifaa, kila kifaa kinalipiwa kwa dola. Kwa mfano gari moja tu linalipiwa kati ya dola 500 hadi dola 800, na inalipwa katika vipindi vya miezi mitatu, mitatu. Tumeshiriki katika UN Mission nyingi, utuambie Mheshimiwa Waziri ni kiasi gani cha fedha za kigeni ambazo Jeshi letu linapata katika mission hizo au pato letu sisi ni yale majeneza tu yanayokuja na maiti hapa tunazika? (Makofo)

Mheshimiwa Spika, hapa lazima tujipange, dunia ya leo, missions hizi za UN ni mtaji. Nchi kama Bangladesh, India, South Africa, Ukraine, wamewekeza sana katika UN Missions majeshi yao na silaha, kwa sababu zinaingiza pato kubwa katika Jeshi la Wananchi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaiomba Serikali sasa, nilisema wakati nachangia Wizara ya Kilimo hapa kwamba Serikali haina vision, tunaiomba Serikali sasa ikae, ipange hapa ili Jeshi letu lisiwe linaenda kule kupigana vita tu, lakini liwe linaenda kule linapigana vita kwa faida ya wao wenyewe, lakini na kwa faida ya nchi yetu na Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali lazima ipange tujuwe ni vifaa gani vinatakiwa vinunuliwe viwepo pale na katika ubora wake ili lile pato katika nchi yetu liwe ni pato kubwa na tusiwe tunapeleka askari wetu na kupoteza maisha tu kule! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli inasikitisha, Serikali hii ya CCM kwamba hata jeshi mnalipatia asilimia ndogo ya bajeti ambayo inapitishwa. Jeshi ambalo linalinda mipaka ya nchi yetu, Jeshi ambalo limekomboa nchi zote hizi za Kusini, Jeshi ambalo ni waaminifu, ni waadilifu, ni wasikivu. [Jeshi ambalo juzi tu limetumika kupindua Mapinduzi kule Zanzibar maamuzi ya wananchi]. **Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard).**

Mheshimiwa Spika, Jeshi ambalo linafanya kazi katika mazingira magumu, yakinokoa maafa sasa hivi hapa daraja limekatika ni wao huko, mvua, juu huko, leo katika bajeti yao wanaambiwa kwamba wanapata asilimia 18 katika bajeti ya maendeleo, hivi jamani kweli!

**SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, naam!

**SPIKA:** Umetumia maneno ambayo kidogo yanatupa taabu.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, yapi?

**SPIKA:** Kwamba Jeshi la Wananchi limepindua Zanzibar? Hebu liweke vizuri hapo.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, Tarehe 25 mwezi wa Kumi kulikuwa na uchaguzi, wananchi wa Zanzibar wakachagua chama cha CUF kuingoza na badala yake maamuzi yale yamepinduliwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naendelea...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika naendelea, kama kuna Mbunge hajaridhika anione kwa wakati wake nimsomeshe. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tunapopeleka Wanajeshi wetu katika *mission* hizi kuna Chapter Seven kuna Chapter Six, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie namna gani askari wetu wanalipwa wanapoenda katika Chapter Seven na wanapoenda katika Chapter Six. Atuambie ni namna gani wanalipwa. Kwa sababu Chapter Seven ni ulinzi wa amani, lakini Chapter Six ni vita kamili. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri utupe ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia utuambie Mheshimiwa Waziri kwa mfano, kama hawa waliokwenda DRC hivi karibuni tu, tumepoteza askari wawili muhimu sana! Luteni Rajabu na Meja Mshindo ni askari ambao ni muhimu sana katika jeshi letu, wamepotea katika kuisambaratisha M23 wamefanikiwa; je, waliporudi askari wale ambao walirudi na roho zao, Serikali imewathamini vipi? Wale ambao wamepoteza maisha katika vita ile ya kuisambaratisha M23 hadi leo ni vita ya kawaida tu pale na wao familia zao zitaenziwa vipi? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwaangalie askari wetu hawa angalau wawe na bima ya afya, wawe na bima ya ajali, wawe wana bima ya kazi hatarishi zile wanazo zifanya. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ni aibu leo kusikia askari mstaafu tena pengine alikuwa na cheo kikubwa anamaliza jeshi anakuwa fundi baiskeli au mziba pancha mtaani au mlinzi, ni vitu vya kusikitisha kwa kweli! Kwa hiyo, angalau basi wapatiwe hizi bima za afya askari wote wawe na bima za afya, wawe na uhakika angalau na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, katika ukurasa wa 24 wa hotuba yake amesema mionganini mwa kazi walizozifanya ni kutoa mafunzo katika jeshi, lakini pia na Jeshi la Akiba. Kwa hiyo atuambie hilo Jeshi la Akiba ambao wamepata mafunzo ni askari wangapi na mafunzo ya aina gani ili tuweze kujua hawa askari wetu wa akiba wamepata mafunzo ya aina gani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kama hatutowathamini wanajeshi wetu na kama tutaendelea na usanii huu wa kwamba tunapitisha bajeti hapa katika Bunge, halafu bajeti zile haziendi hata kwa Jeshi, tunajipalia makaa wenyewe! Tunajipalia makaa sisi wenyewe pamoja na uaminifu na uadilifu waliyonao, lakini hawa ni wanadamu kama wanadamu wengine. Kwa nini bajeti ya Bunge ikamilike, kwa nini bajeti ya Serikali, Mawaziri na Maafisa wengine wapewe kwa ukamilifu, lakini bajeti ya Jeshi iende robo, kwa nini? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata hawa wanaofanya kazi hizi tunashindwa kuwakamilishia bajeti! Ninaiomba Serikali sasa, tumepita katika Awamu Nne tumebabaisha sana, hii Awamu ya Tano ya hapa kazi tu na mmesema kwamba Awamu ya Tano hii ni nzuri sana, sisi tuna imani hiyo kwamba inaweza ikawa nzuri, basi mkae kama Serikali, mpange ili tuone Serikali inaendeshwaje.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf Salim. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Spika, ninaombwa Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), lakini inaendana pia na Kanuni ya 64(1)(a).

Mheshimiwa Spika, hivi punde mchangiaji aliyejita ametumia maneno ambayo kwa kweli hayana ukweli na siyo maneno dhahiri.

Mheshimiwa Spika, maana ya mapinduzi wote tunafahamu na hasa katika uchaguzi maana yake ni nini. Sasa leo tunapotoa taarifa ndani ya Bunge kwamba Jeshi hili la Wananchi ambalo hata Mbunge aliyejewa anachangia amelisifia sana, kwamba ni Jeshi lenye weledi, ni Jeshi ambalo linaaminika siyo ndani ya nchi ya Tanzania tu, hata nje ya mipaka ya nchi yetu. Lakini anapokuja kulituhumu Jeshi la Wananchi wa Tanzania ndani ya Bunge lako Tukufu, kwamba Jeshi hili limefanya mapinduzi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jambo ambalo siyo sahihi kabisa na siyo jambo la ukweli. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baya zaidi wewe umetoa maelekezo hapa kwamba jambo hilo linalozungumzwa siyo sahihi na Mbunge arekebishe kauli hiyo, lakini hakuna kilichofanyika.

Sasa naomba Mwongozo wako, ulishatoa hayo maagizo hayajatekelezeka. Kanuni ya 68(7) imekiukwa, lakini Kanuni ya 64(1)(a) nacho kimekiukwa, jambo hili kweli tunaliacha hivi jinsi liliivyo? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, umesikia maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ushauri wangu ni kwamba ufute kauli!

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, sifuti kauli yangu kwa sababu ushahidi ninao wa kituo kwa kituo, fomu za matokeo zilizosainiwa na waliopiga kura na walio simamia kuonesha kwamba chama chetu kimeshinda. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo siwezi kufuta kauli yangu kwa sababu ushahidi ninao na tulitakiwa kuuleta hapa Bunguni tukauleta hamkutaka kuupokea, kwa hiyo ushahidi tunao na siwezi kufuta kauli yangu, kwa sababu ninachokisema nakiamini ndani ya nafsi yangu na nilishika Msahafu kuapa kwamba nitasema kweli.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, unachonijibu sicho. Unachonijibu wewe ni kwamba unaamini chama chako kilishinda, mimi ninachokizungumzia ni ile sentensi yako kwamba Jeshi la Wananchi limepindua, ndiyo nataka ufute hiyo siyo habari ya vyama. Nakupa nafasi ya mwisho!

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, hiyo ni tafisiri tu ambayo inatafisiriwa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nafuta kauli yangu. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Message sent.

**SPIKA:** Naagiza kwamba watu wa Hansard kauli hiyo futeni kabisa, isionekane mahali popote! Kauli hiyo ni uzushi mkubwa sana! Kwa kweli ni matumaini yangu kwamba mtu mwingine hatarudia kauli hiyo. Tunaendelea na mchangiaji Mheshimiwa Allan Joseph Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii. Pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki kwa kuweza kuniamini niweze kuwawakilisha badala ya wao 188,000 kuingia humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa maana mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, mambo mengi ambayo tuliyoyazunguza tuliyoyajadili kwenye Kamati yamepewa nafasi yake, ushauri umezingatiwa, kwa sababu ushauri umezingatiwa tunaamini kabisa kwamba utekelezaji wake utakuwa kama ulivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, pia ninalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi kubwa linayofanya na limetoa taswira nzuri ndani ya nchi na nje ya nchi. Tunapozungumza mambo ya ulinzi na usalama ni masuala nyeti. Tunasema masuala nyeti kwa sababu yuko Mbunge hapa alizungumza akasema maendeleo yoyote tunayoyategemea, maendeleo ya viwanda, maendeleo ya kilimo, huduma nzuri za afya, lazima usalama uwepo.

Mheshimiwa Spika, tumeona matukio ya kigaidi, matukio ya uharamia, vituo vya polisi kutekwa, lakini Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni nguvu ya ziada ya kuweza kuhakikisha kwamba kunakuwepo na usalama ndani ya nchi yetu na Taifa linakuwa salama na tunaweza kufanya shughuli zetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mama akipika maandazi nyumbani watoto wakila na wakishiba unaweza ukakuta wanacheza mpira, sasa mambo yote haya tunayasema kwa sababu kuna amani na utulivu, tunatembea tunavyotaka, tunafanya mambo yetu tunavyotaka, ndiyo maana tunaweza tuka-undermine au fusione mchango wa Jeshi letu na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia nianze suala la ufinyu wa bajeti; ndani ya hotuba ya Waziri amezungumzia maombi ya fedha na ufinyu wa bajeti. Hilo ni jambo muhimu ambalo Serikali inatakiwa isikie na ione. Kwa sababu Jeshi linapopewa fedha ambazo hazitoshelezi ina maana haliwezi kutekeleza programu zake mbalimbali ambapo programu zote zinazowekwa kwenye bajeti huwa ni *Strategic Program*, programu ambazo zinaaminika

kabisa zina mchango kwa Taifa hili kwa ujumla wake. Kwa hiyo, suala la bajeti ya Wizara linatakiwa liangaliwe kwa macho mawili au kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la madeni. Tumeona kuna madeni karibu shilingi bilioni 483. Madeni hayo ni changamoto kubwa kwa Wizara, kama una madeni mengi namna hiyo au madeni makubwa kwa kiasi hicho hata moyo wa kutaka kutekeleza programu zingine unarudi nyuma kwa sababu ukipa fedha inabidi ulipe hayo madeni kwanza. Pia tunaposema madeni, Jeshi likidaiwa maana yake tunaathiri taswira ya Jeshi, kwa sababu Jeshi ni chombo ambacho hakitakiwi kudaiwa, ni chombo ambacho kinatakiwa kiwe salama salimini ili kiweze kuaminika na kiwe na taswira inayoeleweka. Kwa hiyo, nashauri kabisa, Wizara ya fedha iangalie namna ya kulipa madeni hayo ambayo mengine tunaambiwa ya kimkataba na hata madeni ya kimkataba yanapochelewa kulipwa ina maana yanatengeza riba, ina maana madeni hayo yatakua na kukua kwa maana hiyo, Jeshi litapata changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la tatu ambalo Wabunge wengine wameshalizungumzia ni maeneo ya Jeshi, ni muhimu maeneo ya Jeshi yote yakapimwa. Kwa hiyo, uchukuliwe mkakati wa maksudi wa kuhakikisha maeneo ya Jeshi yanapimwa, mipaka inafahamika siyo kwa wanajeshi tu na kwa wananchi wote na vijiji vinavyozunguka maeneo hayo, hiyo itasaidia kuondoa migororo ambayo tumekuwa tunaona inashamiri na inazidi kukua kwa sababu mgogoro unapokuwa mdogo, unapoona moshi ujue moto upo ndani yake. Kwa hiyo, lazima tuangalie namna ya kuondosha migogoro hii. Wakati tunasuburi fedha za kupima haya maeneo ni muhimu sasa Jeshi au Wizara ikachukuwa hatua ya kushirikisha vijiji husika kukawa na mazungumzo ya awali kuweka mipaka ya awali, kwamba baadaye tutapima mipaka hiyo, hapo tutakuwa tumeanza kutatua migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la mafao ya askari wastaifu wa Jeshi. Wabunge wote tunasema yaanagaliwe upya, yapitiwe na wanajeshi wetu wasijione wanyonge, wametumikia, utumishi wao umekwisha, lakini sasa wanatakiwa waenziwe kwa utumishi wao na kwa amani ambayo wamekuwa wakiisaidia nchi hii kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, iko changamoto ya maakazi ya askari, tumeona wanajenga nyumba 10,000 zimejengwa 4,000 bado haijapigwa hatua ya kutosha, ni muhimu ikatafutwa mikakati mingine ya ziada kuhakikisha kwamba askari wanakuwa na makazi yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya maendeleo. Mwaka huu tunasema kwamba asilimia 40 itakwenda kwenye bajeti ya maendeleo, lakini wenzetu wa Wizara hii wanayo miradi ambayo inahitaji kusukumwa kidogo sana ili iweze

kusonga mbele. Kwa mfano, kuna mradi wa Mzinga, kile Kiwanda cha Mzinga kinaweza kufanya kazi kubwa, kikatoa bidhaa kwa ajili ya Jeshi la Polisi, Magereza na kikatoa hata kuuza nchi za jirani bidhaa zinazozalishwa pale, wenyewe wanaita mazao. Sasa ni muhimu kabisa mwaka huu wa fedha, fedha zikatolewa, idara hiyo ikaweza kujitegemea na ikasaidia katika maeneo mengine. Jambo hilo likifanyika litakuwa na mchango mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia suala la afya, Jeshi lina hospitali zake, lakini kwenye hotuba ya Waziri tumeona wamezungumza kwamba pesa zinazotolewa hazikidhi na Waziri amefikia hatua ya kusema kwamba afya za wanajeshi zinakuwa mashakani, Sasa unapokuwa na wanajeshi wenyewe afya zilizo mashakani usalama huo utapatikana vipi?

Kwa hiyo, tunashauri kabisa kwamba pesa zilizotengwa mwaka huu ziende huko na zifanye kazi hiyo, wenzetu wamekuja na mbadala, mbadala wenyewe ni kwamba wanasema kuwe na aina ya bima ya afya, jambo hilo linatakiwa lifanyiwe kazi kwa haraka ili afya za askari ziweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo vingine vya mapato ambavyo wenzetu wamezungumza, Mheshimiwa Azzan Zungu amezungumzia na msemaji mwengine amezungumza kuhusu UN Mission. Jambo kubwa tuliloliona ni kwamba UN Mission hizi hata zikienda vifaa havitosh, kwa hiyo lazima tuweke mtaji wa kutosha, vifaa vinunuliwe ili tuweze kunufaika na hizo UN Mission. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, upo mradi wa mawasiliano ambaa jana ulitekelezeka kwa kiwango kidogo sana, mwaka huu tunashawishi kabisa pesa zote zitolewe ili mradi huo wa mawasiliano uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu JKT, Wabunge tunashauri kwamba vijana kwanza wote waende JKT wanaostahili kwenda. Tunaposema wote waende maana yake nini, maana yake bajeti iongezwe waweze kwenda. Tuna SUMA JKT itumiwe kulinda Taasisi zote za Serikali na SUMA JKT walipwe, kwa sababu tumeona kwamba yapo madeni, wanalinda hawalipwi, maana yake nini? Nashauri kabisa kwamba wale wanaodaiwa, Wizara ichukue hatua za kupeleka madai yao kwa Mlipaji Mkuu ili pesa ziweze kukatwa juu kwa juu. Kwa sababu inaonekana zikishaingia kule basi kunakuwa na kiini macho ambacho kinaendelea. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mchango wangu ndiyo huo. Naunga mkono hoja. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. tumsikilize sasa Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis (Makofii)

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na kunipa pumzi ya kusimama hapa pia niwashukuru wapigakura wa Jimbo langu la Mfenesini kwa kunipa nafasi hii adhimu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi kama liliyvo jina lake, ina majukumu ya kuhakikisha usalama wa Taifa letu kwa mipaka yake yote ya angani na ardhini. Wizara hii kwa kipindi kirefu sana, kwa uzoefu nilionao imekuwa na matatizo mengi mno na mengi yanababishwa na ukosefu wa fedha ya kutosha ya kuendesha vifaa pamoja na huduma za wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia ulinzi kama ulinzi, lazima vitu viwili vyote vihusihwe kwa pamoja, ukihudumia askari/wapiganaji, basi lazima pia uhakikishe unahudumia vifaa vyao pia wanavyovitumia kufanya kazi za ulinzi. Usiweke vipaumbele kwa watu halafu vifaa ukavidharau, uzoefu mkubwa nilionao katika vifaa vyetu vya kijeshi vya Tanzania, tuna vifaa vizuri vingi tu, vya kisasa kabisa, lakini bado hatujavipa uzito wa kuvihudumia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya nchi za wenzetu, nchi nyingi duniani, vifaa vyao vya kijeshi vinachakaa, vinaharibika kwa sababu ya kutumika sana kwa mazoezi na mambo kadhaa, lakini vifaa vyetu Tanzania vingi vinaharibika kwa kukaa bila kufanya kazi. Vifaa hivi ni kama binadamu, binadamu ukiwa unalala tu na kuamka, kula na kulala, siku utakayotoka pale baada ya miezi mitatu ukiambiwa ukimbie kilometa moja tu huwezi kuondoka na vifaa vyote vya kijeshi ndiyo vinatakiwa viwe katika mfumo huo, lazima viwe vinatumika, vinafanya kazi, magari wanaya-run, ndege zinarushwa kwa mazoezi na kadhalika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ukitaka kurusha ndege utaambiwa mafuta hakuna, ukitaka kufanya hiki utaambiwa mafuta hakuna. Baada ya muda fulani, usije ukategemea vimetokea vita una vifaa vya kutosha, unavyo vifaa vya kutosha lakini havina uwezo mkubwa wa kufanya kazi unayoitegemea. Niiombe sana Serikali iwe inatoa kipaumbele cha hali ya juu katika kuhakikisha kwamba vifaa vyetu vya kijeshi vinatunzwa ipasavyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie suala lililozungumzwa sana na baadhi ya Waheshimiwa hapa Bungeni, hasa la Jeshi la Akiba. Ni kweli wanajeshi wastaafu nao ni moja ya wanajeshi wanaotegemewa endapo ikitokea dharura ya janga la vita ndani ya nchi. Wengi walishaomba kuongezewa pensheni, lakini ninaomba pia Serikali iangalie utaratibu mpya wa kuhakikisha wananjeshi hawa sasa wanawalipa kila mwezi badala ya miezi mitatu mitatu, siyo rahisi, wengi tunaishi kwa kubahatisha kule mitaani, kukopa na kadhalika, siyo rahisi mtu leo akaenda kukopa halafu akamlipe

mfanyabiashara baada ya miezi mitatu! Ninaomba sana Serikali iliangularie suala hili na ilipe kipaumbele chake. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, watu wengi wamekuwa wakisimama hapa, wanapenda sana, hawafurahi bila kuizungumza Zanzibar. Mimi niseme tu, wanajeshi kama wanajeshi, anaposimama Mheshimiwa Mbunge hapa Bungeni halafu akasema vifaru vinatembea, hivi anakijua kifaru. Vifaru vinatembea mjini, wanajeshi wanafanya mazoezi, wanajeshi wakafanye mazoezi mitaani! Mtu anapokuja hapa azungumze kitu halisi, azungumze kitu anachokifahamu. Najua huyu Mheshimiwa hakijui kifaru haijui APC, hajui chochote, ndiyo maana anazungumza kifaru kinatembea mtaani, siyo kweli. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza hapa tusipotoshe wananchi, tusiwapotoshe wananchi tukawaambia kwamba majeshi sasa yameanza kuingia mitaani. Mimi ninachofahamu, nilikuwa mwanaigeshi pia, ninachokifahamu Jeshi linaweza kuingia mtaani kwa kitu kimoja tu, kumetokea labda kuna kitu kimeonekana kimeingizwa kwenye mtaa na Jeshi likafanya quadrant search, basi! Lakini Jeshi kama Jeshi, mazoezi yote ya Jeshi yanafanywa porini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, unapotuambia vifaru vimeingia mitaani, binafsi sikuelewi na najua na wewe pia hujui kitu ndiyo maana ukasema hivyo. Lazima tukubali Jeshi letu bado linafanya kazi kwa nidhamu na kwa kulingana na sheria na Katiba ya nchi. Tunachotakiwa kufanya hapa tuhakikishe Jeshi letu linahudumiwa, linapatiwa uwezo wa kutosha wa kununua vifaa vyao kwa wakati wowote wawe tayari endapo tumevamiwa ama limetokea janga lolote wawe tayari na uwezo wa kufanya lile jukumu walilopewa na Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naomba sana na napenda kusema wapo Waheshimiwa wanasimama hapa Bungeni, mishipa kabisa inawatoka, anakwambia kule Zanzibar uchaguzi haukuwa, mtu kazungumza lugha zote hapa leo, nimeshangaa anapozungumza mapinduzi, huyu katoka wapi, katoka shimoni leo, mapinduzi hayajui? Huyu naomba akatafsiri nini maana ya mapinduzi halafu aje atuambie, siyo vizuri watu wazima wenye heshima, Wabunge, kuja ndani ya Bunge hapa mkatoa lugha za ajabu, tabia hii siipendi, naomba irekebishwe kabisa. Watu tuje hapa tufanye kilichotuleta kulisaidia Taifa letu kusonga mbele. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Mbunge mmoja alisimama hapa akasema ile kesi kule Zanzibar haijaisha bwana, wasifikiri imekwisha. Mimi namwambia hivi, kesi ya Zanzibar tulimaliza Januari 12, 1964. Kama kuna mtu hapa au taasisi yoyote leo inayoweza kumuondoa Dkt. Shein, basi ifanye lakini nakwambia Dkt. Shein atakuwa Rais wa Zanzibar kwa miaka mitano na hakuna mtu wa kumuondoa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, mtu anayesema yeye Mzanzibari mimi ninamwambia nimezaliwa. Sisi Wazanzibar tunasema hivi, Dkt. Shein hakuna atakayemuondoa na huyo anayesema kuna kesi na alete na sisi tupo tayari kufa na nchi yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, najua watu wengine yanawaudhi kwa sababu hawana uchungu na Zanzibar. Mtu yejote mwenye uchungu na Zanzibar na anayeijua Zanzibar, maneno mengine yanayosemwa hapa yanauma sana. Nataka niseme, wakati tukiwa nje hatujawa Wabunge wengine hapa, tulipokuwa tunaona vikao vya Bunge vinavyopita, mambo yanayofanyika humu ndani, watu wengi kule nje yanawakera sana, yapo mambo yanawakera sana. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nilipofika ndani ya Bunge tukajikuta tupo watu wengi wapya humu ndani ya Bunge nikafikiri labda safari hii tutakuwa salama, lakini kumbe bado tunarudi kulekule. Niseme tu na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, yaliyopita tumeshamaliza, anayesema kwamba ule siyo uchaguzi...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**SPIKA:** Utulivu Bungeni! Mheshimiwa nakulinda endelea!

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, anayesema ule uchaguzi si halali sisi tunasema ni halali, anayesema Rais wa Zanzibar siyo halali namwambia atakaa pale kwa miaka mitano na hakuna wa kumwondoa. Kilichotuleta hapa tukifanye kwa ajili ya Taifa lakini malumbano mengine yasiyokuwa na maana tusiyalete hapa Bungeni. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, najua watu wanachukia sana...

**SPIKA:** Jamani, Kanali anaongea halafu raia mnapigapiga kelele! Huyu ni Kanali wa Jeshi. Endelea Mheshimiwa Kanali! (Kicheko)

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ninayoyasema kuna watu yanawakera, lakini tukubali tu kwamba sote tunaipenda nchi yetu, tuna wajibu wa kuhakikisha usalama wa nchi yetu unadumishwa. Niwaombe wenzangu Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi Tanzania bado muendelee kudumisha nidhamu iliyokuwepo Jeshini, tutekeleze majukumu yetu kwa ufanisi. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, na mimi naunga mkono hoja. (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante sana. Huyo ni Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis, sasa nadhani Mheshimiwa Maryam Msabaha utumalizie asubuhi ya leo. Mheshimiwa Maryam u-declare *interest* Jeshini huko! (Makofii)

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu Muumba mbingu na ardhi kwa kuzidi kunitetea, kunipa pumzi, kunipa uhai na kusimama katika Bunge hili Tukufu na kutoa hoja yangu katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ninaipongeza hotuba ya Waziri Kivuli, kaka yangu Mheshimiwa Mwinyi yale mazuri yachukue yafanyie kazi ili tuboreshe Wizara yetu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa isonge mbele. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Waziri ultamka juzi ukasema Jeshi liko *stand by*, nataka niwaambie Jeshi liko *stand by* na Serikali iwe *stand by* kwa kupeleka bajeti ya Wizara kwa wakati ili wapate kutatua matatizo yanayowazunguka wanajeshi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe *stand by* kwa kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vinapatiwa makazi bora na vinapatiwa stahiki zote zinazotakiwa ndani ya Serikali. Tumebakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vinakaa katika mazingira magumu, asilimia kubwa ya vyombo vya ulinzi na usalama havina makazi. Tangu Bunge lililopita, Bunge la mwaka 2010, nimekuwa mdau mkubwa sana wa Jeshi nikilalamika kuhusu vyombo vya ulinzi na usalama, hasa hivi vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo viro mipakani, vimikuwa vikikutana na changamoto kubwa sana. Tuhakikishe sasa hawa mnawapa stahiki zinazostahili, wapate kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, pia hapa pamezungumzwa sana kuhusu mambo ya wastaa fu wa Jeshi, na mimi nitachangia kidogo kwa sababu baadhi ya wenzangu wamechangia.

Mheshimiwa Spika, leo hii tumeona kuna wastaa fu amba o wamepigania nchi hii, wamekwenda Uganda. Tukaangalia, kwa mfano, tuliona wale wastaa fu amba o walikwenda kupigana Uganda, wale wazee wengine wakarudi hawana viango, wengine hawana mikono, leo hii wengine walishakufa, wengine wana ulemavu, wako Mgulani. Hawa wazee hebu kawaangalieni wamewakosa nini? Muwapelekee angalau sabuni, msiwatumie wakati wana viango vyao wakishakuwa hawana viango vyao mnakwenda kuwatafutia mahali mnawaweka kama scrapper. Niombe kwa kweli kazi ya Jeshi ni ngumu sana na Jeshi wanafanya kazi katika mazingira magumu na mwana jeshi hawezi kulalamika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni shahidi. Tumefanya ziara katika Kambi za Jeshi Zanzibar, umeona mazingira ya Zanzibar yalivyo. Ukiangalia miundombinu ya Zanzibar, leo nenda kwenye zile mess za Jeshi zile utofautishe na hizi za polisi, zina tofauti kubwa sana. Sasa hivi mwajeshi anauziwa kitu kwa bei kubwa sana katika mess zao zile za Jeshi. Mlisema kwa kipindi cha zamani walikuwa wakipata angalau vifaa kama vya ujenzi vinashuka bei, chakula kinashuka bei, leo nenda Jeshini pale uende kama mess ya Jeshi pale, nenda mwenyewe tumefanya ziara pale na nikakuambia, uangarie vitu vinavyouzwa ghali pale, hakina tofauti na kitu ambacho unanunua dukani. Sasa huyu mwajeshi ataponea wapi! Ukiangalia yeze ndiyo mnawambia acae *stand by*, hii *stand by* nawaambia siyo nzuri sana. *Stand by* mhakikishe nao mnawapa *stand by* zao. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, uzalendo saa nyingine unaweza ukawa tena uzalendo mtu anashindwa uzalendo. Mhakikishe wanapata nao hizo *stand by* lakini siyo wawe *stand by* kwa Chama cha Mapinduzi kwa kule Zanzibar na huku Tanzania Bara. Kwa kweli hii *stand by* baadaye itakuja kuwageuka nawaambia kabisa! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ukiangalia hawa wasaafu kwa kweli wengi wanapiga ramli wamekuwa waganga wa kienyeji sasa hivi. Mnawapa shilingi 20,000, unayempa shilingi 20,000 au shilingi 50,000 ukiangalia ni mtu ambaye ametumikia Jeshi na unajua ukishakaa katika kazi hii ya ulinzi na usalama, ukirudi uraiani huna rafiki kila mtu anakuona adui na ndiyo maana nasema mhakikishe wakiwa katika kazi hizi muwape hata angalau mikopo wajenge nyumba za kisasa waishi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo kuna rafiki yangu mmoja ni mwendawazimu, alipigana vita Marekani pale DC, lakini Serikali yake inamlipa mshahara, anakula vizuri, vile vitu ambavyo hawezi kutumia jamaa zake wanachukua wanakula. Ukienda kwake anaishi kama mfalme lakini ni mwendawazimu. Ninyi kwa nini watu ambao wana akili zao wengine hawana viungo, hawana nini mnashindwa kuwapa pesa lakini mnaweka pesa zikifika karibia na uchaguzi mnawaambia kaeni *stand by*. Niwaambie wanajeshi wote msikubali kukaa *stand by*, mtakaa *stand by* pale mtakapopata stahiki zenu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukirudi nyumba za wakufunzi hawa ambazo ziko kambi za JKT, nyumba nyingi siku za mvua nendeni mzunguke, zinavuja, wanavujiwa. Mnakuta nyumba ipo lakini yale majengo ni ya zamani, sasa kitu gani hamtaki kuwajengea hawa wakufunzi wa JKT nyumba nzuri ili watoto wale wanaokwenda kwa mujibu wa sheria wapate kufundishwa vizuri na mwalimu. Lakini mwalimu anafundisha wanafunzi saa ya kulala mvua ikinyesha anasimama, baadaye uchaguzi ukifika kaeni *stand by*, hiyo ni sawa? Hakuna kukaa *stand by* hapo. Wote msikae *stand by*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vijana hawa ambao JKT tunawapeleka kwa mujibu wa sheria na katika hotuba yako nimeona umegusia pia Wabunge waende. Kwa kweli Wabunge waende kwa sababu hili Bunge wameingia vijana wengine ni mateja wa unga wamo humu, wengine wanavuta bangi, wengine wanavua mama zao nguo, mama zao wengine walishakufa, wanakuja humu Bungeni wanawatukana mpaka wazazi wao. (Makofi/Kicheko)

Kwa hiyo, niombe kabisa na Mheshimiwa Rais Magufuli vijana wote Wabunge ambao hawana nidhamu, hawana standard ya kuzungumza katika Bunge hili waende JKT. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote vijana ambao hawana nidhamu ya kuzungumza katika Bunge hili na waende na wale ambao hawajapitia, kwa nini watu wanakwenda kwa mujibu wa sheria, *form six* wanakwenda, na Wabunge wote JKT wakirudi wawe na *discipline* ya kuzungumza ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hawa vijana wengine wanaokwenda kwa mujibu wa sheria mkishawachuja wale vijana, ninaomba kwanza muangalie namna gani ya kuboresha vile viwanda vya VETA mle ndani ili wale vijana wengine watakaopata ajira na wengine wabaki pale.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:**  
Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam kuna taarifa sijui iko upande gani.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:**  
Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni ya 68(8)...

**SPIKA:** Aah, Mheshimiwa Possi, karibu!

### TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:**  
Mheshimiwa Spika, nataka tu kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali au kwa watu walioathirika na dawa za kulevyia siyo busara kutumia lugha ambayo siyo staha au ya kinyanyapaa. Kwa mfano, kwa watu wenye changamoto za kiakili hatusemi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**SPIKA:** Naomba tusikilize ndugu zangu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa watu wenye changamoto za kiakili hatusemi tena wendawazimu. Kwa watu walioathirika na dawa za kulevyta ni lugha ya kinyanyapaa kuwaita kwamba ni mateja. Hawa wameathirika na uraibu, wanahitaji kusaidiwa. Ninaposema haya, tunaweza tukatumia lugha hizi kuji-describe wenyewe lakini huko nje kuna watu *innocent* wanaumia. Huo ndiyo muktadha wa taarifa yangu. (Makofii)

**SPIKA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Possi hebu tusaidie vizuri sasa. Kwa hiyo majina rasmi ya watu hawa ni nini, maana majina aliyosema Mheshimiwa Maryam ndiyo tunayoyaelewa sisi!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVUI:** Mheshimiwa Spika, tunatumia watu wenye changamoto za kujifunza au...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, *that is true!* Jamani, nimefanya tafiti za watu wenye ulemavu toka mwaka 2006, kwa zaidi ya miaka kumi.

**SPIKA:** Naomba tusikilize! Taarifa tunayopewa ni muhimu sana kwetu sote.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tunatumia watu wenye uraibu wa dawa za kulevyta siyo mateja, mateja ni neno ambalo lina-diminish na tukumbuke kwamba siyo kila mtu amaeingia katika uraibu kwa kupenda. Tunatumia watu wasioona lakini siyo vipofu kwa sababu neno upofu lina unyanyapaa, exception ni kwa viziwi kwa sababu watu wasiosikia lina negative connotation kwenye kiswahili...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa, ongea na mimi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU :** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo maneno yako mengi ni vizuri pia kwa sababu sisi tunasema kwenye majukwaa na wakati mwingine tunasema bila kujua, mara kwa mara tunapotumia baadhi ya majina ku-describe watu fulani katika jamii ku-consult na kamusi zetu za kiswahili kwa sababu lugha pia ni kielelezo cha utamaduni na tamaduni hizi zimekuwa zikibadilika kutokana na wakati. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kufahamu kwamba baadhi ya maneno yanayotumika na baadhi ya makundi yalikuwa yana-express tunachokiita

kitaalam popular culture (utamaduni wa walio wengi) ambao ulikuwa unafahamu wale waliokuwa wachache.

Mheshimiwa Spika, ni kuelimishana tu. (Makofij)

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Anachangia huyo, naomba muda wangu!

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Mheshimiwa Maryam nitakupa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa ni taarifa muhimu kwetu wote wala siyo kwa Mheshimiwa Maryam pekee yake. Kwa sababu haya majina mimi mwenyewe lazima nikiri huwa yananipa taabu kiasi ambacho nikitaka kuzungumzia haya mambo ya ulemavu na nini naogopa maana yake nitatumia yale majina ninayofahamu mimi ya Kigogo yale, kwa hiyo ni majina ambayo yanaudhi kwa wenzetu. Kwa hiyo, tuwe tayari kujifunza mara kwa mara namna ambavyo inatakiwa tuwa-address wenzetu wenye hali hiyo. (Makofij)

Mheshimiwa Maryam endelea, dakika zako nimezitunza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana najua utanilindia tu muda wangu.

Neno teja pia liko kwenye kamusi ya Kiswahili, kaangalie, mengine kama nini pia na wewe utoe semina elekezi kwenye Wizara ambayo upo na Mheshimiwa Jenista Mhagama. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nakwenda kwenye suala la vijana ambao wamechukuliwa kwa mujibu wa sheria na wengine kwa kujitolea ambao wanapelekwa JKT, kuna wengine wanachukuliwa wanapata ajira, wengine hawapati ajira. Ninaomba Serikali ihakikishe viwanda vyote ndani ya kambi kuwe na VETA vijengwe viwanda ambavyo vijana wale watajajiri, najua kuna mashamba ya kulima hata zile nguo wawe wanashona wenyewe ili tupunguze hizi changamoto kwa sababu wale vijana wakingia uraiani wanakuwa nao hawana kazi halifu wanaingia tena kwenye mambo ya uhalifu. Hilo naomba mlifanyie kazi ili vijana wale wapate kujajiri.

Mheshimiwa Spika, pia zinapotokea nafasi kama nafsi zile za ulinzi, nafasi za ndani ya Serikali, wale vijana wapewe kipaumbele kwa sababu ni vijana ambao mmeshawafundisha namna ya kutumia silaha, kila kitu walishasomea

sasa mkiwaacha kama hivi watashawishika baadaye wanaweza kwenda hata kujiunga na Boko Haram. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu natoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri suala lingine ninazungumzia ni kuhusu hii migogoro ya ardhi. Hii migogoro ya ardhi pia imezungumzwa sana na Mheshimiwa Halima Mdee pia pale kazungumza, utaona sana kwa upande wa Zanzibar kulivyokuwa na migogoro, kambi zote kwa sababu Mheshimiwa pia umekuwa msikiu na umzezunguka. Hizi beacon kuna ambazo zimelewewa tangu mwaka 1962, sasa zile beacons zimeshapotea.

Kwa hiyo pia uangalie namna gani kutatua hi migogoro kwa wakati na pesa zipelekwe. Hakuna kuwa standby mpaka pesa zipelekwe.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Msabaha, ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu, lakini tutaendelea jioni kama kawaida na naomba wafuatao waendelee kuijandaa; Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mheshimiwa Suleiman Nchambi, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na wengine kwa upande wa CCM wataendelea.

Kwa upande wa CHADEMA atakuwepo Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Saed Kubenea, kwa upande wa CUF atakuwepo Mheshimiwa Haji Khatib Kai. Kwa hiyo, uchangiaji uatendelea kuanzia saa kumi jioni ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi leo saa kumi kamili jioni.

(Saa 7.06 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulla Ackson) Alikalia Kiti

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani wote tumepata orodha ya nyongeza ya shughuli za leo. Kabla hatujaendelea na hoja yetu, tutaanza kwanza na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Bunge. Katibu!

**NDG. JOHN JOEL – NAIBU KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Bunge.

## UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA BUNGE

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tutaanza na uchaguzi wa Mwenyekiti Bunge, sasa nachukua nafasi hii kumkaribisha Katibu ili aweze kutupa utaratibu. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 7 ya Kanuni za Bunge, kumekuwepo na nafasi ya nasibu ya Mwenyekiti mmoja wa Bunge baada ya Mwenyekiti mmoja wa Bunge kutoendelea na nafasi hiyo. Kwa muktadha huo, kama Msimamizi wa Uchaguzi (*Returning Officer*) naomba nitoe maelezo ya namna nafasi hiyo inavyojazwa na uamuvi wa kujaza nafasi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tarehe 22 Machi, 2016 yalifanyika mabadiliko ya Wajumbe mbalimbali wa Kamati za Kudumu za Bunge, hali hiyo ilisababisha nafasi moja ya Mwenyekiti wa Bunge kuwa wazi.

Pia, mtakumbuka kwamba kwenye Mkutano wa Briefing tarehe 19 Aprili, 2016, Mheshimiwa Spika alitoa taarifa kwamba pamoja na shughuli nyingine katika Mkutano huo wa Tatoo wa Bunge unaonDELETEA, Bunge litafanya uchaguzi kuziba nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Uongozi katika kikao maalum kilichofanyika leo tarehe 10 Mei, 2016 imempendekeza kwa kauli moja Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taratibu za Bunge hili, pamoja na uendeshaji wa Bunge, kwa kuzingatia taratibu za uchaguzi wa nafasi hiyo, nafasi inayogombewa ni moja na mgombea ni mmoja. Kwa muktadha huo, mgombea huyo anakuwa amepita bila kupingwa. (Makofi)

Hivyo basi, naomba kumpa nafasi Mheshimiwa Naibu Spika ili amtangaze Mheshimiwa Azzan Zungu, kuwa Mwenyekiti mpya wa Bunge kukamilisha idadi ya Wenyeviti wa Bunge watatu wanaotakiwa Kikanuni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kumtangaza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kuwa ndiye Mwenyekiti mpya wa Bunge letu na amepita bila kupingwa. Kwa hiyo, nashukuru nimeona makofi yako pande zote kuonyesha kwamba hata kama tungepiga kura, basi Mheshimiwa Zungu angeshinda kwa kishindo. (Makofi)

Mheshimiwa Zungu, sasa nikupe nafasi ya dakika tano uje hapa mbele uweze kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuonyesha kukuunga mkono kwa pande zote na unaonekana sasa unakuja kwa nguvu kabisa kama Mwenyekiti na watakuona hapa ukionyesha umahiri wako. Karibu sana Mheshimiwa Zungu. (Makofii)

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kaimu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kuweza kusimama hapa kumshukuru yeye na kuwashukuru niyi. Mwenyezi Mungu amesema asiyemshukuru binadamu, basi hata yeye hawezi kumshukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii siyo ndogo. Kazi hii ni kubwa sana na mimi sina sifa kubwa zaidi ya ambazo ninyi Wabunge mnazo. Nitaendelea kuwa mwanafunzi kwenu na nitaendelea kutegemea ushirikiano kutoka kwenu na nitaendelea kutegemea mnisaidie kusaidia nchi yetu iende mbele na kusaidia Serikali yetu iweze kupata mafanikio na wananchi wetu wapate matunda ya Serikali yetu hii inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na wewe, namshukuru *Returning Officer*, Katibu; nawashukuru Wabunge wote. Kazi hii jamani nitaisimamia, nitakuwa *firm* lakini *very fair*. Nawashukuru sana, ahsanteni. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu kwa kuungana na timu hii ya kuweza kuendesha Bunge na naamini utamsaidia vizuri Mheshimiwa Spika katika majukumu yake.

Waheshimiwa Wabunge, basi tunaendelea sasa kwa mujibu wa orodha yetu ya shughuli za leo. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Hoja za Serikali, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

#### HOJA ZA SERIKALI

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

(Majadiliano yanaendelea)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Kuna majina yalisomwa kabla Spika hajasitisha Bunge asubuhi, na mimi nitaanza na haya majina niliyonayo hapa. Tutaanza na Mheshimiwa Mattar Ali Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Nchambi, halafu tutamsikia Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Ulinzi. Vilevile nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi yake nzuri anayoifanya. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, vilevile nachukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kumaliza uchaguzi wao kwa salama na amani na kuhakikisha CCM imeshinda kwa kishindo kikubwa Zanzibar. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Ulinzi kwa hotuba yake nzuri na bajeti yake nzuri inayoashiria mafanikio makubwa sana, ahsante sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwinyi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia na nitagusia kuhusu majengo ya makazi ya askari. Makazi ya askari imekuwa bado ni changamoto kubwa. Namwomba sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwinyi aweze kujitahidi kufanya kazi yake kuhakikisha kwamba askari wetu wanapata makazi bora. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya kikosi hicho wamo mafundi wazuri sana wenyewe uwezo wa kufanya kazi zao kwa uhakika, wenyewe ujuzi mzuri katika Jeshi letu la Tanzania. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kutumia vijana hawa ili kuleta maendeleo ya nchi yetu hata yale majengo yanayojengwa na Jeshi letu la Kujenga Taifa, basi waweze kujenga mafundi hawa kutoka ndani ya Jeshi hili. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nigosie sasa suala la majengo. Nimefurahi sana kusoma katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri kuwa kuna majengo takribani 5,000 ambayo anaendelea kuyajenga. Basi naomba sana kila ukiendelea kuyajenga majengo hayo, basi aweze kuwatumia wanajeshi hao kuhakikisha kwamba tunapunguza matumizi makubwa kuliko kuwapa wakandarasi wa nje. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kusimamisha majengo hayo kwa upande wa Unguja, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie kwa upande wa Unguja, wanajeshi wetu kule Unguja wanahitaji majengo haya na mpaka sasa wanakaa katika majengo ambayo siyo mazuri. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ufanye jitihada zako binafsi kuhakikisha

kwamba na upande wa Unguja unapata majengo mazuri. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa ndugu yangu, Mheshimiwa Mwinyi, alieleze Bunge lako hili, kwa upande wa Unguja ni lini wanajeshi wetu wataanza kujengewa nyumba mpya? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na kuchangia mchango wangu huu, niongelee kuhusu uchukuaaji wa vijana na kupeleka JKT. Mheshimiwa Waziri, naamini kama Serikali ina nia nzuri ya vijana wetu kuwaajiri na kuwapa ajira. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri anapotaka kuchukua vijana hawa kuwapeleka ndani ya JKT, kwanza aangalie uwezo wake wa kuchukua vijana hawa. Vilevile achukue vijana wenye uwezo wa kuajiriwa na sifa za kuajiriwa. Mheshimiwa Waziri vijana hawa kuwachukua na kuwapeleka ndani ya JKT, watakuwa wamepata mafunzo. Vijana hawa wanakosa ajira na baadaye wanarudi mitaani. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana kaka yangu, wanaporudi mitaani vijana hawa, basi inakuwa ni tatizo. Tunajijengea uadui sisi wenyewe. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu, unapotaka kuchukua vijana, jipime na uwezo wako wa kuweza kuajiri pasipo na kuwabakisha kurudi mitaani tena. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar tuna kikosi chetu cha JKU. Hiki kikosi ni imara, kizuri, kina mafunzo mazuri. Mheshimiwa Waziri nikuomba sana, hiki kikosi kinafanana na kikosi cha JKT. Nakuomba sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, kaka yangu mpPENDWA, uweze kuendeleza ushauri pamoja na Wizara husika ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha vijana hawa unawachukua na kuwaweka pale ndani ya kikosi cha JKU, baadaye vijana hawa ndiyo uwachukue katika ajira. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri vijana hawa ukiwaweka pale, basi nafikiri unaweza ukapata mafanikio mazuri na naamini utapata vijana wazuri wa kuwaajiri. Siyo kuwapeleka JKT na baadaye ukawarejesha tena Zanzibar. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, naamini Waziri wewe ni Waziri msikivu, mchapakazi, maoni yangu utayachukua kwa kina. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa ajira kwa upande wa Zanzibar. Bado hali siyo nzuri kwa utoaji wa ajira, vijana wetu ambao wanachukuliwa mpaka sasa ni vijana 300 tu. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana kaka yangu, ajira ambayo imetoka takriban watu 5000. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri kwa upande wa Zanzibar nakuomba sana *at least* tupate vijana 500 angalau ifike asilimia 10 ya vijana ambao wanachukuliwa kutoka Zanzibar kwenda kuajiriwa ndani ya vikosi hivi vya Muungano. Mheshimiwa Waziri, bado hali siyo nzuri

katika kuajiri hawa vijana, bado idadi yetu ni ndogo. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ulione ili kuhakikisha vijana hawa wanapata ajira nzuri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la Jeshi la Tanzania kutumika Zanzibar. Zanzibar ni kati ya sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilishangaa sana, kuna Wabunge wanasema wanashtushwa na Kikosi cha Jeshi kutumika upande wa Zanzibar. Hili ni Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; likifanya kazi Zanzibar, Tanzania Bara, likifanya kazi Dodoma, linafanya kazi kwenye Katiba. Hili linaruhusiwa kufanya kazi popote kwa sababu hili ni Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lina uhalali wa kufanya kazi mahali popote bila kupingwa na yeyote, ni kutohana na Katiba inayowaruhusu kufanya hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Wabunge wenzangu tuliachie Jeshi letu pendwa, Jeshi letu makini, Jeshi letu zuri liendele kufanya kazi zake kama ipasavyo. Tuliachie Jeshi, tusiliingilie katika kufanya kazi katika matakwa yake ya kisheria. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa Zanzibar umeshamalizika tarehe 20 Machi, 2016 hautarudiwa tena, kilichobaki ndani ya Bunge hili tuje kuchangia mambo mengine; tuchangie bajeti ya ulinzi kuliboresha Jeshi letu kuendelea kufanya kazi, siyo ku-discuss masuala ya Zanzibar. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, badala ya Mheshimiwa Nchambi, ambaye atachangia baadaye, halafu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nakushukuru kwa siku hii ya leo adhimu kwa kunijalia kunipa nafasi hii katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leo hii ni siku yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili, nishukuru viongozi wangu wote walioniwezesha kufika hapa pamoja na Mwenyezi Mungu; nimshukuru Rais wangu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa ushindi alioshinda wa kishindo siku ya tarehe 20 Machi, 2016. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwashukuru na wadau wangu walioniwezesha wa Mkoa wa Kusini Unguja, kuniamini na kunithamini wakanipa kura zao ili niwe Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Unguja. Nasema sitawaangusha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia suala la Wizara hii ya Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa. Kwanza niseme, alisimama mwenzangu hapa akazungumzia kwamba Jeshi limepindua Zanzibar. Jeshi halijapindua Zanzibar! Nataka kuuhakikishia ukumbi huu kwamba Serikali ya Mapinduzi tarehe 20...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Mwantumu, hiyo kauli ilifutwa asubuhi. Kwa hiyo, tuendelee. (Makofii)

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuendelea kuchangia, kuna ndugu zetu wa polisi ambao ni trafiki na pamoja...

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Eeeh!

**MBUNGE FULANI:** (*Aliongea nje ya microphone*).

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Usinishuhuliske!

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa jitihada zao wanazozifanya katika Serikali ya Muungano huu wa Tanzania ninawapongeza kwa dhati. Hufanya kazi zao kubwa sana, kuimarisha Muungano ndiyo maana tumekuwa na utulivu, amani na uhuru wa nchi yetu. Nawaomba wazidi kulinda Muungano, wasirudi nyuma na wala wasitetereke. Waulinde, wausimamie na wautetee kwa maslahi ya nchi yetu na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea katika huduma za jamii, mfano afya, ujenzi na utalii kuwa karibu na wananchi kutoa mafunzo ya ulinzi ili wananchi wazidi kufaidika na kujijengea kwenye harakati za maendeleo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Kusini Unguja tuna ulinzi wa uhakika kwenye Jeshi la Ulinzi na wanatusaidia vikubwa kutulinda na wala hatuna tatizo tunakwenda nao vizuri, tunashirikiana nao vizuri na ndiyo tumejivunia mpaka leo hii tumefikia hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichangie kuhusu suala la ujenzi wa Kituo cha Mkoa cha Polisi Jumbi; kuna Kituo cha Mkoa wa Kusini Unguja kilikuwa kinafanya kazi pale Fuoni lakini Kituo kile kilihamishiwa Mkoa wa Kusini, Wilaya Kati pale Jumbi. Naomba Mheshimiwa Waziri, kwa udhati wako wa moyo, kwa imani yako, utusaidie kituo kile kiwe na jengo imara, lenye mvuto na pale lilipo ni njiani basi paonekane kwamba pana jengo la Kituo cha Polisi; na watu wote

wanaopita pale wajue kwamba hili ni jengo la polisi la Mkoa wa Kusini Unguja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jitihada na busara zake jinsi anavyoliendesha Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani katika michango iliyotolewa humu ndani leo, huu mchango wa Mheshimiwa Mwantumu Haji umetia for a, maana pande zote umeshangilia. (Makofi)

Sasa tutamsikia Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Haji Khatibu Kai. (Makofi)

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii. Nafikiri sitakosea kama mwenzangu aliyetangulia. (Kicheko)

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, naomba ni-declare *interest* kwamba mimi nimezaliwa katika quarter za Jeshi...

**MBUNGE FULANI:** Hayo ni matusi!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Na nimekulia huko...

## TAARIFA

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, keti kwanza. Taarifa Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii niweze kutoa taarifa. Nasimama kwa Kanuni ya 68(8).

**MBUNGE FULANI:** Kanuni!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Kanuni ya 68 (8). (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar, ongea na Kiti!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nampa taarifa Mbunge aliyejikuwa akiongea sasa hivi, kauli yake ya kumwambia Mbunge ambaye hafai, ambaye hajui aliloliongea...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli, siyo kitu kizuri, anamdhalilisha Mbunge huyu. Kwa hiyo, namwomba sana Mbunge abadilishe kauli yake kuhakikisha kama anaweka sawa maneno yake. Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Baby.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, nadhani Mheshimiwa Mattar hakusema hajui, alisema amekosea. Mheshimiwa Mwakagenda unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, uko sahihi kwa sababu na wewe umelizungumzia. Naomba ulinde muda wangu. Naendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, nimezaliwa kambini, Jeshi ninalolijua nikua lilikuwa ni Jeshi makini kwa maana ya kipato. Wazazi wetu walituzaa wengi kwa kuwa walikuwa wakiishi maisha mazuri, walikuwa wakipata mishahara mizuri, tulikuwa tukipata ration kwa wakati na vitu kama hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jioni ya leo naomba nichangie. Tukiangalie bajeti iliyopita, ndugu zetu pesa za maendeleo walichangiwa shilingi bilioni 220 kama sikosei, lakini Serikali iliwapatia shilingi bilioni 40 au 41. Mimi najuliza, watawezaje kuishi maisha mazuri tulioishi zamani kama Bunge imepanga na imepitisha hiyo bajeti na hajjaweza kufika kwenye Jeshi waweze kufanya mambo ya maendeleo? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia mambo ya maendeleo, tunazungumzia makazi. Wanajesi wanahitaji nyumba nzuri za kuishi. Ni kweli tumeona, tumetembelea miradi, kuna nyumba zipo zinajengwa, lakini hazitoshelezi. Ninashauri Bunge linapopitisha bajeti tuhakikishe zile pesa zinakwenda kutimiza ahadi tulioahidi, wataenda kuifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi kama tunavyolisifia, ni Jeshi linalohitaji kuilinda nchi yetu, mipaka ya nchi, lakini pia tunafahamu umuhimu wa chombo hiki; kama tunashindwa kuipatia pesa kwa sababu zozote zile, tutakuwa hatujitendei haki sisi wenyewe Wabunge. Shilingi milioni au shilingi bilioni 41, ni miradi gani wafanye, ni miradi gani waache?

Mheshimiwa Naibu Spika, siasa ni nzuri, lakini tusifanye siasa kwenye vyombo vya ulinzi. Tunapozungumzia bajeti; na hii naizungumzia kwa Wizara nzima, nikimaanisha Polisi, Magereza na Jeshi wenyewe. Pesa wanazopata tuhakikishe zikipitishwa kwenye Bunge hili zikafanye kazi sawasawa na tulivyoahidi. Walipata pesa nusu karibu shilingi bilioni 600 hazikwenda kutenda kazi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafika mahali na wengine wameshasema, hawa ni binadamu, wanaweza wakaingia tamaa kwa sababu wakiishi vibaya hawawezi kusimamia uadilifu waliokuwa nao. Ni kweli tutawasifia, lakini ipo siku wanaweza wakaenda pembedi kwa sababu hatujawajali. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Mkuu wa Majeshi leo yupo. Wanawake walioko Jeshini, najua kwamba kuwa mwanamke siyo kwamba huwezi kufanya vizuri. Ninaamini wapo wanawake wenyewe vyeo, ila ninatamani na ninamwomba ikibidi wanawake waongezwe vyeo, siku moja tuwe na CDF mwanamke na sisi Tanzania tuonekane tumeSonga mbele. Ninaamini vyeo kuanzia chini vipo, naomba mchakato wa kuwapandisha vyeo ufanyike sawa sawa na utashi wa kazi wanazofanya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu ni mahiri na wenzangu waliotangulia wamezungumzia habari ya Zanzibar. Sitazungumzia huko ila nina swali la kiufahamu; siku za hivi karibuni nimeona viongozi wa kisiasa waliokuwa ni wastaafu wa Jeshi wakiapa kwa kuva nguo za Jeshi. Naomba nielezwe ni utaratibu wao au ni kitu gani? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mdogo, niliona Mheshimiwa Rais Nyerere wakati wa vita vya Idd Amini akiwa amevaa kombati na nguo za mgambo. Nafahamu kuwa Rais Jakaya Kikwete alikuwa Luteni; mpaka anastaafu sijawahi kumwona amevaa nguo za Jeshi. Sijui nimeshau kama ni Kanali au hivyo! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifahamishwe, inawezekana sifahamu, siku za karibuni Mheshimiwa Rais wetu amevaa nguo za Jeshi. Najua yeye ni Amiri Jeshi Mkuu, hilo nalifahamu, lakini sikuona begani kama amewekwa cheo chochote.

**MBUNGE FULANI:** Nyamaza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielekezwe, utaratibu ukoje? Najua ni Amiri Jeshi Mkuu, lakini begani sikuona cheo chochote. Je, ni sahihi? (Kicheko/Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Ajabu hiyo! (Kicheko/Makofi)

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba, vitu vingi ni ufahamu; ni suala la kuelekezwa. Inawezekana ilitakiwa ifanywe na Marais waliopita, lakini hawakutaka, lakini kama ni utaratibu, tuelekezwe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, Wizara hii inahitaji sana pesa na hasa maeneo ya viwanda. Tunafahamu kwamba Awamu ya Tano mnazungumzia viwanda na jeshi hili lina viwanda; naomba bajeti hii, iongeze pesa kwenye maeneo ya viwanda vya Jeshi. Tukiiongezea pesa tunaomba Serikali badala ya kuagiza vitu vya Kichina, tununue kutoka kwenye Jeshi. Wale wanaopata ten percent wakati huu wasiweze kupata. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwa kumalizia, Jeshi hili linafanya biashara, mbalimbali na ukusanyaji wa maduhuli. Ushauri wangu, maduhuli haya kwa miaka hii miwili tungeweza kuwaachia iweze kuwasaidia bajeti zao. Nasema hivyo, ninajua Serikali haina hela. Bajeti imeshuka, tukiwaachia maduhuli kwa miaka hii miwili waweze kufanya kazi zao vizuri, itatusaidia kama Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapopitisha bajeti, hatupitishi kishabiki, tunapitisha tukimaanisha ujenzi wa Taifa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, maduhuli ya Jeshi yabaki kwenye Jeshi kwa miaka miwili. Ikipita miaka miwili, tutaendelea na utaratibu mwingine, ahsante. (Makofi)

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara, mchangiaji ameshakaa. Kwa hiyo, taarifa hiyo...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Hivi mwanajeshi anakuwa na kadi ya CCM? Ahsante! (Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara naona unataka nikukumbushe... (Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Huyo anaitwa Bwege!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Tutamsikia Mheshimiwa Haji Khatib Kai, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, halafu Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea. (Makofii)

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na dunia, kwa kuniwezesha siku ya leo kuamka salama na afya tele na kuweza kusimama mahali hapa na mimi kuweza kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi ni muhimu kwa Taifa lolote duniani, kwani bila ya ulinzi ulio imara, Taifa haliwezi kuwa salama. Nianze ku-declare interest, kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kati ya miradi ambayo Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikwenda kuyatembelea ni mradi wa ukarabati wa majengo na miundombinu. Mradi huu ilitengewa na Bunge likaidhinisha shilingi bilioni nane kamili, lakini hadi Februari, 2016 hakuna fedha yoyote iliyotolewa kwa ajili ya mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni masikitiko na niaibu kubwa. Ni masikitiko kwa sababu Kamati tulipofika kwenye mradi huu, kwa kweli binafsi sisi Wajumbe wa Kamati tuliogopa hata kuingia hata katika majengo ambayo yalitarajiwa kufanyiwa ukarabati katika pesa ambazo ziliidhinishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika miundombinu hiyo ambayo kuna mess ambayo wanajeshi hawa wanakuwa wanaitumia, kwa bahati mbaya sana wanajeshi hawa ni waungwana na ni waadilifu sana, lakini bahati mbaya sana mess hii inavuja. Ni aibu!

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwininge ambaao tuliutembelea katika Kamati yetu ni mradi wa ulipaji wa fidia katika maeneo ambayo yalichukuliwa na Jeshi. Mradi huu ilitengewa na Bunge shilingi 7,390,000,000. Hadi kufikia mwezi Februari, 2016 fedha zilizopelekwa ni shilingi milioni 180, wananchi wa Tanzania walikuwa na imani na vyombo viwili vya nchi hii, moja likiwa ni Bunge na la pili likiwa ni Jeshi wa Wananchi wa Tanzania. Kwa bahati mbaya sana Watanzania kupitia chombo chao cha Bunge, wameshakata matumaini kwa sababu ya kukatishwa kuoneshwa matangazo ambayo waliona kwamba wanasaidiwa na wanatetewa na Bunge lao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa chombo cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania kuwachonganisha na wananchi kwa kutopeleka fedha ambazo zilitegemewa kulipia fidia kwa maeneo ambayo yalichukuliwa na Jeshi, hii ni

aibu, ni tatizo na mnasababisha kuwachonganisha wanajeshi ambao walikuwa na imani na wananchi, lakini leo imani hiyo itakuwa imetoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uchaguzi wa marudio Zanzibar. Ni mara kadhaa nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa akisema kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania halijapelekwa Zanzibar. Nasema hili siyo kweli, kwa sababu Mheshimiwa Waziri anasahau kwamba wanajeshi hao wanapokwenda Zanzibar hawapitii mbinguni. Wanajeshi hawa wanapokwenda Zanzibar wanapitia baharini, tunawaona wanavyokwenda, lakini pia tunawaona wanaporudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani Mheshimiwa Waziri atafute maneno mengine ya kutuambia, lakini siyo kwamba Wanajeshi hawajapelekwa Zanzibar kwa madhumuni mamaja tu ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri huyo huyo amekuwa akisema kwamba wanajeshi waliopelekwa Zanzibar au waliopo Zanzibar, kazi yao ni kulinda amani na usalama wananchi. Nasikitika kusema kwamba hivi wananchi wanapolindwa kwa usalama au Jeshi linapolinda usalama ni kuwatisha wananchi ambao wametulia? Hii haileti maana kwamba ni kuwasaidia na kuwalinda wananchi walioko Zanzibar. (*Makofii*)

Nasikitika kusema kwamba Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati namheshimu sana, lakini kwa bahati mbaya au bahati njema alisema kwamba watu wamekuwa wakisimama hapa wakizungumza kwamba Zanzibar kulipelekwa vifaru katika uchaguzi wa marudio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie tu Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama, sawa hata kama vifaru hatuvijui, kwa sababu hatujaenda jeshini lakini tunaona. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba watu hawajui, sawa hatujui, lakini tunaona. Kwa hiyo, tunapoona, tunajua hiki ni kirafu. Tumeona na tumeshuhudia wakati wa uchaguzi wa marudio, wanajeshi wakizunguka na vifaa vyat kivita mpaka kwenye vijiji. Sasa tunaposema kwamba jeshi lilikuwa limeingilia shughuli za kisiasa Zanzibar, msituelewe vingine. Tunasema kwa jambo ambalo tumeliona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la malalamiko ambayo yapo kwa wanajeshi wa rank ya chini. Wanajeshi wa rank ya chini na ninaomba Mheshimiwa Waziri hapa atakapokuja atoe ufanuzi, inawezekana hawafahamu lakini pia inawezekana kwamba hawajajua kwa sababu pengine wameingia juzi juzi au hawajakuwa wazoefu katika Jeshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi hawa wa rank ya chini wanasema kwamba kwa kawaida ration allowance inakuwa ni sawa kwa wanajeshi wote, lakini kwa bahati mbaya wamekuwa wakiona kwamba mwanajeshi wa rank ya chini kabisa amekuwa akilipwa shilingi 180,000, lakini kuanzia Koplo, nyota moja hadi nyota mbili wamekuwa wakilipwa kiwango kikubwa ambacho ni tofauti kabisa na difference inakuwa ni kubwa. Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja alitolee ufanuzi ili wale ambao pengine hawafahamu, waweze kufahamu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri tu kwa hili, ni vyema basi, ili kuondoa malalamiko na mambo ambayo yanaweza yakaleta tofauti kwa wanajeshi wetu, basi naomba labda itafutwe njia nyingine ya kuweza kuweka hii tofauti ambayo inaonekana ni kubwa kwa wale askari waliopo rank ya chini. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimalizie kusema kwamba siyo jambo la busara na siyo jambo jema kwa Wizara kama ya Ulinzi na Usalama kwamba inapopangiwa bajeti ambayo itasaidia usalama wa nchi hii, vinginevyo leo bajeti inakuwa haipelekwi na inapelekwa ambavyo Bunge halikuidhinisha. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri usimamie hili, kwa sababu na wewe upo Serikalini upo kwenye Baraza la Mawaziri, utie *lobbying* yako ili uhakikishe kwamba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ilivyopangwa ndivyo inavyopelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nasema ahsante kwa kunisikiliza. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae.

**MHE. FAKHARIA S. KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa na imetoa mwelekeo kwa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Nimezungumza kwa kusema fumbo hilo; tunalizingumzia Jeshi. Jeshi wajibu wake ni kwenda Zanzibar na kuwepo Bara. Sasa kupelekwa Jeshi Zanzibar imekuwa hoja kubwa hapa ndani, kwa nini Jeshi limekwenda Zanzibar?

Mheshimiwa Waziri ukurasa wake wa 20 alizungumza hivi, nanukuu: "Kukamatwa kwa mabomu ya kutengenezwa kwa mkono katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar." Sasa kwanini majeshi yasiende? Atakayeyategua mabomu haya ni nani kama siyo Jeshi? Sasa haya mabomu kayatengeneza nani? Wakasema ni wananchi wa Zanzibar. Sasa ikiwa ni kweli jambo hilo limefanyika Zanzibar, wa kufanya shughuli hiyo ni majeshi; wa kuangalia ulinzi

huo ni majeshi na mabomu yamelipuliwa Zanzibar. Tatizo liko wapi? Anayetaka kusema na aseme tu ili afurahishe roho yake na maamuzi yake, lakini ukweli ndiyo huo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kuhusu mgao wa nafasi za ajira Zanzibar. Nakubali wanajeshi wanaajiriwa Zanzibar, lakini utaratibu unaotumiwa Mheshimiwa Waziri angalieni. Mnapeleka nafasi katika Mikoa, watu wanatafutwa katika mikoa, wanaajiriwa. Kwa nini msiende JKU kama mnavyokwenda JKT? Kwanza kule mtapata vijana tayari wameshapata elimu ya jeshi, wakakamavu, wameshajua nini wanakwenda kutenda; lakini kuchukua Mkoani, hamujui mtu yupo vipi, lakini kwa sababu vipi aajiriwe! Nafikiri hilo mliangalie tena na mlipange tena. Bora vijana wetu wakimaliza, waende JKU wapate elimu ya ukakamavu na inakuwa rahisi kwenu kujua wapo vipi, afya yake ni vipi na uwezo wake uko vipi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuja katika ukarabati wa ujenzi wa majengo ya jeshi Zanzibar. Kambi za Zanzibar zipo kwenye hali mbaya. Ukiangalia Mtoni, Mwanyanya, Mazizini na nyininge zote hazipo kwenye hali nzuri na sielewi toka zilipojengwa lini zimekarabatiwa. Nimeona katika kitabu chako ukurasa wa 37 umeelezea kwamba kuna nyumba kama 4,744; siyo mbaya hiyo kazi mtakayoifanya; na mmesema tayari kwa Pemba. Kama zipo nyumba 320 siyo mbaya; lakini kwa Unguja hali ndiyo mbaya. Kwa Unguja majeshi yetu pale ndiyo Zanzibar City. Sasa tunataka kama mlivyojenga nyumba 320 na Zanzibar tujue nyumba zetu mtazijenga lini? (Makofii)

Mheshimiwa Waziri, malipo ya wanajeshi wastaifu yanakuwa yana matatizo; matatizo yake ni nini? Inabidi lazima mwanaajeshi aende Bara kutoka Zanzibar kufuatialia. Kwani Zanzibar hamwezi kuweka kituo kukawa na kituo kama Bara? Mwanaajeshi kastaifu Zanzibar, anakwenda pale anahudumiwa, anapata malipo yake Zanzibar baada ya kuondoka. Maana akifika Bara kwanza humjui mtu, wala humwelewi mtu, hujui unaanza wapi! Wakati mwingine huyo mwanaajeshi hajapata nafasi hata ya kwenda huko. Mwenyewe yupo Zanzibar tu! Sasa mnampelka Bara akafuate kiinua mgongo, akahangaike! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie Wizara kama inaweza kujigawa na Zanzibar wakawepo wafanyakazi na wakaweza kufanya kazi hiyo vizuri na kwa wepesi bila matatizo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu uvamizi wa ujenzi wa nyumba karibu na kambi za Zanzibar. Kambi za Zanzibar zimevamiwa, zipo katikati ya mji. Kambi hizo kwa kweli ukiangalia Mtoni, Mazizini, Mwanyanya na nyininge kadhalika, pale linalofanywa ndani ya kambi wananchi wa pale wanajua,

kinachotokea wananchi wa pale wanajua na inatakiwa ndani ya kambi kuwe kuna siri. Huwezi kuyajua mambo ya kambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine inawezekana ikatokea madhara itakuwa rahisi kwa wale wananchi kupigwa. Itabidi wananchi wanaokaa karibu na kambi wapate elimu wajue jinsi ya kujihami, maana ukishakaa kambini na wewe ni sawa sawa na mwanajeshi, litakalotokea na wewe umo. Sasa mngechukua wakati wenu mkatoa elimu kwa watu waliokuwepo pale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo, naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tutamsikia Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa na mimi napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Ulinzi, Mheshimiwa Waziri na jopo lake lote, napenda pia kuwapongeza Mkuu na Wakuu wa Majeshi yote ya Ulinzi na Usalama wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ulinzi wa raia na Tanzania kwa jumla ndani na mipaka yote ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuanza kuchangia sasa hivi ni kuhusu kuvamiwa kwa maeneo ya kambi za Jeshi. Kama ilivyoelezwa na Wajumbe waliotangulia, kambi zetu nydingi zimevamiwa na maeneo ya raia. Nataka kuishauri Wizara yako Mheshimiwa Waziri tuangalie kambi ambazo zimeathirika sana na kuvamiwa na raia, tuombe Serikali tubadilishe maeneo ya kambi tupeleke maeneo mengine ambayo yapo nje zaidi na maeneo ya wananchi. Hayo ni kwa sababu ya kunusuru maisha ya wananchi waliozunguka katika maeneo yale, lakini pia usalama wa jeshi lenyewe, pamoja na vifaa viliviyokuwemo ndani ya kambi za Jeshi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kidogo kuhusu mapato yanayopatikana na shughuli za utendaji katika majeshi. Naomba Wizara yako kwa kuititia Wizara ya Fedha kama kuna mapato yanazalishwa na majeshi yanakwenda Serikalini, basi iwekwe percent kidogo ibakie pale ili waweze kujiendesha kwa shughuli nydingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa limezungumzwa suala la wanajeshi wastaifu kuwa waganga wa kienyeji. Baada ya mtu kustaifu kazi ya aina yoyote, ana uhuru wa kufanya analolitaka; na uganga wa kienyeji ni fani, siyo kila mtu anaweza. Kama mtu ana fani yake, sheria haimbani kuwa mganga wa kienyeji, kuwa mshona cherehani, kuwa mtengeneza baiskeli, kuwa fuundi makenika, anaweza! Huo ni uhuru wa raia kufanya anachokipenda! Katika

uganga wa kienyeji huo anapata mapato mengi kuliko mimi ninayefanya kazi Serikalini nilivyokuwa kwa wakati huo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nizungumzie kidogo suala hili la majeshi kwenda Zanzibar, kubakwa kwa demokrasia, kuingilia uchaguzi. Ninachosema, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni Jeshi la Wananchi wote wa Tanzania kama jina lake livilyo. Lina uhuru na lina haki ya kikatiba ya kufanya kazi popote ndani ya Jamhuri ya Tanzania kuanzia Kigoma mpaka Kisiwa Panza mpaka Tumbatu na kazi ya ulinzi ni kazi ya jeshi hili. Kwa wale ambao hawakfurahishwa na kitendo kile, mimi nawahesabu ndiyo wale ambao walikuwa wanataka kuhatarisha amani ya nchi. Kwa sisi ambao tulikuwa tunataka tuwe huru, tufanye uchaguzi kwa amani, tulifurahi sana kuwepo kwa jeshi letu la ulinzi wa Tanzania kuja kutulinda. Wananchi walifurahi, walikuwa wako huru, hawana mashaka kama walivyokuwa mwanzo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Zanzibar ilikuwa inajulikana, wakati wa uchaguzi hali ilikuwa tete, wananchi wanaogopa hata kwenda kununua sukari nje, wanashindwa. Kila asubuhi kukicha unasikia milipuko Kibanda Maiti; milipuko Darajani; milipuko, kumezungushwa uzio. Hivi ninyi mlikuwa mnataka kufanya nini hasa? (Makofi)

Mimi nauliza kulikuwa kuna nia gani na nchi yetu hata leo imekuwa jeshi kila mahali linazungumzwa. Jeshi nalipongeza wamefanya kazi nzuri, wameilinda Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano ambayo ni wajibu wao na wamelinda raia wa Zanzibar kama ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kulipongeza kwa dhati jeshi letu liendelee na juhudhi zake hizo za kulinda amani ya nchi na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa Zanzibar umefanyika kwa kufuata sheria zote za uchaguzi za Zanzibar. Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ndiye Rais wa Zanzibar, ataiongoza Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Nawashauri, tunasikia maneno mengi hapa kuhusu uchaguzi wa Zanzibar, lakini kama kweli walikuwa na nguvu ya umma inayowakubali kwa nini walikataa kuingia kwenye uchaguzi na wao wana mtaji wa kutosha? Kwa nini wamekataa mechi ya marudio? Kama kweli wana mtaji wa kutosha wa wapiga kura, ilikuwa hakuna sababu ya kukataa kuingia kwenye uchaguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Zanzibar ...

## TAARIFA

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija, naomba ukae. Taarifa Mheshimiwa Waitara!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilikuwa nampa taarifa mzungumzaji kwa kanuni ya 68(7). Haya ni mambo ya kawaida, tunayajua tu. Nampa taarifa kwamba kwa hiyo, kwa maelezo yake, anataka kuthibitisha kwamba ni kweli kwamba jeshi liliingilia uchaguzi wa Zanzibar? Maana anasema kwenda kule ilikuwa sawa sawa, maana yake walienda kweli. Ndiyo taarifa nataka nimpe. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, taarifa ni Kanuni ya 68(8) siyo 68(7).

**WABUNGE FULANI:** Hajui huyooo! Huyoooo!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu kazi ya jeshi ni ulinzi wa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie kidogo suala la ajira. Naomba kama yalivyzungumzwa, hawa vijana waliokwenda kupata mafunzo ya JKT ndio wafikiriwe kwanza katika ajira za jeshi. Pia napenda kushauri kwamba hili jeshi letu la JKT ligawe aina ya mafunzo. Kuwe na mitaala ambayo inawahusisha wanafunzi wa vyuo wanapokwenda kupata mafunzo yawe ya aina nyingine na mafunzo ya vijana wanaoandaliwa kuwa wanajeshi au askari yawe ya aina nyingine kwa maana kwamba hapa tutaepuka kuwafundisha mambo yote ya kijeshi vijana ambaa baadaye watakwenda kuajiriwa kwenye taasisi nyingine za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za askari wetu wa Jeshi, na mimi nasisitiza kwamba awamu hii nyumba zijengwe Unguja. Nashauri kutokana na uhaba wa ardhi wa Kisiwa cha Unguja, basi sijaona ramani zao lakini nashauri nyumba hizi zisiwe nyumba ndogo ndogo badala yake ziwe nyumba za ghorofa ili kutumia eneo dogo kwa nyumba nyingi na baadaye eneo litakalobaki huko mbele lije litumike kwa nyumba nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu ni kubwa, limekua, tofauti na jeshi la mwaka 1964 na 1967. Kwa hiyo, kwa sababu jeshi letu limekua, lazima kutakuwa na mahitaji mengi na changamoto nyingi. Kwa hiyo, la kufanya tu ni Serikali kuongeza bajeti katika jeshi hili katika Wizara hii na ifikirie zaidi kutatua matatizo mbalimbali ya Wanajeshi wetu na hasa wakati wa kustaafu walipwe viinua mgongo vyao kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saed Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King. (Makof)

**MHE. SAED A. KUBNEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Kwanza nampongeza kabisa kwa dhati Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi la Tanzania limefanya kazi kubwa sana katika Jamhuri ya Muungano na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaposema hapa kwamba jeshi lisitumike kisiasa, hatuna maana kwamba sisi sio wazalendo, tunalipenda jeshi letu lakini tunaonya kwamba vitendo vinavyofanyika Zanzibar na vilivyofanyika wakati wa uchaguzi na sasa vinaashiria uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa haki za binadamu. Hiyo haina maana kwamba watu hawa siyo wazalendo au hawalipendi jeshi hili. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizotoa askari kulinda amani katika Jeshi la Umoja wa Mataifa. Ripoti iliyowasilishwa tarehe 3 Machi inazungumzia matukio 99 ya ubakaji na udhalilishaji wa watoto yaliyofanyika mwaka 2005 na walinzi wa amani Umoja wa Mataifa katika nchi 69. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 6 Machi, 2016, kwa mujibu wa vyombo vya habari vilimnukuu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi akisema kwamba ripoti ya Umoja wa Mataifa juu ya yaliyotokea katika Afrika ya Kati na maeneo mengine, hajaipata. Leo ni tarehe 10 Mei, takribani miezi miwili tokea Waziri alipowaambia umma kwamba ripoti ile hajaipata. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati anapojibu alieleze Bunge hili Tukufu, ni hatua gani zimechukuliwa kama askari wetu wa Jeshi la Ulinzi na Usalama walihusika na mambo yaliyotokea katika Jeshi la Kulinda Amani?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni muhimu sana kwa kuwa jeshi letu limefanya kazi nzuri, linaheshimika duniani, ili lisiweze kuchafuliwa kwa mambo ambayo hayawahu. Jambo hili ni muhimu pia likawekwa wazi kwa kuwa taarifa hizi zilitolewa hadharani na ziko katika mitandao na zipo katika Ofisi za Umoja wa Mataifa Jijini Dar es Salaam. (Makof)

Jambo la pili, kuna taarifa kwamba Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania limeingia mkataba wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi na Kampuni ya Henan Guijo Industry Investment Co. Ltd. Katika mkataba huo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania litatoa ekari za mraba 26,082.87 katika eneo la plot number 1255 Masaki, Jijini Dar es Salaam. Katika mkataba huu mjenzi

akikamilisha mradi kwa mujibu wa taarifa zilizopo, ataendesha eneo hili kwa muda wa miaka 40 na baada ya hapo eneo litarudi jeshini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri atueleze kama mkataba huo umesainiwa; na kama haujasainiwa nitaliomba Bunge hili Tukufu lielekeze kwamba mkataba huu ambaa unaweza ukawa wa kinyonyaji upelekwe katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ili uweze kupitiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu limewahi kuingia mikataba ya aina hii na ambayo baadaye ilikuja kuonekana imedhalilisha Jeshi, imedhalilisha Serikali ukiwemo mkataba wa Meremeta. Sasa ni vizuri tukajihadhari, lakini kibaya zaidi, ni kwamba kampuni ya *Henan Guijo Industry Co. Ltd.* ambayo imeingia mkataba na Jeshi la Wananchi au inataka kuingia mkataba na Jeshi la Wananchi, inajifunga mkataba mwingine na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hiyo itajenga pia nyumba ya Dkt. Hussein Mwinyi iliyopo plot number 2435/5 eneo la Sea View, Upanga Jijini Dar es Salaam. Kampuni hiyo ndiyo itakayolipia gharama za ujenzi...

## TAARIFA

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea naomba ukae, kuna taarifa. Taarifa Mheshimiwa Nchambi.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(8) ambayo inapelekea Kanuni ya 64(a); "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli." Ekari 26,000 ni sawa hekta 10,000 ambazo ukitembea Masaki unahitaji kutembea kilometra 10 za mraba. Sasa eneo la Masaki utakapolitembelea, halifiki kilometra 10 kwa kwenda straight na baadaye uende mraba tena na kilometra 10. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimpe taarifa mse maji anayesema kama anao uhakika, mimi ninao uhakika kwamba eneo la Masaki halifiki square kilometer 10 ambazo ni heka 26,000. Je, taarifa hiyo ana ukweli gani kuhusiana na hesabu anazozitoa ndani ya Bunge hili? Nashukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema mita za mraba, labda hakusikia vizuri. Naomba pia unilinde kwenye muda wangu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mkataba huu, kama ambavyo unaweza kuwa ama umesainiwa ama haujasainiwa, ni kwamba mjenzi ndiye ambaye atajenga pia nyumba ya Dkt. Mwinyi. Sasa kama madai haya ni ya kweli, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie huu siyo mgongano wa kimaslahi? Je, kwa mkataba huo, haina maana kwamba jeshi letu linaingizwa kwenye mkataba wa kinyonyaji kwa kuwa Waziri ananufaika? (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Tutatafutana sasa hivi hapa! (Kicheko)

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kwamba uchunguzi ufanyike na vyombo vinavyohusika, vimchunguze Mheshimiwa Waziri na vipeleke taarifa kwenye Bunge hili Tukufu kwa kuwa uchunguzi huu ni muhimu kwa sababu unahuhoja muhimu kabisa iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu. (Makofii)

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Kuhusu Utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea, tafadhalii naomba ukae. Mheshimiwa Nchambi, utaratibu!

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo alilolisema liko katika Hansard na ninao uhakika, amesema ni ekari 26,000. Kama yeye anadhani mimi nilipitiwa, ninao uhakika, tuangalie Hansard.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, unapokosea aidha kwa kuteleza ama kutojua, ama kuropoka, vyovyote vile, kanuni zinakutaka umtake afute kauli ambayo hana uhakika nayo. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ukitoa Taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) inasema hivi; "Spika atamtaka Mbunge anayesema aketi na kupata taarifa hiyo." Kifungu kidogo cha (9) kinasema; "Mto taarifa atakapomaliza na kuketi, Spika atamwuliza Mbunge aliyekuwa akisema mwanzo kama anaikubali au haikubali taarifa hiyo, kabla ya kumruhusu kuendelea kuchangia hoja hiyo."

Kwa hiyo, Mheshimiwa Nchambi, nimemwuliza Mheshimiwa Kubenea kama anaikubali taarifa yako. Kama unaomba jambo lingine Kikanuni, hilo pia

nitakuruhusu; lingine lakini! Kuhusu taarifa, utaratibu tuliofuata ndiyo ambao unakubalika Kikanuni. (Makofi)

Mheshimiwa Kubenea, naomba umalizie. (Makofi)

**MHE. SAED A. KUBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumalizia hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Wananchi tunalipenda sana, Taifa letu tunalipenda sana, Bunge letu Tukufu tunalipenda sana, lakini mambo ya namna hii yanatia doa Jeshi letu na Taifa letu. Kuna mambo yanazungumzwa mengi sana kwenye Taifa hili. Baadhi ya kampuni ambazo zinatuhumiwa katika maeneo mengine kwamba zimefanya biashara na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama likiwemo Jeshi la Polisi nazo pia zinatajwa kufanya biashara na Jeshi la Wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kampuni ya Lugumi, baadhi ya nyaraka mbalimbali zinaonyesha kwamba Kampuni ya Lugumi iliwahi pia kufanya biashara na Jeshi la Wananchi na iliwahi kuuza silaha kutoka Taiwan lakini Jeshi letu lilizikataa kwa kuwa zilikuwa chini ya kiwango. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Anasoma!

**MBUNGE FULANI:** Umemwandikia wewe! (Kicheko)

**MHE. SAED A. KUBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri jeshi letu likajiepusha na makampuni kama haya. Kwa nini vitu hivi vinajirudia mara kwa mara? Tunalipongeza sana kwa kazi nzuri ambayo Jeshi limefanya katika Taifa hili, limefanya kazi kiuadilifu, kiuaminifu na kwa kweli mambo mengi limepakaziwa. Jeshi linashinikizwa kufanya mambo kwa sababu za kisiasa. Mikataba mingi ambayo Jeshi hili limeingia ikiwemo Meremeta ni kwa sababu za kisiasa. Mambo mengi ambayo yanatokea Zanzibar, yamefanyika kwa mashinikizo ya kisiasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema haya, tunataka jeshi letu liondoke huko, likafanye kazi ya kulinda amani katika Taifa letu na kufanya kazi ya kulinda mipaka yetu. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kubenea muda wako umekwisha.

**MHE. SAED A. KUBENEÀ:** Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Hassan Omari King atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Suleiman Nchambi ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na salama kwa leo kukutana hapa kujadiliana kuhusu bajeti ya ulinzi na usalama katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa neno moja; kule kwetu kuna ndege kwa kiarabu anaitwa *bull bull*, kwa Kiswahili anaitwa kasuku. Kasuku ukisema hodi, basi naye anasema vilevile hodi! Sasa kasuku yule ile hodi hajui kama maana yake ni nifungulie mlango. Kwa hiyo, imekuwa yeye ame-copy tu kwamba ndiyo amesema hodi. Nafikiri mmeshuhudia, watu wanazungumza ekari, halafu baadaye wanageruza maneno kwa sababu ni maneno ya *bull bull*. Anaondoka *bull bull!* (Kicheko/Makofisi)

Mimi najikita zaidi katika kuongelea masuala ya maslahi ya wanajeshi wanapokuwa kazini na wale wanaostaafu. Nachelea kupoteza muda mwangi, nitakuwa consistency na wale waliochangia suala hili. Nitajaribu kuongelea kuhusu wastaaafu wa Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mawili; kuna watu waliingia kwenye mikataba huko katika majeshi tunafahamu, pengine watachukua kwa mkupuo au watakuwa wanapata pensheni. Badala yake wakaja wakataka ku-reverse, kuja kujirejesha tena upya. Kwa hiyo, hawa ilikuwa wazingatiwe jambo lao hili kwa sababu lengo ni kulinda usalama na amani ya nchi yetu na lengo ni kuwa na wanajeshi wa akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wote hawa walioingia kwenye mambo hayo mawili whether ya kuchukua kwa mkupuo au kupata pensheni, lengo letu kama Taifa sasa hivi ni kuwaweka kama askari wa akiba na tusiwe na wapinzani katika ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kushukuru, watu wengi sana wameunga mkono hii bajeti. Hii bajeti imeungwa mkono kwa vitendo na watu wote, kwa hiyo, na mimi naiunga mkono bajeti hii na hoja hii. (Makofisi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napata mashaka kidogo; inakuaje mtu umekaa ukimwona mwanajeshi unaanza kutetemeka, una nini wewe? Una kitu gani ulichoficha? Kuna ajenda gani? Kwa nini wewe uwe unaona taabu kukutana na majeshi ya ulinzi na usalama? Kwanza anza kujangalia kutokea hapo, una mashaka gani? (Makofisi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongee kitu kimoja; Jeshi la Ulinzi na Usalama kazi yake moja ni kulinda mipaka yetu nje na ndani. Mimi ni shahidi, bomu la mwanzo kulipuka baada ya uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba pale Zanzibar lililipuka mbele ya Kanisa Anglikana Mkunazini, lililipuliwa na majeshi, tulitarajia aende nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, bomu la pili lililipuka *round about* ya Michenzani upande wa njia ya kutokea Bwawani. Likalipuka la kwanza pale, baada ya dakika 10 likalipuka bomu la pili; na mimi mwenyewe nilikuwa niko maeneo ya pale pale kwa sababu ni maeneo yangu ya kujidai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mabomu ikiwa tunao maadui wa ndani, kwa nini Jeshi letu la ulinzi lisifanye kazi ndani? Mabomu mengine mawili yalienda kuteguliwa katika Kambi ya JKU Zanzibar Saateni. Yametegwa na haya mabomu, tunafikiri jukumu hili ya kutegua hayo mabomu akafanye nani? Jeshi la Wananchi wa Tanzania liendelee kufanya kazi zake ndani na nje ya mipaka yetu, kwa sababu bado tunao maadui wa ndani na nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu waliokuwa wanazungumza kwamba jeshi lilienda kuwatisha watu wasishiriki uchaguzi wa tarehe 20 Machi, wamemsahau aliywatisha! Hivi dakika ile ile kiukweli wameshahau? Basi akili hizi zitakuwa za kuku, maana kuku ukimwinga, anaondoka. Baada ya dakika chache kuku anarudi pale pale. Itakuwa wana akili za kuku hawa, wameshahau aliyewaambia wasiingie kwenye uchaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli Jeshi la Wananchi ndiyo limeenda kusimamia kwamba watu wasiingie kwenye uchaguzi wa marudio? Mtu anazungumza maneno hayo hapa wakati anafahamu kwamba kiongozi wake ndiye aliyesema hayo maneno. Sasa leo wanakuja kuyaleta hapa, nashangaa sana! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo lilizungumzwa hapa na wengi kila mtu akikaa anasema kwamba anaunga mkono. Maneno yaliyozungumzwa na Kambi ya Upinzani, mimi namheshimu sana mzee wangu. Maneno aliyozungumza kwamba, demokrasia ya Zanzibar iliharibiwa na majeshi, nashangaa sana. Naweza nikasema, kuna mshairi mmoja anasema; "masikini roho yake, kioo kimemcheza." (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli alijipima na akajiangalia kwamba yeye aje azungumze maneno hayo hapa, amewahi kuwa kiongozi wa ngazi za juu kabisa, maskini roho yake kioo kimemcheza! (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine unapoambiwa ufanye jambo, ujaribu kutazama, wenzako wanakutoea hao! Usiwe zumbukuku ulimwengu uko huku! Ni lazima ujiangalie huko katika hali gani? (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono hoja lakini kingine cha umuhimu kabisa katika kuangalia masuala haya ni hali ya uwiano katika ajira na utawala wa Jeshi la Wananchi, hili ni Jeshi la Wananchi wa Muungano wa Tanzania, ikiwemo Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa hiyo, hata katika utawala, leo wametajwa pale Majenerali nikasema na mimi nitasikia jina la kwetu sikulisikia, tuwe na uwiano katika masuala haya na kwenye ajira pia. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni la msingi na kubwa zaidi, Jeshi letu litatusika na ulinzi wa mipaka katika bahari kuu. Hili liangaliwe kwa sababu ni jambo la kiuchumi na linahitaji zana za kijeshi, lakini pia kuzingatia uharamia unaofanyika katika nchi jirani ikiwemo Somalia lakini uchujaji uwe mzuri kwa sababu pia na wavuvi wetu nao huwa wanakwenda kuvua. Nilimsikia Mbunge wa Bumbwini aliuliza swali katika kipindi cha maswali na majibu kuhusiana na suala hili. Kwa hiyo, naomba masuala hayo yazingatiwe na yafanyike vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo ni muhimu, nimejaribu kupima hapa na nime-synthesis hoja nyingi sana...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo, Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Sasa tutamsikia Mheshimiwa Tauhida Nyimbo ambaye atachangia badala ya Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia toka Bunge hili lianze, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa na wananchi kwa kura nyingi. Pia nimpongeze Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia kwa kuteuliwa, imani yetu wanawake hatatuangusha maana tuna uhakika na kazi anazozifanya. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa wakati huu nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Ali Shein kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na kwa imani yake na Wazanzibari. Nasema nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa sababu ameonesha hakika yeye ni kiongozi na kiongozi wa kupigiwa mfano. Uvumilivu wake, utu wake, ubinadamu wake umefanya leo Zanzibar iwe ni nchi ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu hakuwa kiongozi ambaye ni mchu wa madaraka, hakuwa kiongozi ambaye anashibisha tumbo lake, amekuwa kiongozi mwenye kuitakia wema Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Ukimya wake kwa muda wote na maneno yote kwa muda wote aliokaa kimya lengo lake lilikuwa ni moja kuhakikisha Zanzibar iko salama, kuhakikisha Tanzania iko salama. Kama Rais alikuwa na mamlaka tosha na alikuwa na kila cha kufanya na alikuwa na aina ya sababu ya yeye pia kujitangaza lakini hakufanya hivyo, alitaka kwenda kwa utaratibu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwashukuru Mawaziri wote, imani yangu kwenu ni kwamba tutapiga hatua, hapa tulipo tutaendelea kusonga mbele. Tunaitegemea Tanzania mpya katika miaka mitano hii ijayo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu pia ziende kwa wapiga kura wangu ambao ni Wanawake wa UWT, Mkoa wa Magharibi. Nawashukuru kwa kunirudisha Bungeni na kuniamini kama mtoto wao naweza nikafanya kazi, nawaahidi sitowaangusha. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kama mwanamke, ujasiri wako tumeuona na tumeona ukifanya kazi kama mwanamke ambaye hutuangushi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchangia. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, kwa bajeti yake nzuri aliyoileta na nipongeze kikosi kizima cha Jeshi la Wananchi wa Watanzania. Kazi zenu ni nzuri zinaonekana ndiyo maana ukaona watu wanapiga kelele, mngekuwa hamfanyi kazi watu wangenyamaza kimya lakini kwa kuwa mnafanya kazi ndiyo maana watu wakapata fursa ya kunyanya midomo yao. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wananchi wake kwa ujumla, niwapongeze kwa kumrudisha kila siku Bungeni kwa mbwembwe. Hii yote inaonesha ujasiri wake na uwezo wake wa kufanya kazi. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, sura ya tisa katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri imezungumzia suala zima la maendeleo ya viwanda, kilimo na ajira kwa ujumla. Vijana tumaini kubwa liko kwake. Akitaka kujua kama Tanzania vijana matumaini yako kwake aone wakati unapofika wa kuchukua watakaojiunga na JKT au jeshi kwa ujumla. Vijana wengi huhangaika na nafasi hizi kwa sababu matumaini yao kama vijana wa Tanzania yako kwake. Nadhani ni vema wakashirikiana na Wizara ya Viwanda na Kilimo wakaona ni jinsi gani wanaweza kuwasaidia vijana wa Tanzania. Naamini kwa kufanya hivyo tutaendelea zaidi kama vijana wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye suala zima la uchaguzi. Toka tulipoanza Bunge hili hoja kubwa na michango ya Wizara zote zilizochangiwa ni hoja ya uchaguzi wa Zanzibar. Uchaguzi wa Zanzibar umekwisha, Rais yupo, anatawala, tunaendelea kama kawaida. Sasa hizi kelele unaenda kumpigia Jeshi la Wananchi wa Tanzania amekufanya nini? Kwa sababu wanaposema wanadhani hawana uwezo wa kuingia humu ndani ili kujibu. Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeitendea haki Zanzibar. Kati ya vyombo ambavyo tunastahili kuvipongeza Tanzania ni pamoja na Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa na shida ya kuzungumza hapa, nazungumza kwa sababu jeshi hili halikumpiga mtu, halikumchapa mtu, halikumtukana mtu, halikufanya kitendo chochote cha kuweza kuzungumzwa kwenye Bunge hili. Jeshi lile limekaa Zanzibar kwa amani, limepita kwa mbwembwe, hivi jeshi linapita wewe unaogopa nini? Una masuala gani ya kukufanya uliogope Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Hebu tuambie hoja yako ya msingi juu ya Jeshi hili ni nini ili tuwapeni majibu ya uhakika. Toka Bunge lianze tumekosa jibu la kuwapa kwa sababu hatukuona suala la msingi juu ya masuala yenu mnayozungumza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi limekaa Zanzibar...

**MBUNGE FULANI:** Kwani wewe Waziri ujibu?

**MBUNGE FULANI:** Wewe endelea.

**MBUNGE FULANI:** Nenda huko wewe.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO:** Namsamehe bure.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida ongea na Kiti.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO:** Kwa sababu kati ya wacheza mdundiko naye yumo, endelea na mdundiko wako. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliambiwa niendelee, nilikuwa naweza kuendelea, lakini nilikuwa nataka nimtambulisse tu kati ya walioingia humu ndani wanaocheza ngoma ya mdundiko na yeye yumo ndiyo maana anapiga kelele anahemkwahemkwa hapa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa nane wa kitabu cha hotuba ya Waziri wa Jeshi la Ulinzi kimezungumzia suala zima la kuimarisha muungano, mlidhani muungano unaimarishwaje? Mlidhani ile kuo na kuoana tu kunatosha kuimarisha muungano? Muungano utaimarishwa na Jeshi la Ulinzi. Mimi niwapongeze, kati ya mtu ambaye anajisikia ufahari mkubwa leo kusimama hapa kuziona zile kofia zipo pale mmoja wao ni mimi. Tunawapenda, fanyeni kazi na kila uchaguzi ukifika msimsubiri Waziri awapeni amri. Jenerali upo, viongozi wote wapo tunataka mshuke iwe kwa boti, iwe kwa ndege na kadhalika lakini muingie Zanzibar kufanya kazi. Hata uchaguzi ukirudiwa warudi, wakitaka kuja kesho waje, kitakachotokea tunakuombeni mje msimsubiri amri, fanyeni kama wajibu wenu, fanyeni kama kazi zenu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia mambo mengi kuhusu uchaguzi lakini tu tungependa kuwaambia kwamba uchaguzi pamoja na kwisha, kulikuwa na hoja zinazongumzwa na Tume, Mwenyekiti wa Tume alikaa kwenye TV zikachambuliwa kasoro, kila kitu kilichoonyeshwa kule, hamkuwa na hoja na ninyi kutafuta Kipindi mkajibu, mbona mlinyamaza kimya? Kama masuala mnayozungumzia kwamba document mnazo, mna ushahidi hata sisi document tunazo mpaka leo, kura mbili mbili zipo, saini wanaweka watu wawili wawili zipo, hakuna kilichokuwa hakipo! Mmebaki mnawinda lakini hayo mawindo yenye we mnayowinda hakikisheni kwamba hayapo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo yangu yalikuwa hayo machache, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Nchambi, Mbunge wa Kishapu.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu wa Spika, wabheja sana. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana nchi yetu kwa maana hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya na hakuna mti mbaya uzaao matunda mazuri. Jeshi hili zuri limetokana na matunda yetu sisi Watanzania. Ni mti mzuri umezaa Amiri Jeshi mzuri, umezaa Mkuu wa Majeshi mzuri na Wanajeshi wazuri, watiifu, hodari na wavumilivu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme jambo moja la msingi sana. Unaweza ukawa na sikio halisikii, unaweza ukawa na macho, hayaoni na unaweza ukawa na mikono, miguu, viungo vya mwili wako usijue neema hiyo aliyokupa Mungu ni neema ya aina gani. Maana katika Quran tunasema,

*fa'amma bini'imati rabbika fahaddith (na tuzisimulie neema ambazo ametupa Mwenyezi Mungu). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Wabunge hapa leo nimeshangazwa sana, sisi wengine kwa bahati nzuri treni ya sasa hatukuidandia tumeanza chipukizi darasa la tatu lakini nashangazwa sana na Bunge hili, Mbunge anasimama pengine hajui aelimishwe, *this is not vocational training centre*, hili ni Bunge. Watu wamekutuma hapa siyo kuja kufundishwa. Wamekutuma kuja kufanya kazi wakiamini wewe ni mwakilishi wao, unaomba kufundishwa Bungeni, haya ni mambo ya ajabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka hata Mungu mbinguni ana jeshi lake, malaika na vimetaja vitabu vya Mungu. Jeshi letu naomba sana Mheshimiwa Mwamunyange liheshimike. Nilitegemea sana Wabunge wote tumuunge mkono Rais, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuvaat *combat* ya jeshi na kuanza kukimbia. Nchi zote duniani zinakimbia sisi hapa Wabunge, Bunge liliopita na Mabunge yaliyopita tulikuwa tunalalamika tunatambaa leo Magufuli anaikimbiza nchi watu wamekazana kuleta mambo ya u-baby hapa hatutakubali. Watu wamekazana kuleta mzaha hatutakubali. Watu wanataka kuleta kejeli na jeshi letu hatutakubali. Sisi wengine bado vijana, tunahitaji kuona matunda ya Taifa letu na wajukuu wetu wakute amani ya Taifa hili, jeshi halina siasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mwamunyange kwamba yamesemwa mengi sana lakini mimi nataka kumwambia yeye, Maafisa na Wanajeshi haya yaacheni humu humu, tuchukue mazuri yaliyosemwa. Jeshi sehemu yoyote duniani linalo heshima ya juu sana. Wamesema baadhi ya Wabunge hapa, hawa wote wanaopiga kelele humu wakisikia risasi moja tu wanabanana mlangoni...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Hawatakwenda ulipotokea mlipuko wakaangalie lakini jeshi linakimbilia...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi naomba ukae.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Wabheja sana.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayezungumza anajaribu kupotosha umma kwa kutuchonganisha watu wa Kambi ya Upinzani...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Sikilizeni basi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa ongea na Kiti.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mzungumzaji anayendelea kuchangia anajaribu kupotosha umma...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kwa kutuchonganisha kana kwamba Kambi ya Upinzani na Hoja ya Upinzani inapingana na Jeshi la Wananchi.

**WABUNGE FULANI:** Kanuni.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesimama kwa Kanuni gani?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mimi siyo wa *level* ya kushukuru Magufuli tu naomba unisikilize, kaa kimya wewe. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Asome Kanuni.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kwa hiyo, naomba asipotoshe umma hakuna kwenye Kambi ya Upinzani mtu anayelipinga jeshi wala hakuna mtu ambaye haliheshimu Jeshi la Wananchi.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Aongee hoja za msingi za kujenga Taifa. Hawa Wanajeshi siyo watoto asijikombekombe.

**WABUNGE FULANI:** Soma Kanuni.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Anajikombakomba hawa siyo watoto anapotosha umma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Msigwa?

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri sana huyu ni kama Mchungaji mwenzangu kwa sababu na mimi Vitabu vya Mungu navijua, namheshimu sana. Naomba nisipokee taarifa yake niendelee kutiririka na mtiririko ambao naona una maslahi kwa Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa yamesemwa mambo, silaha feki ziliuja, haya ni mambo very serious. Kama mtu anaweza akajua taarifa za ndani za jeshi, unayo Kamati ya Maadili imuite Mbunge aliyetoa kauli hiyo kwa sababu tunaporopoka hapa ziko nchi jirani zinajua...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Kumbe jeshi letu linazo silaha feki, linaweza likafanya manunuzi ya silaha feki jambo ambalo litahatarisha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi naomba ukae, kuhusu utaratibu, Kanuni gani imevunjwa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kanuni ya 64(1)(a).

**NAIBU SPIKA:** Yes Kanuni gani imevunjwa?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kanuni ya 64(1)(a).

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mtu hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji anayezungumza hapa anasema kuna mchangiaji aliyezungumza juu ya jeshi kununua silaha feki. Mheshimiwa Kubenea alimzungumzia Lugumi na mkataba ambao alitaka kuingia na jeshi akapeleka silaha zikagundulika ziko chini ya kiwango na jeshi likakataa. Pia Mheshimiwa Lugumi huyu huyu ana tuhuma zingine Jeshi la Polisi. Alikuwa anajaribu kutoa warning. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachomshauri ndugu yangu hapa, mosi kama hujajipanga kuchangia usimezeshe watu maneno changia hoja...

**MBUNGE FULANI:** Usihutubue, usihutubie.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa manufaa ya jeshi kwa manufaa ya Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo ili ajipange. Kama alimezeshwa na Jenista hapa akaseme, basi amwambie ammezeshe vizuri. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi naomba uendelee ukizingatia hiyo Kanuni ya 64(1)(a).

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu mtoa taarifa aliyepita hapa wakati...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi naomba ukae Chief Whip amesimama, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Kanuni ile ile ya mwongozo, Kanuni ya 68(7), naomba mwongozo wako. Hapa ndani sasa hivi kinachoendelea...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo tena?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Naomba mwongozo kwa sababu kulikuwa hakuna mtu anayezungumza.

**WABUNGE FULANI:** Nchambi alikuwa anachangia.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hii inasema mtu yeote atasimama wakati hakuna mtu mwingine anayeongea na ataomba mwongozo.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Katibu hapa ameniambia huyu amesimama kabla sijamuita Mheshimiwa Nchambi. Endelea Mheshimiwa Jenista. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ninaouomba ni huu ufuatao. Bunge hili sasa badala ya kutumia muda mchache uliopo kuchangia na kujikita kwenye hoja za msingi za kuboresha huduma za Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kumshauri Mheshimiwa Waziri,

Waheshimiwa Wabunge sasa na hasa tunapoanza kuchangia Wabunge kutoka katika Kambi ya Chama Tawala, imeanza kuonekana tabia ya kukatishwa bila utaratibu na kufanya mjadala huu usiende kwa kuzingatia muda na uhalsia.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa sasa na tabia ya kuunganisha mambo yasiyo ya ukweli kwa mfano Mheshimiwa Halima hapa na yeye anatumia muda wa Bunge vibaya...

**MBUNGE FULANI:** Na wewe unatumia muda vibaya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Anafikiri kwamba hawa Wabunge wote wa CCM wamekuwa wakifundishwa kusema na Chief Whip lakini wana uhuru wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, kama tutaendelea hivi, hatuoni kwamba unaruhusu Bunge hili kutumia muda huu vibaya na kuendelea kupotosha vitu humu ndani vinavyohusu masuala nyeti ya ulinzi na usalama wa nchi hii ya Tanzania? (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Mbunge aliyejewa anachangia ameshashauriwa kwamba azingatie Kanuni ya 64(1)(a). Kwa kuzingatia muda uliobaki sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 72, naomba Waheshimiwa Wabunge mkubaliane tu na mimi tumalizie hawa waliobaki kuchangia ili tuanze sasa kuzungumzia bajeti. Mheshimiwa Nchambi malizia dakika zako zilizobaki ukizingatia hiyo Kanuni ya 64.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wabheja sana lakini naomba muda wangu uulinde, dakika sita zimepotea kwa taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Wewe.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee wakati nikitoa taarifa alisema mimi siyo size yake ni kweli, wala mimi sikatai kwa sababu amemchukua dada yetu amekwenda naye kule ametushinda. Mimi wala siwezi kuona kwamba yeye hajashinda ni kweli ameshinda na mimi upande wao sijachukua mtu wa aina yangu nikamleta huku. Kwa hiyo, yeye ni mshindi, namkubalia kabisa, sawasawa aendelee na dada yetu hatuna shida. (Makofij/Kicheko)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirejee katika hoja. Ninachotaka kusema, Ndugu zangu Wanajeshi, Maafisa wa Jeshi na Mkuu wa Majeshi, Wabunge ndiyo wenye uwezo wa kuongeza fedha ama kupunguza. Wengi wamekuwa hapa wakilalamika kwamba haiwezekani jeshi likose fedha, Bunge hili Afande Mwamunyange ndilo lenye mamlaka ya kuielekeza na kuishauri Serikali itoe fedha. Sasa hawa wenzetu wanaoendelea kubeza na kudharau jeshi, jambo la silaha ambalo lilitolewa taarifa nimesema ni serious sana, naomba sana suala hili lichukuliwe na ofisi yako kuhusiana na Mheshimiwa Kubenea aliyetoa taarifa hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili hatuwezi kukubali kuliingiza jeshi letu katika kashfa kwamba mpaka silaha zimekuja, zimeonekana feki, siri za Kamati ya Ulinzi na Usalama awe nazo mtu mmoja hili ni jambo la hatari sana kwa jeshi letu. Ni jambo ambalo linaweza likahatarisha hata usalama. Sehemu yoyote duniani jeshi ndicho chombo makini kinacholinda Taifa lolote. Tunao uhuru wa aina tatu. Tunao uhuru wa bendera, wa mawazo na kiuchumi lakini yote haya ni bure kama hatuna vyombo vinavyoweza kusimamia uhuru wa mawazo yetu, uhuru wa kiuchumi na hata bendera yetu kusimama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa sana niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tusiweke kejeli kwa jeshi letu. Jeshi letu linafanya kazi nzuri, tusileté jambo lolote linaloashiria kulibeza jeshi letu. Jeshi letu linafanya kazi nzuri. Tena niwaombe sana maana katika Maandiko Matakatifu ukienda katika Mhubiri 9:10 inasema, lolote unaloweza kulifanya lifanye kwa mkono wako sasa maana hakuna hekima, maarifa, busara wala shauri unaloweza kulifanya huko kuzimu uendako. Waheshimiwa Wabunge, mikono yetu ifanye mambo sasa wakati sisi ni Waheshimiwa Wabunge. Tulitengeneze jeshi letu, tulitie moyo, tulisaidie lakini tusiendelee kuwa tunazomea huku tunapuliza kwa utaratibu wa panya. Mimi nishukuru sana kwa sababu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi muda wako umekwisha.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wabheja sana. Naunga mkono hoja na Mungu awabariki. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, atafuatiwa na Ally Seif Ungando na tutamalizia na Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha leo salama na mimi kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme naipongeza hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ni nzuri, iko vizuri na imekaa vizuri. Nimpongeze Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, anafanya kazi nzuri, yuko imara na jeshi liko imara. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika niende moja kwa moja kwenye hoja yangu. Ukitazama Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Cap. Na. 193 ya mwaka 2010, (R.E), kifungu cha 6(2) kinataja umri wa mtu au umri wa Mtanzania kwenda Jeshi la Kujenga Taifa, ni kati ya miaka 16 – 35. Kwa nini nataja vifungu hivi? Nchi yetu zaidi ya 60% ni vijana na vijana ndiyo nguvu kazi ya kujenga nchi hii. Tusipowalea vijana vizuri, tusipowajenga vijana vizuri hakika mustakabali wa nchi yetu na hasa kwenda kwenye maendeleo na hasa kuipeleka nchi yetu katika uchumi wa kati itatuchukua muda mrefu sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji tuwajenge vijana katika uzalendo waipende nchi yao. Tuwajenge vijana katika utii na nidhamu, tuwape stadi za kazi, tuwape uaminifu ili wawe wanaitika kwa sauti moja ya kiongozi anaposema, nchi hii itakwenda vizuri, nilitaka nilisisitize hili. Hakuna chombo kingine kikubwa ambacho kinaweza kuwarekebisha vijana hawa, nalionna Jeshi la Kujenga Taifa hata JKU – Zanzibar, ni vyombo vyaa muhimu sana katika kuandaa vijana wetu. Ni vyaa muhimu sana! Naomba tuwekeze vilivyo kwenye majeshi haya, Jeshi la Kujenga Taifa na JKU. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwekeze kwa namna gani? Wengi wamechangia hapa, kuna chuo kikubwa cha VETA kinataka kujengwa Kongwa, naomba tuharakishe ujenzi huu, tuwapeleke vijana wetu huko VETA. Hata kwenye makambi, namkumbuka sana Mwalimu Nyerere, namkumbuka sana Mzee Karume, walipoanzisha majeshi haya waliainisha maeneo muhimu sana ambayo mpaka sasa hivi tunayatumia kwenye kambi za Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi. Kuna maeneo mazuri ya kilimo, mimi nimepitia pia, tulikuwa Mgambo Tanga kule, tulikuwa tunalima mahindi Gendagenda, tulikuwa tunalima machungwa na maeneo mengine kama Itende na Chita, yamekaa vizuri kwa ajili ya uchumi. Tukiwekeza vizuri hawa hawa vijana watazalisha, watajilisha na watailisha nchi lakini tutakwenda kwa pamoja wakiwa watii ndani ya jeshi na kuititia Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja la msingi sana. Nimesikia maneno ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amesema mambo mazuri, mimi ni muungwana, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Kwenye mazuri mtu nitampongeza, akitengeuka nitamwambia hapo hapana! (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja alilisema, sim-quote lakini najaribu kutoa tu ile maana kwamba anashangaa Mheshimiwa Rais anateua Wanajeshi wastaafu kuwa viongozi kwa mfano Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa kwamba hawa wasingekwenda huko kwa sababu ni Wanajeshi. Mimi nasema hapana! Hawa ni *reserve army*, *reserve army* ni yule mtu ambaye amekwenda jeshi either amepata kazi au hajapata lakini ni *reserve army*, lazima tumtumie. Amejifunza utii, anaweza kufanya kazi na ni mzalendo huyu na wamefanya kazi nzuri sana watu hawa. Tunawaona wanachapa kazi sana hawa Wanajeshi, kwa mfano Wakuu wa Mikoa tumeona wanafanya kazi nzuri sana, tuwatumie. Hiyo ndiyo maana ya jeshi la akiba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nihame hapo niseme jambo moja kuhusu nafasi hizi za kwenda Jeshi la Kujenga Taifa. Vijana wako tayari kila mahali kwenda Jeshi la Kujenga Taifa lakini kumekuwa na ukiritimba kwenye nafasi hizi. Nadhani nafasi hizi zimegawanywa kimikoa na kiwilaya, kila wilaya na mikoa ina nafasi zake. Naomba tulismamie vizuri suala hili kwa mfano Mkao wa Singida wanatoa vijana kutoka Arusha wanawaleta Mkao wa Singida. Wale viongozi, washauri wa Mgambo wanatawala zoezi hili, wanawanyima haki wale vijana wa kwenye maeneo yale. Naomba mlisimamie vizuri jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu. Tuliomba hapa wakati tunachangia Wizara ya Kilimo kwamba Wanajeshi wakati wa amani wasaidie maeneo mengine. Tuna vyombo hivi, wana ma-grader, vijiko, malori ya ujenzi, hebu vyombo hivi vitumike kutusaidia kwa mfano kuchimba labda mabwawa na kujenga barabara, wananchi tuko tayari kuchangia mafuta.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtuka muda wako umekwisha.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, halafu Mheshimiwa Angelina Malembeka ajiandae atachangia nafasi ya Mheshimiwa Ally Seif Ungando.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza leo nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Donge kwa kunichagua tena kuwa Mbunge kwa kipindi cha pili sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kulipongeza sana Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Nawapongeza kwa kazi nzuri, mwanana na yenye kuvutia wanayoifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie rafiki zangu sitawatukana, wewe nisikilize tu na ndiyo maana nimekaa ukanda wa Gaza makusudi. Nataka niwaambie marafiki zangu, mshukuruni sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Washukuruni sana hawa watu wafuataa, Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Mheshimiwa Dkt. Shein, Mkuu wa Majeshi hawa watu ni wastaarabu sana, waungwana sana, washukuruni sana hawa watu. Kwa nini nasema hivyo? (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Tuambie.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika mwenye mamlaka ya kutangaza matokeo ni Tume ya Uchaguzi, ndiyo utaratibu tuliojiwekea. Leo anajitokeza mhuni mmoja anajitangaza ye ye ndiyo Rais, hebu niambieni nyie, nchi gani, jeshi gani...

**MBUNGE FULANI:** Wewe!

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Kama kuna mtu anaweza kuja kunipiga aje mimi nasema. Nchi gani, jeshi gani ambalo mtu amejitangaza kuwa Rais halafu limuachie tu kienyeji hivi hivi? (Makofi/Kicheko)

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Nawaambia washukuruni sana, hawa watu hawa wamewasaidia, wapongezeni.

**MBUNGE FULANI:** Zima *microphone*.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Bibie ukiizima nakupiga makofi. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Hama.

**MBUNGE FULANI:** Zima.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kambi yake huku.

**MBUNGE FULANI:** Zima *microphone* hiyo.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie Waziri wa Ulinzi angekuwa Sadifa...

**MBUNGE FULANI:** Zima microphone hiyo.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Anatutukana hapa.

## TAARIFA

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa naomba ukae ili upewe taarifa. Mheshimiwa Maftaha taarifa.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza hivi sasa kwa kutumia Kanuni hii ya 68(8) kwa wale wasiofahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayezungumza amezungumza maneno ambayo kimsingi hayana ukweli kusema kwamba eti kuna mtu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mhuni amejitangazia matokeo. Naomba nimpe taarifa kwamba hakuna mhuni yejote nchi hii ambaye ameamua kujitangazia matokeo na Jeshi la Wananchi likakaa kimya. Yeye kwa mawazo yake alidhani Jeshi la Wananchi ni jeshi la Chama fulani siyo Jeshi la Jamhuri ya Muungano, nimpe taarifa kwamba hili jeshi ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania wote na siyo Jeshi la Chama cha Mapinduzi. Ahsante. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo itakuwa ni taarifa ya mwisho. Mheshimiwa Sadifa.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika, vyombo vya habari viro, Maalim Seif Sharif Hamad alijitangaza kuwa Rais wa Zanzibar kwamba yeye ndiye aliyeshinda, alijitangaza mwenyewe.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Ndiyo maana nasema kwa kupitia kitendo hicho ni uhuni na hii kauli siifuti, ni uhuni.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Kama sio uhuni ni nini.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo, mwongozo.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Kama ingekuwa majeshi ya wenzetu kwa mfano China, leo hii Maalim Seif angekuwa hayupo, ule ni uhaini!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Nani aliyekuwa hajaona hapa? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Usilete ujinga wewe.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Nawaambia mshukuruni sana Dkt. Mwinyi, Waziri wa Ulinzi angekuwa Sadifa nawaambia mngekuwa mnavuja nyie! Msiniulize wapi panapovuja, nawaambia kweli! Kwa nini niwaambie uwongo huo ndiyo ukweli.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mshukuruni sana huyu Waziri...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mshukuruni sana Mkuu wa Majeshi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa naomba ukae.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Sawa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Anaita viongozi...

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Tumekubaliana hivi, Mheshimiwa Maftaha ametoa taarifa, nimesema hivi kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1) hatutaweza kumaliza hili zoezi lililo mbele yetu.

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa naomba umalizie.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muda wangu uzingatiwe.

**MBUNGE FULANI:** Wewe Sadifa kaa chini!

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa Katiba ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara naomba uzime microphone yako tafadhali.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Afute kauli, hawezi kuita viongozi wetu wahuni, anaitaje viongozi wetu wahuni?

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu unakwenda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa naomba umalizie.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Hawezi kuita viongozi wetu wahuni.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwenye mamlaka ya kuteua wakuu wa mikoa ni Rais pekee wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Bara lakini kwa upande wa Zanzibar ni Rais wa Zanzibar.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie wenzangu hawa, wote aliowateua Rais siyo Wanajeshi wale wameshastaifu.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani walipaza sauti wakisema afute kauli, afute kauli)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa naomba ukae.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadifa naomba ukae. Mheshimiwa Malembeka mchangiaje wetu wa mwisho. (Makofi/Kicheko)

Waheshimiwa Wabunge, naomba mzime *microphone*. Hapo nyuma mwenye nguo ya *blue* naomba uzime *microphone* hiyo tafadhali.

**MHE. HALIMA J. MDEF:** Na umwambie asitukane.

**NAIBU SPIKA:** Naomba uzime *microphone* tafadhali. Mheshimiwa Malembeka endelea.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba wenzangu wa upande wa pili wawe watulivu na hizo *microphone* wasiwe wanawasha kwa sababu sisi huwa hatuwashi. (Makofi)

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio*)

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na timu yake yote. Pia nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya. Kiaina nimpongeze aliyetengeneza kitabu hiki kwa kumwonesha komandoo akiwa kwenye mavazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu kwenye Wizara hii kwanza naunga mkono kwa asilimia mia moja. Nichangie kwenye nyumba za askari. Nimeona juhudini za Wizara katika kujenga nyumba za askari. Naomba Serikali yangu tulivu iendelee kuwajengea nyumba askari hawa ili waweze kuishi vizuri na kufanya kazi zao kwa umakini zaidi. Nimeona maeneo mbalimbali ambapo nyumba zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe Serikali yangu tulivu iendelee kuboresha maslahi ya askari wetu ikiwepo mishahara na vyombo ya usafiri. Niombe pia Wizara hii kwa nguvu za dhati ihakikishe mafunzo kwa askari wapya yanafanyika yakiwa yamelenga kada tofauti. Nimesikitishwa hapa na mwasilishaji wa Kambi ya Upinzani akishangaa Askari mstaafu kuwa mganga wa kienyeji. Mimi naamini kabisa kule kwenye uaskari siyo kwamba wana fani moja tu ya kushika bunduki na kucheza gwaride. Najua kabisa kule tunao Askari ambaa ni wajasiriamali, wana ujuzi wa teknolojia mpya, wanahabari, wanamichezo, madaktari, madereva, marubani, walimu, mafundi umeme na waokoaji. Kwa hiyo, huyo Askari aliyeenda kuwa mganga wa kienyeji ndiyo fani yake usimlaumu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia zaidi katika ajira. Naomba jeshi hili hasa Jeshi la Wananchi liangalie uwiano wa mikoa yote. Kuna baadhi ya maeneo imeonekana kama vile kuna kabilia moja tu ndiyo jeshi hilo kazi yake mpaka inafika kipindi mitaani huko ukiwauliza JWTZ ni nini, wanakwambia ni Jeshi la Wakurya Toka Zamani.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba ajira zile ziangalie mikoa mbalimbali angalau ukikuta Wachaga kumi basi na Wamasai, Waluguru na Wapare wapo isiwe kabilia moja ndio linafanya kazi ya jeshi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia Wizara hii iangalie ubunifu wa vijana wetu. Tunao vijana wengi ambaao katika utundu wao wameweza kubuni redio, TV, simu mpaka helikopta. Ni vizuri jeshi hili likawachukua vijana wale na kuwapa mafunzo halafu baadaye wapate ajira. Nategemea kwa kufanya hivyo tutaendelea kuwa na vijana ambaao watakuwa askari bora zaidi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie pia katika kambi za jeshi. Najua wakati zinaanza zilikuwa nje ya mji lakini baadaye mji jinsi ulivyokua imeonekana kama vile vimeingiliana. Katika kuepuka madhara zaidi ya mabomu kama yale ya Gongo la Mboto na Mbagala au kuepuka migogoro ya ardhi kati Wanajeshi na raia lakini pia kuepuka migororo ambayo mingine inaingilia mipaka ya kimapenzi kati ya Askari na raia, ni vizuri basi tuangalie uwezekano wa kubadilisha makazi hayo. Mapori bado tunayo mengi, wahame kidogo waende kule ili wananchi waweze kukaa katika maeneo hayo kwa utulivu. Yapo maeneo ambayo hayawezekani kuhamishwa kutokana na hali halisi ilivyo basi wale ambaao wanazunguka eneo lile wahamishwe kwa utaratibu unaofaa ili waweze kupisha jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hii itasaidia katika kujenga heshima ya jeshi. Imefika sehemu heshima ya jeshi inaanza kupungua kwa sababu wanajichanganya sana na raia. Katika kujichanganya na raia unakuta kuna mambo mengine ambayo Wanajeshi wanafanya unashangaa. Hata katika foleni za magari unakuta kwenye mchepuko na yeye anaingia, unatazama unaona ni Askari na ana kofia. Napenda zaidi Askari waoneshe wao wako makini na ni watii wa sheria, siyo wote wanaofanya hivyo ni baadhi. Wapo ambaao pia wanakuwa wasumbufu katika maeneo ya watu yaani hata jirani yake anaogopa kukaa jirani na mjeshi. Naomba wale wachache wenyewe tabia kama hizo wabadi like. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kuhusu baadhi ya shule ambazo zinasimamiwa na jeshi zikiwepo shule binafsi nikitolea mfano Mgulani na Lugalo.

Kuna shule ambazo zimeendeshwa vizuri wanafunzi wa pale wanakuwa na maadili mazuri. Ni vizuri shule kama zile ziendelezwe na kupewa ushirikiano ili tuendelee kupata wanafunzi wenyewe nidhamu na wenyewe uchungu na nchi yao ambao hata kesho wakija huku Bungeni wataongea kwa kuitetea nchi yao siyo kuzomeazomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani tulikuwa na vyuo vya ualimu ambavyo vilikuwa vinasimamiwa na jeshi nikitolea mfano ya Monduli, Morogoro TC na Tabora Boys. Vyuo vile vilikuwa vinatoa walimu wenyewe nidhamu nzuri na wenyewe uchungu na nchi yao. Kama kuna uwezekano utaratibu ule urudishwe ili tuendelee kupata Wanajeshi ambao wanakuwa na fani tofauti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kunya maza kimya bila kusemea suala la uchaguzi wa Zanzibar. Tunakubali wote kwamba Amiri Jeshi Mkuu alisema, tena matangazo yalitoka kwenye televisheni, redio na magazeti kwamba yeze kama Amiri Jeshi Mkuu ana wajibu wa kulinda usalama Tanzania hii katika mkoa wowote siyo Dar es Salaam, Pemba au Mwanza na alimalizia kwa kusema atakayefanya fyokofyoko nitamshughulikia. Ukiona mtu analalamika kama alifanya fyokofyoko anashughulikiwa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuonesha, kama angesema halafu wakanyamaza wangedharau wakasema amesema mbona hajafanya lolote, amesema na hawajathubutu kufanya fyokofyoko ndiyo maana wamenyamaza na kama watafanya fyokofyoko, Amiri Jeshi Mkuu aendelee kufanya kazi yake, ndiyo tutaendelea kuheshimiana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee zaidi katika suala zima la mafunzo ya kijeshi kwa vyama vya kisiasa. Kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya vyama vya kisiasa kutengeneza makundi ya kijeshi kwa kujifanya kwamba wanalinda wakati wa kampeni au kulinda kura zao. Naomba jeshi lifanye kazi ya ziada, Mheshimiwa Waziri alisimamie, yapo makundi yanayoijiita mazombe, wenye wanyajua huko ndiyo maana kila saa wanayataja, kuna makundi yanajiita blue guard yapo huko, yanafanya vituko kusingizia vyama vya siasa. Naomba Mheshimiwa Waziri yale...

### **WABUNGE FULANI: Green guard!**

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Green guard umetaja wewe sijataja mimi. Kwa hiyo, ninachoomba yale makundi yote yanayoendesha mafunzo ya kijeshi kwa kusingizia vyama wayadhibiti kwa sababu hayo ndiyo yanayotuletea fujo katika nchi yetu na kusababisha makundi ya wahalifu katika mitaa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na wale waliobana sasa wameachia. Ahsante. (Makofi/Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka wakati ukichangia, kuna tuhuma hapa umezitoa kuhusu ukabila jeshini. Kwa mujibu wa Kanuni ya 72(1) na Kanuni ya 64(1)(a), naomba ufute hayo maneno halafu tuendelee. (Makofii)

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitolea mfano na nafuta kauli hizo. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa January Makamba dakika tano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuzungumza na napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa na kwa mipango mizuri ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taasisi ambapo uongozi unafundishwa vizuri kwa nadharia na vitendo ni pamoja na jeshini na hii ni kote duniani, iwe West Point, Sandhurst au Monduli. Tangu nchi yetu ipate uhuru, viongozi wa Taifa hili tangu Baba wa Taifa mpaka Rais Magufuli wameenda jeshini kuchota katika kisima cha hazina ya uongozi iliyopo jeshini ili kusaidia kuongoza nchi yetu. Askari wetu wote walioombwa au walioteuliwa kutumikia nafasi za uongozi katika nchi na katika siasa kutoka jeshini wamefanya kazi nzuri na kubwa na mifano iko mingi, Jenerali Kimario, Jenerali Sarakikya, Jenerali Luhanga na wengineo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa 12 kuna hoja imetolewa pale, kwamba ili kulinda na kusimamia maadili ya kazi ya jeshi, Wanajeshi wasihusishwe kabisa na kazi za siasa iwe wapo kazini au wamestaafu. Wanaendelea kusema kwamba kwa kuwateua kushika nafasi za siasa wanapostaafu, kunaweza kuwafanya wale wengine waliopo kazini kutozingatia maadili yao ya kazi na kuanza kujipendekeza kwa watawala. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi kumi za uafisa jeshini, ngazi saba Rais ndiye anayepandisha vyeo. Kwa hiyo, kama kuna hoja ya kujipendekeza kwa Askari wetu, isingekuwa kwenye ngazi za siasa hata kule kule waliko jeshini kama tunaamini kwamba kwa weledi wao na mafunzo yao wametengenezwa na wamefundishwa katika hulka za kujipendekeza ingekuwa tunaiona kuanzia sasa kwa sababu bado Rais anapandisha vyeo jeshini. Kwa hiyo, nadhani kwamba ni kuwadhalilisha Askari na Maafisa wetu kwa kusema kwamba wanajipendekeza kwa watawala ili wapate nafasi.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu limewekwa chini ya mamlaka ya kiraia na sisi viongozi wa kiraia tunapigiwa saluti wakati mwengine na Askari. Leo wakati tunapitisha bajeti hii, wamekuwepo Askari na Maafisa wengi na wameshudia jinsi tunavyoendesha mambo yetu, nadhani baada ya kupitishwa bajeti hii na naamini itapita, tutakapokuwa tunarudi nyumbani kwetu tutafakari kama waliyoyaona tunayafanya Askari wetu leo hapa kama kweli watatupigia saluti huku ndani ya miyo yao wakiwa hawaamini kama tunazistahili kama watakuwa wanakosea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu wa Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru Askari wetu wote, Maafisa na wale wanaowaongoza kwa kuendelea kuifanyia kazi nzuri nchi yetu. Napenda kuwashukuru binafsi kwa kutuongoza na kufanya kazi vizuri. Napenda makusudi kabisa niwataje kwa sababu huwa hawatajwi hasa viongozi wale, Mkuu wa Majeshi yetu Jenerali Mwamunyange, ahsante sana. Mnadhimu Mkuu Lieutenant General Mabeyo, ahsante sana. Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali Mwakibolwa ahsante sana. Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, Rogastian Laswai, ahsante sana. Mkuu wa JKT, Brigedia Jenerali Isamuhyo, ahsante sana. Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, Brigedia Jenerali Ingram, ahsante sana. Mnastahili shukrani zetu sana kwa kazi nzuri mnayoifanya, kwa sacrifice mnayoichukua kulinda mipaka ya nchi yetu, kulinda amani ya nchi yetu na wakati mwengine maneno ambayo yanasemwaa humu ndani ya kuwadhalilisha hamuyastahili na Watanzania wote wako nyuma yenu, ahsanteni sana. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nauye, Mheshimiwa January muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na nichangie kwa kifupi sana. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Ulinzi, Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kazi nzuri anayofanya. Kazi hii anaifanya kwa unyenyekevu na uadilifu mkubwa tunakupongeza sana Dokta. Pia nilipongeze jeshi letu kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya. Nchi yetu inaendelea kusifiwa kuwa na amani na utulivu kwa sababu ya kazi yao nzuri wanayoifanya, ahsanteni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuweka rekodi sawa, kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa 11, wameneku Katiba ya CCM, Ibara ya 80(1)(c) na 94(1)(c). Bahati mbaya sana na nadhani ni kwa makusudi, wameneku nusu ya Ibara hizo na wakaamua kwa makusudi kupotosha ukweli. Sasa nimesimama kuweka ukweli sawa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wameneku Ibara ya 80(1)(c) lakini (d) inasema hivi, Mkuu wa Wilaya ambaye anatokana na CCM. Ukienda Ibara ya 94(1)(c) inasema, Mkuu wa Mkoa ambaye anatokana na CCM. Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya nafasi hizi zinateliwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Katiba na sheria zote zinazosimamia uteuzi huu sifa ya kuwa mwanachama wa chama cha siasa haipo. Kwa hiyo, mtu ye yote anaweza kuteeliwa kwenye nafasi hizi bila kujali chama chake cha siasa

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Sikilizeni, kwa utaratibu huo ndiyo maana katiba ya CCM imeeleza Wajumbe wa Kamati za Siasa ambao wao wanalamikia kwamba hawa ni wajumbe imeeleza wajumbe hao ambao ni Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mkoa ambao wanatokana na CCM, siyo kila Mkuu wa Wilaya ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya CCM na siyo kila Mkuu wa Mkoa ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa na ushahidi upo. Tunao Wanajeshi ambao wameteeliwa kuwa Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya na kadri tunavyoongea sasa hakuna hata mmoja ambaye amehudhuria kikao cha Kamati ya Siasa ya Wilaya wala ya Mkoa na ushahidi upo. (Makofii)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri ni vizuri tusitumie Bunge hili kujaribu kupotosha ukweli na kujaribu kulipaka matope jeshi letu...

**WABUNGE FULANI:** Aaah.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Jeshi letu linafanya kazi nzuri, tuache unafiki, tunasimama tunawapongeza tunasema wanafanya kazi nzuri wakati huo huo tunatumia mlango wa nyuma ...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa naomba ukae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Tunalipaka matope na kuweka uongo.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae tafadhali

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Naomba utaratibu Mheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Anapotosha.

**NAIBU SPIKA:** Utaratibu, Kanuni.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kanuni ya 64.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ya 64(1)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(a) inasema:-

"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(a) "Hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli". (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Nape anasahau kwamba sasa hivi yeye ni Mbunge na ni Waziri anafanya kazi ya uenezi wa Chama cha Mapinduzi ndani ya Bunge. Jambo analozungumza Katiba iko wazi Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wote wako kwenye Kamati za Chama cha Mapinduzi na wao ndiyo wanaoongoza shughuli zote...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa umesema utaratibu elezea ni Kanuni imevunjwa kwa vipi?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Anasema uongo, utaratibu ni kwamba amesema uongo na anatupotosha hapa kwa sababu hao Wakuu wa Wilaya...

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Kwa hiyo, utaratibu wako ni kwamba kasema uongo...

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Eeh anasema uongo ...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae umeshaelewaka.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Sijamaliza Mheshimiwa.

**NAIBU SPIKA:** Umesema amesema uongo Mheshimiwa Msigwa.

**MBUNGE FULANI:** Hajamaliza.

**NAIBU SPIKA:** Haya malizia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Naomba uniheshimu kama unavyomheshimu Jenista, mimi nimesimama upande wa Kambi ya Upinzani kama Chief Whip.

**NAIBU SPIKA:** Naomba umalize.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Basi naomba unipe muda kama unavyompa Chief Whip wa upande wa Serikali.

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ya 64 (1)(c).

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kanuni ya 64(1)(c) inasema hivi, hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi, ooh sorry.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Tulia.

**MBUNGE FULANI:** Kaa chini hujui.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa nikusaidie, umetusomea Kanuni ya 64 (1)(a) kwamba anachoongea ni uongo una Kanuni nytingine?

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasema anachokizingumza anazungumza uongo kwa sababu Wakuu wa Wilaya wanaingia kwenye vikao vyote vya Chama cha Mapinduzi, Wakuu wa Mikoa wanaingia wote kwenye vikao vya Chama cha Mapinduzi na hao viongozi wote ni makada wa Chama cha Mapinduzi na yeye mwenyewe kakiri hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba asiendeleze uenezi wa Chama cha Mapinduzi ndani ya Bunge, tuongee mambo ya msingi kwa mustakabali wa Taifa letu tuwaache Wanajeshi huru wafanye kazi yao ya jeshi mambo ya siasa watuachie humu ndani, ndiyo hoja ninayozungumza. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni aliyotumia Mheshimiwa Msigwa Kanuni ya 64(1)(a) ameshaisoma, mimi nitakwenda *straight* kwenye hiyo (a) inasema:-

*"hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli".*

Mheshimiwa Nape ametusomea kwenye hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani, ukurasa wa 11 ambao unaongelea Ibara ya

80(1)(c) ya Katiba ya CCM na Ibara ya 94(1)(c) ya Katiba ya CCM. Kwa hiyo, anatoa ufanuzi wa haya yaliyoko hapa. (Makofii)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo, kwa sababu tukitaka kusema tunataka kubishana nani anayesema ukweli maana yake tunataka atuletee *minutes* za vikao vya CCM huko. Naomba tuelewane vizuri kwa mujibu wa hiki kilichoko hapa na Kanuni alizotusomea zinaweka wazi, maana yake ni kwamba wapo ambao ni wa CCM na wapo ambao siyo wa CCM.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**NAIBU SPIKA:** Naomba Waheshimiwa tuendelee, Mheshimiwa Nape malizia.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano wa wazi kabisa kwa sababu bahati mbaya sana Bunge hili linataka kutumika kucheza siasa za hovyo. Alikuwepo Brigedia Jenerali Balele, aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga akiwa amestaafu. Alipofika Shinyanga akaenda Ofisi ya CCM, alipofika Katibu wa Mkoa alikuwa anaitwa Agusta Muba akamuuliza Jenerali wewe una kadi ya CCM? Huwezi kuingia kwenye vikao vya CCM kama wewe siyo mwanachama wa CCM. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana, mimi hapa sizungumzi kama Katibu Mwenezi, uenezi nilishaacha huko, wenzetu wamekuwa na utamaduni wa kutoheshimu Katiba za vyama vyao. Katiba ya CCM inasema Ukuu wako wa Wilaya, Ukuu wako wa Mkoa haukuingizi kwenye vikao hivi. Katiba ndivyo inavyosema na tunaisimamia. Isipokuwa uanachama wako plus Ukuu wa Wilaya na Ukuu wa Mkoa wako, kama siyo mwanachama huingii na hapa ninapozungumza tunao Wakuu wa Mikoa ambao ni Wanajeshi hawajastaafu na hawaingii kwenye vikao vya CCM. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tukaweka rekodi sawa; ukizoea vya kunyonga vya kuchinja vinakua tabu. Acheni uwongo na kutaka kuwadanganya Watanzania kwa mlango wa nyuma. Lihestimuni jeshi kwa maneno na matendo yenu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimesimama hapa kwanza kabisa kuwapa moyo Wanajeshi wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuwapa moyo, naomba nichukue nafasi hii kuwathibitishia Wanajeshi wetu wote wa jeshi letu, Serikali iliyopo madarakani ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kuwajali na kuwaheshimu siku zote.

**MBUNGE FULANI:** Muwalipe hela zao.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kusema, tunaendelea kuthamini kazi na michango yao mizuri katika kulinda amani ya nchi yetu ya Tanzania bila kujali chama chochote cha siasa katika nchi yetu ya Tanzania.

**MBUNGE FULANI:** Muwape hela zao.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Sisi kama Serikali tutaendelea kufanya nao kazi, wasisikilize propaganda ya mtu ye yeyote. Sisi kama Serikali tunaendelea kufanya nao kazi na tunatambua mchango wao muhimu katika Serikali yetu. (Makofii)

**MBUNGE FULANI:** Muwalipe hela zao sasa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati leo tukizungumza kwenye Bunge hili na tunajua kwamba 61% ya nguvu kazi ya nchi yetu ya Tanzania ni vijana kati ya umri wa miaka 15 na 35 na Jeshi hili la Wananchi wa Tanzania kupitia JKT wamekubali kushirikiana na Serikali na kuamua kuwachukua vijana wa Tanzania kutoka Jimbo la Iringa na majimbo mengine yote katika nchi hii ya Tanzania na wamekwenda kufanya mafunzo ya JKT. Pamoja na mafunzo hayo ya JKT, Serikali imeona umuhimu wa wale vijana wanaokwenda pale kwa kujitolea na imeona wanatakiwa wafanyiwe maandalizi ya kutosha ili tutatue tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumzwa maneno hapa, Serikali haina mpango na hao vijana. Leo nataka kuliambia Bunge hili tayari Serikali imeingia mkataba na Jeshi la Kujenga Taifa, tayari Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Tanzania limeanza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wote wanaochukuliwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwenye JKT kwa kujitolea ili

wanapomaliza mafunzo yale waweze kuunganishwa na vyombo mbalimbali vya mikopo na kujajiri kutokana na skills wanazozipata wakiwa jeshini. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo jeshi hili ambalo linaenda kutatua matatizo ya ajira kwa wapiga kura wetu, ilitupasa humu ndani leo tulipongeze na kulipa heshima kubwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na si vinginevyo. Ndiyo maana imenipasa hapa kusema nawashukuru na kuwapongeza Makamanda wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na kulinda amani ya nchi ya Tanzania bado wamejitolea kuhakikisha malengo ya Jeshi la Kujenga Taifa kama hawafahamu hapa Wabunge ambao wanadharau uwepo wa Jeshi hili, ni haya yafuatayo:-

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza...

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Nani anadharau jeshi, nani anadharau jeshi, nani anadharau jeshi?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tusikilizane.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Nani anadharau jeshi, nani anadharau jeshi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu naomba uzime microphone.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Nani anadharau jeshi, nani anadharau jeshi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu naomba uzime microphone.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu naomba ulindwe.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Nani anadharau jeshi, nani anadharau jeshi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu naomba uzime microphone tafadhali!

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi hili lina kazi ya

kutoa malezi bora kwa vijana, jeshi hili lina kazi ya kutoa mafunzo ya ujasiriamali na jeshi hili lina kazi ya kufundishwa kuwa jeshi la akiba. (Makofii)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Serikali hii...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara naomba ukae. Mheshimiwa Jenista malizia.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara naomba ukae tafadhali! Naomba ukae Mheshimiwa Waitara!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Waitara. Mheshimiwa Jenista malizia.

**MBUNGE FULANI:** Kamaliza huyo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongo huyo.

**MBUNGE FULANI:** Naibu Spika unapendelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri kwamba...

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antony Komu nimekusih sana naomba uzime microphone yako.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Naomba uzime microphone yako tafadhali!

**WABUNGE FULANI:** Unapendelea.

**NAIBU SPIKA:** Naomba uzime microphone yako. Mheshimiwa Jenista malizia!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno haya na umuhimu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania tutasimama imara kulilinda na kulitetea daima. Tutasimama imara kulihestimu na kuwapa heshima Wanajeshi wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. (Makofii)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tunasema tunawaomba waendelee kulinda amani ya nchi ya Tanzania kila siku. Waendelee kukuza maadili ya vijana wetu wa Tanzania kwa namna zote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumaliza mchango wangu kwa kumpongeza sana Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Sisi kama Wabunge tunamtia moyo aendelee kuliongoza jeshi letu sawasawa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana ya kusimamia Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Nakushukuru Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, endelea kutusaidia kulipa moyo Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofii)

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara naomba ukae. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mwongozo wa Spika, mwongozo wa Spika, mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Nchambi, naomba mkae. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Watoe nje hao.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa mwongozo kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Nchambi.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Atoke nje.

**MBUNGE FULANI:** Mtoe nje kama kawaida yako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome tafadhali. Tafadhali Mheshimiwa Salome.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata fursa ya kuchangia kwenye hoja hii muhimu na nakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba yake nzuri na mipango mizuri kwa ajili ya Jeshi hili la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania. Pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao ya kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kutoa ufanuzi wa masuala mawili, matatu hivi ya kikatiba na kisheria ambayo yamejitokeza hapa. Moja, linahusu utumishi wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetajwa na Ibara ya 1 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwamba ni nchi moja nayo ni Jamhuri ya Muungano. Ibara ya 2 ya Katiba inasema:-

“Eneo la Jamhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar, na ni pamoja na sehemu yake ya bahari ambayo Tanzania inapakana nayo”.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya nne (4) inayoorodhesha mambo ya muungano, ulinzi na usalama ni moja ya mambo ya msingi ya muungano. Kwa sababu hili ni Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania, utumishi wao hauna mipaka isipokuwa katika eneo lote la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Ndiyo maana jeshi hili lina kambi Zanzibar na pia inapobidi kama ni kuimarisha usalama na ulinzi halitasita kuwepo Zanzibar kwa ajili ya kusimamia ulinzi na usalama wa Zanzibar, hilo la kwanza. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hili ambalo pia linahitaji ufanuzi. Nimepata fursa hapa ya kuisoma Katiba ya Chama cha Mapinduzi, nimeangalia Ibara ya 80, 94 na 95 ya Toleo la Katiba ya mwaka 2007. Mheshimiwa Waziri Nape amezungumza, Wajumbe wa Kamati za Siasa za Halmashauri Kuu ya CCM ngazi ya wilaya na mikoa, kama ni Wakuu wa Wilaya au Wakuu wa Mikoa ni wale wanaotokana na Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, wengine kama Wanajeshi hawa ambao Katiba kwa kweli imekataza kuwa wanachama wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuwa wajumbe wa hizo Kamati. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho naweza kusema zaidi ni kwamba, Wakuu wa Mikoa kwa mfano, ukisoma Ibara ya 61(1) ya Katiba inasema:-

*“Kutakuwa na Mkuu wa Mkoa wa kila mkoa katika Jamhuri ya Muungano ambaye, bila ya kuathiri ibara ndogo ya (3), atakuwa ni kiongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni viongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siyo viongozi katika vyama vya siasa. Ukiangalia kazi zao purely ni za kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ndogo ya (4) inasema:-

*“Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (5), kila Mkuu wa Mkoa, atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa kazi na shughuli zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika mkoa aliokabidhiwa; na kwa ajili hiyo, atatekeleza kazi na shughuli zote zilizotajwa na sheria, au kwa mujibu wa sheria kama ni kazi au shughuli za Mkuu wa Mkoa na atakuwa na madaraka yote yatakayotajwa na sheria yoyote iliyoitungwa na Bunge”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa huoni ikitajwa kabisa katiba za vyama vya siasa. Kwa hiyo, yeye anafanya kazi za kiserikali na kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetungwa sheria mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa madaraka ya Wakuu wa Mikoa. Kwa mfano, Sheria ya Tawala za

Mikoa, kifungu cha tano (5) kinataja majukumu ya Wakuu wa Mikoa, naomba kunukuu:-

“(1) Mkoo wa Mkoa atakuwa mwakilishi mkuu wa Serikali katika eneo la mkoa ambalo ameteuliwa na kwa madhumuni hayo majukumu yote ya kiserikali yanayohusu mkoa huo yatakelezeza na/au kupitia Mkoo wa Mkoa.

(2) Katika kuendeleza madhumuni na masharti ya kifungu kidogo cha (1) Mkoo wa Mkoa atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria na uwepo wa amani katika mkoa huo, kutoa mwelekeo mahsuswa sera za jumla za Serikali katika mkoa na kutekeleza kazi na majukumu mengine kama yanavyotekeliza au kutolewa kwake na/au chini ya sheria hii au sheria nyingine yoyote”.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba hawa hawahusiki kabisa na shughuli za vyama vya siasa. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waamini kama Serikali ilivyokwisha kufafanua hapa kwamba, hawa ambaa Katiba imewapiga marufuku kuwa wanachama wa vyama vya siasa kama Wanajeshi, hata wanapoteuliwa kuwa Wakuu wa Wilaya au Mikoa, hawawezi kuwa Wajumbe wa Kamati za Siasa za Kamati za Halmashauri Kuu za CCM.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Tunao ushahidi wa kina Msangi ni wa CCM.

**MBUNGE FULANI:** Msangi mstaafu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi hakuna sheria yoyote katika hizi ambazo zimeshatungwa zinazotoa majukumu kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kujihusisha na vyama vya siasa. Kimsingi wanapoteuliwa, mara ya mwisho nilishuhudia pale Ikulu Mheshimiwa Rais alipowateua hawa Wakuu wa Mikoa wa mwisho wakiwemo na Wanajeshi, aliwakabidhi katiba na sheria. Hata Wakuu wa Wilaya wanapoapishwa kule na Wakuu wa Mikoa wanakabidhiwa katiba ya nchi na sheria, hawakabidhiwi hizi katiba za vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri tu kwamba, hili ambalo linaleta wasiwasi humu ndani Waheshimiwa Wabunge hawana sababu ya kuwanalo. Jeshi letu lina watu wanareshimika sana, wana nidhamu kubwa sana, wana utii mkubwa sana, hawawezi wakakiuka masharti ya Amiri Jeshi Mkoo. Mkiangalia sehemu yao kubwa wanapelekwa katika maeneo ambayo yana matatizo ya ulinzi na usalama. Hawa Maafisa wa Jeshi walio teuliwa wamekwenda kwenye maeneo yale ambayo yana matatizo makubwa ya

usalama. Ukiisoma ile Sheria ya Tawala za Mikoa unaona kabisa mojawapo ya majukumu yao ni kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo yao ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (Makofii)

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nchambi naomba ukae tafadhali. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja yangu jioni ya leo. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja hii, wale waliochangia kwa kuzungumza ambao idadi yao ilikuwa ni 24 na wale waliochangia kwa maandishi ambao idadi yao ilikuwa ni 31. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Mdee alinitahadharisha kwamba nisije nikasema muda wa kueleza umekwisha. Ukweli ni kwamba kwa idadi hii si rahisi kumgusa kila mmoja wenu. Nataka niwahakikishie kama kawaida yetu, baada ya kukamilisha kazi hii tutaleta majibu yote kwa maandishi kwa kila mchangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Leo asubuhi wakati tumeanza shughuli za bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nilipata moyo sana kuona kwamba Wabunge wote wa pande zote mbili wakiwa wanaliunga mkono jeshi letu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kabisa kwamba, baada ya uchaguzi siasa huwa zinahamia Bungeni. Pia ni sahihi kabisa kila mmoja kupiga siasa humu ndani ya Bunge lakini naendelea kuwasihii Waheshimiwa Wabunge tujitahidi sana kutoliingiza jeshi katika siasa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwa bahati mbaya sana, nadhani ni kwa sababu ya kuzidiwa tu na hisia zetu za kisiasa zimetoka kauli humu ambazo kwa kweli zisingepaswa kutoka lakini bado tunayo nafasi ya kujirekebisha. Naamini Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani na wa Chama Tawala sote tunatambua mchango mkubwa wa jeshi katika nchi yetu na sote tunaliunga mkono na ndiyo maana asubuhi mlimshangilia sana Mkuu wa Majeshi kwa kutambua mchango wa jeshi katika nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba niingie katika hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nitaanza na hoja

za Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kwanza walisema kwamba Serikali itoe fedha za maendeleo zitakazotengwa katika mwaka huu wa fedha kwa ukamilifu na kwa wakati na pia Serikali ilipe madeni yote yaliyohakikiwa na Hazina. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ambao ni Wabunge tunafahamu kwamba tunapanga bajeti lakini mwisho wa siku inategemea sana na makusanyo ya Serikali. Ni mategemeo ya kila mmoja wetu kwamba Serikali ikikusanya vyema kama ambavyo mwelekeo unaonesha, bila shaka fedha hizi zitapatikana na tutaweza kutekeleza yale ambayo tumeyapanga katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imetakiwa tushiriki kubuni mbinu za kuzalisha mazao ya kiraia ili kuongeza mapato. Napenda kutoa taarifa kwamba mashirika yetu yote, Suma JKT, Mzinga na Nyumbu, yanafanya juhudhi mbalimbali ya kuzalisha mali ili waweze kupata kipato cha ziada. Kwa mfano, shirika la Mzinga wanazalisha risasi za kiraia pamoja na milipuko kwa ajili ya migodi. Nyumbu wanazalisha power *tillers* na mashine za matofali. Suma JKT wanasindika mazao ya nafaka na uunganishaji wa matrekta. Aidha, mashirika haya yanaendeleza ubunifu mbalimbali ili kuweza kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi ya wanajeshi zilengwe kwa askari wa vyeo vya chini. Hapa tunasema katika mradi huu unaoendelea sasa ambapo nyumba 6,064 idadi yote imeelekezwa kwa askari wa vyeo vya chini. Hivyo ushauri huu unaenda sambamba na mpango wetu. Ni awamu ya pili ambayo tunalenga kuwapatia nyumba maafisa na wale askari wa vyeo vya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi kumiliki maeneo ya ardhi kisheria. Suala hili tunalitambua ilikuwa ni kasoro kubwa. Siku za nyuma taasisi za Serikali zilikuwa zinapewa *government allocation* peke yake lakini kila siku zikienda na uhaba wa ardhi imekuwa kuna uvamizi katika maeneo haya na ndiyo maana sasa tumeona umuhimu wa kupima maeneo yote ya jeshi na kuyapatia hati ili waweze kumiliki kisheria. Wakati tunafanya hayo, tutaendelea kuhakikisha kwamba maeneo ya jeshi yanatunzwa hivyo kuweza kupunguza uvamizi unaotokea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji na ulipaji fidia kwa maeneo ya jeshi ufanyike. Kama ilivyoelezwa kwenye hotuba yangu, ibara ya 60 na 61 katika ukurasa wa 43 na 44 na kufafanuliwa katika hoja Namba tatu ya ukurasa wa 57, Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka husika ili kukamilisha upimaji na ulipaji fidia kwa maeneo ya jeshi. Natambua Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia katika maeneo haya ya kutaka uthamini, upimaji na ulipaji wa fidia. Katika bajeti ya mwaka huu kama mtakavyoona katika fedha za

maendeleo, tumeweka shilingi bilioni 27.7 lengo ni kuanza kupunguza yale maeneo ambayo yanahitaji kulipiwa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi kutambua na kulinda mipaka yake. Jambo hili sasa linafanyika kwa nguvu zote, tunaweka mabango na tunapanda miti katika maeneo yetu ya mipaka ili wananchi waelewe fika wapi maeneo ya jeshi yanaanza na wapi yanaishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kurasimisha makabidhiano ya maeneo yanayotolewa na mamlaka za kiraia kwa jeshi na kuweka uzio maeneo yote ya jeshi. Ushauri umezingatiwa, tutashirikiana na mamlaka za mikoa kuhakikisha kumbukumbu za makabidhiano ya ardhi waliyoitoa kwa jeshi zinawekwa vizuri. Uwezekano wa kuweka uzio maeneo yote ya jeshi ni mdogo kwani maeneo hayo ni makubwa sana mfano eneo la Monduli, Tondoroni na Msata. Tunachoweza kufanya ni kuweka ukanda wa tahadhari yaani *buffer zone* na mabango ya tahadhari ya maeneo yote ya jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uboreshaji wa pensheni za wanajeshi wastaifu hasa kwa ngazi ya kuanzia *Private* hadi *Brigedia Jenerali* kwamba limefikia wapi. Serikali imetambua umuhimu wa kuboresha pensheni kwa wastaifu ikiwemo wanajeshi. Hivyo suala hili linaendelea kufanyiwa kazi kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kutenga bajeti ya kutosha kuwezesha JKT kuchukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita kwa ajili ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria. Ushauri huu umepokelewa na ndiyo azma yetu. Hata hivyo, kama tulivyojibu, Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina ili kutoa fedha za kutosha kuliwezesha JKT kuchukua vijana wote wanaomaliza kidato cha sita kujiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kwa wakati mmoja kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia kwa vijana wa JKT wanaoumia wakiwa mafunzoni. Wizara imepokea ushauri wa Kamati na itaufanyia kazi sanjari na kuboresha Sheria ya Ulinzi wa Taifa na sheria iliyoanzisha JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maeneo hayo ambayo yalitolewa na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba sasa niingie kwenye hoja ya Kambi ya Upinzani. Kwanza kulikuwa na hoja ya upendeleo katika ajira za jeshi. Labda nielezee kidogo utaratibu unaotumika katika ajira ili tuondokane na wasiwasi kwamba kuna upendeleo. Kwanza niseme tu kwamba ajira jeshini kwa sasa wanachukuliwa vijana ambao wako katika makambi ya JKT peke yake, jeshi halichukui tena uraiani. Kwa maana hiyo ni kwamba wale vijana wanaokwenda JKT wakati wa ajira wanafanyiwa usaili vijana hao, kwa hivyo sioni upendeleo unatokea wapi. Sasa hawa wa JKT wanapatikanaje? Kila

mwaka tunatoa nafasi kupitia mikoa hadi wilaya, ili wilaya zenyewe zichuje vijana katika maeneo yao na kuwapeleka JKT. Kwa hiyo, hii hoja ya kwamba kuna upendeleo, kwa kweli sioni upendeleo huo utatoka wapi wakati hatuchukui uraiani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyiningine ilikuwa Wizara inalishughulikiaje suala la migogoro ndani ya vyama vya wanajeshi wastaafu. Jibu ni kwamba Wizara kupitia Makao Makuu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, imevishawishi vyama vyote vya wanajeshi wastaafu kuunda chama kimoja tu cha Kitaifa ambacho kitaendeshwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za kijeshi. Hivi sasa kuna vyama kama alivyovitaja lakini viko chini ya kanuni za mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO's). Kwa hivyo, inatupa shida kama Serikali kufanya nao kazi na kuwasaidia kama inavyotakiwa lakini wakiwa chama kimoja ambao watafuata taratibu za kijeshi, bila shaka itakuwa rahisi kwetu kuwapa msaada utakaostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uteuzi wa wanajeshi kwenye nafasi za kisiasa kama ilivyokwishesemwa na walionitangulia AG na wengine, ndugu zangu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumchagua mtu ye yeyote kwa nafasi yoyote. Kwa hivyo, haijavunjwa Katiba hapa na kwa utaratibu wa sasa wanajeshi wote hawaruhusiwi kujihusisha na vyama vya siasa. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu anayo mamlaka ya kumpangia kazi mwanajeshi ye yeyote kadiri anavyoona inafaa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili napenda nikuambieni kwamba yapo maeneo ya nchi yetu ambayo yako katika mipaka yana changamoto nydingi za kiulinzi na usalama ndiyo maana ikaonekana ni busara kupeleka Wanajeshi. Kuna Wilaya kule kuna wakimbizi ambapo hali ya ulinzi na usalama imeharibika kwa sababu ya silaha zinazoingizwa, kwa sababu ya watu wanaoingia kwa mawimbi makubwa ya wakimbizi na kadhalika. Wakipelekwa wanajeshi kule experience imeonesha kwamba kazi ya ulinzi na usalama inafanyika vyema zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali iwaagize Wakuu wa Vikosi vyote vya JKT kutengeneza programu ya uzalishaji mali katika kilimo, uvuvi na mifugo. Kama ilivyoelezwa katika ibara ya 53 ya hotuba yangu, ushauri huu umepokelewa na taarifa za uzalishaji mali na mapato itaendelea kutolewa katika Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Ukweli ni kwamba programu za uzalishaji mali katika vikosi vyote vya JKT zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe fedha zote zitakazotengwa katika bajeti ya Wizara ya Ulinzi. Hili ni kama nilivyosema awali, itategemea sana na mapato ya Serikali lakini ni mategemeo yetu kwamba kwa sasa kwa sababu

ukusanyaji ni mzuri, hatuna shaka kwamba fedha zilizotengwa zitaweza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niingie katika kile kisehemu ambacho kilikuwa kinazua mgogoro, nacho ni jeshi kuingilia kazi za polisi Zanzibar. Ndugu zangu nataka niseme, wakati nachangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais nilitoa maelezo ya kina na nilidhani tumeelewana ni kwa nini jeshi wakati wa uchaguzi linakuwa *standby*. Narudia kusema kwamba wakati wa uchaguzi au nianze kwa kuelezea majukumu ya jeshi, majukumu ya jeshi makuu ni matatu. Kwanza ni ulinzi wa mipaka yetu; pili ni ulinzi wa amani; na tatu ni kutoa msaada kwa mamlaka za kiraia na vyombo vingine vya ulinzi na usalama wanapohitajika kufanya hivyo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati wa uchaguzi Zanzibar, jeshi liliona ni muhimu kukamata *major installations* kwa ajili ya usalama. Maeneo ya airport, bandari, redio na maeneo mengine kama hayo vililindwa na jeshi kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa ziada lakini hakukuwa na nia ya kumtisha yoyote, nia ilikuwa ni kuleta usalama. Kama walivyosema wengi hapa, naomba nirudie kauli ile kwamba, walinzi ni walinzi anayeogopa mlinzi ni mhalifu. Hakuna sababu kwa nini uwaogope walinzi kama huna nia mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachosema ni kwamba, wanajeshi walikuwa on *standby* endapo itatokea vurugu na mamlaka ya vyombo vingine vya ulinzi na usalama watahitaji msaada wao wawe tayari kutoa msaada. Hata hivyo, ukweli unabaki pale pale kwamba wakati wa uchaguzi, ninyi ni mashahidi, mimi pia nilikuwa Zanzibar nimepiga kura, sehemu zote zilikuwa zinalindwa na polisi, jeshi walikuwa kwenye *barracks* zao isipokuwa hizo *major installations* nilizoelezea hapa, basi! (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kwamba ni faida gani tunapata kwa JWTZ kushiriki katika operesheni za amani. Kwanza nishukuru kwa wote waliochangia na kusema kwamba kazi inayofanywa na jeshi kwenye ulinzi wa amani ni nzuri, tumepata sifa nyingi na tunawaunga mkono wanajeshi wetu waendelee kutuwakilisha vyema sehemu hizo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, faida tunazopata kwanza tunapata uzoefu wa Kimataifa na mbinu mpya. Pili, wanajeshi binafsi wanafaidika kwani hupata kipato kwa kushiriki ulinzi wa amani. Tatu, ulinzi wa amani umelilettea sifa jeshi letu Kimataifa. Katika takwimu za ubora zilizotolewa hivi karibuni jeshi letu Kimataifa lipo katika nafasi ya 27 ndiyo sababu sisi tunapata nafasi nyingi za kwenda kulinda amani katika nchi mbalimbali. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na hoja nyingine kama ifuatavyo:-

Ushauri wa kutumia vyombo katika shughuli za maendeleo na uzalishaji. Hili alilitoa Mheshimiwa Shamsi Nahodha nadhani nimeshalisema kwamba taasisi zetu zote zinafanya kazi hii ya kuzalisha mali na kufanya tafiti ili ziweze kupata kipato cha ziada.

Vijana wanaomaliza JKT wasiachwe bila ajira. Kama nilivyosema na alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, tuna mambo mawili, si rahisi kuwaajiri vijana wote ambao wanaingia JKT, lakini ni lazima tujipongeze kwa sababu tumefanya kazi nzuri. Takwimu zinatuonesha kuanzia mwaka 2001 - 2015, katika ya vijana wote waliochukuliwa katika makambi ya JKT walioajiriwa ni asilimia 72.9, hawa wameingia katika vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waliobaki ambao ni wachache kama asilimia 30 sasa ndiyo tumekuja na mpango huu wa uwezeshaji, wanapewa mafunzo kule na wakitoka watapewa mitaji ili waweze kujiajiri wao wenyewe. Kusema kuwaajiri asilimia 100 haiwezekani, ingekuwa vyema na ningependa iwe hivyo lakini kwa bahati mbaya bado uwezo wetu haujafikia hapo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ushauri wa kuwa na database ya vijana wa JKT. Database hiyo ipo kwa wale wanaoajiriwa na wale wanaorudi nyumbani kwa sababu nao ni jeshi la akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuimarisha vyuo vya ufundi stadi JKT ili vijana wapate stadi za kazi. Ushauri umepokelewa, Wizara inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha vyuo vya ufundi stadi JKT kwa kuviwezesha kivifaa na wataalam kadiri bajeti inavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa ardhi Tondoroni, Makuburi na Ihumwa. Tondoroni mgogoro umekwisha kuitia Mahakama kesi namba 48 ya mwaka 2005 ambapo Serikali ilishinda. Hata hivyo, wahusika halali walikwishalipwa fidia kuitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa Makuburi Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni imeandaa mchoro wa mipango miji kwa kuzingatia marekebisho ya mpaka mpya wa kambi ambapo eneo la jeshi litazungukwa na viwanja vilivyopimwa. Tulichofanya pamoja na kwamba wananchi walivamia eneo la jeshi tumeweka mpaka mpya wao tukawatoa nje ya ile mpaka kuweza kuwa-accommodate ili wasilazimike kuondoka au kulipwa fidia. Kwa maana hiyo, tatizo hapa nalionaa limekaa vizuri lakini manispaa nayo imechukua jukumu la kuwapimia wananchi wale ili wawe na hati na isiwe tena ni eneo ambalo halijapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Kambi ya Ihumwa halina mgogoro. Tatizo lililopo ni la eneo dogo la nyongeza ambapo taratibu za kulipima na kulifanyia uthamini bado hazijakamilika. Kama nilivyosema tukipata fedha tutakamilisha taratibu hizo ili tuweze kulimiliki kihalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu alitaka pensheni za vyombo vya ulinzi na usalama ziwe na taratibu zake maalum badala ya taratibu hizi za kawaida za utumishi wa umma. Hili ni wazo zuri, tunalipokea na ushauri huu utazingatiwa na tutawasiliana na wenzetu wa Hazina na Ofisi ya Rais, Utumishi ili tuangalie ni jinsi gani tunaweza kufanya lakini sote tunakubaliana na ninyi kwamba kuna baadhi ya wenzetu ambao walistaafu zamani pensheni zao haziridhishi, ni ndogo sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misheni zetu tunapokwenda nje ya nchi, walitaka kujua fedha za misheni, hili nadhani nimeshalijibu na nitoe tu ufanuzi wa ziada kwamba ziko fedha ambazo zinapatikana ukiacha zile ambazo wanlipwa wanajeshi wenyewe, sisi tunawalipa asilimia 80 ya zile zinazolipwa kutoka kule *UN* lakini jeshi pia linapata fedha kwa ajili ya kuwa na zana zake kule na pili matengenezo na tatu kuweza kupeleka zana mpya. Kwa hiyo, malipo ya fidia ya *UN* yanatolewa na fedha hizo zinalipia posho kwa wanajeshi, kugharamia ukarabati wa zana, kununua vifaa na zana mpya, kuandaa vikosi vipya kwenda kubadili vile vinavyorejea na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja ya kutaka kujua tofauti ya *Chapter Six* na *Chapter Seven* katika malipo. Malipo ya fidia ya *UN* hayatofautishi kama ni *operation* ya *Chapter Six* au ya *Chapter Seven*, yote yanafanana na ni sawa, ni *chapters* zinazotofautisha utendaji katika eneo la ulinzi na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanajeshi wetu waliopoteza maisha au kuumia kwenye *operations* hizo wote walishalipwa kikamilifu kwa mujibu wa taratibu za *UN* na za JWTZ. Kwa sasa hakuna familia yoyote inayolidai jeshi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lililochangiwa lilikuwa ni suala la *Duty Free Shops* kama alivyochangia Mheshimiwa Maryam Msabaha kwamba bidhaa zinazouzwa kule hazina nafuu na zile zinazouzwa mitaani. Tumepata malalamiko haya na nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tunalifanyia kazi kwa nguvu kabisa. Lengo letu ni kwamba mashirika yetu ya jeshi ndiyo yaendeshe maduka haya ikiwemo Mzinga ambao wameshaanza katika baadhi ya vikosi, tunataka Suma JKT waingie ili hatimaye maduka yote ya jeshi yaendeshwe na jeshi lenyewe na kwa kufanya hivyo tutaondokana na tatizo hili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za mabwalo kweli tunalo tatizo na kazi ya ukarabati wa mabwalo linatekelezwa kwa kadiri bajeti zinapopatikana. Ni kweli kwamba mabwalo mengi kwa sasa hali yake sio nzuri kutokana na uhaba wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri kuhusu bajeti, madeni na maeneo ya jeshi, nadhani hili tumeshalitolea ufanuzi. Tumesema kwamba bajeti ikeruhusu tutahakikisha tunaondoa matatizo yote haya yanayoonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii moja liliuja kuhusu wastaafu kulipwa kila mwezi. Tunachosema ni kwamba wala hatuna tatizo na wastaafu kulipwa kila mwezi kwa sababu hapo awali wastaafu walikuwa wanalipwa kila mwezi, ni wastaafu wao wenyewe waliomba kwamba sasa walipwe kwa miezi sita, walidai kwamba ile pensheni ya kila mwezi ni ndogo na wanakuwa wameshakopa, kwa hiyo, angalau wapewe ya miezi sita, wakapewa ya miezi sita. Baadaye wakabadilisha wakasema hiyo inakuwa muda mrefu sana, wakaletewa ya miezi mitatu. Kwa hiyo, kama sasa hivi wako tayari kurudi mwezi mmoja wala sioni tatizo lolote, haya ni matakwa ya wastaafu wenyewe. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uanzishwaji wa bima ya afya kwa wanajeshi hili tunalipokea na tunaona umuhimu wake. Bima ya afya kwa wanajeshi ni muhimu kwa sababu sasa hivi tunapata shida sana, bajeti ya kutoa huduma za afya jeshini haitoshelezi na kwa maana hiyo tunao mpango wa kuanzisha bima kwa ajili ya wanajeshi wote, wawe kazini au wastaafu ili hatimaye tuondoe matatizo yao ya kupata huduma zinazostahili. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yaliyochangiwa kama nilivyosema ni mengi, naomba sasa niingie kwenye hoja za Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Anasema Amiri Jeshi Mkuu kuva sare za jeshi yeye anaona hili sio sawasawa. Kwanza nieleze kwamba Uamiri Jeshi Mkuu siyo cheo bali ni wadhifa. Kwa mujibu wa taratibu za kijeshi, Amiri Jeshi Mkuu anapoamua kuva sare ya jeshi katika shughuli yoyote ile ya kijeshi kama vile kufika katika eneo la mazoezi ya kijeshi, anaruhusiwa kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili wala halijaanza hapa kwetu wala halijaanza katika awamu hii, Baba wa Taifa alivaa sare za jeshi, hapo nchini Kenya juzi juzi tu tumeona Rais Kenyatta kavaa sare za jeshi. Sioni kwa nini hii inakuwa hoja kubwa kwa sababu yeye ndiye Amiri Jeshi Mkuu. Anapoamua kuva afanane na wanajeshi wakati anaenda kwenye mazoezi yao wala hakuna tatizo hata kidogo. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wanajeshi wastaafu kuva sare za jeshi, maelezo ni kwamba mwanajeshi mstaafu anaweza kuva sare za jeshi katika

shughuli yoyote lakini awe amepata kibali cha Mkuu wa Majeshi. Mkuu wa Majeshi huwa anatoa vibali hivyo kwa shughuli maalum ikiwemo ile ya kuapishwa Wakuu wa Mikoa alitoa kibali wavae kwa sababu wala hakuna tatizo, wale ni wanajeshi kwa sasa baada ya kustaa fu ni jeshi la akiba, watakapohitajika wakati wowote wanaitwa ili waweze kufanya kazi za jeshi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kai alikuwa na hoja ya kukosekana kwa fedha za maendeleo kwa Ngome. Hili nimeshalizungumza toka awali, tunaelewa changamoto za bajeti na hii ni kwa Serikali nzima na wala siyo Wizara ya Ulinzi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja pia kukosekana kwa fedha za kulipia fidia maeneo ya ardhi. Kama nilivyosema mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 27.7, ni mategemeo yetu kwa kiwango kikubwa tutaweza kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi wa marudio Zanzibar. Jeshi kupelekwa Zanzibar Waziri atafute maneno mengine lakini siyo kwamba hawakupelekwa. Ndugu zangu naomba nirudie, nilisema hivi, watu wakisikia kwamba tunasema jeshi lilipelekwa Zanzibar wakati wa uchaguzi kila mtu atadhani jeshi halipo Zanzibar. Zanzibar kuna brigade siyo platoon wala siyo kompania kuna brigade. Brigade ya askari wa *infantry* iko Zanzibar na isitoshe kuna vitengo vya wanamaji, kuna vitengo vya *airforce*. Sasa tunapokuwa tunabishana kwamba jeshi lilipelekwa au halikupelekwa, naona haina msingi sana kwa sababu tayari jeshi lipo Zanzibar. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi liko Zanzibar kwa dhumuni moja tu, nalo ni kulinda mipaka ya nchi yetu ya ujumla ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndiyo kazi yake ya msingi kulinda mipaka yetu. Kwa hiyo, haiwezekani wasiwepo wakati mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko mpaka kule Zanzibar. Kwa hiyo, nadhani kama walipelekwa au hawakupelekwa isiwe hoja, hoja ni kwamba jeshi liko pale kwa kazi moja ya kulinda mipaka yetu na wakati wa uchaguzi kama ilivyo *international standard* kwa nchi zote wanajeshi wanakuwa *standby* ili kukitokea machafuko waweze kusaidia, basi! (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi limetumika kuwatisha watu walitolilia. Mimi nasema jeshi limekuweko pale kusaidia watu watulie kwa sababu matukio yalikuwepo na wala hatuwezi kukataa. Mabomu yalirushwa wala sisemi mimi vyombo vya habari vimesema karibia na uchaguzi na wakati wa uchaguzi si kulikuwa na mabomu ya mkono yanarushwa, si yalitokea? Sasa kweli jeshi lisingekuwepo ile hali ya usalama na amani ingekuwepo mpaka leo? Sisi tunasema jeshi liko pale kwa kazi moja ya kulinda amani si kwa kazi ya kumtisha mtu ye yoyote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba wanajeshi wa ngazi ya chini wanalipwa *ration allowance* tofauti na wa ngazi ya juu, si kweli. Jeshini *ration allowance* ni moja tu, anayopata *private* na anayopata *general* ni hiyo hiyo. Kama umepata taarifa kwa mtu yeyote si kweli, hapa nakataa kabisa, *ration allowance* ni hiyo hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fakharia anasema nafasi za ajira za Zanzibar, kwa nini vijana wasichukuliwe kutoka JKU badala ya kupitia mikoani na wilayani. Jibu ni rahisi, sisi huwa tunapeleka nafasi za Zanzibar kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Tunawaachia uhuru wa kuamua wanazigawa kwa taratibu gani. Wakiamua kupeleka mkoani na wilayani ni juu yao, wakiamua kupeleka JKU ni juu yao. Kwa hiyo, kama tunaona JKU ni utaratibu mzuri zaidi kwa pamoja sisi Wabunge wa Zanzibar tuishauri SMZ ichukue vijana hao kupitia JKU. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za makazi zijengwe na Unguja pia, hii iko katika mpango wetu wa Awamu wa II. Awamu ya I kwa Zanzibar ilianza Pemba na Awamu ya II tutapeleka Unguja. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanajeshi wastaafu kulazimika kwenda Bara kushughulikia mafao yao. Hili nalikubali kwamba ni usumbufu, hawa watu hawana fedha, wanatakiwa wasafiri mpaka makao makuu, tutatengeneza utaratibu ili brigade pale ishughulike na mafao haya kwa kuwasaidia kuchukua maelezo yao wao wayapeleke makao makuu ili waweze kupata huduma kwa urahisi bila kusafiri. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maswali ya Khadija Hassan Aboud ambapo yeye alishauri vijana wa JKT waajiriwe jeshini. Napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba ndivyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliendelea kushauri JKT iwe na aina mbili za mafunzo wale wa ujasiriamali na wale wa kuingia jeshini, tunadhani kwa sasa huo hautakuwa utaratibu mzuri sana kwa sababu uwezo wa kufanya hivyo hatuna. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba lengo la JKT si kutoa ajira ni kuwafunza vijana wetu wa Kitanzania uzalendo, utaifa na kuhakikisha kwamba wakiwa pale basi wanapata mafunzo ya kijeshi lakini pia ujasiriamali kwa maana ya stadi za kazi ili waweze kujiajiri. Kwa hiyo, hili tutalitazama kwa wakati ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niingie katika hoja za Mheshimiwa Kubenea ambazo kwa kweli zimenisikitisha sana kwa sababu hazina punje ya ukweli ndani yake. Nasikitika kusema kwamba Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano anaweza akachukua maneno ya mitaani akaingia nayo ndani ya Bunge akayasema bila ya kuwa na ushahidi, hii ni hatari tena ni hatari kubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwarifu Mheshimiwa Kubenea, sijui kama yupo humu ndani...

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuhuma anayoitoa kwamba jeshi limeingia mkataba na kampuni inayoitwa *Hainan Construction* ambapo jeshi litatoa eneo kubwa la ardhi kwa kampuni hiyo ili ijenge nyumba na kwamba kampuni hiyo itatumia kwa miaka 40 hazina punje ya ukweli ndani yake. Si kweli na naku-challenge ukiweza kuniletea uthibitisho huo mimi nitajiuzulu kwa sababu maneno unayoyasema ni ya mitaani. Nasikitika sana Mheshimiwa Mbunge kuleta maneno yasiyokuwa na uthibitisho kwa sababu maneno hayo ni ya uwongo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili alilolisema ambalo limenihuzunisha zaidi, anasema kampuni hiyo hiyo itaingia mkataba pia wa kumjengea nyumba Dkt. Hussein Mwinyi, huu siyo mgongano wa kimaslahi? Naliomba Bunge lako litumie utaratibu wa kikanuni, Mheshimiwa Kubenea akishindwa kuthibitisha maneno haya achukuliwe hatua stahiki. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu tusije ndani ya Bunge tukaharibu majina ya watu, tukawadhalilisha kwa sababu tu ya kuwa na uhuru wa kuzungumza ndani ya Bunge na *immunity* tunayopewa. Nasema uhuru tunao, *immunity* tunayo lakini kudhalilisha watu kwa maneno ambayo hayana ushahidi kukomeshwe. Huu ni uwongo mtupu, hakuna jambo kama hili. Kwanza hiyo kampuni hata kuwajua siwajui. Pili, haiwezekani maneno haya akayaleta kama hakuna mkataba wa ushahidi kama anao alete tuuone, hakuna hiki kitu, ni uwongo mtupu. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kubenea aliendelea kusema kuwa kuna tuhuma za udhalilishaji kwa wanajeshi wetu waliokwenda kulinda amani Kongo, je, ni hatua zipi zimeshachukuliwa hadi hivi sasa? Nataka nimweleze Mheshimiwa Kubenea kwamba, tuhuma zinapotolewa ni wajibu wa mamlaka zinazohusika kuchunguza, huwezi kuvamia tuhuma ukachukua uamuzi. Jeshi liliunda Bodi ya Uchunguzi, wamekwenda Kongo kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa ufanyike uchunguzi wa kina ili watakapokuja kutoa taarifa za uchunguzi na ikithibitika kwamba kuna unyanyasaji wa kijinsia ulifanyika au walifanya askari wetu hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya waliofanya vitendo hivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi hili linaendeshwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za jeshi, kwa hivyo, hakuna mtu anayeruhusiwa kufanya jambo lolote kinyume na utaratibu akaachiwa lakini tunachosema uchunguzi ni lazima ufanyike. Udhalilishaji uliosemwa na Umoja wa Mataifa ni pamoja na ubakaji,

baadhi ya watu wamedai katika ubakaji huo wamepata watoto, unafanyaje uamuzi wa kwamba huyu amekosa bila kufanya DNA test ya kugundua kama hao watoto kweli ni wa huyo anayeambiwa ni baba yao? Kwa hiyo ni kwamba uchunguzi unaendelea na ni mategemeo yetu kwamba utakapokamilia na ukithibitika hatua stahiki zitachukuliwa. Hii ni kawaida kabisa wala Mheshimiwa asipate tatizo lolote hapa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyininge nyingi ambazo zimetolewa, lakini nadhani kwa ujumla wake nimezi-summarize kwa pamoja ili tuweze kupata maelezo ya ujumla lakini nitakuwa tayari kutoa maelezo ya ziada nitakapohitajika. Kama nilivyosema awali wakati wa vifungu pia nitakuwa tayari kutoa maelezo kwa kadiri yatakavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofij)

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono nitawahoji baadaye tukishamaliza utaratibu. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### Fungu 38 - Ngome

Kif. 1001 – Defence Forces Headquaters'

Command ..... .... ..Sh.1,175,433,861,000/=

Kif. 1007 – Land Forces Command.... .... Sh.4,566,951,000/=

Kif. 1008 – Air Defence Command .... .... Sh.3,567,130,900/=

Kif. 1009 – Navy Command.... .... .... Sh.1,884,713,300/=

Kif. 1010 – Military Hospitals.... .... .... ..Sh.2,091,054,800/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### Fungu 39 – JKT

Kif. 1001 – The National Service Force... Sh.282,034,214,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – Administration and HR Management... ... .... ..Sh.17,145,250,065/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, nina orodha hapa ya watakoongea kuhusu kifungu cha mshahara. Tutaanza na Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, ninaposimama hapa sina mpango wa kutoa shilingi au jambo kama hilo kwa sababu mambo mengi Mheshimiwa Waziri ameyafafanua kwa ufasaha kabisa na mimi nampongeza sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ila katika hotuba yake nzuri tunasema brief and to the point, amesema kabisa kazi ya wanajeshi wetu ambao wanafanya kazi nzuri sana, sifa wote tunazijua, Mkuu wa Majeshi ni mahiri sana, nampongeza kwamba amepewa muda na Mheshimiwa Rais, yote haya yanaashiria mambo mazuri. Hata hivyo, kazi yao kubwa ni ya kulinda mipaka yetu, naomba Mheshimiwa Waziri afafanue mpaka mmoja muhimu ambao naona umesahaulika mpaka ndani ya Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapozungumza mpaka ndani ya Ziwa Viktoria wavuvi wetu wanavamiwa, wanaibiwa, silaha zinatoka Nairobi zinaingia mle kwa hiyo ni hali ya hatari. Hili ni jambo la kisera naomba Mheshimiwa Waziri alitolee kauli maana nimeona limesahaulika katika kitabu chake kizuri. Ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Tibaijuka kama ifuatavyo. Jeshi letu liko katika maziwa yetu pia. Tumepeleka boti za doria za navy, Ziwa Viktoria zipo na Lake Tanganyika zipo. Kwa maana hiyo ni kwamba nimwondoe wasiwasi Ziwa Viktoria sasa hivi lina boti mbili za Jeshi la Wanamaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka nilielewa hutoi shilingi, nilidhani akishasema utaelewa, endelea.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini hali halisi kwa sisi ambao tunaweza tukampa mrejesho ni kwamba majeshi yalivyokaa upande wa Ziwa Viktoria kwa mfano Jeshi la Kaboya, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba tulifanyia kazi nilipokuwa ardhi, halina eneo linaloingiza kwenye Ziwa Viktoria ambapo wangeweza kulinda ule mwambao wa ziwa. Kwa hiyo, pamoja na majibu hayo mazuri lakini ule ulinzi wa wavuvi ndani ya Ziwa Viktoria lazima niseme kwamba utahitaji juhudzi za zaidi kwa upande wako Waziri, Mkuu wa Majeshi na wahusika wote. Kaboya pale watusaidie kulinda ziwa maana maharamia wamezidi, wametoka Bahari ya Hindi wote wamerudi Ziwa Viktoria. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea ushauri wa Mheshimiwa Profesa, Mkuu wa Majeshi yuko hapa, tutalifanyia kazi suala hilo ili tuweze kutoa ulinzi zaidi. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilipendekeza kwamba SUMA JKT ambao wanafanya shughuli za kilimo na kuleta zana za kilimo ambapo kipindi cha nyuma walileta matrekta ya kutosha na tunashukuru, Serikali sasa ina mpango wa kuleta matrekta mapya tunaomba badala ya kupeleka katika idara zingine basi SUMA JKT iendelee kufanya jambo hilo. Pia vipuli na service ya yale matrekta waliyotoa karibu maeneo yote nchini basi huduma ile SUMA JKT ingejitahidi sasa kuifikisha mikoani na vile vipuli viendelee kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa muungano wao wakishirikiana na Magereza naomba kufahamu kile kitengo cha kuzalisha mbegu mbalimbali ndani ya nchi kimefikia hatua gani? Ni vema Wizara ya Ulinzi pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa maana ya majeshi yote haya yafanye kazi kwa pamoja ili kuleta tija katika eneo hili la kilimo na kuboresha sekta hiyo.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la matrekta, SUMA JKT itaendelea kuleta trekta. Napenda kutoa taarifa tu kwamba pamoja na uagizaji wa matrekta uliofanyika siku za nyuma, SUMA JKT tayari imeshaweka assembly plant katika Kikosi cha Ruvu na wataendelea kuagiza matrekta yale ili kuja kuya-assemble hapa hapa na kuyauza kwa wananchi na kuyafikisha mikoani. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu, SUMA JKT imeanzisha kampuni ya mbegu na inaendelea kuzalisha mbegu. Changamoto walikuwa wanakabiliana nayo ni kwamba Wakala wa Mbegu ulikuwa haujawalipa fedha nyingi ambazo zinadaiwa, lakini kwa pamoja tutafuatilia ili fedha zitolewe waweze kuzalisha mbegu nyingi zaidi. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Jitu Soni ameridhika, Mheshimiwa Chuachua Rashid.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kuzungumzia kidogo suala la bima ya afya. Suala hili ni adhimu sana kwa Watanzania wote kwa mustakabali wa afya zao na ni ukweli kwamba miongoni mwa mambo ambayo wanajeshi wetu wanayalamikia sana hasa sisi ambao tunakaa nao kule chini tunayasikia ni suala lao la matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kila mahali pana zahanati au hospitali ya jeshi, wanajeshi wetu wanapata shida sana kupata matibabu yao. Nimeiona nia ya Serikali katika hotuba ya Waziri lakini *it is too general*, namwomba Waziri atoe tamko ambalo ni *very specific* ni lini hasa wanajeshi wetu watakuwa wanatumia bima ya afya. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema wakati najumuisha pamoja na kwenye hotuba yangu, tumeona umuhimu wa jeshi nalo kuwa na bima ya afya. Kwa sababu tukitegemea bajeti ya Serikali mara nyingi inakuwa ni ndogo kiasi kwamba huduma zinakuwa hafifu katika vituo vya kutolea huduma vya jeshi. Kwa maana hiyo, sasa hivi tumeanza mchakato wa kuanzisha Shirika la Bima ya Afya kwa Wanajeshi ambalo litahudumia waliopo kazini na waliostaafu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema ni kwamba huu ni mchakato, siyo rahisi kusema kwamba tarehe fulani tutakuwa tumeanza. Ni mategemeo yangu kwamba kwa haraka iwezekanavyo jambo hili litafikishwa mwisho kwa hatua zake zote za mchakato huu ili hatimaye tuweze kuanza bima hii ambayo bila shaka itatusaidia sana katika kutoa huduma bora za afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua naona ameridhika. Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia kabla sijaendelea naomba niweke rekodi sawa kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua umuhimu wa jeshi. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua ulinzi wa amani wa Taifa letu. Kazi yetu ni kukosoa pale ambapo

panatakiwa kuwekwa sawa. Kwa hiyo, propaganda nyepesi zilizofanywa zilikuwa na lengo la kupotosha, hotuba yetu imeeleza wazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba ku-declare kwamba mimi ni askari wa akiba, jeshi halina vyama. Mimi ni mtoto wa mwajeshi mstaafu Meja Bulaya na wapo wadogo zangu Lebanon kule wanafanya kazi ya jeshi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri ambaye namheshimu sana, amezungumzia suala la vijana kuingia JKT, wote tunaunga mkono na mimi nilipitia huko. Tunachozungumzia hapa vijana ambao wataajiriwa wapewe mafunzo ya kivita, wapewe mafunzo ya silaha, lakini vijana ambao hawaajiriwi kwenye vyombo vyatuhusu ulinzi na usalama muwape mafunzo ya ujasiriamali. Kama hiyo progamu bado hamjaanza kuikamilisha chukueni watu ambao mtawaajiri kwenye vyombo vyetu vyatuhusu ulinzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari zake...

(*Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Kelele basi wakati naongea, kimbelembele cha nini? Athari zake ndiyo ambayo yanatokea leo, hawapati ajira na wanajua kutumia silaha, jeshi linachukua wote kila mmoja anaenda na tabia yake. Ndiyo wanaokwenda kuvamia kwenye mabenki, wengine ndiyo wanaotumiwa kupewa laki tano kamuue fulani. Tunazungumzia ulinzi wa nchi yetu, tunazungumzia vijana kukupewa mafunzo ya kiulinzi halafu hawaajiriwi, wanakwenda mtaani baadhi yao wanashiriki vitendo vyatuhusu ulinzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu sahihi, Mheshimiwa Mwinyi nakuheshimu sana, lakini kwa hili nitaondoa shilingi, *I love my country*. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja nadhani wewe utakuwa umepata hoja ya kumjibu, nilikuwa najaribu kufuatilia sijaiona. (Makofi)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane jambo moja ambalo ni la msingi kidogo. Labda niwarudishe nyuma kidogo, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa hayajaanza leo yameanza miaka mingi sana na watu wengi katika nchi hii wamepitia huko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ilikuwa ni nini, nini madhumuni ya Jeshi la Kujenga Taifa? Labda turudi kwanza kwenye madhumuni ya kuingia kwenye Jeshi la Kujenga Taifa. Unajua sasa hivi tumetengeneza kitu ambacho watu wanadhani kuingia JKT maana yake kuajiriwa, siyo sawa, siyo maana yake hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka wananchi wa nchi hii karibu wote ikiwezekana wawe wana mafunzo ya kijeshi. Wakati wa vita vya Idd Amin, waliokwenda vitani ilikuwa siyo jeshi peke yake, kulikuwa kuna vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, kulikuwa kuna mgambo, kwa sababu tunataka watu wawe tayari watakapohitajika, ndiyo maana tunawapa mafunzo ya ulinzi. Kwa upande mwininge Mheshimiwa Bulaya, hivi kuna uthibitisho kabisa wa kusema kwamba matukio yanayotokea katika benki ni vijana wa JKT? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, Serikali tumejitahidi mwaka 2001 - 2015 tumeweza ku-absorb kuajiri katika vyombo vya ulinzi na usalama asilimia 70 ya vijana, hawa waliobaki asilimia 30 tunakubaliana na ninyi kwamba kuwaacha bila ya kazi yoyote ni tatizo na ndiyo maana tumekuja na mpango mpya ambao ameeleza hapa Mheshimiwa Mhagama kwamba sasa kupitia ile Taasisi ya Uwezeshaji tutaweza kuwawezesha vijana hawa wajajiri. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi pale pale Mheshimiwa Bulaya kwamba tukichukua vijana JKT tuisiwa mafunzo ya kijeshi, tutakapohitaji watu wa kusaidia nchi hii itakapotokea mahitaji ya vijana kuingia jeshini au wakati wa vita tutakuwa hatuna watu wenye ujuzi wa ulinzi wa nchi yao. Kwa hiyo, nakuomba usitoe shilingi yangu tuelewane kwamba jambo hili linataka mjadala mpana zaidi lakini ukweli unabaki pale pale. Mheshimiwa Bulaya wewe umechelewa kwenda JKT umekwenda juzi juzi hapa lakini waliokwenda siku za nyuma hakukuwa na hoja kwamba mimi nisipopata ajira maana yake nisiende JKT. Nashukuru. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya nilifikiri umesharudisha hiyo shilingi, haya tuendelee.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ya msingi ambayo hujiona. Nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa umakini sana na nitatoa shilingi Bunge liamue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba jeshi halijaanza leo, ni kweli kabisa. Kipindi kile Mheshimiwa hakukuwa na changamoto za ajira kama zilivyo sasa hivi. Kipindi kile hakukuwa na vijana wengi kama walivyo sasa hivi. Pia anajua Serikali yetu siyo katika jeshi tu hata katika maeneo mengine mfumo wetu unamfanya kijana aamini akitoka kwenye eneo fulani anaenda kuajiriwa siyo kujajiri mwenyewe, mazingira hayo hamkuyatengeneza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Waziri amesema kuna programu ambayo wameiandaa na amekiri wale asilimia 30 waliobaki ni tatizo kwenda mtaani bila kuwa na kazi. Hoja yangu hapa ni nyepesi sana kwamba, mnajua mnahitaji watu wangapi na tangu muanze kutoa mafunzo ya JKT ni

vijana wengi wamepata mafunzo hayo, tayari askari wa akiba wapo nikiwepo na mimi mwenyewe. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema sasa hivi Mheshimiwa Waziri hiyo progamu ni nzuri, lakini mjiandae itakapoanza kufanya kazi ndiyo muwachukue wengi lakini kwa kipindi hiki mchukue wale wachache ambao mna uwezo wa kwenda kuwaajiri kwenye vyombo vya ulinzi na usalama. Programu bado kwa nini mnawachukua wote na mnakubali hiyo asilimia 30 iende mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa shilingi Bunge lichangie halafu muamue, natoa hoja. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Askari haolewi.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, watakaochangia sasa tunachukua majina, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Almas na Mheshimiwa Waziri Mwigulu. Halafu Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Cecilia Pareso na Mheshimiwa Bobali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza sasa kuchangia hiyo hoja, tutaanza na Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Taifa letu ni Taifa linalokua na jeshi letu naamini linafanya *transformation* ya kutosha kulingana na mazingira tuliyonayo. Ukiwa na *spiritual problem* huhitaji *economical solution*. *Challenge* kubwa tuliyonayo katika nchi yetu sasa hivi, nathamini sana mchango wa jeshi letu linafanya kazi vizuri lakini adui mkubwa wa nchi yetu sasa hivi ni umaskini. Kwa hiyo, ni lazima jeshi letu liwe transformed kukabiliana na *challenge* tulizo nazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Bulaya ni jeshi lihame sasa pamoja na ulinzi ambao ni wa muhimu lifikiri zaidi kumwona adui yetu mkubwa ni umaskini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bulaya anachokizungumza ni kuli-transform jeshi liwe na mawazo ya kuwafanya vijana wawe wanaajirika kupambana na huyu adui umaskini kuliko kufikiria zaidi adui wa kuvamiwa na mipaka na nchi za nje. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bulaya. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Ukiwa na ubongo wa kuku huwezi kuelewa ninachokisema.

**MBUNGE FULANI:** Wewe.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Bulaya ni ya msingi kwa sababu tunataka jeshi ambapo hawa vijana wanaokwenda JKT, kwa sababu sasa hivi tukiwaonesha hata kwenye meseji zetu kuna vijana wengi ambao wamekwenda JKT jambo ambalo ni jema lakini wako mitaani kwa sababu *mentality* yao kubwa walidhani watakwenda kuajiriwa, hawajapata mafunzo hayo ya ujasiriamali ambayo Mheshimiwa Bulaya ndiyo anayoyasema. Kwa hiyo, lazima tumjue adui yetu ni nani sasa hivi, nchi yetu ina jeshi imara ambalo linaweza likapambana vizuri, lakini tunataka wanajeshi wasaidie kupambana na umaskini ambao ndiyo adui mkubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana wa nafasi hii ili nichangie hoja hii ya Ndugu yangu Ester Bulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linaloonekana hapa ni watu kutoelewa tu. Vijana wanaokwenda JKT siyo jeshi la miezi mitatu waliokwenda watu, tumekwenda kule mwaka mzima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jeshi lile halifundishi mambo ya kazi tu linafundisha uzalendo, upendo wa nchi yetu na vijana wakatoka kule wameiva. Hao vijana wanaochukuliwa wakabakia asilimia 30 hawatoshi kujaza sekta ya ulinzi binafsi ambayo leo ina makampuni 900 na inahitaji vijana milioni mbili kwa mwaka, hawatoshi! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa hawa wanajeshi wanaobakia baada ya mafunzo ni watu wazuri kabisa, wamefundishwa amani, upendo wa nchi yao siyo wezi, hawajabadilika. Wengi wao ndiyo wanaofanya kazi kwenye *security industry*, lakini pia wanafanya kazi za huu ulinzi shirikishi au polisi jamii, ni watu wazuri. Hawa watu anaoongelea course ya miezi mitatu ya kwenda kutembea jeshini siyo kupata mafunzo, hauwezi kulinganisha na vijana waliokaa miaka mitatu jeshini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na na-declare interest nilikuwa Mwenyekiti wa Makampuni ya Ulinzi Tanzania na makampuni hayo hayana watu, yanafundisha askari wake wenywewe. Watu wote wa JKT wamechukuliwa na waliobaki hawatoshi lakini vilevile tunafundisha askari wetu wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige hoja iliyopo unayoiunga mkono ni ya kuondoa shilingi, naamini ndiyo ulimaanisha hivyo? (Makofi/Kicheko)

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Ester, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Tuendelee, Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Ester, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nitasema kwa nini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni lazima tufahamu majukumu ya msingi ya jeshi letu. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kwanza ulinzi wa mipaka yetu, amani lakini namba tatu inapotokea needs liende likashiriki kwenye shughuli za kiraia, kuna madaraja yamebomoka jeshi likafanye kazi hiyo. Hayo ndiyo majukumu ya msingi ya jeshi letu siyo kutengeneza ajira, hilo limekuja baadaye. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwa nini siungi mkono hoja hiyo, napenda kusema hata hawa vijana tunaowachukua kwa ajili ya JKT, Waziri amesema asilimia 70 wanakwenda kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, asilimia 30 wanajiajiri na mtu anapojiajiri pia anaweza ku-generate ajira ya mtu mwengine. Sasa nimuulize Mheshimiwa Ester Bulaya yeye alipokwenda JKT alikuwa anakwenda kutafuta ajira mbona alishakuwa nayo? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja hizo, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Ester, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya. Ni kweli kwamba kuna umuhimu wa kuwapeleka vijana hawa kwenda kupata mafunzo ya jeshi. Hata hivyo, huwezi ukawapeleka vijana hawa wanajifunza mambo mbalimbali ya utumiaji wa silaha na kila kitu, halafu mwisho wa siku wanarudi mtaani bila kujua wanakwenda kufanya nini. Umewapa ujuzi, wanakwenda mtaani hawana uhakika wa kupata ajira maana yake unakwenda kutengeneza tatizo lingine mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata nafasi ya kwenda *Israel* na sera za *Israel* vijana kati ya umri wa miaka 18-20 kwa wasichana na miaka 18-21 kwa vijana kwa maana ya wanaume, wote wanakwenda jeshini, ni jambo jema. Serikali nafikiri ndivyo ambavyo inafanya au labla inafanya kwa wale wanaomaliza kidato cha tano na sita lakini kwa nchi hii vijana hawa wakitoka wana uhakika wanakwenda kufanya nini, hapa tunawapeleka lakini akitoka hana uhakika

anakwenda kufanya nini. Amejifunza kutumia silaha, anajua kutumia silaha, anarudi mtaani hana kazi. Anakaa mtaani anacheza *pool table* na anajua kutumia silaha, matokeo yake tunatengeneza bomu, tunatengeneza uhalifu mtaani, tunatengeneza tatizo juu ya tatizo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester Bulaya, tusitishe mpango huu kwanza, Serikali ijipange, ifanye tathmini kwenye miaka iliyopita. Kwa sababu amesema asilimia 70 wanapata ajira na asilimia 30 wanabaki mtaani, asilimia 30 siyo ndogo ni vijana wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mnasema mnatumia huu Mfuko wa Uwezesha jani wananchi, ule Mfuko ni wa wananchi wote. Kwanza kwenye bajeti iliyopita tumetenga shilingi bilioni moja tu haitoshi na inachukua vijana wote na watu wote, siyo hao tu. (Makof)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mwigulu Nchomba.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwakumbushe Wabunge kwamba Wabunge tulipokwenda JKT kwa muda mfupi ilikuwa ni katika kuunga hamasa ya Serikali kuchukua vijana wengi iwezekanavyo kwenda JKT. Sisi ndiyo tulikuwa tunahamasisha baada ya JKT kuacha kuchukua vijana. Kwa hiyo, leo hii tunapingana na hamasa tulioifanya sisi wenywewe, la kwanza hilo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ester hiyo hoja unayosimamia kwa mantiki yenye we iko kushoto sana, kwa sababu gani? Maja, unaposema kwamba Serikali ichukue wale tu itakaowaajiri na vyuoni tuchukue wale tu tutakaowaajiri, shule ya msingi tuchukue wale tu tutakaokuja kuwaajiri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja, tunapoongelea vijana kwenda JKT tunalenga kwanza kuwafundisha uzalendo. Pili, tunalenga kuwafundisha namna ya kwenda kwenye shughuli za uzalishaji. Tatu, tunalenga kuwafundisha ukakamavu, hatuwezi tukatenga watu tunaotaka kuwapeleka kwenye ukakamavu. Kwa maana hiyo, hoja yako unayosema wachukuliwe wachache kwanza tutakuwa tuna-defeat the whole purpose ya kutengeneza wazalendo, tulisema uzalendo umeshuka kwa sababu tumeacha kupeleka vijana jeshini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ninachosema, kwanza, hii habari ya kutaka kusema wale waliokwenda jeshini ndiyo wanaofanya mambo

ya uhalifu, nakwambia nenda kafanye utafiti. Naamini wale ambao hawakwenda jeshini ndiyo wanaofanya mambo ya uhalifu na wale waliokwenda jeshini ndiyo ambao wamekuwa wazalendo. Kwa maana hiyo, ningetamani vijana wote wenye uwezo wa kwenda JKT waende na mambo ya uhalifu yatapungua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tutakapoweza kuwa na vijana wengi wenye ukakamavu, wanaweza kufanya mambo ya ulinzi maana yake hata mtaa kwa mataa majambazi yatapungua kwa sababu kila unayekutana naye ni askari. Leo hii ukienda nchi ambazo zimepiga vita sana mambo ya ukwapuaji, ni wale ambao huwezi ukatambua yupi ni mwanajeshi maana karibu kila raia amekuwa mwanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, siungi mkono hoja ya kusema unaondoa shilingi kwa ajili ya kupunguza vijana wanaokwenda JKT.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu muda wako umekwisha. Mheshimiwa Bobali.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Tusiwa-brand watu hawa ambao wameshapitia mafunzo kama kuwa ndiyo wanaofanya uhalifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muda wako umekwisha.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru. Nianze kutambua uwezo mkubwa alionao Waziri kwenye kuliongoza jeshi, sina mashaka na uwezo wa Waziri. Pia sina mashaka na nia thabiti ya Serikali kwenye ku-recruit vijana JKT, sina mashaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bulaya kwenye concept moja tu, amesema tuchukuwe ile idadi ambayo tunaiweza kuajiri. Hapa kuna theory mbili, theory ya Serikali ni training vis-a-vis security. Theory ya vijana wale wanaochukuliwa ni training vis-a-vis employment kwamba akishapata training atapata ajira, ndiyo concept waliyonayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa nafikiri mchakato unaendelea huko wilayani, tunatumwa message Waheshimiwa Wabunge kwamba tufanye mpango majina yao yapite kwa Mkuu wa Wilaya, wao wanadhani ndiyo ajira moja kwa moja. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na hoja ya kwamba vijana waende JKT lakini tuchukue wale tu ambao tuna-capacity nao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu anaposema kwamba watu wanakwenda kufundishwa uzalendo, hivi tumesahau mwaka jana hawa vijana wameandamana Dar es Salaam? (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Wazalendo hao.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mwaka jana wameandamana, wamekwenda kwa Waziri kudai ajira!

**MBUNGE FULANI:** Uzalendo.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Sasa uzalendo huu tuliowafundisha, ni kwa kiwango gani wamehitimu kiwango hicho cha uzalendo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Bulaya. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami napenda nichangie katika hoja hii kwa kupinga suala la kwamba tuwachukue vijana tuwapeleke katika kitu tunakiita Jeshi la Kujenga Taifa halafu tukawafundishe ujasiriamali peke yake bila ile tunayoita jeshi kuwapa kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tabia ya mtu haitokani na umaskini wala utajiri. Wapo humu ndani ambao tunaamini hawana shida yoyote ya umaskini lakini wanafanya vitu vya ajabu ambavyo hata kuvisema vingine tunaogopa kwa hadhi ya jengo hili. Hayo wanayoyafanya hayatokani na kwamba aidha wao ni maskini au ni matajiri, ni malezi yao na tabia zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka vijana kuwafundisha ujasiriamali tuwapeleke VETA, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vingine. Kama tunawapeleka kwenye Jeshi la Kujenga Taifa watafundishwa ujasiriamali lakini pia wafundishwe na mambo yote ya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sikubaliani kwamba wote wanaokwenda JKT waajiriwe, hata maseluwe waajiriwe, hata ambao afya zao zina mgogoro waajiriwe, hata wale ambao hawana utaalam wowote wamefika pale wamekuwa goigoi mpaka siku ya mwisho na wenyewe waajiriwe. Kwa kweli hilo sikubaliani nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa mtoa hoja alikwenda JKT miezi mitatu tu kwa hiyo, hakuiva...

**MBUNGE FULANI:** Wiki sita.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Wiki sita hakuiva. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeenda JKT mwaka mzima nimejifunza ujasiriamali lakini pia nimejifunza na mbini zote za kijeshi na sijawa jambazi hata siku moja na wala sifikihi hata kama nitakuwa maskini wa kutupwa.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ghasia muda wako umekwisha.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewe jambo moja. Uzoefu wa Jeshi la Kujenga Taifa ni uzoefu katika nchi nyingi dunia kote na wala siyo Tanzania tu na unakuwa na makusudi maalum. Tumesema hapa kwamba Jeshi hili la Kujenga Taifa ni maalum kwa ajili ya kuandaa vijana wa Kitanzania kujenga uzalendo, kukuza maadili lakini jeshi hilo pia linatumika kama kitengo cha kuwasaidia vijana hawa kujajiri ili kuweza kupambana na maisha ambayo wanaweza kukutana nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema jambo moja. Waziri hapa amesema, asilimia 70 ya vijana waliokwenda Jeshi la Kujenga Taifa wamepata ajira. Takwimu zinatuambia, mwaka 2006/2007 ajira zilikuwa wastani wa watu milioni 16.6 lakini mwaka 2014/2015 ajira zimeongezeka mpaka watu milioni 20 wakiwemo hiyo asilimia 70 waliokwenda Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, tarehe 22 Oktoba, 2015, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Baraza la Uwezeshaaji Wananchi Kiuchumi limeingia mkataba na Jeshi la Kujenga Taifa kuangalia namna nzuri ya ile asilimia 30 ya vijana ambao wameshafundishwa uzalendo, wafundishwe sasa kujajiri na kuajiri wenzao ili kuongeza ajira katika nchi yetu ya Tanzania. Jambo hilo limeshaanza kuchukuliwa hatua na limeshaanza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba tuache kuchukua hao vijana kwa sababu tayari tumeshajiaandaa kama Serikali kuwachukua vijana hao kwa idadi iliyopangwa, wale watakaoajiriwa waajiriwe, wale wanaobaki wapate opportunity ya kufundishwa

kujajiri na kuweza kuajiri wenzao. Kama Serikali tumeshapanga jambo hili kwa nini Wabunge wasiunge mkono wazo hili zuri la Serikali la kuwasaidia vijana kuweza kujajiri na wakatae vijana hao kupata opportunity hiyo ya kwenda kufundishwa? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono wazo hilo, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri, Serikali ikawafundishe vijana waweze kujajiri. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa michango yote ambayo imetolewa, lakini naomba tu niwarudishe nyuma kidogo kwenye malengo ya JKT. Nadhani nilivyoeleza awali huenda Mheshimiwa Ester hakunielewa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, madhumuni ya Jeshi la Kujenga Taifa tukiacha mambo mengine yote ni kujenga uzalendo na kuleta umoja wa Kitaifa katika nchi yetu. Tunawakusanya vijana kutoka nchi nzima na kutoka katika kila wilaya wanakutana sehemu moja kwa ajili ya kujenga Utaifa kwa vijana wetu. Tukisema tunawachukua wale wa ajira tu hawa wengine wote watapata wapi mafunzo haya? Hilo la kwanza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, watu wanaodhani kwamba hawa vijana hawapewi mafunzo ya ujasiriamali au stadi za kazi, si kweli! Mkataba wa vijana wa JKT ni miaka miwili, miezi sita ya kwanza tu ni mafunzo ya kijeshi baada ya hapo ni uzalishaji mali, ni stadi za kazi, wapo wanaofundishwa kilimo, ufugaji, uvuvi, uashi, useremala, kazi zote wanafundishwa kule. Kwa hiyo, kusema kwamba wakitoka pale basi ndiyo *lost case*, si kweli! Vijana hawa wana uwezo mkubwa zaidi wa kuajirika kuliko yule ambaye hajapita kule. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mnielewe sana, Mheshimiwa Ester naomba anielewe sana kwamba madhumuni ya kuwapa hii miezi sita ya mbinu za kiulinzi ni kwamba huenda tutawahitaji vijana hawa wakati nchi inahitaji jeshi la akiba. Kwa hivyo, sioni ubaya wowote wa kuwapa hizi stadi za kijeshi lakini baada ya hapo njia za kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Ester atakuwa amenielewa kwamba hapa tuna jambo ambalo Kimsingi madhumuni yake ni mema, nia yake ni njema wala sidhani kama kuna haja ya kujadiliana zaidi kuhusu hili lakini ataamua. Ninachosema ni kwamba jambo hili ni zuri na tutaendelea kuhakikisha kwamba wanaokosa *in fact* hata siyo 30 percent wale wanaopata ni 72.9%, kwa hiyo wanaokosa ni *less than* 30 percent na tayari kuna mikakati ya kuwawezesha hawa. Kwa hiyo, nadhani jambo hili ni zuri tu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa mamlaka niliyopewa na Kanuni ya 104(1), naongeza nusu saa ili tuweze kumalizia Kamati ya Matumizi. Mheshimiwa mtoha hoja ya kutoa shilingi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nadhani kuna wengine hawajanielewa kwa hiyo sitapoteza muda wa kuwajibu kama akina Mheshimiwa Hawa Ghasia. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipingani kabisa na Mheshimiwa Waziri, sipingani kabisa na dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa hiyo mipango iliyopo. Nianze na kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu, natambua dhamira ya vijana kwenda jeshini na kweli wote tulihamasisha na kule jeshini wapo wanaokwenda kwa mujibu wa sheria na wapo wanaokwenda kwa hiari na wanaokwenda kwa hiari dhumiuni lao ni kwenda kuajiriwa kwenye vyombo vya ulinzi. Wale wa *form six* ndiyo wanaokwenda kwa mujibu wa sheria, wote hawa wanaunganika. Ndiyo wanafundishwa mafunzo ya kijeshi wanafundishwa pia na mambo mengine. Kwa hiyo, sijapinga hapa eti watu wasiende wote, hapana, tunatofautiana na ninyi kitu kimoja kwamba siyo wote lazima wapewe mafunzo ya kutumia silaha, hicho tu, hicho tu! (Makofi)

(Hapa baadi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Almas kwamba mimi nilienda miezi mitatu sikwenda kutafuta ajira, Mheshimiwa Mwigulu amekusaidia tulienda kuwahamasisha vijana kama viongozi vijana, nimeleka kule nimerudi kwenye ajira. Nakubaliana naye kwamba kuna wengine wanakaa mwaka mzima ndiyo hao ninaowazungumzia mimi. Baadhi yao wanakaa mwaka mzima kile walichokuwa wanakitaka hawakipati na sijasema wote, wengine ndiyo wanakwenda kutumia kwenye vitendo ambavyo si vizuri, wanajua kutumia silaha, ni mbaya! Tuendelee kuwapa *training* wale wote ambao tunasema tunaandaa jeshi la akiba sikatai, tupime tunawahitaji wangapi, tangu tulipoanza kuwaingiza hilo jeshi la akiba halijatosha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo wote waende wapewe mafunzo ya silaha, ni hatari kwa mustakabali wa Taifa letu, ndicho ninachokisema siyo wasiende. Hii mipango anayosema Mheshimiwa Jenista Mhagama, tulijibowi hivi mwaka jana, leo iko wapi? (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Jeshi la akiba pia silaha lipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester naomba utoe hoja yako.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja Bunge liamue niingie katika historia ya kusimamia ulinzi wa ukweli wa Taifa langu. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Sawa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu hoja hii ya Mheshimiwa Ester Bulaya ya kuondoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MWENYEKITI:** Naamini waliosema siyo wameshinda, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri umebaki na shilingi yako. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Ali Salim Khamis lakini Mheshimiwa Ester mimi naamini wewe ni jeshi la akiba linalojua kutumia silaha siyo?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Yes!

**MWENYEKITI:** Vizuri! Mheshimiwa Ali Salim Khamis.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili kuomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kwanza, nimshukuru Waziri Kivuli wa Kambi Rasmi ya Upinzani na pia kulipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-declare interest, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali na ndiye niliyetoa ushauri kwamba yale maduka yaliyoko jeshini kwa sababu jeshi halifaidiki jambo hili lifanyiwe utaratibu mwingine ili Wanajeshi wenye waweze kudhibiti maduka haya na yawape faida tofauti na utaratibu uliopo sasa hivi. Kwa hiyo, hatulichukii jeshi na nashukuru kwamba Katibu Mkuu amelichukua na akalifanya kazi na leo liko kwenye hotuba ya Waziri hapa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, Mheshimiwa ametoa maelezo hapa katika usanifu na upimaji wa maeneo au kambi za jeshi na ameelekeza maeneo ambayo yataanza kufanyiwa malipo, lakini sasa hivi ukiangalia Kambi ya Mtoni kule Zanzibar tayari imezungukwa na wananchi katika maeneo yote. Hali kadhalika ile Kambi ya Msikiti Makufuli ambayo pia nayo imeweza kuvuka maeneo imefika mahali sasa kambi ya jeshi inaishi na wananchi katika eneo lake. Hata hivyo, sijaona eneo hata moja kwa Zanzibar ambalo litaanza kupatiwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie Zanzibar katika Kambi za Jeshi ambazo zimezungukwa na wananchi kwa sasa ni hatua gani za haraka zitachukuliwa ili usanifu huu ufanyike na wananchi walipwe fidia kupisha Wanajeshi kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ali Salim kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka ieleteweke kwamba si maeneo yote ambayo wananchi wamekaribia Kambi za Jeshi watalipwa fidia kwa kuwaondoa. Yako maeneo mengine ambayo kwa makusudi kabisa tunaamua kubadilisha mipaka na tumeshafanya maeneo kadhaa, kwamba sasa wananchi wamekuwa wengi sehemu ile, mipaka ya jeshi inarudishwa nyuma ili kuwe kuna mpaka unaoeleweka kati ya wananchi na jeshi na baada ya hapo tunaweka mabango ili wananchi wasiendelee kusogea. Kwa hiyo, kusema kwamba kila kambi iliyokaribiwa na wananchi watalipwa fidia si sahihi, kwanza hilo naomba lieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ziko kambi kule Zanzibar kwa mfano Kisakasaka, Wabunge wengi wanaielewa hapa, tumeshafanya utaratibu huo wa kubadilisha mipaka ili kuwa-accommodate wale wananchi waendelee kubaki pale lakini bila ya kuondoa jeshi lenyewe au kuwalipa fidia. Tunafanya hivyo si kwa sababu maeneo hatuyahitaji, tunafanya hivyo kwa sababu ya changamoto ya kibajeti. Kwa hiyo, tunalazimika tubadilishe mipaka ili raia walioko pale waendelee kukaa pale bila kuhitaji malipo ya fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika kitabu changu Mheshimiwa Mbunge hakuona kwamba kuna eneo lolote la Zanzibar ambalo litakwenda kulipwa kwa sasa kwa sababu bado tunatafakari yale maeneo ambayo hatuhitaji kulipia fidia basi mipaka ibadilishwe ili wananchi waendelee kukaa pale na hivyo hatutohitaji fidia hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ali Salim Khamis.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Waziri aniambie kwa sababu hili tatizo Zanzibar limekuwa kubwa. Kwa kambi ile ambayo iko pale Makufuli, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini ana nyumba yake na amelipwa na ile nyumba sasa hivi imechukuliwa na jeshi. Kwa nini hawa wananchi wa kawaida huo uharaka haufanywi ili maeneo haya

yakapimwa na kama ni kuondoshwa katika maeneo ambayo yako karibu na kambi za jeshi waondoshwe ili Wanajeshi waweze kufanya kazi zao vizuri? (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumeshauri uongozi wa jeshi ulivyokuja kwamba mpaka sasa hivi haya maeneo ambayo jeshi linasema ni ya kwake hawana hizo hati zinazoonyesha kwamba wao wanamiliki hayo maeneo. Wananchi tayari walikuwepo pale lakini jeshi wakachukuwa wakasema hili ni eneo letu na wananchi wamehamishwa na haki zao hawajapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini tatizo hili kwa kule Zanzibar litamalizwa kwa sababu ukisema tu kwamba mnatafakari muone, mwananchi atatafakari vipi wakati yeye mwenyewe bado anaishi pale na familia? Waziri atuambie ni lini kazi hii itafanyika ili wananchi waache masuala ya kukaa katika maeneo ya kambi za jeshi na Wanajeshi wafanye shughuli zao bila bugudha yoyote. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Ali Salim anielewe, mfano alioutoa wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa kulipwa fidia ili aweze kuondoka na jeshi lichukue eneo lile, hiyo ilitokea kwa sababu kwanza ni nyumba moja, kwa hiyo, kuna urahisi wa kuilipa ili kusiwe tena na mtu pale katika eneo la jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, fidia ile ililipwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kutambua kwamba wao walikosea kumpa mtu katika eneo la jeshi. Kwa hiyo, baada ya kuwa amejenga, wakaona kosa lao ndipo wakaamua kumlipa fidia ili aondoke, jeshi likabaki na lile eneo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukizungumzia maeneo ambayo yana watu wengi, hizo fedha tunazozzungumzia hapa za kuweza kuwalipa watu wote zinakuwa mgogoro. Ndiyo maana nikasema ikitokea hali kama hiyo tunaona ni afadhali kubadilisha mipaka ili waliokuwepo pale waendelee kukaa pale na wasilazimike kulipwa fidia kwa sababu fedha hazipo lakini ikithhibitika wakati wa kubadilisha mipaka kwamba kuna baadhi bado wako ndani tunahitaji kuwalipa, huwa wanalipwa na hayo tumeendelea kufanya, hii haitakuwa mara ya kwanza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, nadhani Mheshimiwa Khamis ameridhika.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo.

**MWENYEKITI:** Hakuna tena nafasi Mheshimiwa kwa mujibu wa Kanuni, umeshapewa nafasi mara mbili.

Mheshimiwa Gekul umetoa taarifa una kifungu kidogo unachotaka kukiulizia, kitaje kifungu tafadhalii.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kifungu kidogo cha 227500, *other supplies and services*. Nilivyopita kwenye randama nikabaini maelezo ya kifungu hicho ambacho kina shilingi bilioni 3.9, maelezo yake ni kwamba fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya stahili za Majenerali wastaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hiki kifungu kinapungua wakati Wabunge tukizungumza suala la hawa wastaifu kwamba wapewe stahiki zao kwa kadri Bunge lilivyopitisha. Fedha zilizoombwa mwaka 2014/2015 zilikuwa shilingi bilioni 2.6, mwaka 2015/2016 ni shilingi bilioni 3.9, *this time imepungua kwa shilingi milioni 64*. Naomba nifahamu ni kwa nini fedha hizi zimepungua ilhali hawa wastaifu bado wapo na hata katika *delivery* yake hizi pesa hazitolewi kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Gekul kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka tuelewe kwamba kwa bahati nzuri sana katika fedha ambazo zinawekewa kipaumbele ni fedha za kulipa stahili za Majenerali wastaifu kwa sababu kwao hii ni kama mishahara, ni jambo la muhimu. Kwa hiyo, fedha za OC zinapopatikana hiki kifungu kinatoa kipaumbele kuwalipa wastaifu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba huu unatokana na mambo kadhaa. Moja ambalo naweza nikalitolea ufanuzi sasa hivi hapa ni kwamba si mara zote tunanunua magari, inategemea na idadi ya wanaostaifu. Kwa hiyo, inapoonekana kwamba kwa mwaka husika watastaifu ni wachache basi fungu hili linaweza likapungua. Mwaka uliopita mathalani walistaifu Majenerali 16 kwa wakati mmoja, tulihitaji fedha nyingi zaidi, mwaka huu inaweza kuwa idadi yao imepungua kwa hiyo fedha hizi tuna matumaini kwamba zitakidhi haja. (Makofii)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 – Finance and Accounts.....Sh.228,995,000/=

Kif. 1003 – Policy and Planning.....Sh.316,607,600/=  
Kif. 1004 – Internal Audit Unit.....Sh.105,674,000/=  
Kif. 1005 – Procurement Management  
Unit.....Sh.76,181,200/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 – Legal Services Unit.....Sh.36,137,200/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba maelezo ya ufanuzi kuhusu kifungu 221300 kinachohusu education material, supplies and services. Katika randama inaonyesha kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kununua majarida ya sheria na natambua kwamba hiki ndiyo Kitengo cha Sheria na sheria mara nyingi zinabadijika na Wanajeshi wana matatizo pia ya kisheria, inawezekana ikatokea cases na kadhalika. Naomba kuuliza, kama mwaka huu hawajatengewa hela yoyote, je, kitengo hiki katika ununuzi wa haya majarida ya kisheria unafanyikaje na haoni kwamba itakuwa ni tatizo kwa kitengo hiki?

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kwamba fedha hizi zinatumika kununua majarida ya kisheria lakini kunapokuwa na ukomo wa bajeti kwa sababu ya kupungua kwa OC ili tuongeze fedha kwenye maendeleo hakuna budi kupunguza maeneo kadhaa. Kwa hiyo, wao wenye Kitengo hiki cha Sheria katika Wizara wameona wapunguze sehemu hii. Kwa hiyo, hakuna maelezo zaidi ya kwamba hii imetokana na upungufu wa bajeti.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1007 – Government Communication  
Unit.....Sh.36,600,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1009 – Independent Telecommunication  
Network.....Sh.84,893,600/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu kifungu kidogo 221200, communications and information. Hili ni suala zima la TEHAMA, lakini ukiangalia mwaka jana walikuwa na shilingi milioni 17, mwaka huu zimepungua almost half, ni shilingi milioni tisa, wakati tunatambua kwamba jeshi letu kitengo hiki ni muhimu sana kwa sababu tunajua kuna masuala ya mitandao. Nataka tu maelezo ni kwa nini fedha hizi zimepungua? Kama pia ni kwa sababu ya ceiling basi sitakuwa na hoja, lakini nadhani kitengo hiki ni muhimu sana kwa ajili ya TEHAMA na TEHAMA ndiyo mpango mzima katika nchi yetu sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwenye hili lakini kwanza nimfahamishe tu kwamba hii ni Wizarani, siyo jeshini. Jeshini kwenye vote yao ya Ngome wana vote hii na JKT wana vote hii, ni pale Wizarani tu ambapo kuna kitengo kidogo. Kwa hiyo, fedha hizi zimepungua kwa sababu tu ya kupungua kwa fedha za OC, kwa hiyo wamejibana hapa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 – Industries, Construction  
and Agriculture ..... Sh.457,497,200/=

Kif. 2002 – Military Research and  
Development ..... Sh.84,952,200/=

Kif. 2003 – Building Consulting Unit ..... Sh.159,942,435/=

(Vifungu Viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 – Estate Mgt and  
Development Unit ..... Sh.267,447,500/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nipate tu maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri maana naona siyo kawaida, kuna vifungu zaidi ya kumi hapa kuna sifuri wakati mishahara ipo, nazungumzia hiki hiki kifungu cha Estate Management and Development Unit. Kule juu mishahara ipo lakini vifungu vingine, operating services na kadhalika vyote zero. Ningombaa maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitengo ambacho kipo Wizarani. Kwa hiyo, ukiona baadhi ya maeneo haya hayajawekewa fedha maana yake fedha hizi zinaweza zikawa zimewekwa katika fungu la utawala.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **FUNGU 38 – NGOME**

Kif. 1001 – Defence Forces  
Headquaters' Command.....Sh.10,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **FUNGU 39 – JKT**

Kif. 1001 – The National Service  
Force.....Sh. 8,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **FUNGU 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – Administration and HR Management.....Sh.0

Kif. 1003 – Policy and Planning.....Sh.250,000,000/=

Kif. 1009 – Independent Telecommunication

Network.....Sh.10,000,000,000/=

Kif 2001 – Industries, Construction  
and Agriculture.....Sh.14,300,000,000/=

Kif. 2002 – Military Research  
and Development.....Sh.177,500,000,000/=

Kif. 2003 – Building Consulting Unit.....Sh.250,000,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2004 – Estate Mgt and Development

Unit.....Sh.27,700,000,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ingawa pia nilitaka nisimame kwenye kifungu 1001 lakini hamkukitaja, naomba nizungumzie kifungu 2004, Estate Management and Development Unit, kifungu kidogo 6103, Defence schemes. Kwenye randama kimeainishwa kwamba ni fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kugharamia maeneo ya jeshi, uthamini na ulipaji wa fidia. Wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha hotuba yake na baadaye wakati anajibu, kwa Tarime alisema fedha ambazo zitatengwa zitakwenda Mtaa wa Ronsoti tu. Atakumbuka kwamba ni kwa muda mrefu kuanzia mwaka 2007 wale Wanajeshi amba wanatakiwa wawe katika Kata ya Nyandoto wamekuja Kata ya Nkende na Nyamisangura, Mtaa wa Msati na Kenyambi hajautaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hizi shilingi bilioni 27.7 zitakwenda pia kufanya tathmini na kulipa hiyo mitaa mingine ambayo hakuainisha kwenye kitabu chake kwa maana ya Msati na Mtaa wa Kenyambi kwenye Kata ya Nkende na ukizingatia wale Wanajeshi wametufuata sisi raia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja ufanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Esther kwamba suala lake tumelijadili na tumeona ni vyema timu ya wataalam ielekee huko katika eneo husika siku ya Jumatatu ya wiki ijayo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kwenda huko ni kupata uhakika wa maeneo haya pamoja na nani anayestahili fidia. Kwa sababu zipo taarifa kwamba kuna eneo moja ambapo jeshi ndiyo liliombwa na mkoa lije likae hapo kwa ajili ya kuzuia mapigano ya koo mbili kule. Kwa hiyo, kama kuna mtu anastahili kulipa fidia ile ilibidi mkoa ndiyo walipe lakini wala hatujalitolea maamuzi ndiyo maana tunatuma timu iende ikaangalie maeneo yote aliyoyataja halafu waje watushauri vizuri, wale amba watakuwa wanastahili fidia tutawalipa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Bunge linarudia.

(Bunge *lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae, mtoa hoja, taarifa. (Makofi)

## TAARIFA

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji. (Makofi)

(Hoja *ilitolewa iamuliwe*)  
(Hoja *iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa kweli Wizara hii naona imeungwa mkono sana maana siyo nimezikia tatu tu, kwa hiyo, naamini waliosema ndiyo wameshinda. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na Wabunge watatu walikuwa wanaomba miongozo, sasa nitawapa nafasi waombe miongozo yao. Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Nape Nauye na Mheshimiwa Nchambi. Mheshimiwa Waitara.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri wa Habari, ndugu yangu Mheshimiwa Nape anazungumza na akafanya rejea ya Katiba ya Chama cha Mapinduzi, niseme pia kwamba na mimi nimewahi kuwa mwanachama wa CCM, nilikuwa Katibu wa Vijana wa Mkoa wa Tanga, kwa hiyo nimeingia kwenye vikao vya CCM ngazi ya Mkoa kama Mjumbe wa Sekretarieti na Katibu

wa Vijana lakini pia kama Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM na vilevile kama Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM wa Mkoa na Taifa pia. Kwa hiyo, naifahamu Katiba ya CCM vizuri na hawajabdalisha sehemu kubwa na nilikuwa naisoma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa sababu ni kweli kwamba tumesikiliza mjadala humu, pamoja na mambo mengine ambayo yalikuwa yanapotoshwa kwamba Kambi ya Upinzani inonekana haiungi mkono Wanajeshi lakini nataka nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri amesema vizuri, tunaliheshimu sana jeshi. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri, Mawaziri wengine waige mfano wake wanapokuwa wana-wind up hoja, kwanza amejibu hoja za Wapinzani vizuri kwa sababu ni maoni sahihi, nampongeza sana na ndiyo maana tumekuwa kimya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe mwongozo wako Mheshimiwa Nape alikuwa anadanganya Bunge hapa. Anadanganya Bunge kwa sababu Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya siyo tu kwamba wanaingia kwenye vikao vya CCM, kwa mujibu wa Katiba tumetaja hapa na naomba niseme hii hoja tumeiandika na mimi ni Naibu Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mkuu wa Wilaya ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa wa CCM na kwa maana hiyo anaingia vikao vingine vyote vinavyofuata kwenye ngazi yake. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara samahani kidogo, tunaangalia muda pale na hatutaweza kuzidi, tuna miongozo mitatu, tafadhali naomba ujaribu kufupisha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi nifupishe.

**NAIBU SPIKA:** Tafadhali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nape zile taarifa ambazo amezitoa hapa na anajaribu kuonyesha kwamba hakuna Wakuu wa Mikoa ambao wanaingia kwenye vikao vya CCM, kama hajadanganya afute ile kauli, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni Wajumbe wa Kamati za Siasa za Mikoa na Wilaya husika na taarifa yake haikuwa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ili kuweka rekodi sahihi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeruhusu miongozo mitatu, mwongozo wa Mheshimiwa Waitara nitaujibu sasa hivi. Amesema kwamba Mheshimiwa Nape alisema Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya hawaingii

kwenye zile Kamati za Siasa. Hiyo wala haihitaji kwenda kwenye Hansard, Mheshimiwa Nape amesema hivi, wanaoingia wapo lakini ni wale ambao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, mwongozo wangu kwenye hili ni kwamba ulivyosema kuhusu Katiba ya CCM uko sawasawa isipokuwa hujamalizia tu ile sehemu kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanaoingia ni wale wanachama wa Chama cha Mapinduzi. (Makofij)

Mheshimiwa Nape, mwongozo.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo wako kwamba, pamejengeka sasa utamaduni hapa na hasa kwa kweli kutoka upande wa wenzetu wa Upinzani, inapofikia mahali inatolewa hoja ambayo hawapendi kuisikia wanaanza kupiga kelele, wanaanza kuzomea na wakati mwingine wanaanza kuzungumza, Mbunge amekaa anazungumza. Kwa mtazamo, nadhani kitendo hiki siyo tu kwamba kinalipotezea heshima Bunge letu, lakini kinavuruga utaratibu wa mazungumzo humu ndani. Kama hoja huipendi isikilize fuata utaratibu ikifika mwisho toa hoja yako kuipinga hoja ya mwenzako. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana Kiti kinavumilia hali hii. Uzomeaji, upigaji kelele na mpaka inafikia mahali kama unakumbuka Mheshimiwa Sadifa alikuwa anazungumza hapa mpaka akakatizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, hii hali inakubalika ndani ya Bunge letu?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo umeombwa na Mheshimiwa Nape kuhusu utaratibu humu ndani, kwamba hoja zikiwa zinatolewa hasa upande mmoja zikionekana zinakera upande mwingine zinapigiwa kelele. Mimi kama kiongozi nikiri ni kweli kunakuwa na kelele sana zinapotokea hoja za namna hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, ziko nyakati ambazo nalazimika kutaja majina ya Wabunge ambao huwa wanapiga kelele. Waheshimiwa Wabunge niombe tujifunze kuvumiliana kwa sababu humu ndani mijadala itakuwa migumu sana kama hoja nyingine hazivumiliwi. Nadhani tuchukuliane hivyo, sisi wote tunazijua Kanuni, tuwe tukifuata Kanuni kila wakati. (Makofij)

Kwa hiyo, mwongozo wangu Mheshimiwa Nape ni kwamba utaratibu huo haikubaliki. Pale inapotokea Kiti sawa inabidi kichukue hatua lakini wakati mwingine hatua zinazochukuliwa ni hizo za kuwataja majina, wakati mwingine wananyamaza wakati mwingine wanaendelea kupiga kelele. Hata hivyo, Kiti

kama bado kinasikia basi kinajaribu kuona hivyo lakini tutajitahidi wakati mwingine kuchukua hatua mahususi. (Makofi)

Mheshimiwa Nchambi.

**MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wabheja sana. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) lakini narejea Kanuni ya 64(1)(a) na Kanuni ya 63(1) ambayo ningependa niisome, kulingana na wakati nisingesoma Kanuni zote hizo. Kanuni ya 63(1) inasema:-

*"Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge ye yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu."*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Kubenea akichangia alitamka mwenyewe akiamini ni kweli kuwa jeshi lilitaka kuingia mkataba wa kununua silaha ambazo ni feki. Jambo hili ni very sensitive, masuala ya kiulinzi ambayo kila mtu iwe Mbunge ama mtu yeyote anafahamu siri kubwa za kiusalama za Taifa letu kuzitoa wazi kiasi cha wenzetu hata nchi jirani ama watu wowote ambao hawana nia njema na ulinzi wa Taifa letu kujua mambo haya ambayo ni sensitive, siyo jambo jema. Nikuombe mwongozo wako, endapo Mheshimiwa Mbunge anao uhakika na jambo hili basi athibitishe na kama hana uhakika na jambo hili pia ni lazima Kamati ya Maadili iliangalie suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko humu kwa sababu ya amani na utulivu lakini pia kupaka matope vyombo vyetu vya kiulinzi na usalama kwamba vilitaka kuingia mikataba feki, hilo nashukuru limetolewa majibu na Mheshimiwa Waziri wakati alipokuwa aki-wind up hapo, ameliweka vizuri. Hili lingine la silaha feki mpaka zinafika nchini Wanajeshi wetu ama Maafisa wa Jeshi wanakuja kuthibitisha silaha hizi feki na yeye Mbunge pengine alikuwa ni shuhuda akashuhudia jambo hili, jambo hili ni sensitive, niombe mwongozo wako lishughulikiwe kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. Wabheja sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na nitatoa mwongozo huo baadaye. Pia kuna ombi alilokuwa ameomba Mheshimiwa Waziri wakati akijibu hoja kuhusu tuhuma zilizotolewa za kampuni ambayo inaonekana jeshi limeingia mkataba nayo na kumhusisha Waziri kwamba kuna mkataba wa yeye kujengewa nyumba. Mwongozo wa Mheshimiwa Nchambi na ombi la Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) nitautoa hapo baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, mambo mawili, moja kuna tangazo hapa kutoka kwa Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, amepoteza simu yake, ni Samsung5, yejote atakayeiona anaomba amkabidhi au akabidhi Ofisi ya Katibu. Naona hizi simu kuanzia jana zinatembea sana humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, lingine ni Kanuni ya 61, ni kukumbushana tu tukaisome. Wabunge wengi huwa wanapenda kusema wana-declare interest kwa kuwa tu Mjumbe wa Kamati ama kwa kuwa tu analifahamu jambo fulani, lakini kimsingi Kanuni hizi zinapoongelea ku-declare interest, zinaongelea maslahi ya kifedha. Kanuni ya 61 Waheshimiwa Wabunge tukaisome, kama huna maslahi binafsi ya kifedha huna haja ya kutuambia kwamba una-declare interest. Kwa hiyo, ni hicho tu nilitaka tukumbushane maana naona tunapata tabu hata saa ya maswali mtu anasema niseme mimi nina lile na lile, kama unayo maslahi binafsi ya kifedha siyo maslahi mengine. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake kupita kwa kishindo. Imepita kwa kishindo kikubwa kwa sababu katika kuona kwangu hii ndiyo bajeti iliyoungwa mkono na pande zote mbili zinazowakilishwa humu Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri, nikutakie kila la kheri na naona vikosi vyako viko hapa, katika utekelezaji wa yale mambo ambayo mmeyaombea fedha. Tunaamini kwamba mwakani hatutakuwa na maswali kuhusu mambo haya kwa sababu tunaamini fedha mlizopewa na Bunge mtazipata kwa kadri mlivyoisikia michango humu ndani. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu.

(Saa 2.27 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 11 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)